# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 5 Mei, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tisa, Kikao cha Kumi na Saba, leo tarehe 5 Mei, 2025.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 210

**Haki za Wastaafu**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, kwa nini Wastaafu hawapewi haki zao mara tu wanapostaafu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ucheleweshaji wa malipo ya mafao ya wastaafu katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa sasa limekuwa historia. Mifuko imeboresha mifumo yao ya TEHAMA, hatua ambayo imeiwezesha kulipa mafao ya wastaafu ndani ya kipindi kilichowekwa kisheria, au hata kwa muda mfupi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kusimamia kwa karibu utendaji wa Mifuko ili kuhakikisha kuwa inaendelea

kuondoa vikwazo na kuwalipa wastaafu mafao yao mapema kadri inavyotakiwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa mujibu wa wastaafu, Serikali iliwaahidi kutoa nyongeza ya pensheni kwa kila mstaafu nchi nzima lakini jambo hili mpaka sasa halijafanyika. Ninataka kujua kauli ya Serikali ni ipi katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; wastaafu wengi kabla ya kustaafu walijiendeleza na wakapandishwa madaraja, lakini baada ya kustaafu hawakulipwa mafao yao kutokana na yale madaraja mapya. Ninataka kujua kauli ya Serikali katika hili?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Fiyao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari zingatio la nyongeza ya pensheni ya wastaafu limekwisha kufanyika tangu mwezi Januari na Februari. Utekelezaji ulikwisha kuanza kutoka kima cha kiwango cha shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000 na hii inafanyika katika pande zote kwa wale wastaafu wa Sekta Binafsi *(NSSF)* na wale walio katika ustaafu wa Sekta ya Umma *(PSSSF)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwamba tayari Serikali kwa maagizo mahususi ya Mheshimiwa Rais, imeendelea kuhakikisha kwamba inaboresha maslahi ya wastaafu kwenye hayo maeneo ikiwa ni pamoja na wale ambao fedha zao

zinapitia Hazina. Kazi kubwa inafanyika ili kuweza kuhakikisha kwamba haki na stahiki zao wanazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, amesema wastaafu wengi wanapata changamoto kuhusiana na pale wanapostaafu, lakini walikuwa wamepandishwa madaraja, ni namna gani malipo yao. Kwa sisi Ofisini mpaka sasa wastaafu wote changamoto zao zimeshughulikiwa. Kama Mheshimiwa atakuwa na orodha mahususi kwa sababu amesema wastaafu wengi, ni vizuri akalileta haraka sana kabla hata ya kuuliza swali tuweze kulishughulikia kwa sababu wanaostaafu ni watu ambao wamelitumikia Taifa hili kwa moyo lakini pia wamekuwa wazalendo na wametumikia kwa utumishi uliotukuka. Mheshimiwa Rais amesema wakati wote tuweze kuzingatia kwenye kuhakikisha kwamba tunawapa kipaumbele katika kutekeleza haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii nimwombe Mheshimiwa Mbunge kama anao atuletee hiyo orodha ili tuweze kulishughulikia mapema. Katika ofisi kwa sasa kwenye *desk* hakuna *pending issue* ya wastaafu katika suala hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Patrobass Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula, Mbunge wa Kuteuliwa, aulize swali lake.

Na. 211

**Kukarabati Shule Kongwe – Missenyi**

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kukarabati Shule Kongwe za Msingi na Sekondari – Missenyi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi ina shule kongwe 55 (msingi 52 na sekondari tatu). Kutokana na hali ya miundombinu ya shule hizo kuwa chakavu, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu kwa kukarabati au kujenga miundombinu mipya kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025, Serikali imetumia shilingi 182,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa vyumba vya madarasa kwenye shule 11 na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule tano katika Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi. Aidha, Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali imetenga shilingi 60,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa vyumba chakavu vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Lugoye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kukarabati shule chakavu za msingi na sekondari kadri ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Missenyi imekuwa ikiahidi kufanya tathmini ya hali ya majengo haya yaliyochakaa sana hususan Shule ya Msingi ya Novati Rutageruka ambayo bahati nzuri au mbaya imeitwa jina la marehemu mzee wangu iliyopo Kijiji cha Kitobo ambayo kwa kweli hali yake ni mbaya sana na inahatarisha maisha ya wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri nilishampelekea *clip* hiyo na kwa kweli ninaomba ipewe kipaumbele hali ni mbaya mno na miundombinu imechakaa sana. Kwa hiyo, ninaomba sasa Serikali itupie jicho hilo na ikibidi Naibu Waziri twende wote Waziri akaone hiyo, maana yake

ninaona kama *video clip* haikutosha, ninaomba twende wote akaone hali halisi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi, ninaamini kabisa Mheshimiwa Waziri ameyachukua hayo na atayafanyia kazi kwa namna ambavyo ameomba. Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Je, ni lini Serikali itakarabati Shule ya Sekondari Mrama katika Jimbo la Singida Kaskazini hasa ukizingatia ni chakavu na ni kongwe sana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuna shule ambazo zimejengwa hata kabla ya nchi yetu kupata uhuru na shule hizi hasa shule za msingi ni shule kongwe na ni chakavu. Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuhakikisha inazifikia shule hizi kwa awamu kwa ajili ya kuzikarabati ili ziwe katika hali nzuri na ziweze kutoa mazingira mazuri zaidi ya wanafunzi wetu kusoma na mazingira mazuri zaidi kwa ajili ya walimu kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Aysharose Mattembe, kwamba katika jitihada zile za Serikali kuendelea kuzifikia shule hizi kongwe, shule aliyoitaja itafikiwa kwa ajili ya kukarabatiwa ili iwe katika hadhi nzuri iendane na shule nyingine ambazo Serikali inaendelea kuzijenga kwa maana ya shule mpya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mbogwe inazo shule nyingi ambazo zimechakaa na ni za muda mrefu tukianzia Kata ya Nanda, Kata ya Ilolwangulu pamoja na Ushirika. Serikali ina mpango gani kutoa pesa ili shule zile ziweze kukarabatiwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka wa fedha, Serikali hasa hii ya Awamu ya Sita imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu katika Sekta ya Elimu. Katika kipindi cha miaka minne tu ya Serikali ya Awamu ya Sita tayari shilingi trilioni 5.1 zimetumika katika kuimarisha Sekta hii muhimu ya Elimu Msingi kwa maana ya shule zetu, madarasa ya awali shule za msingi na shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Nicodemas Maganga kwamba hata katika Halmashauri ya Mbogwe, Serikali imekuwa ikifika kila mwaka wa bajeti kwa ajili ya kukarabati shule hizi kongwe. Nimhakikishie Serikali itaendelea kufanya hivyo katika kila mwaka wa bajeti tutaendelea kutenga fedha na kufikia shule hizi kongwe kwa awamu kuhakikisha kwamba na zenyewe zinakuwa katika hadhi nzuri sambamba na shule mpya ambazo kila mwaka Serikali ya Awamu ya Sita inazijenga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi. Kwanza, niipongeze Serikali; ndani ya Wilaya Missenyi Serikali imefanya kazi kubwa na nzuri. Tumejengewa shule mpya tatu za sekondari, shule mpya ya msingi lakini na vyumba vya madarasa zaidi ya 200. Pamoja na hayo kama alivyosema kwenye majibu ya swali la msingi bado kuna shule chakavu ambazo nazo ukarabati kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri umeendelea kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu la msingi; je, ni lini Serikali angalau itapunguza hizo shule nyingi za msingi ambazo zimechakaa ili angalau watoto wetu waweze kusomea katika mazingira mazuri kama wenzao?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita ina dhamira ya dhati ya kuendelea kuimarisha Sekta ya Elimu na hasa elimu msingi na ndiyo maana utaona kwamba katika kipindi cha miaka minne cha Serikali ya Awamu ya Sita, shilingi trilioni 5.1 zimetumika kuimarisha miundombinu na sekta nzima ya elimu kwa ujumla wake kwa upande wa elimu msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Kyombo, kwamba Serikali itaendelea kuleta fedha kwa ajili ya kukarabati shule kongwe. Tunafahamu shule hizi zilijengwa hata kabla ya Tanzania hii kupata uhuru (kabla ya nchi yetu kupata uhuru). Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuleta fedha ili kuzikarabati hizi shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetenga shilingi milioni 60 kwa ajili ya kuendelea kukarabati shule hizi ambazo ni chakavu. Pia, Mheshimiwa Mbunge umekuwa ukipaza sauti yako sana kutaka kuhakikisha kwamba miundombinu hii katika Sekta ya Elimu inaimarishwa katika Jimbo lako ukiwasemea wananchi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, imetengwa shilingi milioni 157.7 kwa ajili ya kwenda kukarabati Shule ya Msingi Noveti. Pia, shule ile itajengewa madarasa matano, kutakuwa na vyumba viwili vya madarasa ya awali vile vya mfano na kutakuwa kuna matundu ya vyoo 12. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ninaomba ukae mkao wa kupokea neema hiyo kubwa inayoletwa na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Jimbo lako la Missenyi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaona wengi mna maswali ya nyongeza kwenye swali hilo, basi nitaomba Mheshimiwa Waziri kwa wakati wao waweze kumwomba na ataweza kuwasaidia kwa maslahi mapana ya Majimbo yetu. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga, aulize swali lake.

Na. 212

**Kukamilisha Ujenzi wa Barabara ya Mangio hadi Kivisini - Mwanga**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO** aliuliza:-

Je, Serikali kupitia *TARURA* ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Mangio hadi Kivizini Wilayani Mwanga?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mangio hadi Kivisini yenye urefu wa kilometa 7.1 inapatikana ukanda wa milimani katika Wilaya ya Mwanga. Kwa sasa *TARURA* inaendelea na usanifu wa barabara hiyo ambapo utakapokamilika na makisio ya gharama kufahamika itawekwa kwenye mipango ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhudumia mtandao wa barabara na madaraja katika Wilaya ya Mwanga kwa kujenga, kukarabati na kufanya matengenezo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kwenye swali hili la msingi, lakini nina swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza tu kwamba ni lini Serikali itakarabati kwa ukamilifu Barabara za (a) Masumbeni - Butu na (b) Msangeni – Butu ikizingatiwa kwamba barabara hizi zinaelekea maeneo yanayotegemewa kwa uzalishaji wa chakula na Serikali imewekeza mabilioni ya fedha kwenye miradi ya umwagiliaji, lakini barabara hazipitiki mwaka mzima? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara zetu hizi za Wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*. Umuhimu wake ni mkubwa kiuchumi kwa maana ya kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao mbalimbali za uchumi ikiwemo kilimo na kuwawezesha wananchi kuweza kufikia huduma za msingi za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka minne cha Serikali ya Awamu ya Sita, Shilingi bilioni 12.05 zimetumika kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya barabara katika Wilaya hii ya Mwanga. Pia, katika mwaka huu wa bajeti wa 2024/2025, shilingi bilioni 5.2 zimetengwa kwa ajili ya kuhakikisha zinaendelea kuimarisha barabara hizi muhimu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, barabara hizi mbili alizozitaja Serikali itazifikia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zinajengwa na zinapitika katika kipindi cha mwaka mzima ili kuweza kuwanufaisha wananchi kiuchumi kwa maana ya shughuli zao za kilimo na shughuli mbalimbali za uchumi wanazozifanya, lakini pia kuwawezesha kufikia huduma za msingi za kijamii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge umewasemea wananchi wako na Serikali ya Awamu ya Sita imekusikia na itafika kuja kuleta maendeleo hayo kwa ajili ya wananchi wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, nimekuona.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika Jimbo la Lushoto zimeharibu miundombinu ya barabara hasa Barabara ya Malibwi - Kwekanga hadi Makole. Mpaka ninavyoongea sasa hivi wananchi wana miezi miwili hawapati huduma. Je, nini mpango wa Serikali wa dharura kutengeneza barabara zile ili wananchi wangu waendelee kupata huduma hiyo? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikichukua hatua za dharura kuweza kurudisha mawasiliano kwenye barabara ambazo mawasiliano yamekatika. Serikali imekuwa ikiendelea pia kuimarisha barabara zetu za Wilaya kuhakikisha kwamba zinakuwa katika mazingira ambayo zinaweza kupitika katika kipindi cha mwaka mzima ili kuweza kuwanufaisha wananchi, kwa maana ya kuwawezesha kufanya shughuli zao za uchumi na kufikia huduma za msingi za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka huu wa Fedha 2024/2025 kuna bilioni 21 ambazo zimetengwa kwa ajili ya dharura, kuhudumia barabara zetu hizi za *TARURA* kwa dharura. Pia Bunge hili Tukufu lilipitisha nyongeza ya bajeti bilioni 50 kwa ajili ya kuhudumia barabara hizi ambazo zinaharibika kwa utaratibu wa dharura. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutafika katika eneo alilolitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwagiza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa akishirikiana na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya waweze kufika katika eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge, kufanya tathmini na kuleta kwenye mipango ili eneo hilo liweze kupatiwa huduma ya kurudisha mawasiliano ili barabara hii iweze kuwanufaisha wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nancy Nyalusi, nimekuona.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Barabara ya Mdabulo - Ihanu ni barabara inayotegemewa na wananchi katika shughuli zao za kiuchumi. Je, ni lini Serikali itafanya maboresho katika barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imeweka kipaumbele kikubwa sana

katika kuimarisha barabara zetu hizi za Wilaya zinazosimamiwa na *TARURA,* ndiyo maana utaona tangu Awamu ya Sita imeanza kufanya kazi utaona bajeti ya *TARURA* imeongezeka mara dufu kutoka bilioni 275 kila mwaka, mpaka sasa tunatarajia bajeti ya *TARURA* katika mwaka wa fedha ujao 2025/2026 itakuwa ni shilingi trilioni 1.18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita unaiona kwa nyongeza hii ya bajeti. Ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa kwamba, Serikali itafika kwenye barabara aliyoitaja kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaendelea kuiboresha, kuiweka katika hadhi ambayo itapitika mwaka mzima ili iweze kuwanufaisha wananchi kiuchumi na iwawezeshe waweze kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Nancy upokee taarifa hiyo, Serikali itafika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amar nilikuona halafu atafuatia Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, barabara za mitaa kwenye Makao Makuu ya Wilaya pale Karumwa zimeharibika. Je, upo tayari kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Nyang'hwale aweze kuzifungua barabara hizo za Mtaa wa Mahango, Marekana, Bubapa, Busengwa pamoja Butaranda? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendelea kuimarisha barabara zetu hizi za wilaya ambazo zinasimamiwa na *TARURA,* ndiyo maana utaiona dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha hivyo na ndiyo maana kila mwaka bajeti inaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), kumwagiza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa akishirikiana na Meneja wa *TARURA*

wa Wilaya kuweza kuzifanyia tathmini barabara hizi katika mitaa ambayo ameitaja Mheshimiwa Hussein Amar ili ziweze kuwepo katika mpango kwa ajili ya kuja kuhakikisha kwamba zinapatiwa fedha na zinakarabatiwa ziwe katika hadhi nzuri na ziweze kuwanufaisha wananchi wa Jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Kibondo, barabara ya kutoka Kibondo Mjini kwenda Kumhasha imeharibika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika Halmashauri ya Kibondo. Je, Serikali ipo tayari kutengeneza barabara hiyo ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wanaotoa bidhaa kutoka shambani kuleta Mjini Kibondo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za dharura na mpango wa muda mrefu Serikali inaendelea kukarabati na kuhakikisha barabara hizi zinakuwa katika hadhi nzuri kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na kufikia huduma za msingi za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Josephine Genzabuke kwamba, dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha barabara zetu za Wilaya ipo pale pale na ipo kwa vitendo na barabara hizi ulizozitaja na hasa hii katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo zitafikiwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zinaimarishwa na zinaweza kupitika katika kipindi cha mwaka mzima na hatua za dharura kuchukuliwa kwenye maeneo ambayo mawasiliano yamekatika ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na waweze kufikia huduma za kimsingi za kijamii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai.

Na. 213

**Madeni ya Walimu wa Shule za Sekondari Waliohamishiwa Shule za Msingi**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, lini Serikali italipa madeni ya Walimu wa Shule za Sekondari waliohamishiwa Shule za Msingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuboresha ikama ya walimu wa shule za msingi nchini imekuwa ikihamisha walimu kwa kuzingatia ikama ya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2017 hadi 2025, walimu 1,914 wamehamishwa kutoka shule za sekondari kwenda shule za msingi. Fedha iliyohitajika kwa ajili ya uhamisho huo ni shilingi bilioni 2.08 ambapo shilingi bilioni 1.22 zimelipwa na kiasi ambacho hakijalipwa ni shilingi milioni 865.93. Serikali itaendelea kulipa madeni ya uhamisho wa walimu kadri ya upatikaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saasisha Elinikyo Mafuwe.

**MHE. SAASISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninawapongeza Walimu wote wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa elimu kwa wanafunzi wetu katika Wilaya ya Hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika Wilaya ya Hai kuna Walimu 184 ambao walihamishwa kutoka shule za sekondari kwenda shule za msingi, wanaidai Serikali sasa hivi milioni 120. Je, ni lini Serikali italipa madeni haya ya watumishi ambao wamehama kutoka Shule ya Msingi kwenda Sekondari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI alikutana na watumishi wastaafu katika Wilaya ya Hai na watumishi ambao siyo walimu, nao wanadai shilingi milioni 915 na tayari Waziri alikusanya taarifa zao, lakini mpaka sasa hivi watumishi hao wastaafu na walioko kazini ambao siyo walimu hawajalipwa fedha zao. Je, ni lini Serikali italipa madeni kwa watumishi hawa ambayo yamekuwa ni kero kwao?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kazi kubwa sana na nzuri inayofanywa na watumishi wetu ikiwemo watumishi katika kada ya elimu. Serikali imekuwa ikichukuwa hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba inaendelea kuboresha maslahi ya watumishi hawa muhimu, mojawapo ni kuhakikisha kwamba inaendelea kuchukua jitihada za kuwalipa stahiki zao; na Mheshimiwa Mbunge tayari alinifuata akanielezea madai ya watumishi hawa kutoka katika Jimbo lake na ninachoomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, jambo hili kwa sababu ulishalileta tunalifanyia kazi ili liweze kupata Suluhu, watumishi wetu hawa tunatambua kazi kubwa wanayoifanya na tunatambua kwamba wana kila haki ya kuweza kupata stahili zao na tutasimamia ili tuweze kutekeleza kwa wakati jambo hili la kuwalipa stahili zako.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Katimba, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI). Waheshimiwa Wabunge, ninajua maswali ni mengi kwenye Wizara hii, kwa hiyo Mheshimiwa Zainab Katimba usichoke kuwapokea Waheshimiwa Wabunge, ninaamini upo vizuri utaendelea kuwajibu kwa maslahi mapana ya Majimbo yao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 214

**Kukabiliana na Janga la Ukataji Miti**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Taifa wa kupanda miti kwa kipindi cha muda mfupi na mrefu ili kukabiliana na janga la kukata miti?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU K.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii, inatekeleza mpango wa muda mrefu na muda wa kati kuweka mikakati wa kurejesha na kupanda miti maeneo yaliyoharibiwa takribani hekta millioni 5.2 ifikapo 2030. Shughuli zinazoendelea ni pamoja na kuhamasisha wananchi kutunza mazingira kupitia kampeni za upandaji miti milioni 1.5 kwa kila Halmashauri kwa kila mwaka na Kampeni maalum ya 'Soma na Mti' ambapo Serikali itahakikisha wanafunzi wote wa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu kupanda miti na kuitunza katika kipindi chao chote cha masomo wawapo mashuleni na vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS)* imeendelea kuzalisha miche ya miti ya aina mbalimbali na kuigawa bure kwa Wizara na Taasisi, Wadau, Sekta Binafsi pamoja na wananchi kwa lengo la kupanda miti katika maeneo yao kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanarejesha uoto wa asili nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naomba kutoa rai kwa wananchi na sekta binafsi kuendelea kupanda miti kwenye

maeneo mbalimbali nchini ili kukabiliana na uharibifu wa ardhi na kuenea kwa jangwa na ukame.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Prof. Patrick Aloyce Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; majangili wanaotumia msumeno nyororo au *chainsaw,* wamekuwa kikwazo kikubwa sana kwa Serikali kwa sababu wanaharibu mazingira ya miti iliyopadwa, miti ya asili na ile ambayo inatunza vyanzo vya maji. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu ujangili huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, mnayo mipango gani ya kufuatilia na kufanya tathmini ya miradi ambayo umeitaja ya kupanda miti ili kuangalia kama ufanisi au changamoto katika miradi ambayo inatekelezwa hapa nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU K.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, moja hili la kuhusiana na matumizi ya *chain saw*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, pamoja na kuwa mashine hizo zipo zinauzwa hapa nchini, lakini kuna utaratibu maalum ambao upo kwa mujibu wa mwongozo kwamba zisitumike hovyo kwenye maeneo ambayo hayajapewa kibali, matumizi yoyote ya *chain saw* siyo tu kwa Kilimanjaro, lakini nitoe maelekezo kwa nchi nzima kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwamba ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia mashine ya *chainsaw* bila kuwa na kibali halali kutoka kwenye mamlaka zilizopo kwenye maeneo hayo na hasa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwenye maeneo hata yale ya misitu ambayo ipo kwa mujibu wa sheria na inatambulika kwenye maeneo mbalimbali kwa mujibu wa maeneo na Halmashauri au Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, huko nako pia kuna

utaratibu wake wa kuweza kutumia, hata kule kuliko na miti ambayo imepadwa namna ya uvunaji kuna utaratibu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa maelekezo kwamba, ni muhimu wazingatie utaratibu wa kikanuni na kisheria uliowekwa katika matumizi ya *chain saw,* kama atakiuka mtu tutachukua hatua kali sana za kisheria kupitia zetu za Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ni kwamba, zipo timu kuhusiana na suala la *monitoring and evaluation* ambazo zinafanya *monitoring and evaluation* mojawapo ni maafisa viungo walio katika maeneo yote huku nchini hasa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao wanafanya kazi hii ya kuhakikisha kwamba upandaji miti unafanyika, lakini hata ile ambayo imeharibiwa basi waweze kuchukua hatua.  Wapo vile vile Maafisa Mazingira kwenye Halmashauri zetu zote na wanalipwa na Serikali hii ni waajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia mabalozi wa mazingira na hivyo hivyo wapo mameneja wa *NEMC* katika mamlaka zote za Mikoa na Wilaya ambao wanasimamia suala hili, ikiwa ni sambamba na *TARURA* ambao wapo chini ya Ofisi ya TAMISEMI nao wanafanya kazi ya kuhakikisha kwamba miti yote iliyopandwa pembezoni mwa barabara inaendelea kustawi pia kukaa katika hali ambayo inaweza ikaleta usaidizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ni kwamba, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Mamlaka zote za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanalo agizo mahususi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na wanafahamu kwamba maagizo haya yalikuwa ya Mheshimiwa Rais mwenyewe ambaye ni *champion* wa mazingira ndiyo maana akaanzisha *program* mbalimbali za kuweza kuhakikisha kunakuwa na ustawi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuna wimbi kubwa la ukataji wa miti ya mikoko katika ukanda wa bahari hasa Zanzibar na kusababisha maji ya bahari kupanda,

kuvamia katika makazi ya watu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kusimamia *program* ya upandaji wa miti ya mikoko na kuweza kuilinda ili kuepuka athari za tabianchi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU K.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ndiyo maana unaona lipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mipango ambayo ipo chini ya ofisi hii ambayo inasimamiwa na Makamu wa Rais lakini pia Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Masauni pamoja na Naibu Waziri Chilo na Katibu Mkuu Luhemeja, wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kukutana na pande zote mbili za Muungano ili kuweza kuweka mikakati madhubuti ya kudhibiti uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hiki nilichokisema kwenye jibu langu la awali kipo pia katika upande wa Zanzibar na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi anafanya kazi nzuri sana wakishirikiana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha mambo yanakwenda sawasawa katika mazingira kwa sababu tukitambua uhai wetu unategemea sana mazingira mazuri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Patrobas Katambi kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Saada Mansoor Hussein Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. Hayupo, Mheshimiwa Mariam Kisangi kwa niaba yake.

Na. 215

**Matumizi ya Mkaa Mbadala**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha matumizi ya mkaa mbadala yanaenezwa hadi Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba, matumizi ya mkaa mbadala yanaenezwa hadi Zanzibar, Serikali kupitia Shirika la Madini *(STAMICO)* imesajili mawakala wanne kwa ajili ya kuhakikisha mkaa mbadala uitwao *Rafiki Briquettes* unafika Zanzbar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawakala hawa ni Chama cha Ushirika, Maisha Gemu, Salum Omar, *Easy Fix* na Wanawake na Samia Magharibi B. Aidha, juhudi pia zinafanyika ili kupata eneo ambalo *STAMICO* wataweka kontena kubwa ambalo litakuwa linapokea mkaa huu mbadala wa *Rafiki Briquettes* ili kuihifadhi kwa ajili ya kusambazwa katika maeneo yote ya Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, sogea kwenye sehemu ambayo inafanya kazi vizuri.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba, maeneo yote katika nchi ya Tanzania wanapata nishati hiyo mbadala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umelisikia vizuri? Haya naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninashukuru kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisangi, ni kweli Serikali inao mkakati kupitia *STAMICO*, miezi michache iliyopita makontena haya yalisambazwa kwenye mikoa mbalimbali kulingana na *zone* zake, kwenye ile mikoa ambayo haijafikiwa pia *STAMICO* wanao mkakati wa kuendelea kupeleka makontena haya ili kuhakikisha mkaa huu wa *Rafiki Briquettes*

unaendelea kutumika katika maeneo yote ya nchi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inao mkakati sasa hivi makontena yamefika kwenye mikoa mingi na tutaendelea hivyo hivyo kwa awamu zinazokuja.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Judith Kapinga kwa niaba ya Waziri wa Wizara ya Nishati. Tunaendelea na Wizara ya Fedha Mheshimiwa Mharami Shaban Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, aulize swali lake.

Na. 216

**Kusitisha Vibali vya Mashine za Kamari**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kusitisha kutoa vibali kwa mashine za Kamari ili kupunguza umaskini kwa Vijana?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za hivi karibuni kumekuwepo na wimbi la waendeshaji mashine za *slots* pasipo kuzingatia sheria za michezo ya kubahatisha na sheria nyingine za nchi. Mathalani, waendeshaji haramu huweka mashine zao kwenye makazi ya watu, maduka ya bidhaa, maeneo ya vijijini na pia huruhusu watu wa chini ya miaka 18 kushiriki katika michezo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizi, bodi imechukua hatua kadhaa kama ifuatavyo: -

(i) Kusitisha utoaji wa leseni kwa waendeshaji wapya wa mashine za sloti;

(ii) Kuanzisha misako na *operation* ya kusaka waendeshaji haramu wa mashine za sloti nchi nzima kwa kushirikiana na mamlaka nyingine kama vile Polisi, *TRA* na Uhamiaji;

(iii) Kuongeza kaguzi za mara kwa mara katika maeneo mbalimbali ya nchi ilipo biashara ya mashine za sloti;

(iv) Kuendesha kampeni inayowalenga vijana na jamii kufanya kazi za uzalishaji;

(v) Kuongeza udhibiti wa uingizaji wa mashine za sloti hapa nchini kwenye maeneo ya mipakani kwa kushirikiana na *TRA*;

(vi) Kuanza mchakato wa kutumia mifumo ya kielektroniki kudhibiti biashara ya mashine za sloti zinazoendeshwa mitaani;

(vii) Kuingia makubaliano *(MoU)* na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa lengo la kuwa na ushirikiano wa karibu wa kudhibiti waendeshaji haramu wa mashine za sloti; na

(viii) Kupitia mara kwa mara Sheria ya Michezo ya Kubahatisha kwa lengo la kuondoa kasoro na mianya inayotumiwa na waendeshaji haramu wa mashine za sloti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi inakusudia kutekeleza hatua hizi kikamilifu ikiwa ni sehemu ya juhudi yake ya kuhakikisha kuwa, jamii ikiwemo vijana inalindwa dhidi ya athari hasi za michezo ya kubahatisha ikiwemo umaskini. Bodi itaendelea kuchukua hatua zaidi za kuondoa athari zote hasi za michezo ya kubahatisha. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Mashine hizi za *slot* zimemwagika nyingi sana mtaani, lakini majibu yake aliyoyatoa ni mazuri sana. Kuna hili suala la *betting* ambalo kuna vibanda vingi sana vimefunguliwa katika miji yetu na maeneo mbalimbali. Vijana wetu wanafanya *betting* na kujitia umaskini katika kufanya jambo hili. Je, Serikali ina

mpango gani sasa wa kuzuia hizi *betting,* ili vijana wetu waende vizuri katika uchumi wao? Ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Muharani Mkenge, lakini kabla ya kujibu ninampongeza sana kwa namna anavyofuatilia suala hili, ili kulinda maadili ya vijana wetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niielekeze Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kuendelea na zoezi la ukaguzi wa mara kwa mara na ufuatiliaji wa karibu sana ili kuhakikisha Sheria na taratibu zimefuatwa, ili kuhami na kunusuru vijana wetu katika suala zima la maadili. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Fedha, kwa majibu hayo kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, aulize swali lake.

Na. 217

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Kata ya Kate na Kipande, Nkasi Kusini**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Vituo vya Polisi, Kata za Kate na Kipande, kwani tayari maeneo yameandaliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kate umefikia kwenye hatua ya umaliziaji na kiasi cha fedha, shilingi 25,000,000, kimetengwa kwenye Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa

fedha 2024/2025. Katika Kata ya Kipande limetengwa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 8,092 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kata, utakaogharimu shilingi 115,000,000. Fedha hizo zitatengwa kwenye mwaka wa fedha 2026/2027. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Serikali imejenga Kituo Kipya cha Polisi, Kata ya Kala, Kijiji cha Mpasa. Askari wako pale hawana vitendea kazi na ukizingatia ni Ukanda wa Ziwa Tanganyika na Mheshimiwa Waziri aliahidi kupeleka boti pamoja na pikipiki kabla ya mwezi Machi, lakini mpaka sasahivi vifaa havijafika. Ni lini mnapeleka boti na pikipiki katika Kituo Kipya cha Polisi Mpasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, Serikali inatambua kwamba, kuna upungufu wa vitendea kazi kwenye Kituo cha Polisi alichokitaja. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan iko makini na imeongeza vitendea kazi vingi zikiwemo pikipiki pamoja na boti na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutapeleka vifaa hivyo, kwa ajili ya utendaji kazi katika eneo hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Hali ya Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Bunda ambacho kinahudumia majimbo matatu; Bunda Mjini, Bunda kwa Getere pamoja na Mwibara ni mbaya. Ninataka kujua, ni lini watatujengea Kituo kipya cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya ya Bunda na hasa ukuzingatia Mji wa Bunda unakua? Nimeliongelea

sana hapa, kama Mbunge wa wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijenga Vituo vya Polisi vyenye hadhi vya mikoa, wilaya, kata pamoja na shehia hapa nchini. Wilaya ya Bunda pia ni wilaya ambayo ina majimbo matatu, kama alivyosema na tunatambua pia kwamba, wananchi hawa wanatakiwa kulindwa na mali zao. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tumekichukua kituo hicho, tutakiweka kwenye mpango na kukitengea fedha kwa ajili ya kukijenga kwa hadhi ya Wilaya ya Bunda. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hapo.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Oliver Semuguruka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Sogea pembeni hapo.

**MBUNGE FULANI:** Njoo huku, za huku zinafanya kazi.

**MWENYEKITI:** Jaribu nyingine. Waheshimiwa, ninaomba utulivu tafadhali.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Kituo cha Polisi Wilaya ya Ngara, ninafikiri Mheshimiwa Waziri amesikia. Majibu Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nilifika Ngara, ni kweli Kituo cha Ngara kipo kwenye hatua ya lenta. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Mkoa pamoja na Mbunge wa Jimbo kwa ufuatiliaji na ninawapongeza wananchi kwa kutumia nguvu zao kujenga kituo hicho mpaka kufikia hatua ya lenta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali imepanga kumalizia vituo 77 ambavyo ni maboma, kikiwepo pia, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Ngara. Ahsante sana.

*(Hapa vinasa sauti katika Ukumbi wa Bunge vilipata hitilafu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba utulivu. Wanaohusika na mitambo, tafadhali ninaomba tuweke sawa, ili tuweze kusikilizana Bungeni. Tayari zinafanya kazi?

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuvumilie tu kidogo, watu wa *IT* wanashughulikia. Ni lazima tusikilizane Bungeni ili *Hansard* zetu ziweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Waziri, unaweza kukaa kwa dakika chache, ili tusubiri. Waheshimiwa Wabunge kwa busara tu, kuna upande wa pili huku zinafanya kazi. Mwenye swali anaweza kuja kuuliza huku; siyo upande huu, ni upande ule pale. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri, sasa jaribu kujibu kwa upande huu. Mheshimiwa Waziri, basi jibu hapo, inafanya kazi. Endelea Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi cha Ngara ni moja ya maboma 77 ambayo yametengewa fedha kwenye mwaka wa fedha 2025/2026, kwa ajili ya ukamilishaji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera, aulize swali lake.

Na. 218

**Kudhibiti Biashara Haramu ya Binadamu na Dawa za Kulevya**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza:-

Je, Serikali imejiandaaje kukabiliana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu na Dawa za Kulevya kwani mbinu za uhalifu zimebadilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu hapa nchini na kwamba, mbinu za utendekaji wake zimekuwa zikibadilika. Katika kupambana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, Serikali ina mikakati mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuwa na Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu, kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa Sheria na wadau mbalimbali, kuratibu kampeni ya kutoa elimu kwa umma kuhusu uhalifu huu na madhara yake, mpango wa kuanzisha Kituo cha Kupokelea Taarifa za Usafirishaji Haramu wa Binadamu na mpango wa kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya, Kusimamia na Kuhifadhi Taarifa za Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukubaliana na mabadiliko ya mara kwa mara ya mbinu za uhalifu wa dawa za kulevya, Serikali imekuwa ikiwajengea uwezo maafisa wa udhibiti kwa kuwapatia mafunzo, ushiriki wa mikutano na vikao vya kimkakati vya kubadilishana taarifa za uzoefu na nchi na taasisi mbalimbali

za kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; mwaka 2023 Bunge lako lili-*ratify* Mkataba wa Kimataifa kwenye hoja ya kudhibiti biashara ya dawa ya kulevya pamoja na usafirishaji haramu wa binadamu. Je, sisi kama Serikali, tumeanza utekelezaji wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa sababu, sasa ni mwaka wa pili, je, Serikali imeanza kufanya tathmini ili kuona faida, mafanikio na hasara ya *ratification* hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera, kama ifuatavyo; ni kweli, mwaka 2023, kama nchi, tuliridhia Mkataba wa Kimataifa wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na dawa za kulevya. Utekelezaji huo tayari umeshaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, tathmini imefanyika na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tathmini ya kuridhia mkataba huu imekuwa na mafanikio makubwa sana na wanashuhudia jinsi hii biashara ya dawa za kulevya zinavyokamatwa mara kwa mara. Kwa hiyo, kwa kweli, tathmini imefanyika na mkataba huu umekuwa na manufaa makubwa sana hapa nchini. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Tunaendelea, sasa na Wizara ya Madini. Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, aulize swali lake.

Na. 219

**Mpanda Kunufaika na Mauzo ya Mchanga**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, Halmashauri ya Mpanda inanufaika vipi na mauzo ya mchanga wa marudio ya madini katika Kata ya Misunkomilo, Mpanda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Judith Kapinga, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI K.n.y. WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya tani 2,498.16 za makinikia ya shaba *(copper concentrates)* zilichenjuliwa kutoka katika Kata ya Misunkomilo ambapo madini ya shaba yenye thamani ya shilingi bilioni 16.01 yalipatikana na Serikali kunufaika kwa kukusanya shilingi bilioni 1.12 kupitia mrabaha na ada ya ukaguzi. Aidha, jumla ya shilingi milioni 48.02 zilikusanywa, kama tozo ya huduma *(service levy)* ambapo, Halmashauri za Mpanda Mjini na Nsimbo zilinufaika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda wamekuwa wakihifadhi mchanga wa madini *(tailings)* kwa muda mrefu. Kitu cha ajabu ni wao wameambiwa watapewa tozo tu ya huduma. Kwa nini wasipewe sehemu ya asilimia za mauzo ya mchanga huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; awali, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda wamewahi kushiriki biashara ya kokoto katika eneo hilo hilo. Vigezo vilivyoiruhusu halmashauri kufanya biashara ya kokoto, kwa nini visitumike kwenye biashara hii ya *tailings*? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI K.n.y. WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge na ninaomba niyajibu kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusuana na Halmashauri ya Mpanda kuwa sehemu ya mauzo na umiliki wa mauzo ya mchanga huu wa marudio na kuhusiana na swali lake la pili pia, kuhusiana na kushiriki katika biashara hii ya mchanga wa marudio, jambo hili linawezekana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba niishauri Halmashauri ya Mpanda kufanya mazungumzo na mmiliki wa mchanga huo wa marudio, ili kuona uwezekano wa wao kuwa sehemu ya mauzo ya mchanga huo wa marudio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Serikali, kupitia Wizara ya Madini, tutafurahi kushiriki katika kusaidia mazungumzo haya yaweze kufanyika, ili kama kuna uwezekano Halmashauri ya Mpanda iweze kunufaika pia, katika masuala hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Judith Kapinga kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Madini kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali; kwa niaba yake, Mheshimiwa Msambatavangu.

Na. 220

**Kudhibiti Maudhui Yasiyo na Maadili katika Mitandao ya Kijamii**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU K.n.y. MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti maudhui yasiyo na maadili katika mitandao ya kijamii kwa maslahi ya afya ya akili na watoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* imeweka mikakati na inaendelea kuchukua hatua za kiudhibiti kuhusiana na maudhui yasiyo na maadili katika anga la mtandao hapa nchini, ikiwemo mitandao ya kijamii. Kufikia Tarehe 31 Machi, 2025 *TCRA* imeweza kubaini na kufungia tovuti, akaunti za mitandao ya kijamii, majukwaa, *blogs* na kadhalika, zipatazo 80,171 zilizokuwa zinachapisha maudhui yaliyo kinyume na maadili na yenye kuhatarisha afya ya akili na watoto. Zoezi hili ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuendesha na kutoa mafunzo ya weledi kwa waandishi wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na wachapishaji wa maudhui mtandaoni. Mafunzo haya yanawajengea uwezo washiriki katika kutambua maudhui ghushi mitandaoni, uandaaji wa makala pamoja na ujenzi wa taswira ya nchi ili kuendelea kulinda utamaduni ulio salama kwa makuzi ya Jamii ya Watoto wa Kitanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU K.n.y. MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ni upi

mkakati sasa wa kudumu wa kuweka vitu, kama *censorship,* ili kuzuia taarifa na maudhui yasiyo na maadili kusambaa katika Jamii ya Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali imejipanga vipi pia, kuzuia tamaduni na zile ngoma ambazo zinachezwa bila nidhamu, ikiwemo kucheza uchi, akinamama au wanaume wakiwa wanacheza wakiwa kwenye sherehe ambazo zinaadhimishwa katika Taifa letu. Ni upi mkakati wa Serikali kuzuia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo mawili?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa maswali mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Msambatavangu, kwa niaba ya Mheshimiwa Ng'wasi Kamani. Kwanza, Serikali imewekeza katika teknolojia, kupitia *TCRA,* Serikali imewekeza sana kwenye teknolojia, ikiwemo matumizi ya akili za bandia, ili kuhakikisha kwamba, inabaini na kuzuia ama kuondosha habari ambazo zimechapishwa na ziko kinyume na maadili ya Mtanzania kabla hazijawafikia walaji wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali kwa sasa ina ushirikiano mkubwa na kampuni kubwa zinazoendesha shughuli hizi duniani, kwa mfano, *Google* ama *Meta,* ambapo wanaendesha *Facebook* na *Twitter*, ili kuhakikisha habari ambazo hazina maadili, ambazo zimechapishwa, *either* zinazuiwa kuchapishwa ama zinaondolewa haraka. Halikadhalika, Serikali inaendelea kuboresha Sera na Sheria zinazotumika kuendesha masuala ya uchapishaji wa habari mtandao na inaendelea kuelimisha wananchi ili waendelee na wao kujilinda na masuala haya na kuhakikisha maadili hayakiukwi kwa kutumia machapisho haya yaliyoko mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, kimsingi Serikali inafanya kila linalowezekana, ili kuhakikisha kwamba, uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kupata habari hautupeleki kwenye ukiukwaji mkubwa wa maadili na hivyo kuweza kulinda vizazi

vyetu. Swali la pili, ilikuwa ni kuhusiana na ngoma zisizofaa. Haya mengine…

**MWENYEKITI:** Mavazi yanayovaliwa kwenye ngoma zisizofaa. Mavazi yanayovaliwa, ambayo siyo rasmi na mazuri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Hili moja kwa moja linakwenda kwenye uvunjifu wa Sheria za nchi na linatakiwa kuhudumiwa kwa namna hiyo. Kwa hivyo, kama kutakuwa na habari au mwonekano ambao haufai, masuala haya yanatakiwa kuripotiwa kwenye mamlaka zinazohusika yachukuliwe Sheria na yashugulikiwe kwa mujibu wa Sheria za Nchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, nimekuona.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani kwa kuwa hili kundi la watoto ndiyo litakaloathirika baadaye kutokana na maonyesho haya ambayo tunashindwa kuyazuia kwenye mitandao ya kijamii?

**MWENYEKITI:** Hajakuelewa vizuri, ninaomba uliweke kwa ufasaha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri na mikakati mizuri ya Serikali, bado kuna tatizo kwa watoto wadogo kutokana na kufuatilia matangazo hayo kwenye vyombo vya televisheni hasa wanapokuwa wenyewe majumbani na pindi wanapokuwa kwenye ma-*group*. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa wazazi ili kudhibiti hali hii, kwa sababu hili kundi ndilo litakaloathirika baadaye? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umeelewa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilijibu wakati ninajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msambatavangu; moja ya mambo ambayo Serikali inafanya, pamoja na kuboresha sera na sheria zinazoendesha masuala haya, pia ni kutoa elimu kwa jamii nzima ili nayo iweze kujilinda, kujikinga na kuhakikisha kuwa vizazi vyetu havifikiwi na habari ambazo zina uvunjifu mkubwa wa kimaadili. Kwa hiyo ni rai yangu kwa wazazi na walezi kuhakikisha kwamba wanawakinga wanaowalea ama watoto wao kuhakikisha kwamba hawafikiwi na habari hizi na kupelekea mmomonyoko wa maadili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mtandao wa *TikTok* ndio mtandao pendwa wa watoto wetu wanafunzi, lakini ndio mtandao unaoongoza kwa maudhui mabaya. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa wanadhibiti huu mtandao ili kunusuru watoto wetu waweze kukua kwa maadili ya Kitanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ukinzano wa moja kwa moja upo kati ya ukuaji mkubwa wa teknolojia na uvunjifu wa maadili nchini. Serikali inachokifanya ni kuhakikisha kwamba wachapishaji wa habari na hii mitandao wanafuata sheria za nchi, ikiwemo ukaguzi wa mara kwa mara ambao unafanywa na *TCRA*, kwa sababu wote wanatakiwa kuwa wamesajiliwa na *TCRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo udhibiti unaendelea kufanyika, na pale ambapo tunaona kuna haja kabisa ya kuingia na kufuata mamlaka nyingine za kisheria ili kuhakikisha ya kwamba maadili hayaendelei kuvunjwa huwa tunafanya hivyo. Kuna ugumu wa kufanya hivi kwa sababu ya mkubwa wa teknolojia duniani, hata hivyo tunaendelea kurekebisha sera na sheria ambazo zinahudumia haya masuala.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 221

**Maandalizi Mashindano ya *AFCON* 2027**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, Serikali inafanya maandalizi gani kuhakikisha nchi yetu inafanya vizuri katika Mashindano ya *AFCON* 2027?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo katika Majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Visiwani Zanzibar, kwa ajili ya kufanikisha mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (*AFCON*, 2027) yanayotarajiwa kufanyika nchini kwa kushirikiana na Nchi za Kenya na Uganda. Aidha, kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* tunasimamia malezi ya timu ya vijana kimkakati ili kuhakikisha tunakuwa na timu bora yenye viwango wa ushindani wa kimataifa. Baadhi ya masuala yaliyofanyika ni pamoja na kuanzisha programu za kuendeleza vipaji kwa kuzishirikisha timu za vijana waliochini ya miaka 17, waliochini ya miaka 23 na kutumia wachezaji wa *diaspora*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mingine ni kuboresha mikakati ya upatikanaji wa vifaa mbalimbali vya michezo, kuandaa benchi la ufundi lililo bora, kuandaa programu za lishe, kuandaa kambi za mazoezi ya muda mrefu, kuandaa michezo ya kirafiki ya kimataifa na kuboresha na kusimamia maslahi ya wachezaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kuhusiana na utaratibu wa kupata vijana kwa ajili ya kucheza kwenye timu ya Taifa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanafanya *scouting* ili waweze kutambua vijana ambao wanafanya vizuri sana sana katika vilabu vidogo, vidogo huko mikoani, ukiangalia hata kwetu pale Ikungi Mashariki kuna timu ya Kikio *Boys* wanafanya vizuri sana pamoja na Matongo *FC* ya Ikungi; kwa hiyo wanafanya utaratibu gani ili na hawa vijana na wao waweze kupata nafasi ya kushiriki kuwepo kwenye timu ya Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu la pili, kuhusiana na ubora wa viwanja vyetu nchini. Tumeona kwenye vyombo vya habari kwamba Serikali wanafanya marekebisho ya viwanja, ikiwemo Kiwanja cha Benjamin Mkapa. Tuliona wanabadilisha viti pale Benjami Mkapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unafahamu kwamba pale kuna shida ya *pitch*. Yaani mvua ikinyesha ile *pitch* pale uwanja wa Taifa, Benjamin Mkapa inajaa maji. Sasa ninataka kufahamu, kwa nini Serikali wasishughulike na jambo la uwanja kwenye *pitch?* Pamoja na mambo mengine wanayoyafanya. Je, wanafanya utaratibu gani ili kuhakikisha kwamba ile *pitch* inakuwa bora kama ambavyo tunategemea, kwa sababu tunategemea uwanja wa Benjamin Mkapa sasa hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Maswali mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Nusrat Hanje. Hili la *scouting* Serikali kupitia Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania imekuwa ikiendelea kufanya *scouting* na kubainisha vijana ambao wana uwezo, wana vipaji vya kutosha kuchezea timu zetu mbalimbali za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hivi ninavyojibu haya maswali hapa, *TFF* tayari wana vijana takribani 150 katika Kituo cha Maendeleo ya Michezo kule Tanga na vijana hawa wamekusanywa kutoka maeneo mbalimbali ya mikoani ili

kuhakikisha kwamba vipaji vyao siyo tu vinalelewa, lakini wanakwenda shule wakitokea pale kwenye Kituo chetu cha Maendeleo ya Mpira wa Miguu Mianjani Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakachofanya kwa vijana wake wa Ikungi, nitawaelekeza moja kwa moja *TFF* ili waende kwa ajili ya kufanya *scouting* kuangalia vipaji anavyosema vipo kule Ikungi na kuhakikisha kwamba kama kuna vijana wanafaa kwa ajili ya kuchezea timu zetu za Taifa na wao wanapata hii fursa ya kuitwa kwenye timu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili, hili la Benjamin Mkapa; tumekuwa tukifanya ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa na maeneo yote ambayo tulikuwa tunafanya ukarabati hayakuwa yakihusisha eneo la *pitch*. Eneo la *pitch* lilikarabatiwa na *CAF* walipokuja kuendesha mechi ya *African Football League* kati ya Simba na Al Ahly mwaka juzi (2023) mwishoni na walitupatia miaka miwili kwa maandishi kwamba tunaweza kuitumia *pitch* ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo tulikuwa tunayafanyia ukarabati yalikuwa yanahusisha viti kama anavyosema; ubao wa matangazo; mfumo wa umeme; ubadilishaji wa taa; mfumo wa hewa na mambo mengine mengi, lakini haikuwa inahusisha *pitch*. Sasa tumepata bahati mbaya wakati wa mechi ya Simba na Al Masry mvua kubwa ikanyesha na uwanja ukajaa maji. Serikali imechukua hatua za dharura kuhakikisha *pitch* ile inatengemaa kwa ajili ya mchezo wa fainali kati ya Simba na Berkane ambao utafanyika tarehe 27 ya mwezi huu wa tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyosema tumeshaajiri Kampuni ya Kituruki na ipo kazini na watatukabidhi ile kazi yetu tarehe 15 ya mwezi huu, siku 12 kabla ya mechi ile. Kwa hiyo tunashughulika na jambo hili, na tutaiondoa *pitch* nzima baada ya Mashindano ya *CHAN* mwishoni mwa mwezi Agosti na kuweka *pitch* mpya wakati huo utakapofaa kwa vile ndivyo ambavyo tulikuwa tumeelekezwa na *CAF* kabla ya kupata hii bahati mbaya. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kumekuwa na udhaifu na ucheleweshwaji mkubwa wa kiutendaji katika ukarabati unaoendelea kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kiasi cha kutishia mchezo wa fainali kati ya Simba pamoja na Berkane, lakini pia kutishia mechi ya ufunguzi wa michuano ya *CHAN* ambayo itaanza mwezi Agosti. Je, Serikali inatoa *commitment* gani kuhakikisha kwamba mchezo huu muhimu wa fainali unachezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini pia ufunguzi wa mashindano haya ya *CHAN* yanafanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu swali lililopita la nyongeza la Mheshimiwa Hanje, *commitment* ya Serikali ni ileile kuhakikisha mechi hii ya fainali kati ya Simba na Berkane ya tarehe 27 ya mwezi huu, ambayo ni mechi ya kihistoria sana inachezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. Hatutakuwa tayari kupokea kitu chochote chini ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema, Serikali imefanya kila inaloweza ikiwemo kuajiri kwa dharura mkandarasi mwenye uzoefu mkubwa katika masuala ya kutengeneza *pitch* ili kuhakikisha uwanja ule unatengemaa. Jana usiku mimi binafsi nilikuwa nina kikao kirefu cha kwenye simu na viongozo wa *CAF* akiwemo Rais Dkt. Motsepe's ili kuhakikisha kwamba wanatusaidia na wao wenyewe wanatuletea *consultants* wa kimataifa, kuhakikisha tunashauriwa vilivyo namna ya kutunza *pitch* ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Shangazi na wapenzi wengine wa mpira wa miguu wakiwemo wapenzi wa Simba, mechi ile itachezwa palepale na hakuna mahali itaenda. Tukio hili la kihistoria litafanyika mbele ya macho yao wakiwa wanalishuhudia. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi nafikiri alikuwa anataka majibu hayo ninafikiri. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Mkundi, nimemwona.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kwa nini Uwanja wa CCM Kirumba usifanyiwe matengenezo ili ukidhi vigezo vya kutumika kwa michezo ya *AFCON*, 2027? Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umemwelewa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna udhibiti wa kwenye idadi ya viwanja ambavyo vinaweza kutumika kwa ajili ya michezo ya *AFCON*. Hata hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Uwanja wa CCM Kirumba ni miongoni mwa viwanja ambavyo viko katika mpango wetu. Tunaanzisha *Sports Infrastructure Management Agency* kwa ajili ya kutunza viwanja hivi. Majadiliano yanaendelea kati ya wamiliki wa Uwanja wa CCM Kirumba na Serikali ili kuhakikisha kwamba wanatukabidhi kwa makubaliano rasmi ambayo yatakuwa hayampi hasara mtu yeyote na kuhakikisha kwamba vile viwanja vinatengenezwa kwa ajili ya kuendelea kutengeneza miundombinu mingi zaidi ya michezo nchini. Ni miongoni mwa viwanja vitano vya awali, ambavyo tuna mpango wa kuvifanyia ukarabati mkubwa na kuviweka katika kiwango cha kimataifa kwa ajili ya kutumika wakati wowote vitakapohitajika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani ili faida zinazotokana na mashindano haya ziweze kufika maeneo mengi kwa kuhakikisha inaweka viwanja vya mazoezi katika miji iliyopo karibu na maeneo ambayo michezo inachezwa kwa ajili ya kuweka kambi kwa timu zinazoshiriki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matwaka ya *CAF* ni kwamba kila mji ambao mashindano ya *AFCON* yatakuwa yanachezwa unatakiwa kuwa na viwanja vitano vya mazoezi. Sasa kwa mahali ambapo Mheshimiwa Priscus Tarimo anatoka, Moshi ni karibu sana na ni moja ya miji ambayo mashindano haya yanachezwa ambayo ni Arusha. Ninaomba niongee na Mheshimiwa Priscus baada ya Kikao hiki cha Bunge ili kuona kama matakwa ya *CAF* yanaweza kuturuhusu kuweka moja ya viwanja vya mazoezi Jijini Moshi badala ya kuweka vyote vitano Arusha.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Hamis Mwinjuma kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, aulize swali lake.

Na. 222

**Redio za Jamii Kutoa Elimu ya Viuatilifu vya Zao la Korosho**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia redio za kijamii kutoa elimu ya matumizi bora ya viuatilifu katika zao la korosho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikoa inayozalisha korosho, vituo kumi na moja vya redio jamii vinatoa huduma kwa wakulima, hususani teknolojia mbalimbali. Mathalani, mwezi Februari hadi Machi, 2024 tangazo la kuhuisha taarifa kwenye kanzidata inayotumika kusajili na kugawa pembejeo za ruzuku za zao la korosho lilitolewa kupitia Redio za Fadhila *FM*, Mercy *FM*, Mamu *FM* na Safari *FM*. Vilevile, mwezi Agosti hadi Septemba,

2024 kupitia redio Newala *FM* na Rufiji *FM* zilitumika kutoa tahadhari na udhibiti wa ugonjwa wa *blight* kwa wakulima wa Korosho katika Mikoa ya Lindi na Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matumizi ya redio za jamii, Wizara ya Kilimo imeanzisha Kituo cha Huduma kwa Wateja kinachotoa fursa kwa wakulima na wadau wengine wa kilimo kupata elimu na ufafanuzi kuhusu maendeleo ya kilimo ikiwemo zao la korosho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi. Niipongeze Serikali pamoja na zile redio 11 za jamii ambazo zimekuwa zikifanya kazi mbalimbali ikiwemo matangazo kuhusu kuhuisha kwa kanzidata ya wakulima ili kujua kila mkulima na mahitaji yake kwenye shamba lake, lakini pia kutoa tahadhari ya ugonjwa kwa mfano ugonjwa wa *blight* na magonjwa mengineyo ambayo yanashambulia korosho. Sasa nilikuwa nina maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; ni pamoja na kwamba tunatoa hayo matangazo na namna ya kudhibiti hayo magonjwa ya mikorosho, lakini ninataka kufahamu, kwa sababu wapuliziaji wengi ambao sisi tunawaita *operator* kule kwetu huwa wanakwenda shambani wakiwa hawana kinga yoyote ya kuwadhibiti kutokana na athari ambazo wanaweza kuzipata zitokanazo na zile sumu ambazo wanapulizia kwenye nikorosho. Je, kwa nini hizi redio sasa zisitumike pia kutoa elimu kwa wale ambao wanapulizia namna ya kujikinga na madhara yanayoweza kutokea kutokana na sumu zile wanazopuliza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; wewe ni shahidi pia, sisi wakulima wa korosho ukienda shamba utaokota bibo unakula lakini pia unaweza kutengeneza juisi, ukapika uji ukanywa, lakini ukitumia kilevi kinaitwa *uraka*, unakamua ile juisi unaichachusha kesho unakunywa kama pombe. Mabibo yale yanaathiriwa kwa kiasi kikubwa sana na zile sumu za maji ambazo zinapulizwa kwenye mikorosho. Je, Serikali imejipangaje kufanya utafiti wa kubaini ni kwa kiasi gani athari zinaweza kuwapata watumiaji wa

mabibo au matunda haya kutokana na zile dawa ambazo zinapulizwa kwenye mabibo ili kuweza kudhibiti athari zisiwe kubwa huko mbele?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini kwa kazi nzuri anazozifanya kwa wananchi wake hususani kufuatilia masuala ya udhibiti wa afya kwa wakulima wake. Nimwondoe shaka tu kwamba, moja, tutaendelea kutumia hizi redio za jamii katika kuendelea kutoa elimu dhidi ya kujikinga na magonjwa ama matumizi mabaya ya viuatilifu ambayo yametokana na zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeongeza fedha katika Kitengo chetu cha Mawasiliano na Habari kwa Umma ili kuweza kuzifikia hizo redio na zifanye mara kwa mara. Vilevile, tutawafikia Maafisa Ugani pamoja na Maafisa Kilimo katika ngazi za halmashauri ili waendelee kutoa elimu kwa wakulima wetu wa zao la korosho waweze kujikinga na hizi athari ambazo umezianisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, tumekwishaelekeza watu wa *TARI* pamoja na *TPHPA* kuendelea kufanya tafiti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata njia bora ambayo itasaidia kuondoa adha katika matumizi ya mabibo ambayo yanaweza kuwa yameathiriwa na matumizi ya dawa, kwa maana ya Viutatilifu vile ambavyo vimepulizwa.

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri Wizara ya Kilimo Mheshimiwa David Ernest Silinde, ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. Kwa niaba, Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

Na. 223

**Kukabiliana na Wanyamapori Waharibifu Rufiji**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani kuwasadia wananchi wa Kata za Ngarambe na Mwaseni - Rufiji kukabiliana na wanyama waharibifu hasa Tembo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

*(Hapa kipaza sauti kilikuwa na hitilafu)*

**MWENYEKITI:** Imekuwaje? Jaribu upande wa pili. Hiyo imewaka, endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, kuanzia mwezi Julai, 2024 hadi mwezi Machi, 2025 Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo; kufanya doria za kudhibiti matukio 293 ya wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, kuendelea kuimarisha kituo cha kudumu cha udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu kilichopo katika Kata ya Ngarambe. Pia kuvuna mamba 15 na viboko wanne katika Mto Rufiji na maeneo yanayopakana na mto huo; kununua ndege nyuki moja inayotumiwa na Askari wa Pori la Akiba Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ni kutumia Askari wa mkataba 20 waliohitimu Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi Mwanza; kutoa mizinga ya nyuki 100 katika Kijiji cha Ngarambe Kitongoji cha Ngarambe Magharibi ambayo inatumika kuzuia tembo kuingia kwenye mashamba ya wananchi; na kutoa elimu ya uhifadhi na mbinu za namna ya kuepuka madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa wananchi 1,165 wa Vijiji vya Ngarambe, Tapika na Namakono katika Kata

ya Ngarambe pamoja na Vijiji vya Mibuyu saba na Mtanza vilivyopo katika Kata ya Mwaseni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na tunaipongeza kwa juhudi ambazo imefanya kutatua tatizo hili katika Wilaya ya Rufiji Mheshimiwa Subira ana maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; hii Kata ya Ngarambe na Mwaseni, shida hii imekuwa kubwa sana; wameweza kuweka nyuki kwa ajili ya kuzuia hawa tembo. Sasa kwa vile hili suala la kulipa fidia limekuwa ni la kusumbua kidogo na inagharimu sana Serikali. Je, hawaoni sasa kuna haja ya kuwawezesha wananchi wa kata hizi mbili ili waweze kuwa na shughuli mbadala kama ya ufugaji wa nyuki? Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; shida kama hii ipo katika Kata za Wilaya ya Bagamoyo ambayo ni Kata ya Mkange pamoja na Kiwangwa; je, Serikali ina mpango gani pia kuwafikia wananchi wa kata hizi za Wilaya ya Bagamoyo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema kwenye jibu la msingi tumejitahidi kuendana na kutoa mikakati mbalimbali ambayo tumekwenda nayo kwa ajili ya kunusuru wananchi wa eneo hili na mojawapo ni kuanza kutumia mizinga ya nyuki kwa ajili ya kuzuia uharibifu unaoletwa na wanyama hawa (tembo). Ni imani yetu kwamba mizinga hii itatumika vilevile kama sehemu ya shughuli ya kiuchumi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la pili alilolizungumzia kuhusu changamoto kule Bagamoyo, ni kweli tuna changamoto

katika eneo la Bagamoyo tunapopakana na Hifadhi ya Saadan, kuna makundi makubwa yanayoenda kwenye maeneo ya kilimo cha miwa na tumeanza kuchukua hatua kwa kushirikiana na wenye mashamba yale kuona jinsi ambavyo tunaweza kuona jinsi ambavyo tunaweza kuanza kulinda maeneo yale kwa kutumia uzio wa umeme. Tupo katika hatua ya juu kufikia kupata suluhisho hilo lakini vilevile, tumepeleka mabomu baridi kule, na hivi karibuni tayari tuna mpango wa kupeleka ndege nyuki ili kuwanusuru wananchi. Kwa hiyo, ninaamini ndani ya kipindi kifupi suluhu ya changamoto hii itapatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amsabi Mrimi.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti wanyamapori waharibifu wanaotoka ndani ya hifadhi ya Taifa ya Serengeti pamoja na mapori ya akiba ya Ikorongo na Gurumeti na kuvamia vijiji vilivyopo Kata za Nata, Isenye, Nagusi, Mesocho, Sedeko na Mbalibali na kusababisha uharibifu mkubwa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikakati ya kupambana na changamoto ya wanyama wakali na waharibifu ukanda ule wa Serengeti, Serikali imejiimarisha kwa kuongeza doria za udhibiti kwenye maeneo haya, lakini vilevile kuimaraisha vituo vyetu vya kudhibiti wanyamapori. Kama Mheshimiwa Mbunge anavyofahamu hivi karibuni tumeimarisha kituo chetu katika eneo lile lakini vilevile, kwa kushirikiana na wenzetu wa *Frankfurt Zoological Society* tumepeleka gari kwenye eneo hili. Ninaamini kwamba jitihada hizi sasa zitapunguza changamoto hii ambayo wananchi wa ukanda ule wamekuwa wakipambana nayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya nimekuona.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuikumbusha Wizara kuhusu kulipa kifuta machozi kwa familia tatu ya Lundo, Kingerikiti pamoja na Lipingu ambao wapendwa wao (ndugu zetu) walikamatwa na mamba katika Ziwa Nyasa na Mto Mbahwa. Je, kutokana na matukio hayo sasa kuwa ni mengi na mamba wanaonekana wengi wakizagaa zagaa kwenye Ziwa Nyasa ambalo tunatangaza utalii kwa kila hali, inakuwa tishio sasa kwa watalii. Lini Serikali itafanya maamuzi madhubuti ya kuwavuna mamba hao ikizingatiwa kwamba hata ngozi zao vilevile ni biashara kubwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mbunge aliwasiliana na mimi juu ya matukio haya matatu yaliyotokea ya mashambulizi ya mamba na tayari tumewaelekeza wataalamu wetu wa *TAWA* kupeleka timu kwenye eneo lile kwenda kufanya tathmini ya uhalali wa malipo yale, lakini vilevile kuweka mikakati ya kuwavuna mamba katika eneo lile. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, jambo hili tunalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Kungu, atafuata Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu ya tembo kuvamia makazi ya watu ni pamoja na wafugaji kwenda kufuga kwenye hifadhi za wanyamapori. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwahamisha ama kuwaondoa wafugali wanaofanya shughuli za ufugaji kwenye hifadhi ili kuondoa hii adha kubwa ya tembo kuvamia makazi ya watu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba watu walioingiza mifugo kwenye maeneo ya hifadhi wanachukuliwa hatua. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa imetenga maeneo kwa ajili ya wafugaji hao kuelekeza mifugo yao na tayari Serikali inafanya jitihada za kuhakikisha makundi haya ya ng'ombe yaliyopo katika hifadhi zetu yanatoka ili wafugaji aelekezwe kwenye maeneo yale. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kuwa na subira wakati kazi hii inaendelea kufanyika kwenye maeneo yale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tembo wengi sana katika Tarafa ya Mahenge katika Wilaya ya Kilolo wamekuwa wakifanya uharibifu mkubwa wa mazao na mali za watu na kuua watu, lakini kifuta machozi na fidia hailipwi kabisa. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi ambao hawapati fidia hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si kweli kwamba kifuta jasho na kifuta machozi hakilipwi kabisa. Serikali inafanya kazi kubwa ya kufanya tathmini ya pale inapopata madai haya, kwenda kuyafanyia uchambuzi ili wananchi waweze kulipwa na katika kufanya hilo mwezi wa pili tuliwaita Maafisa Wanyamapori wote wa wilaya zote nchini kuja kuwapa semina na maelekezo ya jinsi ya kutumia mfumo wa kidigiti katika kukusanya takwimu za matukio katika maeneo yao na kuweza kuyaleta kwa haraka. Pale tunapoona kwamba kuna ucheleweshaji wa malipo ni kwa sababu wataalam wetu katika ngazi ya halmashauri wamekuwa wakichelewesha kuleta madai haya Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya kazi kubwa ya kulipa madai haya tunapoyapata kwa wakati. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge kama anayo madai ya wananchi wake baada ya kikao hiki cha leo tuwasiliane aweze kunipatia ili tuweze kuyafanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata, atamalizia Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Leo hii tarehe tano mwezi Mei ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu tunamzika ndugu yetu Hassan Napicha ambaye ameuawa na tembo sehemu ya Chinanyila, kwenye Kijiji cha Chinyanyila. Changamoto kubwa iliyopo ndani ya Jimbo langu ni kuongezeka zaidi kwa wanyama hawa (tembo) na wilaya nzima haina ndege nyuki ya kuwafukuza tembo hawa. Je, Serikali ipo tayari kutoa kauli leo, ni lini tutapatiwa ndege nyuki ambayo ikawa stesheni pale wilayani ili iweze kukabiliana na wanyama hawa waharibifu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mhata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa naiba ya Serikali tunaomba kutoa pole kwa ndugu zetu ambao wamepoteza mpendwa wao kutokana na kadhia hii ya tembo katika siku hii ya leo kwenye eneo lile. Pili, Serikali imepeleka ndege nyuki tano katika Ukanda wa Kusini pamoja na maeneo ya Nanyumbu na maeneo mengine. Ninaomba wataalam wetu wafanye haraka kuhakikisha kwamba kunakuwa na *operation* maalum katika eneo lile la Nanyumbu ili kukabiliana na wanyama hawa (tembo).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uharibifu wa wanyama katika maeneo ya Vijiji vya Unyali, Kihumbu, Mariwanda, Sarakwa, Mugeta, Kyandege na Tingirima

ni mkubwa sana na kwa kuwa Kampuni ya *VIP* imeonesha nia ya kuweka *fence* ya waya kwa kulinda tembo. Ni nini kinachosababisha Serikali isii-support Kampuni ya *VIP* ili kuweka fensi kwenye maeneo ya uharibifu? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka unaposikia kwamba kampuni fulani inataka kuweka *fence* ni kwamba tayari imekwishakuwa na mawasiliano na kupata ushirikiano kutoka Serikalini kwa ajili ya kufanya jambo hilo, vinginevyo wasingekuwa hata na ndoto ya kufanya jambo hilo. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inashirikiana na taasisi hizi lakini yapo mambo ya kimsingi lazima yafanyike kuhakikisha kwamba hilo la kuweka *fence* linatokea. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati taratibu hizi za kikanuni zinafanyiwa kazi ili jambo hilo liweze kutokea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungahela nilikuona.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimekuwa nikifuatilia malipo ya fidia ya wananchi wangu katika jimbo langu sasa hivi ni takribani mwaka na jambo hili Mheshimiwa Naibu Waziri analifahamu kwa sababu nimekuwa nikienda kwake mara kwa mara kufuatilia jambo hili. Tumeambiwa turekebishe pale, tukarekebisha, rekebisha hapa tumerekebisha, lakini mpaka sasa hivi hawajalipwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje kuhusiana na jambo hili, ni lini atawasaidia watu hawa kwa sababu miongoni mwao wanahitaji matibabu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mchungahela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru kwa kukiri kwamba taarifa ambazo tumekuwa tukizipokea kutoka kwenye wilaya yake ni taarifa ambazo si sahihi, ni taarifa ambazo zimekuwa na mapungufu makubwa. Wizara kwa kushirikiana na wataalamu wale, tumekuwa tukifanya mawasiliano ya karibu kuhakikisha kwamba taarifa zile zinakuwa na viambatisho vyote vinavyostahili na vitakavyotuwezesha kufanya malipo. Tumepata taarifa zile tupo katika hatua ya kukamilisha jambo hili. Ninaomba kama ambavyo amekuwa na ushirikiano wa karibu kwenye jambo hili, tuendelee kushirikiana ili tukamilishe kuwalipa wananchi wale.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa majibu hayo.

Wizara yetu ya mwisho ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mheshimiwa Mbunge wa Chato, aulize swali lake.

Na. 224

**Kukamilisha Ujenzi wa Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kasagara – Chato**

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI** aliuliza:-

Je, lini Ujenzi wa Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam cha masuala ya samaki eneo la Kasagara - Chato ulioanza 2021 utakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam eneo la Kasagara – Chato ulipaswa kuanza mwaka 2021 na kukamilika mwezi Mei, 2023. Ujenzi huo haujakamilika kutokana na changamoto za mkandarasi kushindwa kuendelea na ujenzi kwa muda mrefu hivyo kupelekea

Serikali kuanza mchakato wa kusitisha mkataba wa utekelezaji wake. Taratibu za kufunga mkataba huo kisheria zinaendelea na mara zitakapokamilika Serikali itaanza mchakato wa kumtafuta mkandarasi mwingine ili kuendelea na ujenzi. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri ninakupongeza sana kwa hatua zako za kufuatilia ujenzi wa Chuo Kikuu cha Chato ahsante sana Mheshimiwa, Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitoe shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha shilingi milioni 900 kuanza ujenzi wa Chuo Kikuu hiki cha Kasagara Mjini Chato. Mheshimiwa Naibu Waziri tufikishie shukrani nyingi sana za Wananchi wa Chato kwa ujenzi wa chuo kikuu kwa Mheshimiwa Rais wetu. Nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; ni kweli ujenzi ungeanza mwaka 2021, lakini kwa sababu za kimkataba, mkandarasi ameshindwa kuendelea na ujenzi sasa swali langu la kwanza, ni lini Serikali itapata mkandarasi huyo mpya na kuanza ujenzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ninapenda nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa sababu yupo tayari kufuatana na mimi, ni lini tutaongozana wote kwenda kuwaambia Wananchi wa Chato kuhusu kukamilisha ujenzi wa chuo kikuu na hasa ndani ya kipindi hiki kabla ya mwisho wa Bunge hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Mbunge wa Chato, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba, ujenzi huu ulianza toka mwaka 2021 na umesimama au ulisimama kutokana na changamoto hizo za kimkataba. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tarehe 27 Januari, 2025 mkandarasi pamoja na Chuo kikuu cha Dar es Salaam pamoja na *consultant* tuliwaita Wizarani kwa lengo la kujua maendeleo na changamoto za mradi huu. Baada ya kikao kile ndipo ilipobainika kwamba warudi sasa waende wakakae wafanye *settlement* ya mkataba ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo yalikuwa ni lazima yafanyike ambayo la kwanza, ikafanyike *conditional survey;* pili, ifanyike *evaluation* ya kazi iliyofanyika mpaka pale tulipofikia pamoja na *remeasurement*; tatu, iandaliwe *final account;* lakini la mwisho, kabisa yalipwe yale malipo ya mwisho kulingana na kazi pale ilipofikia na baada ya hapo sasa ndipo tunaweza tukafanya *engagement* ya kutangaza ile kazi kwa ajili ya kumpata mkandarasi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo katika hatua za mwisho michakato hii yote niliyoitaja tayari imekamilika na ni matarajio yetu kwamba itakapofika mwezi Juni utaratibu wa kutangaza kazi hii na kumpata mkandarasi mwingine kwa ajili kuanza kazi hii itakapofika mwaka ujao wa fedha tuwe tumeanza rasmi. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Chato jambo hili Mheshimiwa Rais lakini Serikali hii ya Awamu ya Sita inasimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hiki cha chuo kikuu ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tumeshajenga tayari kule Zanzabar eneo la Buyu, lakini tumejenga Kunduchi kituo kama hiki sasa hivi vilikuwa vinahudumia maeneo yale ya Bahari ya Hindi. Kwa upande wa maji baridi tulikuwa hatuna kituo chochote, kwa hiyo, kituo hiki ni muhimu na Serikali inaona umuhimu wa mradi huu kwa hiyo utaendelea kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la pili, kwamba ni lini? Ninaomba Mheshimiwa Mbunge aridhie kwa sababu wiki ijayo tuna bajeti ya Wizara ya Elimu mara baada tu bajeti yetu

kupitishwa hapa tutapanga siku katika wikiendi zitakazofuata tuweze kwenda kule Chato kwenda kuwaambia wananchi nini mkakati wa Serikali juu ya jambo hili. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, nimekuona.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilayani Kilwa ili elimu ya ufundi stadi iweze kutolewa kwa vijana wetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Ndulane, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwondoe hofu Mheshimiwa Ndulane na Waheshimiwa Wabunge wote ambao tunajenga vyuo 64 vya wilaya vile vya *VETA* na chuo kimoja cha mkoa katika Mkoa wa Songwe. Maendeleo ya miradi hii yote ni mizuri tayari tumeshapata fedha kwa ajili ya umaliziaji. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge *target* yetu au malengo yetu ifikapo mwezi Agosti mwaka huu vyuo hivi vyote viwe vimekamilika katika maeneo yote yale 64 na kile kimoja cha mkoa ili mwezi wa kumi zile *course* fupi ziweze kutolewa. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, halafu atamalizia Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia nafasi hii kutoa pole kwa wananchi wangu ambao wamekumbwa na mafuriko, jana nilikuwa Bungeni. Sasa kwa kuwa Serikali ina mpango mkakati mkubwa wa maendeleo ya kilimo katika Bonde la Kilombero hasa katika kilimo cha mpunga na miwa ya sukari na tuna chuo chetu cha *Kilombero Agriculture Training and Research Institute (KATRIN)* kina ekari karibu 400 na Serikali imepeleka pesa nyingi sana pale kwa kujenga mabweni na baadhi ya majengo kwa ajili ya *training*

hiyo. Je, Wizara ya Elimu ina mpango gani wa kuhakikisha *KATRIN* sasa inakuwa tawi la Chuo Kikuu cha Kilimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Asenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Asenga kwa kufuatilia jambo hili. Ninakumbuka alishawahi kuja Wizarani kwa ajili ya kufuatilia jambo hili. Kwa hiyo, nikupongeze na kuahidi tu bado Serikali kupitia Wizara ya Elimu, tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya ya kuanzisha matawi mbalimbali ya vyuo vikuu, ni masuala ambayo yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Asenga pamoja na Wabunge wote, Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya Awamu ya Sita tayari hivi sasa tunavyozungumza tunajenga Kampasi ya Chuo Kikuu hiki cha Kilimo kule Mpimbwe kwa Mheshimiwa Pinda. Kazi inaendelea kuhakikisha tawi lile linaimarika na limeshaanza kutoa huduma na kule Tunduru nako vilevile tunafanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Butiama tuna chuo kingine tunaanzisha ambacho kitakuwa cha kilimo, lakini ukienda Lindi kupitia chuo chetu cha Dar es Salaam tuna tawi ambalo tunaanzisha pale. Ninaomba nichukue tu ushauri huu wa Mheshimiwa Asenga ili tuhakikishe kwamba tunaingiza kwenye tathmini yetu ya Serikali tukishirikiana na wenzetu wa Wizara ya Kilimo ili kuona namna bora ya kufanya na eneo hili alilolitaja kama linaweza likawa ni kituo au *branch* ya Chuo chetu cha Kilimo cha Sokoine. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Cherehani, lakini pia nilimwona Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ushetu ni kati ya jimbo ambalo liliahidiwa kujengewa shule ya ufundi mwaka juzi lakini haikutekelezwa, mwaka jana pia nikaahidiwa, lakini haikutekelezwa. Sasa ninataka nijue *commitment* ya Serikali. Je, mwaka huu Serikali itaenda kunijengea shule yangu ya ufundi katika Jimbo la Ushetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Ushetu. Mheshimiwa Mbunge tayari alishakuja Wizarani chungu nzima, tumekuwa tukijadili hapa Bungeni mara kadhaa juu ya ujenzi wa shule yake ya ufundi katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe hofu, katika mgao uliopita wa awamu ya kwanza, zile shilingi milioni 528 bahati mbaya Jimbo la Ushetu halikuwa *allocated,* lakini tuna mgao wa awamu ya pili kwa sababu ujenzi ule wa shule zote za ufundi zaidi ya shule 103 unajengwa kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu katika awamu hii ya pili ambayo tunatarajia kati ya mwezi huu au mwezi Juni, awamu ya pili ya zile fedha shilingi milioni 528 zitakuwa zimetoka na Jimbo la Ushetu litakuwemo kwa maana ya kuanza ujenzi wa shule hiyo ya ufundi katika jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kuna hivi vyuo vishiriki vinajengwa vingi sasa kila mahali, *branches* nyingi za vyuo vikuu. Je, Serikali sasa mko tayari kutoa jedwali litakaloonesha hivi vyuo vyote vipya vinavyojengwa vimefikia asilimia ngapi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, majibu kama unajua hiyo asilimia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nikijibu swali la Mheshimiwa

Dkt. Thea Ntara, kuhusiana na maendeleo ya kampasi zetu za vyuo vikuu katika mikoa zaidi ya 14 ya Tanzania Bara pamoja na Tanzania Zanzibar na yeye lengo lake ni kutaka kujua tu *project report* kwa maana ya kutengeneza jedwali la asilimia mahali ilipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Mheshimiwa Dkt. Thea aridhie jedwali hili lipo na kama atalihitaji basi tunaweza tukawasiliana ili tuweze kuwasilisha kwa sababu kila mwezi taarifa hizi zimekuwa zinakuja Wizarani, lakini na sisi tumekuwa tunaziwasilisha kule Benki ya Dunia kwa maana ya kupata mrejesho na kujua ni namna gani fedha zitaendelea kutolewa na Benki ya Dunia. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, ninakushukuru sana kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali ndiyo umefikia mwisho na sasa ni wakati wa matangazo. Nitaanza na tangazo la wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Tunao wageni ambao wamekaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, wageni wa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega (Mb) ambaye pia ni Waziri wa Ujenzi, hao ni viongozi na Watendaji Wakuu kutoka hiyo Wizara ya Ujenzi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Balozi Mhandisi Aisha Amor, Katibu Mkuu; Dkt. Charles Msondo, Naibu Katibu Mkuu; Mhandisi Amin Mcharo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Barabara wa Tanzania *(TANROADS);* Ndugu Musa Nati, Mwenyekiti wa Bodi Mfuko wa Barabara *(RFB);* Mhandisi Deogratius Nyanda, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Huduma za Ufundi na Umeme (TEMESA); Wakili Menye Manga, Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili ya Wahandisi *(ERB);* Mhandisi Joseph Nyamhanga, Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi *(CRB)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Mhandisi Mohamed Besta, Mtendaji Mkuu Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS);* Ndugu Lazaro Kilahala,

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma za Ufundi na Umeme *(TEMESA)*; Ndugu Daud Kondoro, Mtendaji Mkuu Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA);* Mhandisi Rashid Kalimbaga, Mtendaji Mkuu Mfuko wa Barabara *(RFB),* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wapya wengine ni familia ya Mheshimiwa Ulega, hao ni Ndugu Mariam Abdallah Ibrahim, mke wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ulega, hayo makofi kwa ndugu yetu Mariam Abdallah Ibrahim, ni makofi ya upendo, ndugu yetu tunaye hapa salama na tunakushukuru sana kwa uvumilivu wako muda wote anapokuwa yupo kazini na Mwenyezi Mungu aendelee kukupa subira ili aendelee kufanya kazi za Taifa. Pia, ndugu yetu huyu ni mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji UWT Taifa. *(Makofi)*

Tunaye pia Alhaj Hamisi Ulega, ni baba mzazi wa Mheshimiwa. Ahsanteni sana kwa makofi hayo ya upendo. Mwenyezi Mungu akujalie afya njema na umri wenye furaha ili uweze kuona matunda ya kizaa chema. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Mohammed Abdallah, mtoto wa Mheshimiwa na mtoto mwingine anaitwa Tulia Abdallah, karibu sana Tulia mdogo. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Ulega kwa kumpa jina la Mheshimiwa Spika wetu. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Asha Abdallah ambaye ni shemeji wa Mheshimiwa, karibuni sana familia ya ndugu yetu huyu ambaye mna mtunza vizuri na anaweza kufanya kazi zake vizuri, tunaomba mwendelee kuwa na subira naye. *(Makofi)*

Sasa tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni 10 wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii, ni viongozi wa UVCCM kutoka Mkoa wa Njombe, karibuni sana ndugu zetu viongozi wa UVCCM kutoka Njombe. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu Philipo Emmo, mpiga

kura wake kutoka Babati Vijijini. Karibu sana mpiga kura wa ndugu yetu Daniel Sillo. *(Makofi)*

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Viongozi wa Taifa letu Kesho Yetu *(TK)* kutoka Mkoa wa Katavi. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Mizengo Pinda, kutoka huko Katavi. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Viongozi wa Taifa letu Kesho *(TK)*, kutoka Wilaya ya Sumbawanga, Mkoani Rukwa, karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Deus Clement. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili ambao ni wangu mwenyewe, ni Wajumbe wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM kutoka Liwale Mkoa wa Lindi. Tunaye Ndugu Hidaya Mbinga ni Katibu Elimu Malezi Liwale, lakini pia Ndugu Brigita ni mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji. Wao walikuja kwenye semina ya TK, karibuni sana, lakini pia nao ni wapiga kura wangu. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Ndugu Daniel Musa kutoka Kampuni ya *Soya One Limited* ya Tarime Mjini Mkoani Mara, karibu sana ndugu yetu. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, wapiga kura wake kutoka Nanyamba Mkoa wa Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, wapiga kura wake kutoka Mbogwe Mkoani Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 20 wa Mheshimiwa Maganga kutoa Taasisi ya Taifa letu Kesho Yetu kutoka Mkoa wa Geita, karibuni sana wageni wetu hao wa TK. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke, ni mkwe na rafiki zake kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Oran Njeza (Mb), lakini pia hawa ni walimu, viongozi wa *Girl Guide* kutoka Mkoa wa Mbeya. Karibuni sana *Girl Guide* wetu kutoka Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine ambao wametembelea Bunge siku ya leo. Ni wageni sita kutoka Manispaa ya Bukoba Mkoani Kagera. Karibuni sana wageni wetu kutoka Manispaa ya Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Tunao wanachama 100 wa Shirika la *International Peace Information (*Umoja wa Amani Kwanza) kutoka mikoa mbalimbali nchini wakiongozwa na Rais wa Umoja huo Profesa Wilson Munguza. Karibu sana wanaushirika wetu kutoka huko Umoja na Amani Kwanza. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 79 na walimu kumi wa shule ya sekondari ya Dr. Salmin Amour kutoka Mkoani Singida. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko Mkoa wa Singa. *(Makofi)*

Tunao vijana 14 wa kikundi cha mafundi wa vyombo vya moto wa Mkoa wa Dodoma, wanaounga mkono juhudi za Serikali kupeleka vijana Chuo cha Ufundi, VETA. Karibuni sana vijana wetu wa kikundi hiki cha mafundi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo yetu ya leo. Katibu, tuendelee.

**NDG. MKUTA MASOLI - KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Abdallah Ulega ili aje kuwasilisha hoja za

Serikali kwa Wizara yake ya Ujenzi, karibu sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima kubwa na taadhima mbele yako, niweze kuwasilisha Bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi, Bajeti ya Kazi na Utu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka wa fedha 2024/2025, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu liridhie kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii adhimu na kwa unyenyekevu mkubwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ujenzi tangu tarehe 8 Disemba, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia kwako nimuahidi Mheshimiwa Rais kuwa kwa kushirikiana na watendaji wenzangu katika Wizara nitatekeleza majukumu haya niliyopewa, kusimamia kwa uaminifu na kwa moyo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na shukrani hizo kwa Mheshimiwa Rais, kipekee nitumie fursa hii kumpongeza kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya ya kuliongoza Taifa letu. Sote ni mashuhuda wa namna alivyofanya mapinduzi makubwa katika sekta zote nchini, chini ya uongozi wake tumeshuhudia miradi mikubwa katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta ya ujenzi inayoendelea kutekelezwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa miradi hii kuna chochoea maendeleo ya sekta nyingine za kiuchumi na kijamii na hivyo kukuza uchumi wa mtu mmojammoja na Taifa kwa ujumla, hakika Watanzania tunajivunia na tunatembea kifua mbele chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kumsaidia na kumshauri vyema Mheshimiwa Rais katikia uongozi wa nchi yetu. Pia, viongozi hawa wamekuwa wakitoa miongozo na maelekezo mbalimbali ambayo yamesaidia sana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa namna wanaovyoongoza kwa weledi Bunge hili la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo litafikia tamati katika mkutano huu. Aidha, nitumie nafasi kutoa shukrani kwa ofisi yako Katibu wa Bunge na watendaji wa ofisi kwa ushirikiano ambao wametupatia wakati wote katika utekelezaji wa majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninaomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya uongozi wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Kamati hii imekuwa bega kwa bega na Wizara katika kutekeleza majukumu yake kupitia maelekezo, maoni na ushauri katika masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, Kamati hii ilifanya uchambuzi wa kina wa mpango na bajeti hii ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kutoa ushauri ambao umezingatiwa katika bajeti hii ninayoisoma mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii vile vile kutoa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Bunge, Chama Cha Mapinduzi, wananchi wa Jimbo la Kigamboni, marafiki na familia kufuatia kifo cha mpendwa wetu Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, apumzike kwa amani Dkt. Faustine Ndugulile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 16 Novemba, 2024 yalitokea maafa makubwa kutokana na kuporomoka kwa jengo la ghorofa nne katika eneo la Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Ajali hiyo ilisababisha vifo, majeruhi pamoja na upotevu wa mali. Nitumie nafasi hii kutoa pole kwa wote walioathirika kwa namna moja au nyingine na maafa haya na ninawaombea marehemu wote wapumzike kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Wizara ya Ujenzi tuliguswa na utu uliooneshwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kwenda yeye mwenyewe kuona kilichotokea na alifika Kariakoo moja kwa moja akitokea Uwanja wa Ndege baada ya kurejea nchini kutoka Brazil alikohudhuria Mkutano wa Mataifa Tajiri Duniani *(G - 20)*. Ule ulikuwa ni upendo na uongozi wa aina yake kwa Watanzania. Shukrani na pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kutokea kwa ajali ile, Wizara yangu, ikiwa ni mdau na msimamizi wa shughuli za majenzi nchini, inaendelea na taratibu za kutunga Sheria ya Majengo kwa ajili ya kusimamia sekta ndogo ya majengo nchini. Sheria hii itakapoanza kutumika itakuwa ni muarobaini wa changamoto zilizopo hususan katika masuala ya uratibu, usimamizi na udhibiti wa sekta hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu imara kama barabara na madaraja ni mojawapo ya nguzo muhimu za maendeleo ya Taifa lolote duniani. Ninaomba kununukuu mojawapo ya taarifa za Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB)* inayoeleza ifuatavyo; "Barabara nzuri na madaraja hayafanyi kazi ya kuunganisha maeneo peke yake bali pia huunganisha watu

na fursa, watoto na shule, wakulima na masoko na kwa ujumla huchochea maendeleo ya nchi.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 ninayowasilisha Bungeni leo, imeandaliwa kwa kuzingatia misingi na maono yafuatayo ya Taifa na Serikali yetu: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Mpango Mkakati wa Wizara; Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Bajeti ya 2024/2025; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi ilitengewa shilingi 81,407,438,000 ikiwa ni bajeti ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 76,588,233,000 ilikuwa ni bajeti ya mishahara na shilingi 4,819,205,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2025 jumla ya shilingi 63,506,309,562 zilipokelewa. Kati ya fedha hizo, shilingi 61,152,975,329.92 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi na shilingi 2,353,334,232.32 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya miradi ya maendeleo. Bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Wizara ya Ujenzi ni shilingi 1,687,888,714,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,141,803,989,000 ni fedha za ndani na shilingi 546,084,725,000 ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani, shilingi 599,756,467,800 ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na shilingi 542,047,521,200 ni fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2025 fedha zilizopokelewa ni shilingi 1,535,092,021,470.55. Kati ya fedha hizi, shilingi 944,881,583,335.76 ni fedha za ndani na shilingi 590,210,438,134.79 ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani zilizopokelewa, shilingi 482,085,328,011.98 ni kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 462,796,255,323.78 ni za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafanikio yaliyopatikana; baada ya kuwapa taarifa ya kiasi ambacho Bunge lako Tukufu liliidhinisha kwetu, ni vema nikasema hapa ni masuala yapi makubwa na muhimu tuliweza kuyatekeleza kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa na maono na maelekezo ya Jemedari wetu, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, baada ya kupata kibali cha mhimili huu muhimu wa dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara na madaraja; Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS* inasimamia mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 37,435.04. Kati ya hizo, kilometa 12,527.44 ni barabara kuu na kilometa 24,907 ni barabara za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha2024/2025, miradi ya barabara kuu iliyopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 385 kwa kiwango cha lami, ukarabati wa kilometa 35 kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja 17, ukarabati wa daraja moja, kufanya maandalizi ya ujenzi wa madaraja tisa na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa madaraja mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2025, utekelezaji wa malengo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 109.49 umekamilika na ujenzi wa kilomita 275.51 unaendelea; Ujenzi wa madaraja matano unaendelea na ujenzi wa madaraja matano upo katika hatua za maandalizi; Jumla ya kilometa 98.89 za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa 192.89 zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Aidha, ujenzi na ukarabati wa madaraja madogo 12 kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na 13 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi saba ya barabara iliyokuwa itekelezwe kwa utaratibu wa *EPC+F* sasa inatekelezwa kwa utaratibu wa ‘sanifu na jenga’ *(Design and Build)*. Hadi sasa, maboresho ya kimkataba *(addendum)* ya miradi sita

yameshasainiwa. Aidha, Mradi mmoja wa Igawa – Songwe – Tunduma sasa utatekelezwa kwa njia ya *PPP,* ambapo taratibu za kusaini mkataba zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa ziara yake mkoani Tanga aliagiza ujenzi wa barabara ambayo hapo awali ilikuwa itekelezwe kwa utaratibu wa *EPC+F* kutoka Kibirashi hadi Singida sasa utekelezwe kwa utaratibu wa *PPP*. Tayari *TANROADS* na *TPA* wameanza majadiliano ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa agizo hilo la Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la JP Magufuli (Kigongo - Busisi); nitumie nafasi hii kueleza kuhusu mafanikio ya mradi mmoja wa kielelezo ambao tumeukamilisha mwaka huu. Mradi huo ni ujenzi wa Daraja la JP Magufuli (Kigongo Busisi) Mkoani Mwanza. Wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akiingia madarakani mwaka 2021, ujenzi wa daraja hili ulikuwa umefikia takribani 25% na kutokana changamoto za kutetereka kwa uchumi wa dunia baada ya janga la UVIKO 19, kulikuwa na wasiwasi kuwa ni wapi tutapata shilingi bilioni 539.28 za kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kutoa pongezi na shukrani kubwa kwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye si tu amelipa fedha zote hizo kwa mkandarasi kwa wakati, lakini amekamilisha mradi wa ujenzi uliokuwa ndoto ya mtangulizi wake ambapo Mwenyezi Mungu akaamua ukamilishwe wakati huu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuliarifu Bunge kwamba mradi huo sasa umekamilika kwa 99% na tayari kwa heshima zote, tumemuomba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgeni rasmi na kusherehekea tukio hili muhimu kwa Watanzania, hususan wananchi wa Kanda ya Ziwa, la uzinduzi rasmi wa Daraja la John Pombe Magufuli (Kigongo Busisi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa daraja hili kutakuwa faraja kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa ambao wamekuwa

wakitumia muda wa takribani masaa mawili kuvuka kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine. Baada ya Daraja kukamilika, muda wa kuvuka unatarajiwa kupungua hadi kufikia wastani wa dakika tatu tu. Aidha, Daraja hili linategemewa kuongeza shughuli za kiuchumi ndani na nje ya mikoa ya Kanda ya Ziwa na hata nchi jirani na Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja hili pia litakuwa ni mojawapo ya alama na fahari ya Taifa letu kwani kwa urefu wake wa kilometa 3.2, litakuwa ndilo Daraja refu zaidi katika ukanda wetu huu wa Afrika Mashariki na Kati. Ninaomba kuliarifu Bunge kuwa vivuko vyote vilivyokuwa vinatumika katika eneo la Kigongo – Busisi sasa vitapelekwa katika maeneo mengine ambayo yana uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko na maegesho ya vivuko. Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) inasimamia uendeshaji wa vivuko nchini. Hadi kufikia Aprili, 2025, ujenzi na upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza umekamilika na miradi mingine ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitumie nafasi hii kushukuru maono ya Rais wetu, jemedari Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuchochea na kuhamasisha uhusiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi yaliyosaidia kutatua changamoto ya usafiri kwa wananchi wa Kigamboni jijini Dar es Salaam. Kutokana na changamoto zilizovikumba vivuko vya Serikali, wananchi wanaotoka na kwenda Kigamboni walikuwa wakipata adha na usumbufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya utu, maono, uzalendo na ubunifu wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali sasa imeruhusu kampuni ya Bakhresa kutumia vivuko binafsi ili kupunguza usumbufu huo. Hivi sasa, wale wanaotaka kutumia kivuko cha Serikali wanatumia na wale wanaotaka kutumia kivuko cha Azam, nao wanatumia na kwa kiasi kikubwa, tumeondoa usumbufu wa usafiri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya hatua za utekelezaji wa miradi mingine ya vivuko yameoneshwa katika Kitabu cha Hotuba yangu kuanzia aya ya 145 hadi aya ya 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* inatekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, miradi mbalimbali imetekelezwa ikiwemo ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi wa umma katika maeneo mbalimbali nchini, ukarabati wa nyumba za viongozi wa Serikali pamoja na usimamizi wa majengo ya Wizara 19 katika Mji wa Serikali (Mtumba). Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo na mingine mingi inayotekelezwa na *TBA* imeoneshwa kuanzia aya 151 hadi aya ya 156 ya Kitabu cha Hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* imehuishwa kupitia *GN* Na. 595 ambayo inaruhusu Wakala kuhusisha Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi yake pamoja na kuwauzia na kuwapangisha nyumba wasiokuwa watumishi wa umma kwa bei ya soko. Aidha, Wakala umeainisha maeneo yake yaliyoiva (*Prime Areas*) katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Mwanza kwa ajili ya kuyaendeleza kwa njia ya ubia pamoja na mikopo kutoka Taasisi za kifedha. Hivyo tunawakaribisha wawekezaji wote wa ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza nasi. Kufuatia kuhuisha Sheria hiyo, Wizara inategemea kupungua kwa changamoto za makazi kwa watumishi wa umma na kuiwezesha kupata mapato yatakayopelekea Wakala kujiendesha na kupunguza utegemezi wa ruzuku katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti uzito wa magari na masuala ya usalama barabarani. Serikali kupitia *TANROADS* imeendelea kujenga na kuboresha mizani ya kupima uzito wa magari ili kulinda barabara zisiharibike mapema na kuimarisha udhibiti wa uzito wa magari. Aidha, ili kukabiliana na changamoto ya msongamano kwenye vituo vya mizani pamoja na vitendo vya rushwa, Serikali kupitia *TANROADS* imejipanga kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kufunga mizani ya kisasa isiyotumia binadamu *(unmanned weighbridge)* ili kupunguza matumizi ya binadamu na vitendo vya rushwa katika vituo vya mizani. Mfumo huo utaunganishwa na mifumo mingine ya Serikali kama vile mfumo wa Benki Kuu na *GePG* kwa lengo la kurahisisha huduma;

(ii) Kuendelea kufunga mizani ya kieletroniki ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo *(Weigh in Motion System)* katika vituo vyote vya mizani mpaka mwaka 2030 ili kupunguza msongamano wa magari katika vituo vya mizani. Hadi sasa, mizani ya aina hii imefungwa katika Vituo vya Mizani vya Vigwaza, Mikese, Mikumi, Wenda, Mpemba, Nala, Njuki, Kimokouwa, Dakawa na Rubana; na

(iii) Kufunga mfumo wa ufuatiliaji (*CCTV Camera)* na *Data Management System* katika vituo vyote vya mizani ifikapo 2027. Kwa sasa, Serikali kupitia *TANROADS* ipo katika hatua ya manunuzi kwa ajili ya kufunga mfumo huo katika mizani 58 iliyobakia kati ya mizani 66 ambayo haijafungwa mfumo wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara inayotekelezwa na Wizara huzingatia pia masuala ya usalama barabarani ili barabara hizo zisiwe chanzo cha ajali na maafa kwa watumiaji. Hatua mbalimbali zinachukuliwa ili kuhakikisha barabara zetu zinakuwa salama. Miradi inayotekelezwa ni pamoja na kufanyia maboresho maeneo hatarishi, kuweka alama na michoro muhimu barabarani, kufunga taa za barabarani, taa za kuongoza magari katika maeneo ya miji mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari ametoa maelekezo ya kuwepo kwa taa za barabarani kama mojawapo ya njia za kupunguza ajali na kuokoa maisha ya watu hapa nchini. Kama sehemu ya utelekezaji wa maelekezo hayo, jumla ya taa za barabarani 4,680 zimefungwa nchi nzima. Aidha, miradi yote mikubwa ya ujenzi kwa kiwango cha lami inahusisha uwekaji wa taa za barabarani. Kwa mfano, barabara yote ya Mzunguko wa Nje *(Outer Ring*

*Road)* katika Jiji la Dodoma, kilometa zote 112 zitawekwa taa za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, taa za barabarani zitawekwa katika kila Mkoa katika Miji takriban 200 ambapo inatarajiwa tutanunua taa 5,200 kwa ajili ya kueneza mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zinazofanywa na Wizara kupitia *TANROADS* zimezaa matunda na zimeanza kutambuliwa kimataifa. Kwa mfano, Wizara kupitia Wakala ya Barabara ilipokea tuzo ya heshima katika mashindano ya Kimataifa ya Usalama wa Miundombinu ya Barabara inayoitwa *iRAP Gary Liddle Memorial Trophy* kutokana na mchango wa Wakala *TANROADS* katika kuboresha usalama wa miundombinu ya barabara nchini ili kupunguza ajali za barabarani na kuhakikisha usalama wa watumiaji wote wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzo hii imetoa motisha kubwa kwa *TANROADS* kuendelea kuimarisha usalama wa miundombinu ya barabara kuu na za mikoa ili kufikia lengo la Umoja wa Mataifa la kupunguza ajali kwa 50% ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege. Wizara kupitia *TANROADS* imeendelea kutekeleza miradi ya uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Msalato, Geita, Kigoma, Tabora, Songwe, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Tanga na *Lake* Manyara. Miradi hii ikikamilika viwanja vitarejeshwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya viwanja vya ndege yameoneshwa kwa kina katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia aya ya 168 hadi 177.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara; Wizara ya Ujenzi ina taasisi tisa ninazosisimamia ambazo zinatekeleza majukumu ya Sekta ya Ujenzi, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo hadi kufikia Aprili, 2025 ni kama yalivyooneshwa katika aya 178 hadi 211 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto; pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, zipo changamoto kadhaa ambazo zimechangia kutokufikiwa malengo yaliyokusudiwa kwa 100%. Changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua zimeoneshwa katika kitabu cha hotuba yangu katika aya ya 219.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makisio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026, kauli mbiu yetu ni Bajeti ya Kazi na Utu. Vipaumbele vitaendelea kuwa ni kutekeleza miradi ambayo ina manufaa kwa maendeleo ya Taifa letu, kuangalia maeneo yenye uhitaji zaidi, lakini pia kuwezesha miundombinu itakayofanya Watanzania waishi maisha ya utu zaidi na wakati huo huo watumishi wa Wizara wakichapa kazi usiku na mchana kwa kuzingatia uwajibikaji, ubora wa kazi na uzalendo. Tunasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo hayo ya jumla, Wizara itajikita katika vipaumbele mahususi vifuatavyo, ikiwa ni pamoja na kutekeleza ahadi na maelekezo mahususi ya Mhe Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan:-

(i) Ujenzi wa barabara za kimkakati zenye kufungua fursa za kiuchumi, kuimarisha shughuli za kijamii na zinazounganisha barabara na njia nyingine za usafiri;

(ii) Ujenzi wa barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa, nchi jirani na zile za ulinzi;

(iii) Ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano katika miji inayokua na majiji;

(iv) Ukarabati na matengenezo makubwa ya barabara kuu na mikoa ili kuzirejesha na pia zipitike majira yote ya mwaka;

(v) Kuimarisha usafiri na miundombinu ya vivuko;

(vi) Miradi ya usalama barabarani ikiwemo ujenzi wa mizani;

(vii) Kujenga nyumba za watumishi wa umma na majengo ya Serikali;

(viii) Kuwajengea uwezo wataalam na wakandarasi wa ndani katika masuala ya ujenzi; na

(ix) Kukamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vilivyokasimiwa kwa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida; Wizara ya Ujenzi imetengewa Shilingi 90,468,270,000 ikiwa ni bajeti ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2025/2026. Kati ya fedha hizo, shilingi 85,028,585,000 ni bajeti ya mishahara na shilingi 5,439,685,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo; bajeti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inajumuisha fedha za ndani shilingi 1,209,223,117,000, fedha za nje ni shilingi 980,504,441,000, fedha za ndani zinajumuisha shilingi 688,756,470,000 kutoka Mfuko wa Barabara, na shilingi 520,466,647,000 ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha umeoneshwa katika Kiambatisho Na.1. Aidha, maelezo ya kina kuhusu miradi itakayotekelezwa yameoneshwa katika aya 225 hadi 365 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi itakayotekelezwa inajumuisha pia miradi ya matengenezo ya dharura za miundombinu ya barabara na madaraja ambayo iliharibiwa na mvua za *El–Nino* na Kimbunga Hidaya mwishoni mwa mwaka 2023. Kupitia programu iliyoidhinishwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya *Crisis and Emergency Response Component (CERC)* jumla ya mikataba 81 yenye thamani ya shilingi 556,928,617,822.49 kwa ajili ya matengenezo ya dharura imesainiwa na wakandarasi wanaendelea na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mikataba hiyo 81, miradi 72 inatekelezwa na wakandarasi wazawa sawa na maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2206,

Serikali itafanya matengenezo makubwa ya barabara ili zisiendelee kuharibika. Barabara zilizopangwa kufanyiwa matengenezo ni pamoja na Dar es Salaam – Mkuranga - Kibiti - Lindi hadi Mingoyo kilometa 463 ambayo ilifungwa kutokana na mvua kubwa zilizonyesha hivi karibuni. Barabara hii itajengwa kwa awamu. Niwahakikishie watumiaji wa barabara hii kuwa, matengenezo haya makubwa yatakapokamilika yatakuwa ni suluhisho la changamoto ya kukatika mawasiliano mara kwa mara kwa barabara hii wakati wa msimu wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia nafasi hii kulitangazia Bunge kwamba wakandarasi wawili wa matengenezo ya Barabara ya Mtwara – Mingoyo (Mnazi Mmoja) na Mnazi Mmoja – Masasi kwa gharama ya shilingi bilioni 427 wamepatikana na tayari fedha za awali zimeshalipwa. Mkandarasi wa kipande cha Mtwara – Mingoyo tayari yupo kazini na yule wa Mingoyo – Masasi anatarajiwa kuwa uwandani mwezi huu. Kwa hiyo, kazi kubwa ya maendeleo inaendelea kufanywa hata katika Mikoa hii ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubunifu na utu. mojawapo ya changamoto kubwa ambayo imeikumba Sekta ya Ujenzi kikanda na kimataifa katika miaka ya hivi karibuni, ni suala zima la mabadiliko ya tabianchi. Ongezeko la vimbunga na mvua zinazosababisha mafuriko yasiyo ya kawaida imekuwa ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nimejionea mwenyewe hali hii wakati wa ukaguzi wa athari za mvua zilizonyesha hivi karibuni na kusababisha kukatika kwa mawasiliano katika barabara kuu ya Dar es Salaam kuelekea Mikoa ya Kusini hususani katika eneo la Somanga na pia Mkoani Morogoro katika Wilaya za Mlimba, Ifakara na Malinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia kwa macho yangu namna mabadiliko haya ya tabianchi yanavyoumiza miundombinu, lakini pia kuathiri utu wa watu. Kila nilipofika kuangalia uharibifu, nilikuwa na maelekezo ya Mfariji Mkuu, Rais wetu, Dkt Samia Suluhu Hassan, aliyeniagiza kuhakikisha mawasiliano yanarejea na watu wanaishi maisha yao kwa utu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niliarifu Bunge kwamba Mheshimiwa Rais alikuwa akifuatilia kwa karibu kila kinachoendelea katika mikoa yote iliyokumbwa na maafa ya mvua na mara zote alitaka kujua kuhusu hali za wananchi hususan usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Serikali hii ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, suala la ujenzi wa barabara na madaraja si suala la idadi ya kilometa, namba au ufahari pekee bali ni suala nyeti linalogusa utu na maisha ya watu wetu. Ninaomba niwaeleze kisa kimoja cha Ndugu Lawrence Chilumba ambaye alikuwa anasafirisha mwili wa marehemu mama yake kutoka Dar es Salaam kwenda Masasi mnamo tarehe 16 mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu Chilumba alilazimika kukesha na mwili huo katika eneo la Somanga akisubiri wataalam wetu wafanikishe ukarabati wa eneo ambalo halikuwa linapitika. Ndugu Chilumba alikesha nasi na alikuwa wa kwanza kuruhusiwa kupita barabarani na wafiwa wenzake ili aweze kwenda kumsitiri marehemu mama yake mara wataalam walipofanikiwa kurekebisha barabara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie jukwaa hili kuwapa pole Watanzania wote walipatwa na kadhia ile na ninaomba nitumie jukwaa hili kuwapongeza sana wataalam wetu wa barabara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Balozi Aisha Amour lakini na Mkurugenzi wa taasisi yetu ya *TANROADS Eng.* Mohamed Besta na wote waliokesha siku nne pamoja nami katika eneo lile la Somanga kuhakikisha kwamba barabara inarejea. Pia, ninaomba nimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Lindi Mheshimiwa Zainab Telack na wote walioshiriki katika kuhakikisha kwamba tunashirikiana kufanikisha barabara kufunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali hii ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inapopanga mipango ya kujenga barabara kwa Taifa letu, taswira za matukio ya namna hii ya wananchi wetu kama Lawrence Chilumba hutuongoza pia kwenye mipango yetu. Barabara ya kilometa tano katika eneo ambako hakujawahi

kuwa na barabara, ina thamani kubwa kuliko kutokuwa na barabara kabisa. Wananchi wetu wanaujua ukweli huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nilihakikishie Bunge ya kwamba itakapofika mwezi Septemba mwaka huu maeneo ya Somanga ambayo yamekuwa ni maarufu sana kwa barabara kukatika, Wakandarasi watakuwa wamemaliza kazi yote ya urekebishaji wa barabara katika eneo hilo na inawezekana mvua za mwaka huu ikabaki kuwa historia ya ubovu wa barabara katika maeno yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *TANROADS* imejipanga kukabiliana na majanga ya asili kama mafuriko katika sehemu mbalimbali nchini kwa kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kuainisha maeneo yanayokumbwa na mafuriko ya mara kwa mara kwa lengo la kuimarisha kwa kujenga miundombinu inayoweza kuhimili mafuriko ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa baadhi ya madaraja na barabara kuhimili vishindo vya mabadiliko ya tabianchi umekuwa mdogo. Kwa kuzingatia hali hiyo, Wizara yangu sasa inajielekeza katika ujenzi wa barabara na madaraja unaozingatia mahitaji ya kisasa ya dunia yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine tunazochukua ni kuendelea kuimarisha kituo cha kukabiliana na dharura za majanga *(Emergency Response Centre)* kilichopo katika Ofisi za *TANROADS* Mkoa wa Pwani pale Kibaha. Katika Mwaka wa Fedha wa 2024/2025 kituo kimefanya manunuzi ya vifaa mbalimbali vya kukabiliana na dharura ikiwa ni pamoja na makalavati ya chuma *(armco)* yenye urefu wa mita 5,750, nyavu za kushikilia mawe katika kingo za madaraja *(gabion boxes)* na magodoro yake *(reno mattresses)* yenye jumla ya mita za ujazo 4,500, vyote vikiwa na thamani ya Shilingi Bilioni 4.91. Aidha, vituo vingine vimepangwa kuanzishwa katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na uimarishaji na uanzishaji wa vituo vingine vya kukabiliana na majanga ya asili,

Wizara kupitia *TANROADS* inaboresha miongozo ya usanifu na vifaa vya ujenzi *(building materials)* ili kuhakikisha miundombinu mipya inayojengwa inahimili mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezeshaji wazawa. kufuatia maelekezo mahsusi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wizara imefanya uamuzi wa kimapinduzi wa kuongeza ukomo wa kuwapa kazi wakandarasi wazawa kutoka kiasi cha shilingi bilioni 10 za zamani hadi shilingi bilioni 50. Hili limewekwa katika Sheria ya Manunuzi na maana yake ni kwamba kama kazi ya ujenzi ina thamani ya mpaka shilingi bilioni 50, kipaumbele cha kwanza kitakuwa ni kwa wakandarasi wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi huu uliotokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, siyo tu kwamba ni kwa sababu za kizalendo pekee bali pia ni kwa sababu za kiutendaji. Baadhi ya kampuni za hapa nyumbani zimeonesha uwezo mkubwa unaofanana na wakati mwingine hata kuzidi wajenzi kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi huu utaongeza mzunguko wa fedha kwenye uchumi wetu, kukuza uwezo wa wakandarasi wetu wa ndani, kufanya kazi kubwa zaidi na kuongeza kada ya Watanzania wenye uwezo wa kufanya miradi mikubwa ya ujenzi. Kubwa zaidi, hatua hii itaongeza ajira kwa vijana wetu kwa sababu sasa wakandarasi wa nyumbani watalazimika kuongeza nguvu kazi kwa sababu ya ukubwa wa miradi watakayoanza kupewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayapongeza baadhi tu ya kampuni chache za kizalendo kati ya nyingi ambazo zimetupa nguvu ya kuchukua uamuzi huu kutokana utendaji wao. Ninaomba niwapongeze kampuni ya Makapo *Contractors & General Supplies,* imefanya vizuri sana. *ESTIM Construction*, Nyanza *Road Works*, Mlumangi *Construction, Kings Builders*, *ROCKTRONIC Limited,* UMOJA KILOSA, Mtwivila *Traders* na *M/s Technics Construction Group.* Hizi ni miongozi mwa kampuni nyingi za kizalendo zilizofanya kazi ambayo tunajivunia.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufuatiliaji, ninaomba kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba endapo litaidhinisha bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026, tutahakikisha tunasimamia ipasavyo matumizi ya fedha hizo ili kile kinachotarajiwa kionekane. Watatuona sana huko uwandani tukifuatilia kinachoendelea. Usiku na mchana, wataona watumishi wa Wizara na wakandarasi wakifanya kazi kwa kasi ili kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hotuba hii ya bajeti ya Wizara, ninaomba kutoa onyo kwa wakandarasi wote nchini, wa nyumbani na wa kigeni, kwamba kuanzia sasa hatutasita kuvunja mikataba pale itakapoonekana kuna uzembe, ukosefu wa viwango na kupitiliza kwa muda wa kukamilika mradi kusiko na sababu za msingi, huku tukizingatia sheria za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya watumishi wa Wizara ya Ujenzi, ninaomba nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuongeza mishahara ya wafanyakazi, ahadi yetu Wizara ya Ujenzi kwake na kwa watanzania wote ni kufanya kazi usiku na mchana ili kukuza uchumi wa nchi na kujali utu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho; ninapohitimisha, kwa dhati ya moyo wangu ninaomba nitoe shukrani kwa watendaji wenzangu Wizarani. Kipekee nawashukuru sana viongozi wenzangu wa Wizara wakiongozwa na mtu muungwana, Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya, Mbunge wa Ileje, Balozi Mhandisi Aisha Salim Amour, Katibu Mkuu pamoja na Dkt. Charles Enock Msonde, Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan, kwa kuniunganisha na timu hii mahiri ya mchanganyiko wa wanasiasa na watendaji ambao wamerahisisha sana utendaji kazi ndani ya Wizara yetu. Ama kwa hakika, katika kipindi hiki kifupi nilichoiongoza nimepata ushirikiano wa kutosha kutoka kwao katika usimamizi wa Wizara hii. Aidha, sitakuwa muungwana nisipoishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa moyo wa uzalendo na kujitolea wakati

wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kipekee kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Mkuranga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika majukumu yangu ya kuwawakilisha na kuwasemea. Nitumie fursa hii, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mkuranga na Watanzania kwa ujumla, kumshukuru na kumpongeza sana Rais wetu, Jemedari Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuidhinisha na kuridhia upanuzi wa Barabara ya Rangitatu – Kongowe. Upanuzi wa barabara hii utapunguza usumbufu na adha ya kukaa barabarani kwa muda mrefu na kuchochea uchumi wa watumiaji wa njia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, niishukuru sana familia yangu, ikiongozwa na mke wangu mpendwa, Hajat Bi. Mariam Abdallah Ibrahim, kwa kuendelea kuniombea, kunivumilia na kunipa amani ya moyo wakati wote nikitekeleza majukumu ya ujenzi wa Taifa letu. Sina maneno mazuri zaidi ya kusema Ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Wizara umefanikiwa kupitia ushirikiano wa Serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na wa nje. Na hapa, Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, naomba kuwatambua wachache kati ya walio wengi walioshirikiana nasi kwa namna moja au nyingine kama ifuatavyo; Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*, Benki ya Dunia, *Japan International Cooperation Agency (JICA), OPEC Fund,* Korea Kusini *(KOICA),* Abu Dhabi Fund, Shirika la Maendeleo la Ufaransa, Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Kuwait Fund, Barick, *EACOP*, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Japan, China, Norway, *NSSF*, Taasisi za fedha za *CRDB, NMB, NBC*, *TCB* na Asasi mbalimbali zisizokuwa za Serikali, Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hii nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitamshukuru tena, kwa mara nyingine, Mhe Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan, kwa diplomasia yake ya uchumi

iliyoifungua nchi yetu Kimataifa. Matunda yake ndiyo haya yanayoonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia, katika tovuti ya Wizara *(www.mow.go.tz)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muhtasari wa Maombi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi katika mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,280,195,828,000.00, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 90,468,270,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi na shilingi 2,189,727,558,000.00 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi 85,028,585,000.00 ni za Mishahara ya Watumishi na shilingi 5,439,685,000.00 ni za Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inajumuisha fedha za ndani shilingi 1,209,223,117,000.00 na fedha za nje ni shilingi 980,504,441,000.00. Fedha za ndani zinajumuisha shilingi 688,756,470,000.00 kutoka Mfuko wa Barabara na shilingi 520,466,647,000.00 ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii nimeambatisha mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa na Wizara katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Kiambatisho Na. 1 – 5). Ninaomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja yangu.

## HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, MHESHIMIWA ABDALLAH HAMIS ULEGA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka

wa fedha 2024/25, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2024/25. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu liridhie kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/26.

**2. Mheshimiwa Mwenyekiti**, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii hapa Bungeni.

**3. Mheshimiwa Mwenyekiti**, nitumie nafasi hii adhimu, na kwa unyenyekevu mkubwa, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini, na kuniteua kuwa Waziri wa Ujenzi tangu tarehe 08 Desemba, 2024. Naomba kupitia kwako nimuahidi Mheshimiwa Rais kuwa, kwa kushirikiana na watendaji wenzangu katika Wizara, nitatekeleza majukumu haya niliyopewa kwa uaminifu na moyo wa uzalendo.

**4. Mheshimiwa Mwenyekiti**, sambamba na shukrani hizo kwa Mheshimiwa Rais, kipekee nitumie fursa hii kumpongeza kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya ya kuliongoza Taifa letu. Sote ni mashuhuda wa namna alivyofanya mapinduzi makubwa katika sekta zote nchini. Chini ya uongozi wake tumeshuhudia 2 miradi mikubwa, katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta ya ujenzi inavyoendelea kutekelezwa nchi nzima. Kukamilika kwa miradi hii kunachochea maendeleo ya sekta nyingine za kiuchumi na kijamii na hivyo kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Hakika Watanzania tunajivunia na tunatembea kifua mbele chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Rais.

**5. Mheshimiwa Mwenyekiti**, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumsaidia na kumshauri vyema Mheshimiwa Rais katika uongozi wa nchi yetu. Viongozi hawa pia wamekuwa wakitoa miongozo na maelekezo

mbalimbali ambayo yamesaidia sana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi. Nawashukuru sana.

**6. Mheshimiwa Mwenyekiti**, nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa namna mnavyoongoza kwa weledi Bunge hili la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo litafikia tamati katika Mkutano huu. Aidha, nitumie nafasi hii kutoa shukrani kwa Ofisi yako, Katibu wa Bunge na watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano ambao mmetupatia wakati wote katika utekelezaji wa majukumu yetu.

**7. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya uongozi wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb.). Kamati hii imekuwa bega 3 kwa bega na Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kupitia maelekezo, maoni na ushauri katika masuala mbalimbali. Hali kadhalika, Kamati hii ilifanya uchambuzi wa kina wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/25 na kutoa ushauri ambao umezingatiwa katika bajeti hii ninayoisoma mbele ya Bunge lako.

**8. Mheshimiwa Mwenyekiti**, nitumie fursa hii pia kutoa mkono wa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako, Chama cha Mapinduzi, wananchi wa Jimbo la Kigamboni, marafiki na familia, kufuatia kifo cha Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

**9. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mnamo tarehe 16 Novemba, 2024, yalitokea maafa makubwa kutokana na kuporomoka kwa jengo la ghorofa nne katika eneo la Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Ajali hiyo ilisababisha vifo, majeruhi pamoja na upotevu wa mali. Nitumie nafasi hii kutoa pole kwa wote walioathirika na maafa haya, na ninawaombea marehemu wote wapumzike kwa amani. Wizara yangu, ikiwa ni msimamizi wa shughuli za majenzi nchini, inaendelea na taratibu za kutunga Sheria ya Majengo kwa ajili ya kusimamia Sekta ndogo ya Majengo nchini. Sheria hii itakapoanza kutumika itakuwa muarobaini wa changamoto zilizopo hususan

katika masuala ya uratibu, usimamizi na udhibiti wa sekta hiyo hapa nchini.

**10. Mheshimiwa Mwenyekiti**, nitumie fursa hii kwa mara nyingine kutoa pole kwa wananchi kutokana na adha iliyotokea baada ya daraja la dharura la Somanga1Mtama kukatika na kusababisha changamoto ya 4 mawasiliano baina ya mkoa wa Pwani na Mikoa ya Kusini. Daraja hili lipo katika eneo linapojengwa daraja jipya la kudumu katika mpango wa matengenezo yanayoendelea kufuatia uharibifu uliotokea mwaka jana kutokana na mvua za El-nino na Kimbunga Hidaya. Aidha, nitoe pole kwa wananchi katika maeneo mengine nchini yaliyoathirika kutokana na uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja. Niwaondoe hofu na kuwapa matumaini wananchi kuwa Serikali, chini ya Mheshimiwa Rais, Daktari Samia Suluhu Hassan ipo kazini mchana na usiku ili kurejesha mawasiliano katika hali yake ya kawaida kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

**11. Mheshimiwa Mwenyekiti**, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, niruhusu sasa nitoe taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/26. Aidha, kabla ya hayo, naomba nitoe taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020.

## B. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YALIYOAINISHWA KATIKA ILANI YA CCM YA MWAKA 2020

**12. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mwaka huu ni wa kipekee kwani nchi yetu itafanya uchaguzi mkuu wa kuchagua Rais, Wabunge na Madiwani. Tunapoelekea katika uchaguzi huo, ni vyema tutoe taswira ya jumla ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 ambayo iliaminiwa na wananchi hadi kuipa CCM dhamana ya kuongoza nchi kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025. Nitumie fursa hii kwa muhtasari 5 kutoa taarifa ya utekelezaji wa Ilani hiyo kwa masuala yanayohusu Wizara ya Ujenzi yaliyopo katika **Ibara 55 (a-b) – Masuala ya Kisera; 55 (c-g) - Barabara na Madaraja na Usalama Barabarani; 55 (h) – Nyumba**

**na Majengo ya Serikali; 57 (j) – Vivuko na 59 (h) – Viwanja vya Ndege.** 13. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, utekelezaji wa masuala haya ni kama ifuatavyo:

**a. Kuimarisha Mfuko wa Barabara**

**14. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mfuko wa Barabara ulianzishwa mwaka 2000, mahsusi kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara nchini. Serikali imefanikiwa kuongeza makusanyo ya Mfuko wa Barabara kutoka Shilingi bilioni 899.2 mwaka 2020/21 hadi Shilingi bilioni 1,113.3 mwaka wa fedha 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 24. Aidha, hadi Aprili, 2025, makusanyo ya fedha za Mfuko kwa mwaka wa fedha 2024/25 yalikuwa yamefikia Shilingi bilioni 905.2. Ongezeko hili limewezesha kuimarika kwa uwezo wa Mfuko kugharamia matengenezo ya barabara nchini.

**b. Kuunganisha makao makuu ya mikoa na nchi jirani kwa barabara za lami**

**15. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara imeendelea kujenga barabara za lami za kuunganisha makao makuu ya mikoa na nchi jirani. Miradi iliyokamilika katika kipindi hiki ni kuunganisha mikoa ifuatayo:

i. Tabora na Singida kupitia barabara ya Chaya – Nyahua (km 85.4);

ii. Tabora na Katavi kupitia barabara ya Tabora – Koga – Mpanda (km 342.9); na

iii. Kigoma na Kagera kupitia barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu (km 260.6).

Vilevile, miradi mbalimbali ya barabara za kuunganisha nchi yetu na nchi jirani imetekelezwa katika kipindi cha miaka mitano. Miradi iliyokamilika ni kuunganisha Tanzania na nchi zifuatazo:

i. Tanzania na Malawi kupitia barabara za Mpemba – Isongole (km 50.3) na Mbinga – Mbambabay (km 66) ambazo zimekamilika; na

ii. Tanzania na DRC kupitia barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107).

**16. Mheshimiwa Mwenyekiti**, aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya barabara mbalimbali za kuunganisha mikoa ambayo haijaunganishwa kwa barabara za kiwango cha lami kama ifuatavyo:

i. Rukwa na Katavi; ujenzi wa sehemu ya Kibaoni – Sitalike (km 50) unaendelea;

ii. Katavi na Kigoma; ujenzi wa sehemu ya Vikonge – Mishamo Jct (km 62.7) unaendelea;

iii. Kigoma na Tabora; ujenzi wa sehemu ya Uvinza – Malagarasi (km 51.1) unaendelea;

iv. Singida na Mbeya; ujenzi wa sehemu ya Mlongoji – Itigi – Mkiwa (km 56.9) unaendelea;

v. Morogoro na Njombe; sehemu ya Ifakara – Mbingu – Chita (km 100) ujenzi unaendelea;

vi. Morogoro na Ruvuma; ujenzi wa sehemu ya Ifakara – Lupiro – Mtimbira (km 112) Mkandarasi yupo katika hatua za awali za kuanza ujenzi;

vii. Tanga na Manyara; Ujenzi wa sehemu ya Handeni – Mafuleta – Kileguru (km 50) unaendelea. Mkandarasi wa sehemu ya Handeni – Kang'ata (km 30) yupo katika hatua za awali za kuanza ujenzi;

viii. Arusha na Mara; ujenzi wa sehemu ya Waso – Sale (km 49) umekamilika na ujenzi wa sehemu ya Natta – Sanzate unaendelea;

ix. Arusha na Shinyanga; Mkandarasi wa sehemu ya Nkoma – Lalago (km 65) yupo katika hatua za awali za kuanza ujenzi; na

x. Njombe na Mbeya; ujenzi wa sehemu ya Njombe – Makete (km 107) umekamilika na ujenzi wa sehemu ya Kitulo – Iniho (km 36.3) unaendelea.

**c. Kushirikisha kikamilifu vikundi vya wananchi Pamoja na Makandarasi wadogo katika kazi za matengenezo ya barabara**

**17. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali kupitia TANROADS imekuwa ikitoa kazi za matengenezo ya barabara zisizotumia mitambo (Labour based methods) kupitia mikataba na Makandarasi wadogo au nguvu kazi ya ndani ya Wakala (Force account). Kupitia mikataba hii, TANROADS hutekeleza shughuli za matengenezo kwa kutumia vifaa na/au vibarua kutoka katika maeneo ya miradi.

**d. Kuendelea kuwajengea uwezo Makandarasi wazalendo ili kushiriki kikamilifu kwenye kazi kubwa za ujenzi**

**18. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali imeendelea kutoa vipaumbele kwa Makandarasi wazawa kwa zabuni zote za ujenzi na matengenezo ya barabara zinazoendelea hapa nchini. Serikali kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma, (Sura ya 410) na kanuni zake za mwaka 2024 inaekeleza miradi yote yenye thamani chini ya Shilingi billioni 50 itekelezwe na Makandarasi wazawa. Jumla ya mikataba 5,264 ya matengenezo ya barabara yenye thamani ya kiasi cha Shilingi trilioni 1.963 ilisainiwa na kutekelezwa na makandarasi wazawa. Aidha, TANROADS inaendelea na taratibu za ununuzi kwa Makandarasi wanawake wazawa ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/25 jumla ya miradi minne (4) yenye urefu wa kilometa 20 yenye thamani ya Shilingi milioni 53,627.123 imetengwa kwa Makandarasi wanawake na kwa sasa iko katika hatua za mwisho za ununuzi.

### e. Kukamilisha ujenzi na ukarabati wa barabara unaoendelea kwa kiwango cha lami

**19. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali imepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa **1,365.87** zimejengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami. Barabara hizo ni pamoja na:

i. Kasulu - Kabingo (km 184);

ii. Mbinga – Mbamba Bay (km 66);

iii. Mpemba – Isongole (km 50.3);

iv. Lusitu - Mawengi (km 50);

v. Njombe – Moronga Section (km 53.9);

vi. Moronga – Makete Section (km 53.5);

vii. Rudewa – Kilosa (km 24);

viii. Morocco – Mwenge (km 4.3);

ix. Makutano – Natta (Sanzate) Section (km 50);

x. Loliondo – Mto wa Mbu (sehemu ya Waso – Sale Jct (km 50);

xi. Chunya – Makongolosi (km 39);

xii. Tabora (Usesula) – Koga – Mpanda; Sehemu ya Kwanza: Usesula – Komanga (km 115); Sehemu ya Pili: Komanga- Kasinde (km120) na Sehemu ya Tatu: Kasinde – Mpanda (km 118); na

xiii. Nyahua-Chaya (km 85.4).

### f. Kuanza ujenzi mpya na ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami

**20. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, barabara mbalimbali zenye urefu wa kilometa **3,140.67** zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami nchi nzima na zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Maelezo ya kina kuhusu hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo imeoneshwa kuanzia **Aya 48 hadi 142**.

### g. Miradi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina

**21. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali imekamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa kilometa **3,848.13** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara kuu na za mikoa. Aidha, usanifu wa madaraja mapya manne **(4)** ambayo ni Godegode (Dodoma), Mkundi (Morogoro), Malagarasi Chini (Kigoma) na Mirumba (Katavi) pamoja na Upembuzi Yakinifu wa kilometa 365 kwa ajili ya ukarabati wa barabara kuu na za mikoa kwa kiwango cha lami umekamilika. Vilevile, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa jumla ya kilometa **3,694.64** upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

### h. Ujenzi wa Madaraja

**22. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kipindi hicho, jumla ya madaraja makubwa nane (8) yamekamilika. Madaraja hayo ni; Kitengule (Kagera), Wami (Pwani), Msingi (Singida), Tanzanite (Dar es Salaam), Kiyegeya (Morogoro), Gerezani (Dar es Salaam), Mpwapwa (Dodoma) na Ruhuhu (Ruvuma). Aidha, ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi (JP. Magufuli) unatarajiwa kukamilika mapema mwezi Mei, 2025.

**23. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Vilevile, madaraja mengine makubwa 17 yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi, ambayo ni; Mirumba, Pangani, Mbangala, Simiyu, Mbambe, Doma, Nzali, Chakwale, Nguyami, Suguta, Sukuma, Jangwani, Mwanjiri, Mkili, Kalebe, Kavuu, na Mitomoni. Aidha, Madaraja makubwa saba (7) ya Mpiji Chini, Kibakwe, Kerema Maziwa, Sanza, Munguli na Godegode yako kwenye hatua mbalimbali za maandalizi ya kazi za ujenzi.

**24. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kupitia hadhira hii, naomba kutoa pongezi na shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Rais, kwa kutoa fedha zilizowezesha kukamilika kwa mradi wa kimkakati wa ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi. Wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia 25 na ndani ya miaka minne amefanikisha Mkandarasi kulipwa kwa wakati jumla 11 ya Shilingi Bilioni 539.28 na kukamilisha ujenzi wa daraja hili la kielelezo. Kukamilika kwa daraja hili kutakuwa faraja kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa ambao wamekuwa wakitumia muda wa takriban masaa mawili (2) kuvuka kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine. Baada ya daraja kukamilika muda wa kuvuka unatarajiwa kupungua kutoka masaa mawili (2) hadi wastani wa dakika tatu (3).

**i. Kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam**

**25. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya kilometa 52.5 za barabara za kupunguza msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam zimejengwa kwa kiwango cha lami. Barabara zilizokamilika ni pamoja na:

i. Barabara ya Kimara – Kibaha (19.2)

ii. Barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya II kutoka Maktaba – Mbagala (km 19.3)

iii. Barabara ya Ardhi – Makongo (km 4)

iv. Barabara ya Wazo Hill – Madale (km 9).

v. Daraja la Tanzanite (km 1.03).

vi. Madaraja ya juu ya Chang'ombe na Uhasibu.

Vilevile, miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

i. Ujenzi wa Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya III kutoka Maktaba – JNIA - Gongolamboto (km 23.3);

ii. Ujenzi wa Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya IV kutoka Maktaba – Morocco – Mwenge - Tegeta na Mwenge - Ubungo (km 30.1); na

iii. Maandalizi ya kuanza ujenzi wa Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya V kutoka 12 Ubungo – Bandarini, Makutano ya Tabata – Tabata Segerea na Tabata – Kigogo (km 27.6).

Aidha, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Buguruni (Mandela/Uhuru), Magomeni, Fire, Ally Hassan Mwinyi/UN, Ally Hassan Mwinyi/ Kinondoni, Mwenge na Morocco umekamilika. Wizara ya Ujenzi inaendelea na majadiliano na JICA ili kuweza kufadhili ujenzi wa flyovers mbili katika makutano ya barabara ya Ally Hassan Mwinyi na Sam Nujoma (Mwenge) pamoja na makutano na barabara ya Kawawa (Morocco).

**j. Kupunguza msongamano katika Majiji mengine**

**26. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Jiji la Dodoma, jumla ya kilometa 70 kati ya 112.3 za barabara ya Mzunguko wa Nje zimekamilika. Vilevile Serikali inaendelea na taratibu za ununuzi ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Morogoro (Kimbinyiko R/ About – Chamwino Jct km 32). Aidha, kwa barabara ya Dodoma – Iringa (Bahi Rd R/About - Mkonze km 8.5) na Dodoma – Arusha (Bahi Rd R/About – Msalato Airport Jct km 10.7) upembuzi wa awali unaendelea chini ya mradi wa Dodoma Intergrated and Sustainable Transport (DIST) unaopokea mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Kukamilika kwa miradi hii kutachochea shughuli za kiuchumi na kijamii kwa watumiaji wa barabara hizo. Natoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa fedha za ujenzi wa barabara hizi muhimu.

**27. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa upande wa Jiji la Mbeya, upanuzi wa sehemu ya Uyole – Ifisi – Songwe Airport (km 36) unaendelea. Aidha, katika mji wa Iringa, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Mchepuo wa Iringa (km 7.3) unaendelea.

**k. Udhibiti uzito wa magari na masuala ya usalama barabarani**

**28. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali kupitia TANROADS imeendelea kutekeleza ilani ya CCM kwa kujenga na kuboresha mizani ya kupima magari ili kulinda barabara zisiharibike mapema na kuimarisha udhibiti wa uzito wa magari na kupunguza muda wa upimaji kwa kufanya yafuatayo:

i. Kufunga mizani ya kisasa (Electronic load cells) ambayo hutoa taarifa ya mwenendo mzima wa hali ya mizani wakati gari linapimwa ili kupata vipimo sahihi katika mizani. Hadi sasa, Load Cell za kidigitali zimefungwa katika mizani kumi (10) ambayo ni Mpemba, Njuki, Mikese North, Mikese South, Mikumi North, Nala, Makuyuni, Mutukula, Mingoyo na Himo II.

ii. Kufunga mfumo wa kielektroniki ambao unawezesha magari kupimwa kwenye mizani bila kuwa na operator (human intervention). Hadi sasa, mizani 20 ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh-in-Motion) imefungwa katika vituo vya mizani vya Vigwaza, Mikese, Mikumi, Wenda, Mpemba, Nala, Njuki, Kimokouwa, Dakawa na Rubana.

**l. Miradi ya Nyumba na Majengo ya Serikali**

**29. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi 2025, Serikali kupitia Wakala wa Majengo (TBA) imekamilisha ujenzi na usimamizi wa jumla ya majengo ya ofisi za Serikali 321 zikiwemo 19 zilizojengwa katika mji wa Serikali Mtumba - Dodoma pamoja na nyumba 2,685 za Watumishi wa Umma katika mikoa mbalimbali. Aidha, Serikali imekamilisha mradi wa kimkakati wa ujenzi wa Ikulu ya Chamwino. Vilevile, ukarabati wa Karakana sita (6) za kutengeneza samani katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Tabora, Mwanza na Mbeya uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**30. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi 2025 Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na

Umeme (TEMESA), imekamilisha miradi ifuatayo iliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2020: Kusimika Mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato katika kituo cha Magogoni - Kigamboni pamoja na maboresho ya Mfumo wa tiketi za kielektroniki katika kituo cha Kigongo – Busisi. Aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya ununuzi wa vivuko vipya ambavyo utekelezaji wake umefikia hatua zifuatazo; Bwiro-Bukondo (asilimia 92), Kisorya-Rugezi (asilimia 90), Ijinga - Kahangala (asilimia 90), Nyakaliro -Kome (asilimia 90) na Mafia - Nyamisati (asilimia 35).

**31. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali imeendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini. Viwanja vya ndege vilivyokamilika ni: Ujenzi na ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Songwe, Mtwara, Songea, Iringa Awamu ya I na kiwanja cha ndege cha Geita. 15

**32. Mheshimiwa Mwenyekiti**, utekelezaji wa miradi mingine ya viwanja vya ndege ni kama ifuatavyo: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato Package I (asilimia 87) na Package II (asilimia 53.2); Kiwanja cha Ndege cha Kigoma (asilimia 20); Kiwanja cha Ndege cha Tabora (asilimia 93), Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga (asilimia 60), Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga (asilimia 80) na Kiwanja cha Ndege cha Musoma (asilimia 58).

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

**33. Mheshimiwa Mwenyekiti**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Ilani ya CCM, Wizara pia imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Wizara, Mipango Mingine ya Kitaifa na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/25 ni kama ifuatavyo.

## C.1: MATUMIZI YA FEDHA

### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**34. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 81,407,438,000.00** ikiwa ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 76,588,233,000.00** ilikuwa ni Bajeti ya Mishahara na **Shilingi 4,819,205,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

35. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 63,506,309,562.24** zilipokelewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 61,152,975,329.92** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 2,353,334,232.32** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake.

### Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

**36. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Bajeti kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2024/25 kwa Wizara ya Ujenzi ni **Shilingi 1,687,888,714,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,141,803,989,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 546,084,725,000.00** ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani, **Shilingi 599,756,467,800.00** ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na **Shilingi 542,047,521,200.00** ni fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**37. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 1,535,092,021,470.55.** Kati ya fedha hizi, **Shilingi 944,881,583,335.76** ni fedha za ndani na **Shilingi 590,210,438,134.79** ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani zilizopokelewa, **Shilingi 482,085,328,011.98** ni kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 462,796,255,323.78** ni za Mfuko wa Barabara.

## C.2: UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Barabara na Madaraja

**38. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara ya Ujenzi kupitia TANROADS inasimamia mtandao wa barabara wenye urefu wa

**kilometa 37,435.04.** Kati ya hizo kilometa **12,527.44** ni barabara kuu na kilometa **24,907.60** ni barabara za mikoa.

**39. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/25, miradi ya barabara kuu iliyopangwa kutekelezwa ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 385**, ukarabati wa **kilometa 35** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **17**, ukarabati wa daraja **moja (1)**, maandalizi ya ujenzi wa madaraja **tisa (9)** na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa madaraja **mawili (2).**

**40. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi kufikia Aprili, 2025, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 109.49** umekamilika na ujenzi wa **kilometa 275.51** unaendelea.

Kwa upande wa madaraja, ujenzi wa madaraja **matano (5)** unaendelea na ujenzi wa madaraja matano (5) upo katika hatua za maandalizi. Vilevile, taratibu za ununuzi ya Makandarasi wa ujenzi wa madaraja **matano (5)** zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa madaraja 11 na ukarabati wa daraja 1 katika mikoa mbalimbali nchini.

**41. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi ya barabara za mikoa iliyopangwa kutekelezwa ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 98, ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara zenye urefu wa kilometa 925 pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja/ makalavati 107.

**42. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025 jumla ya kilometa 98.13 za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa 192.9 zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Aidha, ujenzi/ukarabati wa madaraja madogo 7 kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na 9 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara umekamilika na madaraja 91 yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Miradi ya Matengenezo ya Barabara na Madaraja**

**43. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara kupitia TANROADS ilipanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mikoa ambayo yalihusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa kilometa 35,095.63, matengenezo ya muda maalum kilometa 3,206.63, matengenezo ya sehemu korofi kilometa 383.84 pamoja na matengenezo ya madaraja 2,904.

Hadi kufikia Aprili, 2025, kazi zilizofanyika ni matengenezo ya kawaida kilometa 16,533.79, matengenezo ya muda maalum kilometa 1,167.97 matengenezo ya sehemu korofi kilometa 120.72 pamoja na matengenezo ya madaraja 1,358.

**44. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, Wizara ilipanga kuendelea na udhibiti wa uzito wa magari, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

**45. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025 jumla ya magari 8,344,978 yalikuwa yamepimwa katika mizani 79 iliyopo nchini ambapo kati ya hayo, magari 22,585 sawa na asilimia 0.27 yalikuwa yamezidisha uzito zaidi ya asilimia 5 ya uzito unaoruhusiwa kisheria. Wasafirishaji waliozidisha uzito walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

**46. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi saba (7) ya barabara iliyokuwa itekelezwe kwa utaratibu wa EPC +F sasa inatekelezwa kwa utaratibu wa ‘sanifu na jenga’ (Design and Build). Hadi sasa, addendum za maboresho ya miradi sita (6) zimeshasainiwa. Aidha, mradi mmoja wa Igawa – Songwe – Tunduma sasa utatekelezwa kwa njia wa PPP, ambapo taratibu za kusaini mkataba zinaendelea. Sambamba na hilo, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa ziara yake Mkoani Tanga aliagiza ujenzi wa barabara ambayo hapo awali ilikuwa itekelezwe kwa utaratibu wa EPC+F kutoka Kiberashi hadi Singida sasa utekelezwe kwa utaratibu wa PPP. Tayari TANROADS na TPA wameanza majadiliano kuhusu namna bora ya utekelezaji wa agizo hilo.

**47. Mheshimiwa Mwenyekiti**, utekelezaji wa miradi yote ya barabara na madaraja iliyotengewa fedha kwa mwaka 2024/25 hadi kufikia Aprili, 2025 ni kama ifuatavyo:

**48. Mheshimiwa Mwenyekiti**, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74) sehemu ya Soni – Bumbuli – Funta (km 30) na Kwameta – Kwashemshi (km 10) zinaendelea kufuatia kutangazwa upya kwa zabuni ya ujenzi.

**49. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 210), ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za Mnivata – Mitesa (km 100) umefikia asilimia 18 na Mitesa – Masasi (km 60) umefikia asilimia 26. Vilevile, taratibu za ununuzi wa kuwapata Makandarasi wa ujenzi wa barabara za Mangamba – Madimba - Msimbati (km 35) na Namichiga – Ruangwa (km 20.6) zinaendelea baada ya kufanya marejeo ya usanifu.

**50. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50), Mkataba wa ujenzi wa barabara hii sehemu ya Likuyufusi – Muhukuru (km 60) utasainiwa mwishoni mwa Mei, 2025.

**51. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mkataba wa EPC+F kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Nachingwea – Liwale (130km) umeboreshwa na kuwa Sanifu Jenga (Design and Build). Ujenzi wa barabara hii utafanyika kwa awamu kwa kuanzia sehemu ya Liwale – Kihangara (km 55), ambapo mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kutumia fedha za ndani.

**52. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11), umeanza na unaendelea.

**53. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24) unafanyika kwa awamu ambapo ujenzi wa kilometa 4.7 umekamilika na ujenzi wa kilometa 3.6 umefikia asilimia 60. Aidha, ujenzi wa sehemu ya Pangani – Mapinga (km 13.59) umefikia asilimia 11.

Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7).

**54. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92), taratibu za ununuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Musoma – Kusenyi (km 40) kwa kiwango cha lami zipo hatua za mwisho kwa ajili ya kusaini mkataba wa ujenzi.

**55. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98) unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2025, ujenzi wa sehemu ya Mpwapwa – Idilo (km 3) ulikuwa umekamilika. Aidha, ujenzi wa sehemu ya Kongwa Jct – Ngambi – Mpwapwa (km 32) upo katika hatua za awali za kuanza ujenzi. Vilevile, Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 46.9) upo tayari kusainiwa.

**56. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 154) kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu ambapo kilometa 43.55 zimekamilika; ujenzi wa sehemu ya Ilambika - Kalela unaendelea na umefikia asilimia 10.

**57. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104) upo katika hatua za awali. Aidha, ujenzi wa barabara ya Iringa 22 (Ipogolo) – Kilolo (km 33.2) kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 50.

**58. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara ya Muheza – Amani (km 36) kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu ambapo ujenzi wa sehemu ya Kwemhosi – Bombani (km 4) umefikia asilimia 98.

**59. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200.51), mikataba ya ujenzi wa sehemu za Mtwara – Mingoyo (km 82.27) na Mingoyo – Nanganga – Masasi (km 118.24) imesainiwa. Hivi sasa, Makandarasi wanaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za ukarabati.

**60. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu (km 189), hadi kufikia Aprili, 2025, ujenzi wa sehemu ya Ntendo – Kizungu (km 25) kwa kiwango cha lami unaendelea na umefikia asilimia 50. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Kizungu – Muze (km 12) na barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152).

**61. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi mwezi Aprili ujenzi wa Daraja la J.P. Magufuli (Kigongo – Busisi) na barabara Unganishi ulikuwa umefikia asilimia 99. Aidha, ujenzi wa barabara ya Kagera Sugar Jct – Kakunyu; Sehemu ya Kagera Sugar Jct – Kitengule Jct (km 25) unaendelea. Mkataba wa ujenzi wa daraja la Mzinga (Dar es Salaam) ikihusisha upanuzi wa barabara ya Mbagala Rangi Tatu - Kongowe (km 3.8) umesainiwa tarehe 19 Machi, 2025. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa daraja 23 la Ugalla (Katavi).

**62. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Morogoro – Dodoma pamoja na Daraja la Mkundi imekamilika. Maandalizi ya kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara ya SUA Main Gate – Mzinga Factory Gate (km 11) kwa kiwango cha lami yanaendelea.

**63. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Njombe – Makete – Isyonje (km 157.4), ujenzi wa sehemu ya Isyonje – Makete (km 50) sehemu ya Kitulo – Iniho (km 36.3) unaendelea na umefikia asilimia 15. Vilevile, ujenzi wa sehemu ya Njombe – Njombe Referral Hospital (km 3) unaendelea kwa awamu ambapo mita 900 zimekamilika.

**64. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105), taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Businde – Murongo (km 53.4) zipo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kusaini Mkataba.

**65. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 145), ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nanganga – Ruangwa (km 53.2) umefikia asilimia

83 na kwa sehemu ya Ruangwa – Nachingwea (km 55.7) umefikia asilimia 3. Kwa sehemu ya Nangurukuru – Liwale (km 210), taratibu za ununuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Choya – Liwale (km 72) zipo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kusaini Mkataba. Vilevile, katika barabara ya Masasi – Nachingwea (km 45), mkataba 24 wa EPC+F umeboreshwa na kuwa Sanifu Jenga (Design and Build) na kuanza ujenzi wa barabara hii kwa awamu kwa kuanzia sehemu ya Liwale – Kihangara (km 55) ambapo mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kutumia fedha za ndani.

**66. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.1), ujenzi wa sehemu ya Isongole II – Ndembo (km 46) na Ndembo Spur Road (km 6) upo katika hatua za awali. Aidha, majadiliano na Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Mlowo – Kamsamba (km 10) yanaendelea. Vilevile, taratibu za ununuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (Iboya OSIS) zinaendelea kwa kuzingatia marejeo ya usanifu.

**67. Mheshimiwa Mwenyekiti**, taratibu za kusaini mkataba kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21) zinaendelea. Barabara hii itajengwa na Makandarasi Wanawake ikiwa ni mkakati wa kuwajengea uwezo. Aidha, kwa sehemu ya Chang'ombe – Mkwajuni – Makongolosi (km 61), majadiliano na Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya kilometa 5 kuanzia Mkwajuni – Makongolosi yanaendelea.

**68. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54).

**69. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Sengerema – Nyehunge (km 54), ununuzi ya kumpata Mkandarasi mpya unaendelea baada ya kusitisha mkataba na Mkandarasi wa awali. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya

Kamanga – Katunguru – Sengerema (km 35) kwa kiwango cha lami.

**70. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa upande wa barabara ya Omurushaka – Nkwenda – Murongo (km 125), ujenzi wa sehemu ya Kyerwa – Chonyonyo (km 50) unaendelea. Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa sehemu iliyobaki ya kilometa 75 zinaendelea.

**71. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa Upanuzi wa barabara Kuu zinazoingia katikati ya Jiji la Dodoma (km 51.2), taratibu za ununuzi ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Morogoro (Kimbinyiko R/ About – Chamwino Jct km 32) zinaendelea. Aidha, kwa barabara ya Dodoma – Iringa (Bahi Rd R/About - Mkonze km 8.5) na Dodoma – Arusha (Bahi Rd R/About – Msalato Airport Jct km 10.7) upembuzi wa awali unaendelea chini ya mradi wa Dodoma Intergrated and Sustainable Transport (DIST).

**72. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct (km 76.07), sehemu ya Ntyuka Jct – Ntyuka (km 8) na Kikombo Jct – Mapinduzi (km 16.4) umefikia asilimia 53. Aidha, ujenzi wa barabara ya Ntyuka – Mvumi Hospital - Kikombo (km 53) upo katika hatua za awali. Vilevile, Usanifu wa Kina wa 26 barabara za Ihumwa – Hombolo - Mayamaya (km 60) unaendelea. Kwa Barabara ya kuingia Hospitali ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) Msalato (km 5.5) taratibu za ununuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea.

**73. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara ya Tarime – Mugumu (km 87.14) kwa kiwango cha lami, sehemu ya Mogabiri – Nyamongo (km 25) unaendelea na umefikia asilimia 54. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu za Tarime – Mogabiri (km 9.3), Nyamongo – Mugumu (km 48.15) na Barabara unganishi ya Mugumu Roundabout (km 3.6) ameshakabidhiwa eneo la mradi na hivi sasa anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi. Kwa upande wa barabara ya Mika – Utegi – Shirati – Kirongwe (km 56.8), zabuni za ujenzi sehemu ya Utegi – Shirati (km 27)

zimetangazwa na tathmini ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea.

**74. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Shelui – Nzega (km 123) unaendelea. Aidha, taratibu za ununuzi kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Shelui – Sekenke – Tulya – Tyegelo (km 62); sehemu ya Shelui – Sekenke – Ntwike (km 20) zinaendelea.

**75. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65), kwa sehemu ya Kagongwa – Sojo (km 18) Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina umekamilika. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 50); sehemu ya 27 Isabdula – Bukwimba Station (km 10) umefikia asilimia 5. Vilevile, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 136); sehemu ya km 3 kutoka Mwanangwa unaendelea na umefikia asilimia 40.

**76. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Mafinga – Mgololo (km 81), mkataba wa EPC+F umeboreshwa na kuwa Sanifu Jenga (Design and Build). Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kutumia fedha za ndani. Aidha, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Nyololo – Mtwango (km 40.4) umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

**77. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Singida – Sepuka – Ndago (km 77.4) unaendelea.

**78. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 90.0) pamoja na daraja la Mnywamaji, ujenzi wa barabara hii sehemu ya Amanimakoro – Ruanda (km 35) unaendelea na umefikia asilimia 37. Aidha, Mkandarasi wa sehemu ya Ruanda – Ndumbi Port (km 50) ameshakabidhiwa eneo la mradi na hivi sasa anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

**79. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara za Kuelekea Katika Vituo vya Reli ya Kisasa ya SGR (km 87.6), ujenzi wa barabara ya Kizota – Zuzu SGR Station (km 14) unaendelea na umefikia asilimia 77. Vilevile, ujenzi wa barabara za Morogoro – Kihonda SGR Station (km 10) na Rudewa – Kilosa SGR Station 28 (km 3) upo katika hatua za awali. Aidha, taratibu za ununuzi katika barabara za Gulwe – Gulwe SGR Station (km 2), Igandu – Igandu SGR Station (km 27), Ihumwa – Ihumwa Marshalling Yard (km 5.50), Bahi – Bahi SGR Station (km 4) na barabara za ndani za kituo cha SGR cha Dodoma (Access Roads to Dodoma SGR Station) zinaendelea. Katika barabara ya Mlandizi – Ruvu SGR Station (km 22) Mkataba wa ujenzi upo tayari kusainiwa.

**80. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (km 174.5), ujenzi wa sehemu ya Tanga – Pangani (km 50) unaendelea na umefikia asilimia 77. Ujenzi wa sehemu ya Pangani – Mkange (km 124.5) sehemu ya Tungamaa – Mkange (km 95.2) umefikia asilimia 47 na ujenzi wa daraja la Pangani umefikia asilimia 55. Aidha, kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Mkata – Kwa Msisi (km 36) inaendelea.

**81. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara ya Kisarawe – Maneromango – Mloka (km 150.46) sehemu ya Kisarawe - Maneromango (km 54) kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2025 kilometa 24.25, ujenzi kwa kiwango cha lami, sehemu ya Kisarawe – Sungwi – Kisanga (km 27.65) umekamilika. Aidha, kwa sehemu ya Sungwi – Masaki (km 2.1) ujenzi umefikia asilimia 25. Vilevile, mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Masaki – Maneromango (km 34.5) unatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa mwezi Mei, 2025.

**82. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 120), hadi kufikia Aprili, 2025 ujenzi sehemu ya Kahama - Bulyanhulu Jct – 29 Kakola (km 73) umefikia asilimia 7. Aidha, mkataba kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Geita – Bukoli (km 57.4) na barabara ya kuingia mji wa Bukoli (km 3.8) unatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa mwezi Mei, 2025. Vilevile, taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Nyikonga – Kashelo (km 10.5), Kashelo –

Ilolangulu (km 15) na Ushirombo – Kilimahewa – Nanda (km 15.7) zinaendelea.

**83. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50); kwa sehemu ya Nyamirembe Port – Nyamirembe Jct (km 1.7) ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea na umefikia asilimia 25. Kwa sehemu ya SIDO – Chato Zonal Hospital (km 5.3) ujenzi umefikia asilimia 12.

**84. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Barabara ya Geita – Nzera - Nkome (km 54); sehemu ya Sungusila - Nzera – Nkome (km 20.36) ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami upo katika hatua za awali.

**85. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 199.51), ujenzi wa barabara ya Mianzini – Ngaramtoni (km 18) umefikia asilimia 48. Aidha, kazi ya Usanifu wa Kina wa barabara ya Tengeru – USA River (km 9.3), Daraja Jipya la Kikafu (m 560) pamoja na Barabara Unganishi (km 4.06) na Barabara za Moshi Mjini (km 8.4) inaendelea.

**86. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa ujenzi wa barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji, ujenzi wa barabara ya Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78) kwa 30 kiwango cha lami upo katika hatua za awali. Katika barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11), ujenzi kwa kiwango cha lami umeanza.

**87. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 178); sehemu ya Ngerengere – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 166.4) kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea. Vilevile, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina katika barabara ya Chalinze – Utete (km 354.9) zipo katika hatua za mwisho. Aidha, kazi za matengenezo ya barabara za Maneromango – Vikumburu – Mloka (km 100) na Kibiti – Mloka – Mtemele – Rufiji JNHHP (km 203) kwa kiwango cha changarawe zinaendelea.

**88. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi za ukarabati (overlay) wa sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24) zinaendelea. Ukarabati kwenye Barabara ya Msoga – Msolwa (km 10.2) (Chalinze Bypass) sehemu ya km 7 unaendelea na umefikia asilimia 80. Aidha, kwa sehemu ya Kibaha – TAMCO (km 4.5) maandalizi ya kutafuta Mkandarasi wa upanuzi wa sehemu hii kwa kiwango cha lami zinaendelea ambapo Mhandisi Mshauri yupo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha usanifu pamoja na nyaraka za zabuni.

**89. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa upande wa barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 118.10), ukarabati na upanuzi wa sehemu ya Tegeta/Kibaoni – DAWASA/Basihaya (km 2.9) unatekelezwa kupitia mradi wa ujenzi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Nne (BRT IV). Serikali inaendelea kutafuta fedha za 31 ukarabati na upanuzi wa sehemu ya DAWASA/Basihaya – Bagamoyo (km 47).

**90. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara za Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel (km 141) kwa sehemu za Rulenge – Kabanga Nickel (km 32), Kumubuga – Rulenge – Murusagamba (km 75) na Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34), Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami.

**91. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 265), ujenzi wa sehemu ya Uvinza – Malagarasi (km 51.1) umefikia asilimia 77.

**92. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (km 346.43), Makandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za Ifakara – Mbingu (km 62.5) na Mbingu – Chita JKT (km 37.5) wameshakabidhiwa maeneo ya mradi na hivi sasa wanaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi. Katika Barabara ya Njombe (Kibena) – Lupembe – Madeke (km 126); Sehemu ya Kibena – Kidegembye (km 42) taratibu za ununuzi ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zipo katika hatua za mwisho. Aidha, Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu ya Kihansi – Mlimba – Madeke (km 95.26).

**93. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389), kazi za ujenzi wa sehemu ya Mbulu – Garbabi (km 25) zimefikia asilimia 28. Vilevile, Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu 32 ya Labay – Haydom (km 25) ameshakabidhiwa eneo la mradi na hivi sasa anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi. Aidha, katika sehemu ya Nkoma – Lalago (km 65), mkataba wa EPC+F umeboreshwa na kuwa Sanifu Jenga (Design and Build). Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kutumia fedha za ndani. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mogitu – Haydom (km 68).

**94. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga /Bomang'ombe – Sanya Juu (km 105.16), sehemu ya Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16), ujenzi wa daraja la Kikafu Juu (m 25) na barabara unganishi (m 400) upo katika hatua za awali. Kwa upande wa barabara ya Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8) ujenzi unaendelea kwa awamu ambapo jumla ya km 6 zimekamilika na kilometa 1 ipo katika hatua za ununuzi. Aidha, Mikataba ya ujenzi wa sehemu ya Sanya Juu – Kamwanga (Elerai – Kamwanga (km 39.5) na barabara ya Tarakea – Holili (km 53); sehemu ya Munga – Kitangara Mrere (km 10) inatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa mwezi Mei, 2025. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya Bomang'ombe – Sanya Juu (km 25).

**95. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 60.6), Makandarasi wa ujenzi wa sehemu za Katumba – Lupaso (km 35.3) na Mbaka – Kibanja (km 20.7) wameshakabidhiwa maeneo ya mradi na hivi sasa wanaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Mbambo – Ipinda (km 19.7).

**96. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi wa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara ya Kuingia Manyoni Mjini (km 4.8) umekamilika. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station –

OSIS) cha Muhalala (Manyoni). Mkataba wa awali wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa OSIS umesitishwa kutokana na changamoto za kimkataba ambapo utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia 50. Ujenzi utaendelea baada ya kufikia makubaliano ya stahiki za pande zote mbili. Rasimu ya makubaliano ya stahiki za pande zote mbili imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi (vetting).

**97. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo (km 114) unafanyika kwa awamu, ambapo ujenzi wa sehemu ya km 1 kutoka kijiji cha Uduka umekamilika. Taratibu za ununuzi sehemu ya mita 400 zipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba.

**98. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8) kwa kiwango cha lami.

**99. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 141), Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72) kwa kiwango cha lami.

**100. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107), ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) sehemu ya Matai – Tatanda (km 25) unaendelea na umefikia asilimia 42 na ujenzi wa sehemu ya Tatanda – Kasesya (km 25) upo katika hatua za awali.

**101. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025, katika mradi wa Ujenzi wa Madaraja Makubwa, ujenzi wa daraja la Mbambe umefikia asilimia 26, Mbangala asilimia 67, Mirumba asilimia 20, Simiyu asilimia 42, Doma asilimia 7, Nzali asilimia 7, Chakwale asilimia 18, Nguyami asilimia 10, Mitomoni asilimia 7 na Sukuma asilimia 33.1. Aidha, ujenzi wa barabara unganishi katika Daraja la Sibiti (Singida) umefikia asilimia 6.

Vilevile, Makandarasi wa ujenzi wa Madaraja ya Mpiji Chini, Kibakwe, Kerema Maziwa, wanaendelea na maandalizi ya ujenzi. Mikataba ya ujenzi wa madaraja ya Sanza, Godegode ipo katika

hatua za mwisho za kusainiwa. Usanifu wa Kina wa madaraja ya Munguli na Malagarasi Chini umekamilika. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa daraja la Kirumi na ujenzi wa daraja la Mtera Dam. Aidha, ujenzi wa daraja la Suguti utatekelezwa kupitia mradi wa TANTIP.

**102. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.10), ujenzi wa sehemu ya Bugene – Kasulo – Kumunazi & Kyaka – Mutukula (km 124) sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60) unaendelea na umefikia asilimia 41.

**103. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242), kazi za ukarabati wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 92) zinaendelea na zimefikia asilimia 20. Kwa upande wa ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Nyakanazi, mkataba wa awali umesitishwa kutokana na changamoto za kimkataba. Ujenzi utaendelea baada ya ya kufikia makubaliano ya stahiki za pande zote mbili. Rasimu ya makubaliano ya stahiki za pande zote mbili imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi (vetting). Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nyakasanza – Kobero (km 58).

**104. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Usanifu wa Kina kwa ajili ya ajili ya ukarabati wa barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102) kwa kiwango cha lami umekamilika. Hatua za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa upanuzi wa sehemu ya Mwanza - Usagara - JPM Bridge (km 37) kutoka njia mbili hadi njia nne zinaendelea.

**105. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/25 kwa ajili ya miradi ya Barabara za Mikoa ni ukarabati wa jumla ya kilometa 600 kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa 60 kwa kiwango cha lami na ujenzi wa Madaraja/Makalavati 70. Hadi kufikia Aprili, 2025, kilometa 117.50 za barabara za mikoa zilikuwa zimekarabatiwa kwa kiwango cha changarawe na kilometa 70.22 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa madaraja/makalavati 7

umekamilika na yaliyobaki 63 yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**106. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam, taratibu za ununuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya upanuzi wa Barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1) na ujenzi wa barabara za Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 27); sehemu ya km 10 na Mbezi Victoria – Magoe Mpiji (km 9.55); sehemu ya km 6.55 zinaendelea.

**107. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara ya Goba – Matosa – Temboni (km 6) unaendelea kufanyika kwa awamu ambapo kilometa moja (1) imekamilika na ujenzi wa kilometa 5 unaendelea. Vilevile, upanuzi wa barabara ya Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry (km 25.1) unaendelea kwa km 1.4 na umefikia asilimia 80, ujenzi wa barabara za Kipata (m 700), Livingstone (m 350) na Msikitini – Sharif Shamba (km 1) unaendelea na umefikia asilimia 85, Kibamba Shule – Mpiji Magoe (km 9.2) umefikia asilimia 95, Chanika – Mbande (km 3.8) umefikia asilimia 75, Mbezi Msakuzi – Makabe Jct (km 8.36) asilimia 90 na Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi (km 6.73) unaendelea na umefikia asilimia 13.

**108. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kolandoto – Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 122) kwa awamu.

**109. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa barabara ya Ndundu – Somanga (km 60), ujenzi wa barabara ya Utete – Nyamwage (km 33.7) unaendelea na umefikia asilimia 9. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu za Kongowe – 37 Malendego (km 160.65) na Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95).

**110. Mheshimiwa Mwenyekiti**, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu Mjini (km 68) unaendelea na umefikia asilimia 84.

**111. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa upande wa mradi wa barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2 - km 112.3), ujenzi wa sehemu ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3) unaendelea na umefikia asilimia 86 na ujenzi wa sehemu ya Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60) umefikia asilimia 82.

**112. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mzunguko wa Ndani katika Jiji la Dodoma: Bahi R/About – Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3), majadiliano na Serikali ya Japan kuhusu ugharamiaji wa ujenzi wa barabara hii yanaendelea. Vilevile, kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Dodoma City Middle Ring Road inayoanzia Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Mkonze – Ntyuka – Nanenane (km 47.2) umekamilika. Aidha, kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Msalato – Mtumba – Chamwino IKULU (km 30) inaendelea.

**113. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa upande wa barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499), kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Kidatu – Ifakara 38 (km 66.9) na ujenzi kwa kiwango cha changarawe wa barabara za kuelekea mashamba ya wakulima wa miwa ya Mbigiri (km 50) zimekamilika. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Chalinze – Magindu – Lukenge – Seregete B – Kabwe Jct – Mkulazi (km 77.50).

**114. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 365.36), ujenzi wa barabara ya Mpanda Airport – Kasimba Jct (km 3) umekamilika.

**115. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 185), hadi Aprili, 2025, kazi za ujenzi wa sehemu ya Sanzate – Natta (km 40) zimefikia asilimia 55. Aidha, mkataba wa ujenzi wa barabara ya Wasso – Loliondo (km 10) unatarajiwa kusainiwa mwishoni wa mwezi Mei, 2025. Taratibu za ununuzi za kuwapata Makandarasi wa barabara za Mto wa Mbu – Selela (km 23) na Ngaresero – Engaruka (km 39) kwa kiwango cha lami zinaendelea. Vilevile,

Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Natta – Mugumu (km 45).

**116. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa Ibanda – Itungi Port/Kajunjumele – Kiwira Port (km 32), kazi za ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (OSBP) cha Kasumulu/Songwe (Tanzania/Malawi Border) unaendelea na umefikia asilimia 95. Aidha, ukarabati wa barabara ya Ibanda – Itungi Port (km 26) na Kajunjumele (Iponjola) – Kiwira Port (km 6) umefikia asilimia 2 na taratibu za ununuzi ya Mkandarasi mpya zinaendelea baada ya kusitishwa kwa mkataba wa awali kutokana na utendaji usioridhisha wa Mkandarasi.

**117. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 803.6), ujenzi wa barabara ya Mpanda – Mishamo – Uvinza; Sehemu ya Vikonge – Uvinza (km 159) kazi za ujenzi wa barabara hii sehemu ya Vikonge – Luhafwe (km 25) zinaendelea na zimefikia asilimia 60 na ujenzi wa sehemu ya Luhafwe – Mishamo/Bulamata Jct (km 37.35) unaendelea na umefikia asilimia 15. Kwa barabara ya Kibaoni – Sitalike (km 71) sehemu ya Kibaoni – Mlele Jct (km 50) ujenzi umefikia asilimia 15 na taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Sitalike – Mlele Jct (km 21) kwa utaratibu wa sanifu na jenga (design and build) zinaendelea.

**118.** Kwa barabara ya Kagwira – Ikola – Karema Port (km 112), ujenzi wa sehemu ya Kagwira – Kasekese (km 54.14) umefikia asilimia 5 na Kasekese – Ikola (km 56.91) umefikia asilimia 1. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu za Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86) na Lyazumbi – Kabwe (km 65).

**119. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Nyanguge – Musoma/ Mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 202.25), Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4).

**120. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 152.8), sehemu ya Handeni – Kang'ata (km 30), maandalizi ya nyaraka za zabuni za ujenzi yanaendelea.

**121. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini DSM na Barabara Unganishi, Serikali inaendelea na majadiliano na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) kwa ajili ya ujenzi wa makutano ya barabara kwenye maeneo ya Morocco na Mwenge. Maboresho ya makutano ya Tabata/Mandela yamejumuishwa katika mradi wa BRT V na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya maboresho ya makutano yaliyosalia.

**122. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa (km 172) unatekelezwa kwa awamu ambapo, ujenzi wa daraja la Msula (m 10) na barabara unganishi m 600 unaendelea.

**123. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa upande wa barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25), ujenzi wa sehemu ya Kibondo Junction – Kabingo (km 62.5) umekamilika, Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5) umefikia asilimia 85.8, Mvugwe – Nduta Junction (km 59.35) umefikia asilimia 90.7 na Nduta Junction – Kibondo (km 25.9) umefikia asilimia 87. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kibondo – Mabamba (km 48) unaendelea na umefikia asilimia 31.5.

**124. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa barabara za kuingilia kiwanja cha ndege cha Mafia, maandalizi ya nyaraka kwa ajili ya kutangaza zabuni za ujenzi wa barabara ya Kilindoni – Ras Mkumbi (km 54.4) kwa kiwango cha lami yanaendelea.

**125. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu mradi wa ujenzi wa Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Unganishi (km 46.3), ujenzi wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (Km 41) kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 15.

**126. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 215.8) Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bukoba – Busimbe – Maluku – Kanyangereko – Ngongo (km 19.1) unaendelea.

Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya km 10 za sehemu ya Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7) na Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 112), sehemu ya Muhutwe – Kagoma zinaendelea.

**127. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34), kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Bunju – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma – Kigamboni (km 61) na Mbezi – Mbezi Mwisho – Kifuru – Banana – Kipara – Kigamboni (km 49.0) zinaendelea.Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119) kwa kiwango cha lami.

**128. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Singida – Shelui (km 110) umekamilika. Aidha, ujenzi wa Barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga (Singida) – Mkalama (km 46) kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu ambapo kwa sasa ujenzi wa sehemu ya Kitukutu – Kinampanda (km 7.7) unaendelea na umefikia asilimia 64.

**129. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road), mkataba kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa sehemu ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8) umesainiwa tarehe 19 Machi, 2025 na maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea.

**130. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 535.25), taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Morogoro – Iringa (Tumbaku Jct. Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi) (km 158.45) ziko kwenye hatua za mwisho. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152.0) kwa kiwango cha lami.

**131. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Same – Mkumbara – Korogwe (km 172.5), ujenzi wa sehemu ya Ndungu – Mkomazi (km 36) umefikia asilimia 2.4. Aidha, maandalizi ya kusaini mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Same – Kisiwani – Mroyo (km 56.83) yapo katika hatua za mwisho. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara za Same – Himo (km 76), 43 Mombo – Lushoto (km 32) na ujenzi wa barabara ya Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5).

**132. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa barabara ya Mbeya – Chunya - Makongolosi (km 267.9), ujenzi wa barabara ya Noranga – Itigi – Mkiwa (km 56.9) sehemu ya Noranga – Itigi (Mlongoji) km 25 umefikia asilimia 76, ujenzi wa barabara za Itigi Mjini (km 10) umefikia asilimia 98 na ujenzi wa sehemu ya Noranga – Doroto (km 6) na Itigi – Mkiwa (km 25.6) umefikia asilimia 6. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Makongolosi – Rungwa – Noranga (km 356) na Mbalizi – Makongolosi (km 50).

**133. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211), ujenzi wa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50) kwa kiwango cha zege umefikia asilimia 23.4.

**134. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Handeni – Kibirashi – Kibaya – Njoro – Goima - Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 424.24), ujenzi wa sehemu ya Handeni – Mafuleta (km 20) umefikia asilimia 46 na ujenzi wa sehemu ya Mafuleta – Kileguru (km 30) upo katika hatua za awali. Kwa sehemu ya Kileguru – Singida, ujenzi utatekelezwa kwa utaratibu wa PPP.

**135. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu barabara ya Makambako – Songea na Barabara ya Mzunguko ya Songea (km 295), taratibu za ununuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Lutukila – Songea (km 95) na Mchepuo wa Songea (km 11) zipo 44 katika hatua za mwisho. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Ramadhani – Ilembula Hospital – Iyayi (km 75) na ukarabati wa barabara ya Makambako – Lutukila (km 200) kwa kiwango cha lami.

**136. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu ujenzi wa barabara ya Dodoma – Iringa (km 264), ujenzi kwa kiwango cha lami wa mita 450 za Barabara ya Mchepuo wa Iringa (km 7.3) na ujenzi wa madaraja madogo 7 umekamilika. Aidha, Mkataba wa ujenzi wa sehemu iliyobaki ya Igumbilo – Tumaini Jct (km 6.85) umesainiwa na Mkandarasi yupo katika maandalizi ya kuanza kazi.

Kazi za uimarishaji wa matabaka ya barabara katika barabara ya Iringa – Dodoma (km 264) zinaendelea kwa awamu ambapo jumla ya km 25.3 zimekamilika na uimarishaji wa sehemu ya km 3 zinaendelea. Vilevile, taratibu za ununuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Iringa – Pawaga (km 71.93); sehemu ya Pawaga Jct – Ikonongo (km 5) na Itundu – Ilolo Mpya (km 20) kwa kiwango cha lami zipo hatua za mwisho.

**137. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati (km 263.4) ujenzi wa barabara ya Dareda – Dongobesh (km 60) sehemu ya Dareda Mjini – Dareda Mission (km 8) upo katika hatua za awali. Ujenzi wa barabara ya Miteremko ya Magara (Magara Escarpment - km 15) kwa kiwango cha zege unaendelea ambapo jumla ya km 5 zimekamilika na ujenzi wa sehemu ya mita 700 unaendelea.

**138. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa barabara za Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute (km 8.8), kwa kiwango cha lami unatekelezwa kwa awamu ambapo hadi Aprili, 2025 jumla ya mita 600 zimejengwa.

**139. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu mradi wa Barabara za Igawa – Songwe – Tunduma na Mchepuo wa Mbeya (km 266.9), upanuzi wa sehemu ya Uyole – Ifisi – Songwe Airport (km 36) unaendelea na umefikia asilimia 21.7. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Iwambi – Mbalizi Bypass (km 6.5) kwa kiwango cha lami.

**140. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili hadi Tano (km 69.8), kazi za ujenzi wa barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (CBD – Mbagala, km 20.3) zimekamilika na ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya

Tatu (CBD – Gongolamboto km 23.33) umefikia asilimia 80. Aidha, ujenzi wa Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Nne (Ali Hassan Mwinyi – Morocco – Mwenge - Ubungo (km 13.5), Mwenge – Tegeta/Basihaya (km 15.6) na ujenzi wa Miundombinu ya Majengo ya Mbuyuni, Simu 2000 na Kivukoni umefikia asilimia 23.4.

**141. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi za maboresho ya miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza, zimefikia asilimia 45. Aidha, maandalizi ya kuanza ujenzi wa Daraja la Jangwani (m 390) pamoja na barabara unganishi (m 710) yanaendelea. Taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Mabasi Yaendayo 46 Haraka Awamu ya Tano, unaohusisha ujenzi wa barabara ya Nelson Mandela kuanzia Ubungo hadi daraja la Mwalimu Nyerere pamoja na barabara ya Tabata kutoka Segerea kupitia Tabata Dampo hadi Mzunguko wa Kigogo katika barabara ya Kawawa (km 27.6) zinaendelea.

**142. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT), ujenzi wa jengo jipya la Taaluma na Utawala ICoT Morogoro unaendelea na umefikia asilimia 50. Aidha, Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), umefikia asilimia 65. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

**143. Mheshimiwa Mwenyekiti**, fedha za Mfuko wa Barabara zinatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara nchini. Katika mwaka 2024/25 ilipangwa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa kilometa 8,451.32 za barabara kuu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Hadi Aprili, 2025 Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa miradi 25 yenye jumla ya km 1,394.06 umekamilika. Miradi mingine 78 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ambapo miradi 32 yenye jumla ya km 2,966.19 ipo katika hatua ya Usanifu wa Kina na miradi 46 yenye jumla ya km 4,091.47 ipo katika hatua ya ununuzi kama ifuatavyo:-

**a. Miradi ambayo Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina umekamilika:**

i. *Barabara ya Singida Urban – Ilongero – Haydom (km 93);*

ii. *Barabara ya Morogoro (Msamvu Round About) – Morogoro Centre – Bigwa Junction (km 10);*

iii. *Barabara ya Simanjiro (Orkesumet) – KIA - Mererani (Sehemu ya Kongwa Ranch - Kiteto - Simanjiro - KIA) (km 119);*

iv. *Barabara ya Nyakato – VETA – Buswelu (km 3);*

v. *Barabara ya Mbamba Bay - Lituhi (km113);*

vi. *Barabara ya Nangurukuru – Liwale (km 230);*

vii. *Barabara ya Goba - Matosa - Temboni/Morogoro Road Jct na Makabe/Mbezi Mwisho - Goba Jct - Msakuzi (km 15);*

viii. *Barabara ya Utete – Nyamwage (km 34);*

ix. *Barabara ya Njia Mbili Kila Upande ya Mwanza – Nyanguge (km 25);*

x. *Barabara ya Njia Mbili Kila Upande ya Arusha - Kisongo (km 9);*

xi. *Barabara ya Kagwira - Ikola – Karema (km 112);*

xii. *Barabara ya Bariadi – Kisesa – Mwandoya – Ngoboko – Mwanhuzi – Sibiti – Mkalama - Iguguno (km 89);*

xiii. *Barabara ya Geita - Nzera - Nkome Port (km 58.3);*

xiv. *Barabara ya Bungu - Nyamisati (km 40.2);*

xv. *Barabara ya Mbulu - Magugu (Mbuyu wa Mjerumani)(km 63);*

xvi. *Barabara ya Kuruya - Kinesi (km 18.42);*

xvii. *Barabara ya Nanenane - Miyuji - Mnadani Sekondari - Ntyuka Jct - Nanenane (km 47.2);*

xviii. *Barabara za Mika - Utegi - Shirati - Ruari Port na Masonga - Kirogwe (km 48.73);*

xix. *Barabara ya Mkuranga – Kisiju (Pwani)(km 39);*

xx. *Barabara ya Kiluvya - Mpuyani (Pwani)(km19.8);*

xxi. *Barabara ya Mkongo 2 – Ikwiriri (km 24.74);*

xxii. *Barabara ya Old Bagamoyo (km 43.17);*

xxiii. *Barabara ya Puge – Ndala – Ziba – Choma (km 109);*

xxiv. *Barabara za Maingilio za TISS (km 3.5); na*

xxv. *Barabara ya Mzunguko wa Mji wa Tunduma (km 27).*

**b. Miradi ambayo Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina unaendelea:**

i. *Sehemu ya Barabara ya Mlima Kitonga (km 10);*

ii. *Barabara ya Morogoro (Tumbaku Jct) - Mangae/Melela - Mikumi - Iyovi pamoja na Daraja la Doma (km156);*

iii. *Barabara ya Mbalizi - Mkwajuni (Sehemu ya Galula – Mkwajuni - Makongolosi) (km 61);*

iv. *Barabara ya Bariadi – Salama – Ng'haya – Magu (km 76);*

v. *Daraja la Bujonde;*

vi. *Barabara ya Old Korogwe-Kwandolwa-Magona1Mabokweni (km 127.54);*

vii. *Barabara ya Longido - Siha (km 56), (Sehemu ya Longido – Tingatinga, km 38);*

viii. *Barabara ya Tengeru – Mererani (km 28);*

ix. *Barabara ya Katesh - Haydom (km 68);*

x. *Barabara ya Kimotorok - Sukuro - Terati/Rotiana (km128);*

xi. *Barabara ya Nyankanga - Rung'abure (km 91);*

xii. *Barabara za Mjini Geita (Mtakuja - Buhalahala) sehemu ya barabara kuu ya Nyamuhama - Bwanga - Ibanda (T003) (km 24);*

xiii. *Barabara ya Nyakahanga - Nyabiyonza - Nyakakika (km 96);*

xiv. *Barabara ya Katumba - Kafwafwa - Kyimo (km21.98);*

xv. *Barabara ya Mbalizi - Shigamba (km 52);*

xvi. *Barabara ya Ihumwa - Hombolo - Mayamaya (km55);*

xvii. *Barabara ya Sanya Juu (Nyumba Moja) - Longido 56km (Sehemu ya Nyumba Moja - Tingatinga (km 15);*

xviii. *Barabara ya Ngongo - Mandawa - Chukuani km 85);*

xix. *Barabara ya Gairo – Nongwe (km 55.54);*

xx. *Barabara ya Miyombo - Lumuma – Kidete (km 71);*

xxi. *Barabara ya Mtama - Mkwiti - Newala (km 74);*

xxii. *Barabara ya Fulo – Nyambiti – Mallya (km73);*

xxiii. *Barabara ya Busisi – Nyang'wale (km 55);*

xxiv. *Barabara ya Inyonga – Ilunda – Kishelo – Kitunda (km163);*

xxv. *Barabara ya Mandera – Mkange - Saadani (km 63);*

xxvi. *Barabara ya Chimala - Matamba – Kitulo (km 51);*

xxvii. *Barabara ya Katumba - Songwe - Kasumulu - Ngana - Ileje (km 60)*

xxviii. *Barabara ya Katoma - Kanyigo - Bukwali (km 38.83);*

xxix. *Barabara ya Newala - Makong'onda - Mbuyuni (km 42);*

xxx. *Barabara ya Mutukula - Kakunyu (Barabara ya Usalama) (km 56);*

xxxi. *Barabara ya Tutuo - Usoke (km 69); na*

xxxii. *Barabara ya Balili - Mugeta Chini (km 41.4).*

**c. Miradi ambayo ipo katika taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina:**

i. *Barabara ya Mpanda - Ugalla - Kaliua - Ulyankulu – Kahama (km 457);*

ii. *Barabara ya Omurushaka - Murongo (km 125);*

iii. *Barabara ya Kibaha - Mlandizi - Chalinze (km 75);*

iv. *Barabara ya Chalinze-Manga (km 93);*

v. *Barabara ya Ikungi (Singida) - Londoni - Kilimatinde (Solya) (R431) (km117.9);*

vi. *Barabara ya Nyankumbu - Kharumwa - Nyang'holongo - Kahama (km 149);*

vii. *Mpango Kabambe wa Mtandao wa Barabara (National Road Network Master Plan);*

viii. *Barabara ya Bariadi - Kisesa - Mwandoya - Ngh'oboko (km 102);*

ix. *Daraja la Sanga;*

x. *Barabara ya Kisarawe - Bwawa la Mwalimu Nyerere (km 187);*

xi. *Barabara ya Longido - Kitumbeine – Oldonyolengai (km 98);*

xii. *Barabara ya Makutano (Zerozero) - Sirari (km 83) na Barabara ya Maingilio ya Tarime (5.4Km);*

xiii. *Barabara ya Nachingwea - Liwale - Ilonga - Mwaya - Mahenge (km 345);*

xiv. *Barabara ya Usagara – Kigongo na Busisi – Sengerema (km 56);*

xv. *Barabara ya Manyoni - Heka - Ikasi - Chaliingongo (Singida/Dodoma Brd) - Kipanga - Kidiho - Bihawana Junction (km 192);*

xvi. *Barabara ya Singida (Magereza) - Mtunduru - Iyumbu (km 113);*

xvii. *Barabara ya Mambali – Bukumbi - Ishilimulwa – Shitage – Kahama (km105);*

xviii. *Barabara ya Makutano ya Umba – Makutano ya Mkomazi Junction (km 82.24);*

xix. *Barabara ya Bombomtoni – Makutano ya Umba (km 46.33);*

xx. *Barabara ya Maneromango - Vikumburu - Mloka – Geti la Mtemela (km 105);*

xxi. *Barabara ya Mwandiga - Chankele - Mwangogo – Kagunga (km 60);*

xxii. *Barabara ya Laela - Mwimbi – Kizombwe (km 98);*

xxiii. *Barabara ya Simbo - Ilagala – Kalya (km 234);*

xxiv. *Barabara ya Kalambanzite - Ilemba (km 26);*

xxv. *Barabara ya Chenene - Itiso – Izava R.464 (km 72.81);*

xxvi. *Barabara ya Ilula - Kilolo (km 91);*

xxvii. *Barabara ya Rwamishenye - Kyakailabwa (km 3.06);*

xxviii. *Barabara ya Kigarama - Mabira - Kyerwa (km 50.95);*

xxix. *Barabara ya Rutenge - Rubale – Kishoju (km74.06);*
xxx. *Barabara ya Kwasadala - Kware - Lemira (km 15);*

xxxi. *Barabara ya Mugumu - Fort Ikoma (km 30);*

xxxii. *Barabara ya Musoma - Makutano Chini (T17) (km 0.5);*

xxxiii. *Barabara ya Ilongo - Usangu (km 36.85);*

xxxiv. *Barabara ya Iyogwe - Chakwale - Ngilori (km 41.7);*

xxxv. *Barabara ya Kitama - Litehu - Matipa (km 58);*

xxxvi. *Barabara ya Magu - Mahaha (km 51.3);*

xxxvii. *Barabara ya Bukonyo - Murutunguru - Bukongo (km 6);*

xxxviii. *Barabara ya Ngudu – Mallya (km 24);*

xxxix. *Barabara ya Mzunguko ya Njombe (km 22);*

xl. *Barabara ya Ikonda - Lupila – Mlangali (km 78.84);*

xli. *Barabara ya Kasansa - Muze (km 31.3);*

xlii. *Barabara ya Segera - Tanga Harbours (km 74);*

xliii. *Barabara ya Ngiloli - Chakwale - Iyogwe - Tunguli - Kwekivu (km 70);*

xliv. *Barabara ya Bulamata - Mishamo (km 90);*

xlv. *Barabara ya Kwaluguru - Songe – Kiberashi (km125.13); na*

xlvi. *Barabara ya Mwembe - Myamba - Ndungu (km 90.10).*

**144. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kupitia mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Kitengo cha Utafiti (Research Development Unit - RDU) Katika Kupima Vifaa vya Ujenzi na Kuanzisha Teknolojia ya Kisasa ya Asphalt Mix Design, kazi iliyofanyika ni kuboresha mfumo wa usimamizi wa maabara za upimaji ikiwa ni pamoja na kununua vifaa.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko.**

**145. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) inasimamia uendeshaji wa vivuko nchini. Hadi Aprili, 2025, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko na miundombinu ni kama ifuatavyo:

**146. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi iliyokamilika ni ujenzi na upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam awamu ya

l. Mradi mwingine 53 uliokamilika ni Maboresho ya Mifumo ya tiketi za kielektroniki katika kituo cha Magogoni-Kigamboni.

**147. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi mingine inayoendelea ni pamoja na maandalizi ya utekelezaji wa awamu ya pili ya upanuzi wa maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni. Mradi wa usimikaji mfumo wa kielektroniki wa udhibiti matumizi ya mafuta katika vivuko 19 vya MV Kazi, MV Kigamboni, MV Kilindoni, MV Misungwi, MV Sengerema, MV Mwanza, MV Sabasaba, MV Ilemela, MV Mara, MV Chato II, MV Tegemeo, MV TEMESA, MV Kome II, MV Musoma, MV Ujenzi, MV Tanga, MV Pangani II, MV Kilambo na MV Mafanikio umefikia asilimia 80.

**148. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni ujenzi wa maegesho ya Mayenzi – Kanyinya (asilimia 80), Ijinga – Kahangala (asilimia 48), Buyagu – Mbalika (asilimia 47), Bwiro – Bukondo (asilimia 97), Kisorya – Rugezi (asilimia 35), Ilunda – Luchelele (asilimia 30) na Bukimwi (asilimia 35). Aidha, ujenzi wa maegesho ya Chato, Kikumbaitale, Zumacheli na Nkome (Chato – Nkome) umefikia asilimia 60. Mikataba ya ujenzi wa maegesho ya Nyakaliro-Kome na miundombinu ya vituo vya Nyakarilo – Kome na Bugorola – Ukara imesainiwa tarehe 29 Januari, 2025. Miradi ya ujenzi wa maegesho ya Magogoni – Kigamboni, Muleba – Ikuza, Kilambo – Namoto na Kamanga – Kirumba Mwaloni upo kwenye hatua ya ununuzi.

Vilevile, ujenzi wa maegesho ya Rusumo – Nyakiziba na Rugasa pamoja na ukarabati wa maegesho ya Kasharu – Buganguzi upo katika hatua ya usanifu. Aidha, ujenzi/ukarabati wa miundombinu katika vituo 54 vya Ilunda – Luchelele, Buyagu – Mbalika, Ijinga – Kahangala, Kahunda – Maisome na Bezi – Bukimwi ipo katika hatua ya usanifu.

**149. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025, kwa upande wa miradi ya ununuzi/ujenzi wa vivuko, ujenzi wa vivuko vipya sita (6) umefikia hatua zifuatazo; Bwiro-Bukondo (asilimia 92), Kisorya-Rugezi (asilimia 90), Ijinga - Kahangala (asilimia 90), Nyakaliro-Kome (asilimia 90), Buyagu – Mbalika (asilimia 81) na Nyamisati – Mafia (asilimia 35).

**150. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kuhusu miradi ya Ukarabati wa Vivuko, hadi Aprili, 2025, ukarabati mkubwa wa vivuko uko katika hatua zifuatazo: MV Kilombero II (asilimia 90), MV Nyerere (asilimia 81), MV Magogoni (asilimia 62) na MV Ukara I (asilimia 20). Mradi wa ukarabati mkubwa wa kivuko MV Kigamboni na MV Pangani II upo katika hatua za awali. Aidha, mkataba ya utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa vivuko na MV Mafanikio umesainiwa. Ukarabati wa vivuko MV Mwanza, MV Ukara II, MV Sabasaba, MV Malagarasi pamoja na boti ya uokoaji (Rescue Boat SAR II) vipo hatua ya ununuzi. Utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa MV Kome II unasubiri kupatikana kwa kivuko mbadala.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

**151. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali.

**152. Mheshimiwa Mwenyekiti**, utekelezaji wa Awamu ya II ya ujenzi wa nyumba 150 za watumishi wa Umma jijini Dodomaeneo la Nzuguni umefikia asilimia 40. Ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi wa Umma katika eneo la Magomeni Kota Awamu ya II "Block B" umekamilika. Aidha, ujenzi unaendelea kwa jengo C ambao umefikia asilimia 37 na jengo D ujenzi umefikia asilimia 22.

Ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi wa Umma za Temeke Kota Jijini Dar es Salaam umefikia asilimia 40 na Ghana Kota "Block II", Jijini Mwanza umefikia asilimia 25. Vilevile, TBA inasimamia ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara za Ujenzi na Uchukuzi katika Mji wa Serikali - Mtumba jijini Dodoma ambao umefikia asilimia 73.5.

**153. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa ukarabati wa nyumba 40 za Viongozi jijini Dodoma uliohusisha nyumba kumi na moja (11), utekelezaji unaendelea ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 nyumba saba (7) umekamilika. Aidha, ukarabati wa nyumba tatu (4) unaendelea na umefikia asilimia 28. Utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa nyumba 30 za Viongozi mikoani unaendelea

ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 ukarabati wa nyumba sita (6) umekamilika katika maeneo ya Oysterbay na Kijitonyama Jijini Dar es Salaam. Aidha, hadi Aprili, 2025 utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI katika mikoa 20 zilizohamishiwa TBA unaendelea. Katika mradi huo kwa mwaka 2024/25 nyumba 50 zilizopo mikoa ya Kagera –18 (asilimia 20), Njombe - 19 (asilimia 80) na Songwe - 13 (asilimia 45) zinakarabatiwa.

**154. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi mwingine unaotekelezwa ni Ujenzi na Ukarabati wa Karakana za TEMESA na TBA katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam, Tabora, Morogoro na Arusha. Hadi Aprili, 2025, ukarabati wa karakana za samani mbili (2) za TBA katika Mikoa ya Mwanza na Dar es Salaam unaendelea na umefikia asilimia 40 na 70 mtawalia.

**155. Mheshimiwa Mwenyekiti**, utekelezaji wa miradi ya ukarabati wa Karakana za Matengenezo ya Magari za TEMESA umefikia hatua ifuatayo; karakana ya Mkoa wa Tabora (asilimia 85), Kigoma na Mwanza (asilimia 75), Arusha (asilimia 61), Mara (asilimia 45), Mtwara (asilimia 43), Dodoma (asilimia 28). Aidha, ukarabati wa karakana za mikoa ya Ruvuma na Mbeya upo katika hatua za awali. Vilevile, ukarabati wa karakana za MT Depot awamu ya II, Lindi, Kagera na Tanga, pamoja na karakana ya mitambo Morogoro upo katika hatua ya usanifu.

**156. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi wa Ujenzi wa karakana mpya ya kisasa ya Dodoma upo katika hatua ya usanifu.

**157. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa Majengo Tanzania imehuishwa kupitia GN Na. 595 ambayo inaruhusu Wakala kuhusisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi yake pamoja na kuwauzia na kuwapangisha nyumba wasio watumishi wa umma kwa bei ya soko. Aidha, Wakala umeainisha maeneo yake oevu yaliyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Mwanza kwa ajili ya kuyaendeleza kwa njia ya ubia pamoja na mikopo kutoka Taasisi za kifedha. Kufuatia kuhuisha Sheria hiyo, Wizara inategemea kupungua kwa changamoto 57 za makazi kwa Watumishi wa Umma na kuiwezesha kupata mapato

yatakayopelekea Wakala kujiendesha na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini katika utekelezaji wa miradi ya nyumba za makazi.

**Udhibiti Uzito wa Magari, Masuala ya Usalama Barabarani na Mazingira**

**158. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kuboresha usalama barabarani, Wizara ya Ujenzi kupitia TANROADS imefanya ukaguzi wa usalama barabarani (Road Safety Audit) ili kutambua maeneo hatarishi na kuyafanyia maboresho. Wizara kupitia TANROADS imeweka alama na michoro muhimu ya barabarani na kufunga taa za kuongoza watumiaji wa barabara (traffic signals) katika makutano ya barabara pamoja na taa za barabarani (street lights) katika maeneo mbalimbali ya miji.

**159. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kupambana na ajali zinazosababishwa na uchovu wa madereva, Wizara kupitia TANROADS inafanya usanifu wa kujenga maeneo ya kupumzika. Vituo vilivyopangwa kujengwa kwa upande wa Ushoroba wa Kati ni Muhalala (Manyoni) na Nyakanazi (Kagera) na ushoroba wa Dar es Salaam-TANZAM vitakuwa maeneo ya Vigwaza (Pwani), Ruhaha Mbuyuni (Morogoro), Idofi (Makambako) na Iboya (Songwe) na kwa upande wa ushoroba wa Kaskazini vituo hivyo vitajengwa maeneo ya Segera (Tanga) na Himo (Kilimanjaro).

**160. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi nyingine zilizofanyika ni kutoa elimu ya usalama barabarani kwa jumla wananchi 18,906 Tanzania Bara, ikiwemo wanafunzi 58 wa shule za msingi na sekondari ili kupunguza ajali za barabarani. Aidha Wizara kwa kushirikiana na TANROADS imetoa elimu kuhusu maombi ya vibali vya mizigo maalum na kudhibiti uzito wa magari kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti Uzito ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2018. Elimu hii imetolewa kwa wasafirishaji mbalimbali na watumishi wa mizani katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Kigoma na Tabora.

**161. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mkutano Mkuu wa 4 wa Mawaziri wanaohusika na masuala ya Usalama Barabarani kutoka Mataifa mbalimbali Duniani uliofanyika nchini Morocco

mnamo tarehe 17 Februari 2025. Wizara kupitia Wakala ya Barabara (TANROADS) ilipokea tuzo ya heshima katika mashindano ya Kimataifa ya Usalama wa Miundombinu ya barabara inayoitwa 'iRAP Gary Liddle Memorial Trophy' kutokana na Mchango wa Wakala (TANROADS), katika kuboresha usalama wa miundombinu ya barabara nchini ili kupunguza ajali za barabarani na kuhakikisha usalama wa watumiaji wote wa barabara. Tuzo hii imetoa motisha kubwa kwa TANROADS kuendelea kuimarisha usalama wa miundombinu ya barabara kuu na za mikoa ili kufikia lengo la Umoja wa Mataifa (UN Decade of Action 2021-2030) la kupunguza ajali kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2030.

**162. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Mradi wa Usalama Barabarani, Wizara kupitia TANROADS inaendelea na ujenzi wa Mizani ya Kizengi (Tabora) ambao umefikia asilimia 46 na Mizani ya Igagala asilimia 50. Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kupata Mkandarasi atakayefunga mizani ya kisasa 32 yenye uwezo wa kupima uzito wa magari yakiwa kwenye 59 mwendo (Weighing in Motion System - WIMS) zinaendelea. Mizani hii ya kisasa itajengwa katika mikoa ya Njombe, Mbeya, Singida, Tabora, Shinyanga, Kagera, Mwanza, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Lindi, Ruvuma na Kagera. Vilevile, Wizara kupitia TANROADS inajenga mizani ya kupima gari kwa kutumia kundi la mitaimbo kwa wakati mmoja (Group of axle weighbridge) ili kupunguza muda wa kupima uzito wa magari na msongamano katika vituo vya mizani vya Ilolanguru (Tabora), Makambako North (Njombe) na Ndumbwe (Mtwara).

**163. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara kupitia TANROADS inaendelea na taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi atakayefunga mfumo wa Kamera za CCTV na taarifa za vipimo vya uzito wa magari katika mizani 58.

**164. Mheshimiwa Mwenyekiti**, uthamini kwa ajili ya kulipa fidia ili kupisha ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Iboya (Songwe) na Himo (Kilimanjaro) umekamilika na hivi sasa Serikali ipo katika hatua ya kufanya malipo ya fidia. Aidha,Usanifu wa Kina wa miradi ya OSIS ya Idofi (Makambako) na Iboya (Mpemba) umekamilika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa

ajili ya ujenzi wa vituo hivyo. Vile vile, uthamini kwa ajili ya kulipa fidia kupisha ujenzi wa mizani katika maeneo ya Kidyama - Kasulu, Kilemba - Kibondo na Mnanila - Manyovu unaendelea.

**165. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Ujenzi na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) zimeanza kutekeleza mradi wa mashirikiano (Technical Cooperation) katika uimarishaji wa 60 usalama barabarani hapa nchini. Mradi huu unalenga kuboresha mfumo wa usimamizi wa masuala ya usalama barabarani nchini na kuhakikisha taarifa za usalama barabarani zinasimamiwa kikamilifu na kujumuishwa ipasavyo katika Sera.

Aidha, katika kutekeleza mradi huu taasisi mbalimbali zinazohusika na masuala ya usalama barabarani kama vile Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya kupitia hospitali ya rufaa ya Amana, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Jeshi la Zimamoto, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhi (LATRA), Wakala ya Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) pamoja na wadau wengine watahusishwa. Mradi huu utatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu (3) kuanzia Aprili, 2025.

**166. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi wa menejimenti ya usimamizi wa mazingira una lengo la kuelimisha na kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 katika Sekta ya Ujenzi. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) imeanza maandalizi ya Mkakati wa Wizara wa Usimamizi wa Maafa.

Vilevile, kupitia TANROADS miradi sita (06) ya barabara imefanyiwa tathmini za athari kwa mazingira ambapo miradi miwili (2) imepata vyeti vya tathmini za athari kwa mazingira na miradi minne (04) inaendelea kufanyiwa tathmini za athari kwa mazingira.

**167. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara kupitia TANROADS imetoa elimu kwa lengo la kuwajengea uwezo wananchi kuhusu uhifadhi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya mradi kumi

na sita (16) ya ujenzi wa barabara. Aidha, ili kupendezesha mazingira 61 ya barabara na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi jumla ya miti 166,635 imepandwa katika hifadhi za Barabara za mikoa ya Dodoma, Arusha, Manyara, Mbeya, Songwe, Singida, Kilimanjaro, Geita, Tanga, Pwani, Dar es salaam, Iringa, Njombe, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Simiyu, Mara, Mwanza, Lindi, Mtwara, Morogoro na Kagera.

**Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege.**

**168. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara kupitia TANROADS inasimamia ujenzi, ukarabati, upanuzi na uboreshaji wa jumla ya viwanja vya Ndege kumi (10) nchini ambavyo imekasimiwa. Utekelezaji wa miradi hiyo hadi kufikia Aprili, 2025 ni kama ifuatavyo:

**169. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, utekelezaji wa Package I unaohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege (runway), barabara ya viungio (taxiway), maegesho ya ndege (apron) pamoja na usimikaji wa taa za usalama na kuongozea ndege umefikia asilimia 87. Aidha, utekelezaji wa Package II unaohusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, Kituo cha Zimamoto, Kituo cha Hali ya Hewa na vituo vidogo nane (8) vya kufua umeme unaendelea na umefikia asilimia 53.22.

**170. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, kazi za ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu yake, ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, usimikaji wa 62 taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa uzio wa usalama, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa zinaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 20.

**171. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika Kiwanja cha Ndege cha Tabora, kazi za ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu yake, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la

uchunguzi wa hali ya hewa zinaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 93.

**172. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi wa uboreshaji na ukarabati wa kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga unaohusisha kazi za ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege umefikia asilimia 60.

**173. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi za ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege katika Kiwanja cha ndege cha Shinyanga zimefikia asilimia 80.

**174. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi ya upanuzi na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege, maegesho ya ndege, barabara ya kiungio na uzio wa 63 usalama katika kiwanja cha Ndege cha Musoma inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 58.

**175. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kiwanja cha Ndege cha Iringa, ukarabati na upanuzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, maegesho ya ndege, mitambo na taa za kuongozea ndege, barabara ya kiungio na uzio wa usalama (Awamu ya I) umekamilika. Utekelezaji wa Awamu ya II (Jengo la Abiria) upo katika hatua za awali za ujenzi.

**176. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa upande wa Kiwanja cha Ndege cha Geita, kazi ya ujenzi wa uzio wa usalama na barabara ya mzunguko, inaendelea na imefikia asilimia 80.

**177. Mheshimiwa Mwenyekiti**, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kupata Makandarasi na Washauri Elekezi wa miradi ya ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Tanga na Lake Manyara

zimekamilika. Mikataba ya ujenzi na usimamizi kwa kiwanja cha ndege cha Iringa Awamu ya II imesainiwa. Aidha, kwa upande wa kiwanja cha Lake Manyara, mkandarasi wa ujenzi amepatikana na amesaini mkataba tarehe 23 Desemba, 2024, na kwa kiwanja cha ndege cha Tanga mkataba wa usimamizi umesainiwa.

## C.3 UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA UJENZI

**178. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara ya Ujenzi ina Taasisi tisa (9) inazosisimamia ambazo zinatekeleza majukumu ya Sekta ya Ujenzi. Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo hadi kufikia Aprili, 2025 ni kama ifuatavyo:

### Bodi ya Mfuko wa Barabara

**179. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/25, Bodi ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi 856,794,954,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 594,069,614,922 ni kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo ya barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi. Aidha, kiasi cha Shilingi 254,601,263,538 zilitengwa kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo ya barabara za Wilaya ambazo husimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mgawanyo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: Wizara ya Ujenzi Shilingi 59,406,961,492; TANROADS Shilingi 534,662,653,430; Ofisi ya Rais – TAMISEMI Shilingi 25,460,126,354, TARURA Shilingi 229,141,137,184 na Shilingi 8,124,075,539 ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji wa Mfuko wa Barabara.

**180. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025, jumla ya makusanyo ya fedha za Mfuko yalikuwa Shilingi 819,662,377,083 sawa na asilimia 95 ya bajeti ya mwaka.

**181. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Bodi pia inaendelea kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara kwa kutumia wataalam wa ndani na nje ya taasisi ili kupata thamani

halisi ya fedha katika miradi inayotekelezwa. Kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 jumla ya miradi 786 ilifanyiwa ukaguzi kwa kutumia wataalam washauri na wataalam wa ndani. Kufuatia ukagzi huo, Bodi ilibaini kuwa fedha zilizopelekwa kwa Wakala za Barabara zilitumika kulingana na mipango iliyokubalika.

Vilevile, Bodi imeendelea kuratibu na kutekeleza zoezi la kuchukua takwimu na taarifa za hali ya barabara (road inventory and condition survey) kwa lengo la kuzitumia katika kuandaa mipango kazi na utekelezaji wa kazi za barabara. Aidha, Bodi imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto ya kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kugharamia matengenezo ya barabara. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha uwezo wa kukusanya mapato yatokanayo na matumizi ya hifadhi ya barabara na kufanya utafiti juu ya uwezekano wa kugharamia matengenezo maalum ya barabara kwa kutumia hatifungani.

**Wakala wa Majengo Tanzania**

**182. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) umeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutumia fedha za ruzuku ya Serikali pamoja na mapato ya ndani ya Wakala. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na kutoa huduma za ushauri kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali, kujenga majengo ya Washitiri mbalimbali; kuuza na kupangisha nyumba zinazojengwa na TBA kwa Watumishi wa Umma na kupangisha baadhi ya majengo ya Serikali kwa wasio watumishi wa Umma ili kuongeza uwezo wa Wakala kujiendesha.

**183. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi inayotekelezwa kwa kutumia fedha za ndani za Wakala ni pamoja na ujenzi wa jengo la ghorofa kwa watumishi wa Umma eneo la Canadian Masaki, Dar es Salaam ‘‘Block II” na III ambapo utekelezaji umefikia asilimia 74, Ujenzi wa ofisi ya TBA Mkoa wa Geita umefikia asilimia 60 na ujenzi wa Ghorofa za Watumishi wa Umma za Ghana 66 Kota ‘‘Block I” jijini Mwanza ambao umefikia asilimia 50. Ukarabati wa Majengo mbalimbali nchini umefikia asilimia 68 ambapo ukarabati wa nyumba 63 umefanyika katika Mikoa ya Dar es

Salaa – 15, Dodoma 17, Manyara – 5, Arusha - 5, Ruvuma - 5, Kagera – 2, Iringa – 2, Mara – 2, Pwani – 2, Kigoma – 2, Kilimanjaro – 1, Katavi – 1, Lindi – 1, Rukwa – 1, Mbeya – 1 na Shinyanga – 1. Aidha, Wakala umekarabati ofisi tatu (3) katika mikoa ya Lindi, Pwani na Katavi.

**184. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wakala pia umetekeleza miradi 103 ya Washitiri. Miradi hiyo ni pamoja na miradi sita (6) ya Buni Jenga (Design and Build) ambayo ni ujenzi wa jengo la ofisi ya kanda ya Sekretarieti ya Maadili ya Umma jijini Dodoma na ujenzi wa ofisi ya Tumbaku Wilaya ya Urambo – Tabora ambayo imekamilika na kukabidhiwa kwa washitiri; ujenzi wa nyumba ya Makazi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita ambao umefikia asilimia 96 pamoja na ujenzi wa wodi na jengo la Mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Burigi Chato awamu ya II ambao umefikia asilimia 90. Ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nkasi – Rukwa awamu ya kwanza umefikia asilimia 92; ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama - Mara umefikia asilimia 72 na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi - Simiyu umefikia asilimia 97.

**185. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wakala pia umeendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba Dodoma ikiwemo ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora awamu ya pili ambao umekamilika na kukabidhiwa kwa mshitiri. Wakala pia umeendelea kutoa huduma ya ushauri katika miradi ya ujenzi wa majengo ya 67 Wizara 13 na Taasisi tano (5) ambapo utekelezaji wa miradi hii upo katika hatua mbalimbali.

**186. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, Wakala umetekeleza miradi 65 ya Ushauri (Consultancy). Miongoni mwa miradi hiyo, miradi nane (08) imekamilika ambayo ni:- Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Usevya na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mpanda - Katavi; ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Mwanzo Kinesi - Mara; ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Kabanga - Kagera; ujenzi wa uzio wa Ikulu ndogo Arusha.

Miradi inayoendelea ni pamoja na ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali jijini Arusha ambao umefikia

asilimia 33 na ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Moshi - Kilimanjaro ambao umefikia asilimia 50.

**187. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wakala vilevile umetekeleza miradi 12 ya Ujenzi na Ukarabati. Miradi ya ujenzi na ukarabati iliyotekelezwa inajumuisha: ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro (asilimia 98), ukarabati wa majengo 15 katika Taasisi ya Mafunzo ya Kilimo ya Maruku, Kagera (asilimia 97) na ujenzi wa Jengo la Uchunguzi na Mionzi katika Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto mkoani Kilimanjaro Awamu I ambao umekamilika na awamu ya pili umefikia asilimia 97.

**188. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wakala pia ulitekeleza mradi mmoja (1) wa Usimamizi (Project Management) ambao ulihusisha usimamizi wa Mifumo ya joto, hewa na viyoyozi; Mifumo ya umeme; Mifumo ya vitambua moto na vitoa sauti; Mifumo ya majisafi na majitaka; Mitambo ya kangavuke 68 (generators) na transfoma pamoja na usimamizi wa samani katika Ukumbi wa Bunge Dodoma.

**189. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa Majengo Tanzania imehuishwa kupitia GN Na. 595 ambayo inaruhusu Wakala kuhusisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi yake pamoja na kuwauzia na kuwapangisha nyumba wasio watumishi wa umma kwa bei ya soko. Aidha, Wakala umeainisha maeneo yake oevu yaliyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Mwanza kwa ajili ya kuyaendeleza kwa njia ya ubia pamoja na mikopo kutoka Taasisi za kifedha. Kufuatia kuhuisha Sheria hiyo, Wizara inategemea kupungua kwa changamoto za makazi kwa Watumishi wa Umma na kuiwezesha kupata mapato yatakayopelekea Wakala kujiendesha na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini katika utekelezaji wa miradi ya nyumba za makazi.

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania**

**190. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ulipanga kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo

ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo na kutoa ushauri katika mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozi kwenye majengo ya Serikali. Kazi nyingine ni uendeshaji wa shughuli za usafiri wa vivuko vya Serikali 69 zinazohusisha ujenzi na ukarabati wa vivuko, maegesho na miundombinu ya vivuko (majengo na uzio).

**191. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025, utekelezaji wa miradi ya maegesho ya vivuko, Ukarabati wa Vivuko, Ujenzi wa Vivuko Vipya na Ujenzi na Ukarabati wa Karakana kwa kutumia fedha za ruzuku ni kama inavyooneshwa katika Aya 145-150.

**192. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wakala pia ulipanga kutekeleza Miradi ya Washitiri na Ushauri iliyohusisha kufanya matengenezo ya magari 31,581, matengenezo na usimikaji wa mifumo 267 ya umeme, 665 ya majokofu na viyoyozi na mifumo 23 ya elektroniki. Aidha, Wakala ulipanga kutoa ushauri wa Kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo 90 ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu na kusimamia mifumo hiyo 50. Wakala pia ulipanga kuendelea na usimamizi wa vivuko vya Serikali 33 na ukodishaji wa mitambo ya ujenzi wa barabara.

**193. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025, Wakala umefanya matengenezo ya magari 19,778, usimikaji wa mifumo ya umeme 114, elektroniki 7, viyoyozi na majokofu 222. Miradi 30 ya usanifu wa kazi za umeme, mitambo na elektroniki imetekelezwa. Aidha, Wakala kupitia huduma za vivuko umevusha abiria wapatao18,729,975, tani za mizigo 103 na magari 352,348. Vilevile, Wakala unaendelea na usimamizi vivuko 32 katika vituo 22 nchi nzima na ukodishaji wa magari na mitambo kwa ajili ya kazi za ujenzi.

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi**

**194. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/25 Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) ilipanga kusajili jumla ya wahandisi 3,200, mafundi sanifu 300, kampuni za ushauri 16 na maabara za kupima ubora wa kazi za uhandisi na vifaa vya ujenzi 5.

Hadi kufikia Aprili, 2025 Bodi imesajili jumla ya wahandisi 3782, mafundi sanifu 409, kampuni za ushauri 13 na maabara 1. Katika kipindi hicho Bodi ilifuta usajili kwa wahandisi wataalamu 41. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya miradi 665 ilikaguliwa. Aidha Bodi imesajili miradi 1,323 kati ya miradi 1,500 iliyojipangia mwaka huu.

**195. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Bodi pia iliandaa mafunzo elekezi manne (4), kwa wahandisi wahitimu. Vilevile, Bodi iliendelea kuwaapisha Wahandisi Wataalam Kiapo cha Utii kwa Taaluma (Professional Oath) ambapo jumla ya wahandisi 7,083 hadi sasa wamekwishaapishwa. Aidha, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu 4,711. Jumla ya wahandisi wahitimu 14,970 wameshapitia Mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003.

Bodi vilevile iliandaa na kuadhimisha Siku ya Wahandisi 2024 (Annual Engineers' Day 2024) ambayo ilihudhuriwa na wahandisi zaidi ya 5,102. Mada iliyojadiliwa katika siku ya wahandisi ilikuwa ni "Setting the Engineering Workforce for the Artificial Intelligence Era: Training and Upskilling Engineering Practitioners".

**196. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile Bodi imeanzisha shule ya umahiri na uongozi (School of Professional Engineering and Leadership) kwa ajili ya kujenga uwezo wa wataalam wetu wa kada za uhandisi na uongozi ambao itawasaidia kusimamia miradi yetu nchini bila kutegemea wahandisi kutoka nje ya nchi. Aidha, Bodi imeanzisha mradi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuboresha ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya sayansi na hisabati (Stem Support Program) ili baadaye waweze kujiunga na vyuo vikuu kusomea taaluma ya uhandisi na hivyo kuongeza wataalam wa kada ya uhandisi nchini.

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi.**

**197. Mheshimiwa Mwenyekiti**, majukumu makuu ya Bodi hii ni kusajili, kusimamia na kuratibu mienendo ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi pamoja na Kampuni zao za Ushauri elekezi. Aidha, Bodi ina jukumu la kukagua miradi ya ujenzi ili kuhakikisha

ubunifu na usimamizi wa ujenzi unafanywa na Wataalam waliosajiliwa.

**198. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/2025, hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya wataalam 161 wamesajiliwa na Bodi, ikiwa ni asilimia 89 ya lengo na imesajili Watalam wa kati (semi1professionals) 361 ikiwa ni asilimia ya lengo. Bodi imesajili kampuni za Kitaalam 26 ikiwa ni asilimia 81 ya lengo. Aidha, Wahitimu wa Vyuo Vikuu 260 wanaendelea na Mafunzo kwa Vitendo ikiwa ni asilimia 104 ya malengo yaliyopangwa. Vilevile, miradi ya ujenzi 1,325 ilisajiliwa ambayo ni asilimia 94.6 ya malengo yaliyopangwa.

**199. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, miradi ya ujenzi 4,354 ilikaguliwa ikiwa ni asilimia 116 ya lengo. Miradi ambayo ilikutwa na kasoro, Wataalam au Waendelezaji wake walichukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya mwaka 2010 (kama ilivyorekebishwa 2023) ikiwemo, kutozwa faini au kufunguliwa mashtaka Mahakamani. Vilevile, Bodi iliweza kuandaa mkutano mmoja (1) wa Wadau wa fani zinazosimamiwa na Bodi ambao ulihudhuriwa na Wataalam wapatao 818 wa fani hizo.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

**200. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/25, Bodi ilipanga kusajili jumla ya Makandarasi wapya 1,400 na kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi 3,450. Aidha, Bodi ilipanga kuendesha kozi sita (6) za mafunzo na kuendesha warsha moja (1) ya mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika mkoa wa Mtwara. Vilevile, Bodi ilipanga kuendeleza Mfuko Maalum wa kutoa dhamana ya kuwezesha Makandarasi wa ndani (Contractor’s Assistance Fund – CAF) pamoja na kuendelea na jitihada za kuhamasisha Makandarasi wazalendo kujiunga ili kuomba zabuni kwa mfumo wa ubia.

**201. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025, Bodi ilisajili jumla ya Makandarasi 1,284 na kukagua jumla ya miradi 3,069. Aidha, Bodi imeendesha kozi za mafunzo katika vituo vitano (5) pamoja na kuendesha warsha moja (1) ya mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika mkoa wa Mtwara.

**Baraza la Taifa la Ujenzi.**

**202. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2024/25 Baraza lilipanga kuendelea kutekeleza jukumu kuu la usimamizi wa sekta ya Ujenzi nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ujenzi nchini. Hadi Aprili, 2025 Baraza limekamilisha kazi ya kuandaa mapendekezo ya rasimu ya Kanuni za Majengo (Building Codes), kuendelea kuandaa rasimu ya viwango msawazo vya ujenzi wa majengo na samani za Serikali (Building specifications and standards for government buildings and furniture).

**203.** Baraza pia limetoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kwa wadau wa sekta ya ujenzi ikiwa ni pamoja na taasisi za NSSF, NHC, TEMESA, BOT, PPRA, TANROADS na EWURA. Aidha, kwa kipindi husika Baraza limesajili na kuratibu utatuzi wa migogoro 50 iliyojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi nchini.

**204. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, Baraza limeratibu uendeshaji wa kozi mbili (2) za mafunzo ya kujenga uwezo kwa wadau 152 wa Sekta ya Ujenzi nchini. Kazi nyingine zilizofanyika ni kukusanya na kuchapisha takwimu za mwenendo wa bei za bidhaa na huduma za ujenzi kwa kipindi cha Julai, 2024 – Machi, 2025, kuunda mfumo wa kusaidia utatuzi wa changamoto za wadau wa sekta ya Ujenzi (CONTAS) na kuimarisha kanzidata ya taarifa za Sekta ya Ujenzi inayowezesha wadau wa sekta ya Ujenzi kupata taarifa muhimu za Sekta ya Ujenzi.

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

**205. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka 2024/25, Kituo kimeendelea kushirikiana na Kitengo cha Utafiti na Maendeleo (Research Development Unit - RDU) cha Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kufanya tathmini na ufuatiliaji wa teknolojia mbalimbali mpya na mbadala katika ujenzi na matengenezo ya barabara nje na ndani ya nchi ili kuwezesha Wizara kupata teknolojia stahiki zenye ufanisi na gharama nafuu kwenye utekelezaji wa miradi. Ili kujiimarisha zaidi, Kituo kinaendelea na

hatua za kufufua na kuboresha Maktaba Mtandao yake (e-library) kupitia ICoT ili kuendeleza jukumu lake la kutoa huduma za kusambaza teknolojia kwa njia ya maktaba. Mradi huu wa kubuni na kuendeleza Mfumo wa Maktaba mtandao (e-library) ya TanT2 na ICoT upo katika hatua za usajili katika Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA). Kituo vilevile kinaendelea kushiriki kuandaa na kuhariri Jarida Na. 3 la Shirikisho la Barabara la nchi za Kusini mwa Afrika (ASANRA) ambalo baada ya kukamilika litasambazwa kwa wadau wote wa SADC.

**206. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Vilevile, Kituo kilishiriki katika mikutano mbalimbali ya kikanda na kimataifa kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na kujenga uwezo Mikutano hiyo ni pamoja na mkutano wa Kamati ya Kujenga Uwezo wa Usambazaji wa Teknolojia ya usafirishaji ya SADC (Regional Technology Transfer and Capacity Building Committee) kwenye masuala yanayohusu usambazaji wa teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji cha ASANRA.

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi**

**207. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT) ina jukumu la kutoa mafunzo ya muda mrefu katika fani za uhandisi ujenzi, umeme na mitambo katika ngazi za Astashahada na Stashahada, Elimu ya ufindi Stadi (VET) pamoja na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kuhusu udereva wa magari na matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.

**208. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025 wanafunzi 40 walihitimu mafunzo ya Stashahada na wanafunzi 191 walihitimu Elimu ya Ufundi Stadi (VET). Aidha, Taasisi ilidahili jumla ya Wanafunzi wapya 126 wa Stashahada katika ngazi za NTA level 4 - 6 na kudahili wanafunzi wapya 203 wa Elimu ya Ufundi Stadi (VET).

**209. Mheshimiwa Mwenyekiti**, hadi Aprili, 2025 Taasisi inaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 271 wa Stashahada katika fani za Uhandisi Umeme, Mitambo na Ujenzi. Vilevile, Taasisi inaendelea kutoa mafunzo ya Elimu ya Ufundi Stadi (VET) kwa

wanafunzi 440 wa daraja la I,II na III. Taasisi imeendesha kozi fupi mbili (2) kwa washiriki 307 katika kozi ya udereva wa awali na 137 katika kozi ya udereva wa magari ya abiria (PSV).

**210. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, Taasisi imeendelea kusimamia kwa karibu ujenzi wa jengo jipya la Taaluma ambapo, hadi Aprili, 2025 maendeleo ya ujenzi yamefikia asilimia 50.

**211. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, Taasisi iliandaa na kutoa Mafunzo ya kozi fupi kuhusu matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika kazi za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara ambapo kozi nne (4) zimekamilika na jumla ya wahitimu 52 wamepatiwa mafunzo. Aidha, Taasisi imefanya uhamasishaji wa matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Halmashauri za Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Njombe na Ruvuma. Taasisi imefanikiwa kupata Hati Miliki ya eneo la ardhi ya Taasisi katika Kampasi ya Mbeya.

## D. MATENGENEZO YA MIUNDOMBINU ILIYOHARIBIWA NA MAFURIKO NA KIMBUNGA HIDAYA

**212. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Barabara zetu zilikumbwa na athari kubwa kutokana na mafuriko yaliyosababishwa na mvua za El Nino na Kimbunga Hidaya mwishoni mwa mwaka 2023. Katika mwaka wa fedha 2024/25 Wizara imeanza kazi ya matengenezo ya dharura ya miundombinu iliyoathirika na majanga hayo. Kupitia programu ya Crisis and Emergency Response Component (CERC) jumla ya mikataba 81 yenye thamani ya Shilingi 556,928,617,822.49 kwa ajili ya matengenezo ya dharura imesainiwa na Makandarasi wanaendelea na kazi. Kati ya hiyo, miradi mitano (5) inatekelezwa katika mradi wa Msimbazi Basin Development Project, Miradi sita (6) inatekelezwa katika mradi wa RISE na Miradi 70 inatekelezwa chini ya TanTIP. Kati ya mikataba hiyo, miradi 72 inatekelezwa na Makandarasi wazawa.

**213. Mheshimiwa Mwenyekiti**, aidha, katika mwaka 2025/26, kipaumbele kitakuwa kufanya matengenezo makubwa ya barabara ili zisiendelee kuharibika. 77 Barabara zilizopangwa kufanyiwa matengenezo ni pamoja na Dar es Salaam – Kibiti -

Lindi – Mingoyo (km 463) ambayo ilijifunga kutokana na mvua kubwa zilizonyesha hivi karibuni. Barabara hii itajengwa kwa awamu. Niwahakikishie watumiaji wa barabara hii kuwa, matangenezo haya makubwa yatakapokamilika itakua ni suluhisho la changamoto ya kujifunga mara kwa mara kwa barabara hii wakati wa msimu wa mvua.

## E. MATUMIZI YA HIFADHI YA BARABARA

**214. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara imehuisha kanuni za matumizi ya hifadhi ya barabara kwa lengo la kuwezesha matumizi endelevu ya hifadhi ya barabara. Aidha, Wizara imeandaa Kanuni mahsusi ya kusimamia maegesho kwenye mtandao wa barabara. Maeneo yanayofaa kwa matumizi ya biashara ikiwa ni pamoja na maegesho ya magari ya mizigo yamebainishwa. Kutokana na uwekezaji mkubwa unaohitajika katika hifadhi ya barabara, ili kufikia lengo la kukusanya mapato hayo, Serikali itashirikisha Sekta Binafsi kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

**215. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara imechukua hatua hizi ili kuimarisha usalama barabarani, kupunguza msongamano wa magari, kupendezesha maeneo ya miji, kuongeza fursa za ajira na kipato kwa wananchi na kuongeza mapato kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara. Wizara itashirikiana na wadau wote kuhakikisha hifadhi ya barabara inatumika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazosimamia matumizi yake.

## F. MASUALA MTAMBUKA

### Matumizi ya Teknolojia Mpya katika Ujenzi na Matengenezo ya Barabara

**216. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara inaendelea na matumizi ya Teknolojia mbalimbali katika ujenzi na matengenezo ya barabara ambazo zinafanya zidumu kwa muda mrefu. Lengo ni kukabiliana na changamoto mbali mbali zikiwepo gharama na ubora wa malighafi na vifaa vya ujenzi vinavyotumika.

Teknolojia mpya ya lami yenye uwezo wa kuhimili mzigo mkubwa na hali ya hewa tofauti tofauti imetumika kwa barabara ya Njia Nane kutoka Kimara – Kibaha (km 19.2) kwa kutumia Mwongozo Mpya ulioandaliwa na RDU. Teknolojia hii inayoitwa 'Stone Mastic Asphalt' na 'Dense Graded Asphalt' huzingatia uhimili wa kokoto zenye ukubwa tofauti tofauti katika mchanganyiko wa lami.

**217. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Teknolojia nyingine iliyotumika ni matumizi ya mitambo ya kisasa kama Road Scanner, Falling Weight Deflectometer, Light Weight Deflectometer, n.k ili kuboresha usimamizi wa ubora wa barabara kwa kufanya uchunguzi wakati ujenzi unaendelea.

**Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi Katika Miradi ya Ujenzi**

**218. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Kibaha – Chalinze – Morogoro (km 163.8), kwa utaratibu wa PPP kama ifuatavyo:-

i. Sehemu ya Kibaha – Chalinze (km 78.9), kazi inayoendelea ni mazungumzo ya namna ya utekelezaji kati ya TANROADS na Mwekezaji baada ya Kamati inayosimamia mradi kuidhinisha Taarifa ya Uthamini wa Mwekezaji.

ii. Kwa sehemu ya Chalinze – Morogoro (km 84.9), Mshauri Elekezi amekamilisha Upembuzi Yakinifu ambao umewasilishwa kwa Kamati inayosimamia mradi ili kupata idhini.

Aidha, kuhusu Ushoroba wa TANZAM, sehemu ya barabara ya Igawa – Tunduma (km 218) imeanza kufanyiwa Upembuzi Yakinifu na Mshirika aliyeonesha nia ya ujenzi wa barabara hii kwa utaratibu wa PPP. Upembuzi huo unatarajiwa kukamilika baada ya mwaka mmoja.

## G. CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA

**219. Mheshimiwa Mwenyekiti**, changamoto kadhaa zimechangia kutokufikiwa malengo utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Changamoto hizo ni pamoja na:

**a) Mabadiliko ya Tabianchi**

Mabadiliko ya tabianchi yanasababisha mafuriko kwa baadhi ya maeneo nchini na hivyo kusababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja.

Aidha, kumekuwa na vipindi vya joto kali kupita kawaida hadi kufikia nyuzi sentigredi 36, hali ambayo huathiri uimara wa lami kwa kusababisha kokoto kumeguka kutokana na kuyeyuka kwa lami.

**Mkakati**

Wizara inaboresha miongozo ya usanifu na matumizi ya malighafi za ujenzi kwa kuzingatia uhimilivu (Resilience) wa miundombinu.

**b) Shughuli za kibinadamu na usimamizi wa utupaji wa taka ngumu**

Shughuli za kiuchumi ikiwemo kilimo na ukataji miti kwenye vyanzo vya maji na maeneo yenye miinuko husababisha kusombwa kwa udongo na kujaa katika madaraja na barabara. Hali hii husababisha mabadiliko ya uelekeo na kupunguza kina cha mito na hivyo kuharibu kingo za barabara na madaraja. Aidha, kumekuwa na changamoto ya utupaji holela wa taka ngumu na hivyo kusababisha kuziba kwa mitaro na madaraja madogo. Vilevile, uchafuzi mkubwa umeshuhudiwa katika njia na maeneo ya vivuko, hususan katika kituo cha Magogoni - Kigamboni (Dar es Salaam) na Kigongo - Busisi (Mwanza). Taka ngumu zinazotupwa ovyo kwenye njia za kivuko pamoja na nyavu za samaki zimekuwa zikinasa kwenye mifumo ya uendeshaji wa vivuko na kusababisha uharibifu wa mara kwa mara wa vivuko. Hii

husababisha gharama kubwa za matengenezo ya vivuko na uendeshaji wa vivuko kwa ujumla.

**Mikakati**

i. Kushirikiana na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ili kutoa elimu kwa watumiaji bahari, maziwa na mito kuhusu athari za uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya vivuko, mitaro ya maji na madaraja.

ii. Kuendelea kutoa elimu kwa wavuvi kutofanya shughuli za uvuvi kwenye njia za vivuko.

## H. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

**220. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara ya Ujenzi imeandaa Mpango na Bajeti wa mwaka wa fedha 2025/26 kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Mpango Mkakati wa Wizara (2021/22 – 2025/26); Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26.

**221. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2025/26 ni:

i. Kuendelea na ujenzi wa barabara za kimkakati zenye kufungua fursa za Kiuchumi, kuimarisha shughuli za kijamii pamoja na zile zinazounganisha barabara na njia nyingine za usafiri;

ii. Kuendelea na ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, nchi jirani pamoja na barabara za ulinzi kwa kiwango cha lami;

iii. Kuendelea na ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano katika miji inayokua kwa kasi na majiji ya

Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Morogoro;

iv. Kuendelea na ukarabati na matengenezo ya barabara kuu na mikoa ili kuhakikisha kuwa barabara zinapitika katika majira yote ya mwaka pamoja na matengenezo makubwa ili kuhakikisha kuwa barabara haziendelei kuharibika na kupoteza thamani;

v. Kuendelea kuimarisha usafiri na miundombinu ya vivuko ili kuunganisha maeneo ya nchi kavu ambayo yametenganishwa na maji katika maeneo ya bahari, maziwa na mito;

vi. Kuendelea na miradi ya usalama barabarani ikiwemo kujenga mizani pamoja na kusanifu na kujenga barabara za michepuo na zile zinazozingatia mahitaji ya watumiaji wote wa barabara.

vii. Kuendelea kujenga nyumba za watumishi wa umma na majengo ya Serikali kwa kuupa kipaumbele utaratibu wa kushirikisha Sekta Binafsi.

viii. Kuwajengea uwezo wataalam wa ndani kwa lengo la kuongeza wataalam wabobezi wa ndani, pamoja na kutoa kipaumbele kwa kampuni za ndani zinazohusika na masuala ya ujenzi;

ix. Kuendelea na mapitio ya Sera, miongozo na mifumo inayosimamiwa na Wizara ya Ujenzi ili iendane na wakati ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya teknolojia na maendeleo endelevu; na

x. Kukamilisha ujenzi wa viwanja vya ndege vilivyokasimiwa Wizara ya Ujenzi, ikiwemo Msalato.

**H.1: MAKADIRIO YA BAJETI**

**Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

**222. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara ya Ujenzi imetengewa Shilingi 90,468,270,000.00 ikiwa ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

katika mwaka wa fedha 2025/26. Kati ya fedha hizo, Shilingi 85,028,585,000.00 ni Bajeti ya Mishahara na Shilingi 5,439,685,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

**223. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi niShilingi2,189,727,558,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,209,223,117,000.00 ni fedha za ndani na Shilingi 980,504,441,000.00 ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani, Shilingi 688,756,470,000.00 ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni Shilingi 520,466,647,000.00.

Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 1. Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/26 ni kama ifuatavyo:

**H.2: UTEKELEZAJI WA MIRADI**

**Miradi ya Barabara na Madaraja**

**224. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi ya barabara na madaraja itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/26 ni kama ifuatavyo:

**Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74)**

**225. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 3,200.00 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, sehemu za Soni – Bumbuli (km 22) na Kwameta – 84 Kwashemshi (km 10). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Old Korogwe – Kwamndolwa – Magoma – Mashewa – Bombomtoni – Mabokweni (km 127.69) sehemu ya Old Korogwe – Kwamndolwa (km 10) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii sehemu ya Maramba – Mabokweni (km 10).

**Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 210)**

**226. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 59,911.34 zinazojumuisha Shilingi milioni 3,610.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 56,301.34 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi: sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) na kuendelea na ujenzi wa sehemu za Mnivata – Mitesa (km 100) na Mitesa – Masasi (km 60) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Namichiga – Ruangwa (km 20.6), Magamba – Madimba – Msimbati (km 35) na Mtama – Tandahimba (km 5) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)**

**227. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,200.00 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2025/26, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii sehemu ya Likuyufusi – Mhukuru (km 60) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130)**

**228. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 3,200.00 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2025/26, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, sehemu ya Liwale – Kihangara (km 55) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Masasi – Nachingwea (km 45) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6)**

**229. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)**

**230. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 2,000.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7)**

**231. Mheshimiwa Mwenyekiti**, barabara hii imetengewa jumla ya Shilingi milioni 660.00 kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)**

**232. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, barabara hii imetengewa jumla ya Shilingi milioni 1,510.00 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Musoma – Kusenyi (km 40) kwa kiwango cha lami na kulipa deni la Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Suguti – Kusenyi (km 5).

**Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98)**

**233. Mheshimiwa Mwenyekiti**, barabara hii imetengewa jumla ya Shilingi milioni 3,500.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kongwa Jct – Ngambi – Mpwapwa (km 32) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 46.9) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)**

**234. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 1,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104)**

**235. Mheshimiwa Mwenyekiti**, barabara hii imetengewa jumla ya Shilingi milioni 49,900.29 zinazojumuisha Shilingi milioni 550.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 49,350.29 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Iringa – Ruaha National Park (km 104) na Iringa (Ipogolo) – Kilolo (km 33.2) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muheza – Amani (km 36)**

**236. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 880.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200.51)**

**237. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 71,099.77 zinazojumuisha Shilingi milioni 500.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 70,599.77 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa sehemu za Mtwara – Mingoyo (km 82.27) na Mingoyo – Nanganga – Masasi (km 118.24) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu (km 189)**

**238. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 3,800.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu; sehemu ya Ntendo – Kizungu (km 25) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152); sehemu ya Kibaoni – Usevya (km 5) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kizungu – Muze (km 12) kwa kiwango cha lami.

**Daraja la Kigongo – Busisi (J.P. Magufuli) na Barabara Unganishi**

**239. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 33,355.36 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa daraja hili na barabara unganishi.

**Daraja la Mzinga**

**240. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 275.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja la Mzinga katika Barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe Jijini Dar es Salaam.

**Daraja la Ugalla**

**241. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 550.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa daraja hili lililopo katika mkoa wa Katavi.

**Daraja la Kitengule na Barabara Unganishi**

**242. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,010.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kagera Sugar Jct – Kakunyu; sehemu ya Kagera Sugar Jct – Kitengule Jct (km 25) na kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja la Kitengule.

**Barabara ya Morogoro – Dodoma (km 260) pamoja na Daraja la Mkundi**

**243. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,750.00 zimetengwa kwa ajili ya malipo ya madai ya Mhandisi Mshauri aliyefanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii pamoja na Daraja hilo ili kuikarabati kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya SUA Main Gate – Mzinga Factory Gate (km 11.0) kwa kiwango cha lami.

**Daraja Jipya la Wami**

**244. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 10.00 zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja hili lililopo katika barabara ya Chalinze – Segera.

**Barabara ya Njombe – Makete – Isyonje (km 157.4)**

**245. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 3,320.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete; sehemu ya Kitulo – Iniho (km 36.3), Mzani wa Igagala na barabara ya Njombe – Njombe Referral Hospital (km 3) kwa kiwango cha lami na kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa hii kwa sehemu za

Njombe – Moronga (km 53.90) na Moronga – Makete (km 53.50). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Bulongwa – Iyoka – Madihani – Kidope (km 22), Madihani – Lufilyo (km 15.1), Kitulo – Matamba – Chimala (km 41) na Matamba – Mfumbi (km 33).

**Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105)**

**246. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 3,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za Businde – Murongo (km 53.4) na Omugakorongo – Businde (km 51.6) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 108.9)**

**247. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 6,250.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Nanganga – Ruangwa (km 53.2), Nachingwea – Ruangwa (km 55.7) na kuanza ujenzi wa barabara ya Nangurukuru – Liwale (km 228); sehemu ya Choya – Liwale (km 72) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mpemba – Isongole (km 50.3)**

**248. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,659.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za Mlowo – Kamsamba (km 10), Chang'ombe – Mkwajuni – Makongolosi (km 61) sehemu yenye urefu wa kilometa 5 kuanzia Mkwajuni kwa kiwango cha lami na ujenzi wa kituo cha pamoja cha ukaguzi cha Iboya (One Stop Inspection Station – OSIS). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Utambalila - Chitete (km 17) kwa kiwango cha lami na kulipa madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 50.3).

**Barabara ya Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21)**

**249. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 1,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ndembo (km 90.10)**

**250. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 3,200.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Isongole II – Ndembo (km 52) na barabara ya kuingia Mji wa Ndembo (Ndembo Spur Road) kwa kiwango cha lami na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ndembo (km 44.10) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54)**

**251. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 1,050.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Sengerema – Nyehunge – Kahunda (km 89)**

**252. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,500.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Sengerema – Nyehunge (km 54). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Kamanga – Katunguru – Sengerema (km 35) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Omurushaka – Nkwenda – Murongo (km 125)**

**253. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,200.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii sehemu ya Kyerwa – Chonyonyo (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Upanuzi wa Barabara Kuu Zinazoingia Katikati ya Jiji la Dodoma (km 220)**

**254. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 22,399.78 zimetengwa zijumuisha Shilingi milioni 1,000.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 21,399.78 fedha za nje kwa ajili ya kuanza upanuzi wa barabara kuu zinazoingia katika Jiji la Dodoma (km

51.2) zinazohusisha barabara ya Dodoma – Morogoro (km 32), Dodoma – Iringa (km 8.5) na Dodoma – Arusha (km 10.7).

**Barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct. (km 76.07)**

**255. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 5,500.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii sehemu za Ntyuka Jct – Ntyuka (km 8), Kikombo Jct – Mapinduzi (km 16.4) na Ntyuka – Mvumi Hospital - Kikombo (km 53) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya kuingia Hospitali ya JWTZ Msalato (km 5.5). Kazi nyingine ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Ihumwa – Hombolo - Mayamaya (km 60) ili kuijenga kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Tarime – Mugumu (km 86.05)**

**256. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 5,200.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mogabiri – Nyamongo (km 25) na Tarime – Mogabiri (km 9.3), Nyamongo – Mugumu (km 48.15) pamoja na barabara ya kuelekea Mugumu Roundabout (km 3.6). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Mika –Utegi –Shirati – Kirongwe (km 56.8); Sehemu ya Utegi – Shirati (km 27).

**Barabara ya Shelui – Nzega (km 123)**

**257. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 1,550.00 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Shelui – Nzega (km 123). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Shelui – Sekenke – Tulya – Tyegelo (km 62); sehemu ya Shelui – Sekenke – Ntwike (km 20) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65)**

**258. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 550.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 50)**

**259. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 4,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 10) na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 136); sehemu ya km 3 kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mafinga – Mgololo (km 81)**

**260. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,500.00 zimetengwa kwa ajili kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nyololo – Mtwango (km 40.4)**

**261. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 550.00 zimetengwa kwa ajili kuanza ujenzi wa barabara ya Nyololo – Mtwango (km 40.4); sehemu ya Nyololo Jct – Nyololo (km 5) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kongwa – Kibaya- Arusha (km 430)**

**262. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,500.00 zimetengwa kwa ajili kuanza ujenzi wa barabara hii sehemu ya Tanganyika Packers/ Mbauda Jct - Losinyai (km 70) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Singida – Sepuka – Ndago – Kizaga (km 77.4)**

**263. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 3,500.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa

barabara ya Singida – Sepuka – Ndago – Kizaga (km 77.4) kwa kiwango cha lami na kuanza ujenzi wa barabara ya Sepuka – Mlandala – Urugu – Mtoa – Shelui (km 97.6).

**Barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) pamoja na Daraja la Mnywamaji**

**264. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 4,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) pamoja na daraja la Mnywamaji; sehemu za Amanimakoro – Ruanda (km 35) na Ruanda – Ndumbi Port (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Barabara za Kuelekea Katika Vituo vya Reli ya Kisasa ya SGR (km 94.3)**

**265. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 8,890.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kizota – Zuzu SGR Station (km 14). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za kuelekea katika vituo vya reli ya kisasa (SGR) ambazo ni Morogoro – Kihonda SGR Station (km 10), Rudewa – Kilosa SGR Station (km 3), Gulwe – Gulwe SGR Station (km 2), Igandu – Igandu SGR Station (km 27), Ihumwa – Ihumwa Marshalling Yard (km 5.5), Bahi – Bahi SGR Station (km 4), Mlandizi – Ruvu SGR Station (km 22), barabara za ndani za kituo cha SGR cha Dodoma (Access Roads to Dodoma SGR Station (m 100) na barabara ya Pugu – Kiltex (km 6.7). Kazi nyingine ni kuanza Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina barabara za Ipuli - Tabora SGR Station (km 4.6), Ikungu - Malampaka SGR Station (km 15), Mwigerezi - Mabama SGR Station (km 2.74), Urambo Sec. - Urambo SGR Station (km 2.58), Kintinku - Makutupora SGR Station (km 12), Manyoni - Manyoni SGR Station (km 1.2).

**Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (km 174.5)**

**266. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 50,499.49 zinazojumuisha Shilingi milioni 3,500.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 46,999.49 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za

Tanga – Pangani (km 50), Pangani (Tungamaa) – Mkwaja – Mkange (km 95.2) kwa kiwango cha lami na daraja la Pangani (m 525) na barabara unganishi (km 25.6). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mkata – Kwa Msisi (km 36).

**Barabara ya Kisarawe – Maneromango – Mloka (km 150.46)**

**267. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 1,500.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 133.9)**

**268. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 60,334.42 zinazojumuisha Shilingi milioni 4,185.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 56,149.42 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Kahama – Bulyanhulu Jct – Kakola (km 73.9) na kuanza ujenzi wa barabara za Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3), Nyikonga – Kashelo (km 10.5), Kashelo – Ilolangulu (km 15), Ushirombo – Kilimahewa – Nanda (km 15.7). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Katoro – Nyikonga – Ushirombo (km 47):sehemu ya Ushirombo – Nyikonga (km 22.5), Masumbwe – Kashelo (km 60) na Kahama – Tulole – Muhulidede - Bukumbi – Mambali – Tabora (km 152.27): sehemu ya Kahama - Tulole (km 20) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)**

**269. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,400.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Chato Ginery – Bwina (km 8.1) na SIDO – Chato Zonal Hospital (km 5.3) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50).

**Barabara ya Geita – Nzera – Nkome (km 54)**

**270. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 1,800.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii sehemu ya Nzera – Nkome (km 20.36).

**Barabara ya Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 199.51)**

**271. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 17,809.86 zinazojumuisha Shilingi 13,799.86 fedha za nje na Shilingi 4,010.00 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mianzini – Ngaramtoni (km 18), kuanza ujenzi wa barabara ya USA River – Ngarenanyuki – Oldonyosambu (km 10), kuanza upanuzi wa sehemu ya Tengeru – USA River (km 9.3), Arusha – Kisongo (km 9.3), daraja jipya la Kikafu (m 560) pamoja na barabara unganishi (km 4.06) na barabara za Moshi Mjini (km 8.4). Kazi nyingine ni kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Sakina – Tengeru, barabara ya mchepuo ya Arusha (Arusha Bypass) na Kijenge – Usa River (km 20).

**Barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji (Access Roads To Rufiji Hydropower Project) - km 760.9**

**272. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 4,800.00 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78) pamoja na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara za Maneromango – Vikumburu – Mloka (km 100) na Kibiti – Mloka – Mtemele – Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (km 50). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Chalinze – Utete (km 354.9) na Ngerengere – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 166.4) ikiwa ni mandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro – Dodoma Expressway (km 531.8)**

**273. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 3,540.00 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati (overlay) wa barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44) na Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass km 10) na maandalizi ya upanuzi wa barabara ya Kibaha – TAMCO (km 4.5), kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kibaha – Mlandizi – Chalinze – Morogoro - Dodoma Expressway (km 465) kwa utaratibu wa PPP; sehemu za Kibaha – Mlandizi - Chalinze (km 78.9), Chalinze – Morogoro (km 84.6) na Morogoro – Dodoma (km 260). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Kwa – Mathiasi (Morogoro Road) – Msangani (km 8.3) pamoja na Mkandarasi aliyefanya kazi ya kuboresha maeneo hatarishi (Assorted Accident Blackspots) ya barabara ya Dar es Salaam – Morogoro na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Vigwaza.

**Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 118.1)**

**274. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 1,000.00 kwa ajili ya kuanza ukarabati na upanuzi wa barabara hii (sehemu ya Tegeta/DAWASA – Bagamoyo (km 46.9).

**Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 110)**

**275. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 10.00 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi kwa sehemu za Uyovu – Bwanga (km 43) na Bwanga – Biharamulo (km 67).

**Barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel Road (km 141)**

**276. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 3,000.00 kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Nyakahura –

Kumubuga – Murusagamba (km 34), Kumubuga – Rulenge – Murugarama (km 75) na Rulenge – Kabanga Nickel (km 32).

**Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 265)**

**277. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 36,069.65 zinazojumuisha Shilingi milioni 1,950.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 34,119.65 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Uvinza – Malagarasi (km 51.1) na Kazilambwa – Chagu (km 36) na barabara ya kuingia mji wa Usinge. Kazi nyingine ni kuendelea na usanifu wa barabara ya Tabora – Ulyankulu (km 90) pamoja na kulipa madeni ya Makandarasi waliojenga barabara za Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52), Kaliua – Kazilambwa (km 56), Urambo – Kaliua (km 28) na Urambo Roundabout.

**Barabara ya Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (Njombe) (km 346.43)**

**278. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 7,260.48 zinazojumuisha Shilingi milioni 5,260.50 fedha za ndani na Shilingi milioni 1,999.98 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ifakara – Kihansi (km 124) sehemu za Ifakara – Mbingu (km 62.5) na Mbingu – Chita (km 37.5) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibena – Lupembe – Madeke (km 126); sehemu ya Kibena – Kidegyembe (km 42) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu ya Kihansi – Mlimba – Madeke (km 81) ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389)**

**279. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 7,000.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii sehemu za Mbulu – Garbabi (km 25) na Labay – Haydom (km 25) na kuanza ujenzi wa Nkoma – Lalago (km 65). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mogitu – Hydom (km 68).

**Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga /Bomang'ombe – Sanya Juu (km 105.16)**

**280. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 5,830.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16) na Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8). Kuanza ujenzi wa barabara za Sanya Juu – Kamwanga: sehemu ya Elerai – Kamwanga (km 39.5) na Tarakea – Holili (km 53): sehemu ya Munga - Kiwanda (km 10). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Marangu – Rombo Mkuu – Tarakea (km 64), Sanya Juu – Kamwanga (sehemu ya Sanya Juu – Elerai, km 32) na KIA – Mererani (km 26). Mradi huu utahusisha pia kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Bomang'ombe – Sanya Juu (km 25).

**Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 60.6)**

**281. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 4,110.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Katumba – Lupaso (km 35.3), Mbaka – Kibanja (km 20.7) pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbambo – Ipinda (km 19.7). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Bujesi – Mbambo (km 10).

**Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127)**

**282. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 7,849.92 zinazojumuisha Shilingi milioni 50.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 7,799.92 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni).

**Barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo (km 114)**

**283. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 500.00 kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

**Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8)**

**284. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 1,000.00 kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8); sehemu ya Namanyere – Mfili II Bridge (km 20) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 141)**

**285. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 520.00 kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu za Dumila – Rudewa (km 45) na Rudewa – Kilosa (km 24). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72) kwa kiwango cha lami; sehemu ya Ulaya (km 2).

**Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107)**

**286. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 4,610.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50); sehemu za Matai – Tatanda (km 25) na Tatanda – Kasesya (km 25). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Laela – Mwimbi – Kizombwe (km 93) kwa kiwango cha lami.

**Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

**287. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 19,330.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi katika madaraja ya Sibiti (Singida) na Itembe (Simiyu), ujenzi wa madaraja ya Mbambe (Pwani), Mbangala (Mtwara), Mirumba na Kavuu (Katavi), Mpiji Chini (Dar es Salaam), Nzali (Dodoma), Doma (Morogoro), Chakwale (Morogoro), Nguyami (Morogoro), Kalebe (Kagera), Mkili (Ruvuma), Kibakwe (Dodoma), Kerema Maziwa (Dodoma), Mwanjiri (Dodoma),

pamoja na Simiyu na Sukuma (Mwanza). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa madaraja ya Sanza (Singida), Mkenda na Mitomoni (Ruvuma), Godegode (Dodoma) pamoja na ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara). Aidha, mradi huu utahusisha kuanza maandalizi ya ujenzi wa Madaraja ya Munguli (Dodoma), Mtera, Kondoa, Pahi, Mnenia, Mjonga, Suguta, Kisorya/Ukerewe (Mara/Mwanza), Suguti (Mara). Kazi nyingine kuendelea na utafiti kuhusu changamoto ya maji kufurika katika daraja la Muhuwesi (Ruvuma), kununua vipuri vya madaraja ya dharura na kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa madaraja ya Magufuli na Kiyegeya (Morogoro), Ruhuhu (Ruvuma), Momba (Rukwa), Mara (Mara), Magara (Manyara), Msingi (Singida) na Mpwapwa (Dodoma).

**Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta (km 17.2)**

**288. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 10.00 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3).

**Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1)**

**289. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 4,010.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kumunazi – Kasulo – Bugene (km 133); sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60) pamoja na kuanza ujenzi wa sehemu za Burigi Chato – Kimisi (km 15) na Nyakahanga - Nyabiyonza - Nyakakika (km 96): sehemu ya Nyakahanga – Nyabiyonza - Chabalisa (km 22.5). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi wa sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.1).

**Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 392)**

**290. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 21,059.79 zinazojumuisha Shilingi milioni 1,060.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 19,999.79 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi – OSIS cha

Nyakanazi pamoja na ukarabati wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 92). Mradi huu utahusisha pia maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nyakasanza – Kobero (km 58) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110).

**Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.75)**

**291. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 12,129.88 zinazojumuisha Shilingi milioni 130.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 11,999.88 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35), Nyahua – Chaya (km 85.4) na Tabora – Nyahua (km 85). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa Mizani ya Kizengi.

**Barabara za Mikoa (km 734.59)**

**292. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, jumla ya Shilingi milioni 61,585.00 zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya kilometa 480 kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa 45 kwa kiwango cha lami na ujenzi wa Madaraja/ Makalavati 45. Aidha, kati ya fedha hizi, Shilingi milioni 726.00 zitatumika kwa ajili ya programu ya mafunzo kwa vitendo (Structured Engineers Apprentinceship Programme – SEAP) kwa wahandisi wahitimu. Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika Kiambatisho Na. 2.

**Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)**

**293. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,500.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati wa barabara hii pamoja na kuanza upanuzi wa barabara ya Mwanza - Usagara - JPM Bridge kwa njia nne (km 37); Sehemu ya Mwanza – Usagara (km 22).

**Mradi wa Kupunguza Msongamano Barabara za Dar es Salaam (km 165.16)**

**294. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 9,781.49 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi (km 6.73), Goba – Matosa – Temboni (km 6), Kibamba Shule – Mpiji Magoe (km 9.2), Mbezi Msakuzi – Makabe Jct (km 8.36) na Chanika – Mbande – Rangi Tatu (km 3.8). Aidha, fedha hizi zitahusisha kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66), Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry (One Lane Widening: km 25.1), Mbezi Victoria – Mpiji Magoe – Bunju (km 9.55), na Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 10). Vilevile kazi nyingine ni kuanza upanuzi wa barabara za Mwai Kibaki (km 9.1), Mbagala Rangi Tatu - Nzasa Jct (km 1.8), Chamazi Centre (km 1.2), Mbande - Chamazi Complex (km 1.0) na Gongo la Mboto - Buyuni (km 10). Fedha hizi pia zitatumika kulipa madeni ya Makandarasi wa barabara za Kipata (m 700), Livingstone (m 350), Msikitini – Sharif Shamba (km 1), Tangi Bovu – Goba (km 9), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6), Wazo Hill – Madale (km 6) pamoja na Ardhi – Makongo – Goba; sehemu ya Ardhi – Makongo (km 5).

**Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 107.4)**

**295. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 520.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nansio – Lugezi (km 6). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu za Kisorya – Bulamba (km 51) na Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4).

**Barabara ya Kolandoto – Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 122)**

**296. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kolandoto – Kishapu – Lalago (km 64); Sehemu ya Kolandoto – Kola Bridge (km 10) na Iguguno Shamba – Nduguti – Mkalama (km 89); Sehemu ya Iguguno Shamba – Mnolo (km 10).

**Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)**

**297. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 3,810.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Utete – Nyamwage (km 33.7), kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa barabara za Malendego – Tingi (km 50), Bungu – Nyamisati (km 40.03) na Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ikwiriri – Mkongo (km 27.74) na kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga (km 60).

**Barabara ya Kasulu – Manyovu (km 68)**

**298. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 32,752.49 zinazojumuisha Shilingi milioni 550.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 32,202.49 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68) na kuanza ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Manyovu/Mugina.

**Barabara ya Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2 (km 112.3)**

**299. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 60,538.48 zinazojumuisha Shilingi milioni 4,500.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 56,038.48 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa Nje katika Jiji la Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road) sehemu za Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3) na Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60), Kikombo Jct – Chololo – Mapinduzi (JWTZ HQ) ) (km 16.40) na Ntyuka Jct – Mvumi – Makulu (km 8.6). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Msalato – Mtumba – Chamwino IKULU (km 30) kwa kiwango cha lami pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mzunguko wa Ndani katika Jiji la Dodoma (Dodoma Inner Ring Road) kwa sehemu ya Bahi R/About – Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3) na Mzunguko wa Kati katika Jiji la Dodoma

(Dodoma City Middle Ring Road) inayoanzia Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Mkonze – Ntyuka – Nanenane (km 47.2).

**Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499)**

**300. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 5,000.00 kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 66.9) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Chalinze – Magindu – Lukenge – Seregete B – Kabwe Jct – Mkulazi (km 77.5). Mradi huu utahusisha pia kuendelea na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara ya Dakawa Jct – Mbigiri (km 7) na barabara zenye jumla ya kilometa 50 kuelekea mashamba ya wakulima wa miwa ya Mbigiri. Aidha, mradi huu utahusisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396) sehemu ya Ifakara – Lupilo – Mtimbira (km 112).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 383)**

**301. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 17,036.13 zinazojumuisha Shilingi milioni 540.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 16,496.13 fedha za nje kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Usesula – Komanga (km 115), Komanga – Kasinde (km 120), Kasinde – Mpanda (km 118), Tabora – Sikonge (km 30) na Mpanda Airport – Kasimba Jct (km 3) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235)**

**302. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 10,220.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Sanzate – Natta (km 40), kuanza ujenzi wa sehemu za Waso – Loliondo (km 10), Engaruka - Ngaresero (km 39), Mto wa Mbu – Selela (km 23), Selela – Engaruka (km 27) na Monduli – Engaruka (km 115): sehemu ya Ngarashi - Enguik (km 11) pamoja na kuendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Natta –

Mugumu (km 45). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Makutano –Sanzate (km 50) na Waso – Sale Jct (km 49).

**Barabara ya Ibanda – Itungi Port (km 26)**

**303. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 4,020.00 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa barabara za Ibanda – Itungi (km 26) na ujenzi wa sehemu ya Iponjola – Kiwira Port (km 6). Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi mpakani Kasumulu/Songwe (Kasumulu/Songwe– Tanzania/Malawi Border OSBP), pamoja na kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach (km 39.1) na barabara ya Uyole – Kasumulu (sehemu ya Ilima Escarpment, km 3).

**Barabara ya Nzega – Tabora (km 116)**

**304. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 1,220.00 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Puge – Ziba – Choma (km 109): sehemu za Ziba – Choma (km 1), Ziba – Nkinga (km 5) na Puge – Ndala (km 5). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Nzega – Puge (km 58.6) na Puge – Tabora (km 56.1).

**Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 803.6)**

**305. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 40,590.05 zinazojumuisha Shilingi milioni 12,240.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 28,350.05 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Mpanda – Mishamo – Uvinza: sehemu ya Vikonge – Luhafwe (km 25), Kibaoni – Mlele Jct (km 50), Luhafwe – Mishamo/Bulamata Jct (km 37.7), Mlele Junction – Sitalike (km 23.5), Kagwira – Ikola – Karema Port Lot 1: Kagwira – Kasekese (km 54.14) na Lot 2: Kasekese – Karema Port (km 59.3). Mradi huu utahusisha pia kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Mishamo –

Uvinza (km 100), Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.31) na Lyazumbi – Kabwe (km 65). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Sitalike – Mpanda (km 36) na Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 37.65).

**Barabara ya Nyanguge – Musoma/Usagara – Kisesa Bypass (km 202.25)**

**306. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 1,530.00 kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa sehemu ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4) na kuanza ujenzi wa barabara ya Airport – Kayenze – Nyanguge (Airport Bypass) (km 46): sehemu ya Airport Jct – Igombe (km 10). Kazi nyingine ni kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi wa barabara za Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5).

**Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 152.8)**

**307. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 1,010.00 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Handeni – Kang'ata (km 30) na kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Magole – Turiani (km 48.80).

**Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini DSM na Barabara Unganishi**

**308. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 510.00 kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo (Ubungo Interchange) pamoja na kuendelea na maandalizi ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, Fire pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct).

**Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 181)**

**309. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 30.00 kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Mwigumbi – Maswa (km 50.3), Maswa – Bariadi (km 49.7) na barabara ya Mchepuo wa Maswa (Maswa Bypass; km 11).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa (km 172)**

**310. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 1,000.00 kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25)**

**311. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 40,230.44 zinazojumuisha Shilingi milioni 5,520.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 34,710.44 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Kanyani Jct – Mvugwe (km 70.5), Mvugwe – Nduta Jct. (km 59.35), Nduta Jct. – Kibondo Jct. – Kabingo (km 62.5), Nduta Jct – Kibondo (km 25.9) na Kibondo – Mabamba (km 48). Kazi nyingine ni kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Kidahwe – Kasulu (km 63) na Nyakanazi – Kakonko (km 50).

**Barabara ya Kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mafia (Mafia Airport Access Road (km 16)**

**312. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 2,000.00 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kilindoni – Ras Mkumbi (km 54.4).

**Daraja la Kigamboni (Nyerere) na Barabara Unganishi**

**313. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 2,030.00 kwa ajili ya mchango wa Serikali kwenye

ujenzi wa Daraja la Nyerere, kuanza ujenzi wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (Kibada – Mwasonga – Songani Jct Section (km 41). Kazi nyingine ni kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Daraja la Nyerere – Vijibweni (km 1.5) na Tungi – Kibada (km 3.8).

**Barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 215.8)**

**314. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 3,300.00 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7): sehemu ya Kanazi (Kyetema) – Kalebe Bridge (km 10) pamoja na upanuzi wa barabara ya Bukoba – Bukoba Port (km 5). Kazi nyingine ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Bukoba Mjini – Busimbe – Maruku – Kanyangereko – Ngongo (km 19.1) na Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 136).

**Fedha za Matengenezo na Ukarabati wa Barabara**

**315. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 688,756.47 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2025/26 kwa ajili ya mradi huu. Kazi zitakazofanyika ni matengenezo na ukarabati wa barabara, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa vivuko pamoja na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya barabara na vivuko. Fedha hizi zinasimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati**

**316. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 330.00 kwa ajili ya maandalizi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati. Aidha, ujenzi wa mradi huu utajumuishwa kwenye Usanifu wa Kina kabla ya kufanya

ukarabati wa barabara za Ukanda wa Kati zilizopangwa kufanyiwa Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina ambazo ni Morogoro – Dodoma (km 260), Singida – Shelui (km 110) na Shelui – Nzega (km 110) ambazo Usanifu wa Kina unaendelea.

**Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

**317. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 500.00 kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7); sehemu ya Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2) na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji.

**Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119)**

**318. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 800.00 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**

**319. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 1,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu za Bunju – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma – Kigamboni (km 61) na Mbezi Mwisho (Kwa 116 Msuguri) – Kifuru – Banana – Kipara – Kigamboni (km 49).

**Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km 172.50)**

**320. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 10.00 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Muleba – Kanyambogo – Rubya (km 18.5).

**Barabara ya Singida – Shelui (km 110)**

**321. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 3,900.00 zimetengwa kwa ajili ya malipo ya madeni kwa Mhandisi Mshauri aliyefanya kazi ya Usanifu wa Kina wa barabara ya Singida – Shelui (km 110) na upanuzi wa barabara hii eneo la Mlima Sekenke (km 6). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Singida Urban – Ilongero – Haydom (km 93): Sehemu ya Singida Urban (Igauri) – Ilongero (km 11), kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga – Mkalama (km 46) na kuanza upanuzi wa barabara za Singida Mjini (km 10).

**Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road)**

**322. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 8,010.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza upanuzi wa sehemu za Mbagala Rangi Tatu – Kongowe - Mwanambaya (Vikindu) – Mkuranga (km 29.8) kutoka njia mbili kuwa njia sita. Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa sehemu ya Ikwiriri - Nyamwage – Malendego (km 56) na kuanza ujenzi wa barabara ya Mkuranga – Kisiju (km 46). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa daraja la Gerezani.

**Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 234.8)**

**323. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,510.00 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ukarabati wa sehemu ya Mafinga – Igawa (km 137.9) na kuendelea na upanuzi wa eneo la Mlima Kitonga (km 10). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152) pamoja na kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Morogoro – Iringa; sehemu ya Tumbaku Jct – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi (km 158.45).

**Barabara ya Korogwe – Mkumbara – Same (km 172)**

**324. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 6,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa

barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi (km 100.5); sehemu ya Ndungu – Mkomazi (km 36) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Same – Kisiwani – Mroyo (km 56.83). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa sehemu za Same – Himo (km 76) na Mombo – Lushoto (km 32) pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5).

**Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni (km 479.9)**

**325. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 8,330.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Itigi Mjini (km 10), sehemu za Noranga (Doroto) – Itigi (Mlongoji) km 25, Noranga – 118 Doroto & Itigi – Mkiwa (km 31.6) pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Makongolosi (km 56) na Makongolosi – Rungwa (km 256) pamoja na kuanza kazi ya usanifu wa barabara ya Manyoni East – Heka – Sanza – Chaligongo – Bihawana. Kazi nyingine ni kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Mbeya – Lwanjilo (km 36), Lwanjilo – Chunya (km 36) na Chunya – Makongolosi (km 39).

**Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211)**

**326. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 4,010.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha zege wa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nkomang'ombe – Mchuchuma (km 7) na sehemu ya tatu ya Mawengi - Ludewa – Manda (km 111) kwa kiwango cha lami. Aidha, fedha hizi zitatumika kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Lusitu – Mawengi (km 50).

**Ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (Tanzanite)**

**327. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 10.00 zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (km 1.03) na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa kilometa 5.2.

**Handeni – Kibirashi – Kibaya – Njoro – Goima – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 424.24)**

**328. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 6,500.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kwa sehemu za Handeni – Mafuleta (km 20) na Mafuleta – Kileguru (km 30). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kileguru – Kibirashi – Kibaya – Singida (km 374.24) sehemu ya Kisima – Kibaya (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makambako – Songea na Barabara ya Mchepuo ya Songea (Songea Bypass) (km 295)**

**329. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 22,999.79 zinazojumuisha Shilingi milioni 3,000.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 19,999.79 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea sehemu ya Lutukila – Songea (km 95.18), ujenzi wa barabara ya Mchepuo wa Songea (Songea Bypass: km 11) pamoja na kuanza ujenzi wa barabara ya Ramadhani – Iyayi - Ilembula Hospital (km 75); Sehemu ya Ramadhani – Itulike (km 10). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Makambako – Lutikila (km 184).

**Barabara ya Dodoma – Iringa (km 267.1)**

**330. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 4,810.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass km 7.3), kuimarisha matabaka ya barabara ya Iringa – Dodoma (km 20), kulipa madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa Mizani kwenye barabara ya Iringa – Dodoma na kuanza ujenzi wa barabara ya Iringa – Pawaga (km 71.9); Sehemu ya Pawaga Jct – Ikonongo (km 5) na Itunundu – Ilolo mpya (km 20) na Bihawana Jct - Bihawana roundabout (km 10).

**Barabara ya Dodoma – Babati (km 263.4)**

**331. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 1,930.00 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Dareda – Dongobesh (km 60): sehemu ya Dareda Mjini – Dareda Mission (km 8) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35) na Mela – Bonga (km 88.8).

**Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 343.2)**

**332. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 690.00 kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Tunduru – Matemanga (km 59), Matemanga – Kilimasera (km 68.2), Kilimasera – Namtumbo (km 60) na Mbinga – Mbamba Bay (km 66). Aidha, mradi huu unahusisha kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi – Tunduru (km 300).

**Ujenzi wa Barabara za Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute)**

**333. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 220.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za ndani ya eneo la Chuo cha Uongozi Bagamoyo (km 8.8).

**Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma na Mbeya Bypass (km 266.9)**

**334. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 5,300.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa sehemu ya Mlima Nyoka - Nsalaga - Uyole - Ifisi - Songwe Airport; sehemu ya Uyole – Ifisi – Songwe Airport (km 36) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Uyole – Songwe (Mbeya Bypass: km 48.90) na Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa PPP. Aidha, mradi huu utahusisha kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mbalizi – Shigamba (km 52) na Iwambi – Mbalizi Bypass (km 6.5).

**Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT Phase I – V: km 69.8)**

**335. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 107,121.58 zinazojumuisha Shilingi milioni 2,960.00 fedha za ndani na Shilingi milioni 104,161.58 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu na Nne. Aidha, fedha hizi zitatumika kuendelea na maboresho ya miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka iliyojengwa katika Awamu ya Kwanza, kuanza ujenzi wa daraja la Jangwani pamoja na kuanza ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano. Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili.

**Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT)**

**336. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 2,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT) Mkoani Morogoro na majengo ya ICoT tawi la Mbeya. Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania

**337. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 4,070.21 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala ya Barabara (TANROADS) pamoja na kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

**Udhibiti Uzito wa Magari, Masuala ya Usalama Barabarani na Mazingira**

**338. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi wa Usalama Barabarani umetengewa jumla ya Shilingi milioni 1,232.63 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa kituo cha mizani cha Buhigwe katika barabara kuu ya Kasulu-Manyovu; Ujenzi wa kituo cha mizani cha Kidyama katika barabara kuu ya Kasulu- Kibondo na Ujenzi wa kituo cha mizani

cha Marolegwa katika barabara kuu ya Kibondo - Kakonko. Kazi nyingine ni kujenga mizani 32 ya kisasa inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo. Vilevile, fedha za mradi huu zitatumika kuwezesha utengenezaji na usimikaji wa mfumo wa usimamizi wa mizani kwenye mizani 58 na kuwezesha huduma ya ushauri kwa mapitio ya Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani. Kazi nyingine ni kuwezesha ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Pamoja - One Stop Inspection Stations (OSIS) vya Idofi (Njombe), Iboya (Songwe), Himo (Kilimanjaro) na Segera (Tanga) pamoja na kuwezesha uboreshaji wa maeneo ambayo ajali nyingi zimekuwa zikitokea (Black spot areas) katika barabara kuu maeneo ya Sekenke (Singida) na Iyovi (Iringa).

**339. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi Katika Masuala ya Usalama Barabarani na Mazingira umetengewa Shilingi milioni 55.81 kwa ajili ya kuwezesha huduma za ukaguzi wa barabara (Road safety audits) kwa baadhi ya barabara za mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Mbeya, Songwe, Manyara, Singida, Arusha na Tanga.

**340.** MheshimiwaSpika, mradi waMenejimenti ya Usimamizi wa Mazingira umetengewa Shilingi milioni 81.71 kwa ajili ya kuandaa mkakati wa Wizara ya Ujenzi wa usimamizi wa maafa; kufanya mapitio ya miongozo ya tathmini na usimamizi wa mazingira ya Sekta ya Ujenzi na kuandaa mpango kazi wa mazingira kisekta wa miaka mitano (Sector Environmental Action Plan, 2025-2030).

**Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

**341. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26 mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko umetengewa jumla ya Shilingi milioni 24,207.99 kwa ajili ya kazi zifuatazo:

**342. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi wa Maegesho ya Vivuko na Mifumo, umetengewa jumla ya Shilingi milioni 2,929.08 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wakazi wa Kigamboni watakaopisha eneo la upanuzi wa maegesho Kigamboni pamoja na ujenzi na ukarabati wa maegesho 12 (Magogoni – Kigamboni, Bugolora -

Ukara, Iramba - Majita, Nyakarilo - Kome, Ilagala - Kajeje, Rusumo - Nyakiziba, Musoma - Kinesi, Kasharu - Buganguzi, Kisorya - Rugezi, Kahunda - Maisome, Bukimwi na Rugasa). Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, majengo ya abiria na uzio kwenye vituo 23 vya vivuko ambavyo ni; Ilagala - Kajeje, Iramba - Majita, Kinesi, Ilunda - Luchelele, Kasharu - Bungaguzi, Rusumo - Nyakiziba, Buyagu - Mbalika, Mlimba - Malinyi, Kilambo, Ijinga - Kahangala, Bwiro - Bukondo, Nkome - Kikumbaitale, Kahunda - Maisome, Msanga Mkuu - Msemo, Kisorya - Rugezi, Bezi - Bukimwi, Nyakarilo - Kome na Bugolora – Ukara.

**343. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi nyingine ni ujenzi wa maegesho mapya ya vivuko vya Kayenze - Kanyinya, Muleba – Ikuza mkoani Kagera, Ijinga - Kahangala (Magu), Bwiro – Bukondo (Ukerewe) mkoani Mwanza, Buyagu-Mbalika, Ilunda-Luchelele, Kilambo - Namoto, Utete - Mkongo na Kamanga - Kirumba Mwaloni, Chato, Muharamba, Kikumbaitale, Zumacheli na Nkome katika kituo cha Chato – Nkome; ujenzi wa maegesho na miundombinu katika vituo vya Boza – Kuruti, Shungubweni (Ngwevu) na Kisiju Pwani kisiwa cha Kwale(Pwani); kusimika Mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa vivuko na Mifumo ya Tiketi katika vituo 22; kufanya matengenezo kinga ya maegesho ya vivuko vyote pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya miradi hiyo.

**344. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi wa Ujenzi wa Vivuko Vipya umetengewa Shilingi milioni 9,691.28 kwa ajili ya ununuzi wa vivuko vipya vya Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo, Nyakarilo – Kome, Nyamisati – Mafia, Buyagu – Mbalika na ununuzi wa boti mbili kwa ajili ya kutoa huduma maeneo ya Boza – Kuruti, Shungubweni (Ngwevu) na Kisiju Pwani – Kisiwa cha Kwale. Kazi nyingine ni ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA, kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Maboresho ya Utendaji Kazi wa TEMESA (TEMESA Transformation Strategy), huduma za ushauri pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo.

**345. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi wa Ukarabati wa Vivuko umetengewa jumla ya Shilingi milioni 11,587.63 kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa vivuko MV Mara, MV Ujenzi, MV Kome II, MV Misungwi, MV Nyerere, MV Kyanyabasa, MV Kitunda, MV Lindi, MV Kazi, MV Magogoni, MV Kigamboni, MV Ukara I, MV Ukara II,

MV Sabasaba, MV Pangani II pamoja na ukarabati wa MV Kilombero II kabla ya kukihamishia eneo la Mlimba – Malinyi. Kazi nyingine ni ukarabati wa boti ya uokozi ya MV SAR III, ukarabati wa kivuko MV Malagarasi na MV Mafanikio pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya miradi hiyo. Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

**346. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, jumla ya Shilingi milioni 28,897.23 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali. 347. MheshimiwaSpika, jumla ya Shilingi milioni 2,000.00 zimetengwa kwa ajili ya Ujenzi wa jengo la makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Temeke Kota. Aidha, mradi wa Ujenzi wa jengo la makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Magomeni Kota Wilaya ya Kinondoni umetengewa Shilingi milioni 3,000.00 na Shilingi milioni 1500.00 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Ghana Kota (Block II) katika Mkoa wa Mwanza.

**348. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ujenzi wa jengo la Makazi kwa ajili ya watumishi wa Umma katika eneo la Kaloleni Kota (Block II) katika Mkoa wa Arusha umetengewa Shilingi milioni 2,330.82. Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 200.00 kimetengwa kwa ajili ya Ununuzi wa nyumba (Chimala Apartments) za Watumishi wa Umma, jijini Dar es Salaam. Kiasi cha Shilingi milioni 4,050.00 kimetengwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa nyumba 20 za Viongozi Dodoma, Shilingi milioni 2,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 150 za Watumishi wa Umma Nzuguni jijini Dodoma na Shilingi milioni 1.00 kwa ajili ya ushauri katika ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi awamu ya II.

**349. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 6,500.00 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa Ukarabati wa Nyumba. Kazi zitakazofanyika ni ukarabati wa nyumba 40 za viongozi Dodoma na nyumba 30 za Viongozi Dar es Salaam, nyumba za makazi 644 Magomeni Kota. Kazi nyingine ni ukarabati wa nyumba nyingine 66 zilizokuwa zinamilikiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) zilizohamishiwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), pamoja na ukarabati wa

nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI zilizohamishiwa TBA katika mikoa 20.

**350. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 5,076.70 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi na ukarabati wa Karakana za TEMESA na TBA. Kazi zitakazohusika ni ukarabati wa karakana 14 za TEMESA katika Mikoa ya Tabora, Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya, M.T Depot - Dar es Salaam, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani, Dodoma, Tanga, Kagera na Lindi. Aidha, fedha hizi zitatumika kufanya ukarabati wa karakana ya mitambo (heavy plant) ya TEMESA iliyopo Morogoro inayotumika kutengeneza mitambo ya barabara ambayo baadae itatumika kama karakana ya Mkoa wa Morogoro. Vilevile, zitatumika kuendelea na ujenzi wa karakana za TEMESA katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe, Katavi na karakana mpya ya kisasa Jijini Dodoma pamoja na kugharamia ushauri na usimamizi wa miradi ya Karakana za TEMESA. Kazi nyingine ni ukarabati wa karakana sita (6) za TBA katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Morogoro, Tabora, Dar es Salaam na Mbeya.

**351. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, kazi ya Kusanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari, Umeme na Elektroniki imetengewa jumla ya Shilingi milioni 350.00. Aidha, jumla ya Shilingi milioni 512.83 zimetengwa kwa ajili ya Ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi ya ujenzi na ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali pamoja na wahitimu wa Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi.

**352. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, kazi za Kujenga Uwezo wa Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi na Huduma za Ushauri zimetengewa jumla ya Shilingi milioni 778.28 kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kupitia Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB). Kazi nyingine ni huduma za ushauri katika ujenzi wa jengo la Wizara za Ujenzi na Uchukuzi (awamu II) katika eneo la Mtumba Jijini Dodoma pamoja na kuendelea na kazi ya utungaji wa Sheria ya Majengo, kanuni pamoja na miongozo ya viwango msawazo (standard specifications).

**353. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi awamu ya pili zimetengewa jumla ya Shilingi milioni 0.90 kwa ajili ya ujenzi. Aidha, kazi ya uandaaji wa "Building Code", Sheria za Majengo, viwango na viwango msawazo vya majengo ya Serikali imetengwa jumla ya Shilingi milioni 596.70.

**Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege**

**354. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege imetengewa jumla ya Shilingi milioni 343,869.66. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni 45,843.35 ni fedha za ndani na Shilingi milioni 298,026.31 ni fedha za nje. Miradi ifuatayo imepangwa kutekelezwa:

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**

**355. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 22,910.24 zinazojumuisha Shilingi milioni 8,248.49 fedha za ndani na Shilingi milioni 14,661.75 fedha za nje. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu yake (ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani). Kazi nyingine ni ujenzi wa uzio wa usalama, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

**356. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 12,728.67. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni 3,728.67 ni fedha za ndani na Shilingi milioni 9,000.00 ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria na miundombinu yake, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe**

**357. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 4,317.37 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Washauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege pamoja na eneo la usalama (Runway End Safety Area-RESA), usimikaji wa taa za usalama na taa za kuongozea ndege na umaliziaji wa jengo la abiria.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

**358. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 4,380.57 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi za upanuzi na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maungio ya ndege, maegesho ya ndege, jengo la kuongozea ndege, jengo la mizigo pamoja na ujenzi wa mifumo ya maji safi na majitaka.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

**359. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 1,717.44 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi zilizokamilika ambazo ni ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake, maegesho ya ndege, kusimika taa za kuongozea ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na uzio wa usalama.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**

**360. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 16,540.20 zinazojumuisha Shilingi milioni 1,878.45 fedha za ndani na Shilingi milioni 14,661.75 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi nyingine ni usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na ujenzi wa uzio wa usalama.

## Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga

**361. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 12,763.27 zinazojumuisha Shilingi milioni 2,878.46 fedha za ndani na Shilingi milioni 9,884.81 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa. Aidha, kazi nyingine ni usimikaji wa mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa uzio wa usalama.

## Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa

**362. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 153,595.79 zinazojumuisha Shilingi milioni 16,095.59 fedha za ndani na Shilingi milioni 137,500.20 fedha za nje. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Iringa, Musoma, ujenzi wa uzio wa usalama kwenye kiwanja cha ndege cha Geita pamoja na kulipa madeni ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Songea. Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Lake Manyara, Iringa (awamu ya pili) na Tanga.

## Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato

**363. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 114,866.66 zinazojumuisha Shilingi milioni 2,548.86 fedha za ndani na Shilingi milioni 112,317.80 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Kimataifa cha Msalato mkoani Dodoma.

## Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)

**364. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mradi huu umetengewa jumla ya Shilingi milioni 49.45 fedha za ndani kwa ajili ya kulipa madeni

ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi za ujenzi wa jengo la tatu la abiria.

**Mradi wa Kujenga Uwezo (Institutional Capacity Building)**

**365. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi milioni 246.37 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu kwa lengo la kujenga uwezo wa watumishi wa Sekta ya Ujenzi kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi vya ofisi kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi.

**Fedha za Mfuko wa Barabara**

**366. Mheshimiwa Mwenyekiti**, fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi katika mwaka wa fedha 2025/26 ni jumla ya Shilingi 688,756,470,000.00. Kati ya fedha hizo, TANROADS imetengewa Shilingi 608,466,468,597.12 kwa ajili ya kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara kuu na za mikoa na Wizara ya Ujenzi imetengewa Shilingi 67,607,385,399.68 kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara za mikoa, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, Shilingi 12,682,616,003.02 zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**367. Mheshimiwa Mwenyekiti**, mgawanyo wa Shilingi 67,607,385,399.68 zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ni kama ifuatavyo: Shilingi 15,820,073,000, ni kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara zenye urefu wa kilometa 8,049.67 na Shilingi 38,931,644,607.68 zimetengwa kwa ajili ya miradi ya barabara za mikoa itakayohusisha ukarabati wa jumla ya kilometa 340 kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa kilometa 30 kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja/makalavati 33 katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, Shilingi 4,281,315,083.52 ni kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho na miundombinu ya vivuko; Shilingi 3,570,357,225.92 ni kwa ajili ya miradi ya usalama Barabarani na Mazingira na Shilingi 5,003,995,182.60 ni kwa ajili ya kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara pamoja na kujenga uwezo wa watumishi.

*Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi umeoneshwa katika Viambatisho Na. 3 na 4.*

**368. Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya Shilingi 608,466,468,597.22 fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zimetengwa kwa ajili ya TANROADS zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja na uendeshaji wa mizani.

*Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika Viambatisho Na. 5, 5A - 5D.*

**H.3: MPANGO WA KAZI ZA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26**

**Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)**

**369. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wakala wa Barabara Tanzania umepanga kujenga barabara kuu zenye urefu wa kilometa 365 kwa kiwango cha lami, ukarabati wa kilometa 45 kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja 19, ukarabati wa daraja 1, kuanza ujenzi wa madaraja manne (4) na kufanya maandalizi ya ujenzi wa madaraja 9. Kazi nyingine ni kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara zenye urefu wa kilometa 8,049.67 na madaraja mawili (2) ambayo ni Bujonde (Kyela) na Sanga (Simiyu) katika barabara kuu na baadhi ya barabara za Mikoa (Kasma 4126).

**370. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi ya barabara za mikoa iliyopangwa kutekelezwa na Wakala ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 85. Kati ya hizo, kilometa 45 zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na kilometa 30 zitajengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. Vile vile, Wakala umepanga kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara zenye urefu wa kilometa 820. Kati ya hizo, kilometa 480 zitakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na kilometa 340 zitakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, Wakala umepanga kujenga na kufanya ukarabati wa madaraja/makalavati 78,

ambapo kati ya hayo, madaraja/makalavati 45 yatatumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na 33 yatatumia fedha za Mfuko wa Barabara.

**371. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wakala pia umepanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa kilometa 35,311.01 matengenezo ya muda maalum kilometa 2,994.31, matengenezo ya sehemu korofi kilometa 305.47 pamoja na matengenezo ya madaraja 2,865. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

**372. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, Wakala utaendelea na majukumu ya kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege vilivyokasimiwa Wizara ya Ujenzi. Miradi iliyopangwa kutekelezwa imeainishwa katika Aya 354-364.

**Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)**

**373. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) utaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutumia fedha za ruzuku ya Serikali pamoja na mapato ya ndani ya Wakala. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kutoa huduma za ushauri kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali, kujenga majengo ya Washitiri mbalimbali; kuuza na kupangisha nyumba zinazojengwa na TBA kwa Watumishi wa Umma na kupangisha baadhi ya majengo ya Serikali kwa wasio watumishi wa Umma ili kuongeza uwezo wa Wakala kujiendesha.

**374. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa kutumia fedha za ruzuku imeoneshwa katika Aya 346-353.

**375. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi itakayotekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ya Wakala ni:- Kupata hati miliki za mali za TBA (viwanja); Ununuzi wa mitambo na mashine saba (two weighbridges for batching plants,two lawbeds trucks, two block

making machinery and one generator); Ujenzi wa nyumba 72 za watumishi wa umma Mikoani; Ujenzi wa jengo 1 la Ghorofa kwa ajili ya watumishi wa umma huko Ghana Kota Mwanza (Block I); Ujenzi wa Jengo 1 la Ghorofa kwa ajili ya watumishi wa umma katika kijiji cha Kanada Jijini Dar es Salaam; Ujenzi wa maabara ya kupima ubora wa vifaa vya Ujenzi; Ujenzi wa Jengo 1 la Ghorofa kwa ajili ya watumishi wa umma Kaloleni – Arusha; Ujenzi wa ofisi ya TBA Mkoa wa Geita na Ujenzi wa maduka 93 eneo la Nzuguni Dodoma

**376. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi mingine ni:- Ukarabati wa Majengo mbalimbali Jijini Dar es Salaam na Mikoani; Ukarabati wa ofisi za mikoa za TBA katika Mikoa 20; Ujenzi wa Magorofa ya Watumishi wa Umma Misheni Kota Geita na; Ukarabati Karakana 2 mikoa ya Rukwa na Ruvuma.

**377. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wakala pia umepanga kutekeleza miradi 317 ya Washitiri. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: miradi 24 ni ya Buni1Jenga (Design and Build) ambapo hadi sasa miradi sita (6) inaendelea kutekelezwa.

**378. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, Wakala utaendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba Dodoma ikiwemo ujenzi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, Wakala utatekeleza miradi 17 ya Ushauri Elekezi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi za Serikali.

**379. Mheshimiwa Mwenyekiti**, halikadhalika, Wakala umepanga kutekeleza miradi 193 ya Ushauri (Consultancy) ambapo kati ya hiyo 59 inaendelea. Aidha, Wakala umepanga kutekeleza miradi 79 ya Ujenzi ambapo miradi 15 inaendelea na miradi minne (4) ya Usimamizi (Project Management) ambapo kati ya hiyo miradi miwili (2) inaendelea.

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA)**

**380. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wakala umepanga kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa vivuko vya Serikali, kutoa huduma ya ukodishaji wa

magari na mitambo ya ujenzi pamoja na kufanya matengenezo ya magari, usimikaji wa mifumo ya umeme, majokofu, viyoyozi na elektroniki. Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa maboresho ya Utendaji kazi wa TEMESA (TEMESA Transformation Strategy) ulioidhinishwa mwezi Disemba, 2024 ambapo moja ya mabadiliko makubwa yaliyofanywa na Wakala ni kuanza kutoa huduma ya matengenezo ya magari kwa malipo kabla (prepaid) kuanzia Januari, 2025.

**381. Mheshimiwa Mwenyekiti**, miradi ya Ruzuku itakayotekelezwa na Wakala katika mwaka wa fedha 2025/26 inahusisha maegesho na miundombinu ya vivuko, Ukarabati wa Vivuko, Ujenzi wa Vivuko Vipya na Ujenzi na Ukarabati wa Karakana ni kama inavyoonekana kwenye Aya 341-345.

**382. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wakala umepanga kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa vivuko vya Serikali vipatavyo 32 ambavyo vinatarajiwa kutoa huduma kwa abiria 18,103,134 magari 586,279 na tani za mizigo 634 kwa mwaka. Wakala umepanga kufanya matengenezo ya magari 29,063, matengenezo na usimikaji wa mifumo 55 ya umeme, 312 ya majokofu na viyoyozi na mifumo 17 ya elektroniki. Vilevile, Wakala umepanga kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo 37 ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu na kusimamia mifumo hiyo inayofikia 58. Wakala pia utaendelea kutoa huduma ya ukodishaji wa mitambo ya magari na mitambo ya ujenzi wa barabara.

**Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB)**

**383. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 983,937,814,285 katika mwaka wa fedha 2025/26 kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, Shilingi 676,073,853,997 ni kwa ajili ya kugharamia kazi za barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi (Fungu 98). Aidha, Shilingi 289,745,937,427 ni kwa ajili ya kugharamia kazi za barabara za Wilaya ambazo husimamiwa na Ofisi ya Rais –TAMISEMI (Fungu 56). Mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara kwa kila taasisi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni

kama ifuatavyo: Wizara ya Ujenzi Shilingi 67,607,385,400; TANROADS Shilingi 608,466,468,597; Ofisi ya Rais – TAMISEMI Shilingi 28,974,593,743; TARURA Shilingi 260,771,343,684; na Bodi ya Mfuko wa Barabara Shilingi 18,118,022,861.

**384. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kazi zitakazotekelezwa na Bodi ni pamoja na kuendelea kufuatilia matumizi ya fedha zinazopelekwa kwa wakala wa barabara (TANROADS na TARURA) ili kuhakikisha kuwa zinatumika kwa madhumuni yaliyowekwa. Aidha, Bodi itaendelea kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za barabara katika mikoa yote nchini ili kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inakidhi thamani ya fedha zilizotumika (value for money).

**385. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa fedha za matengenezo ya barabara, Bodi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imepanga kuendelea kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali ili kupata vyanzo vipya vya mapato na teknolojia ya gharama nafuu ya matengenezo ya barabara. Vilevile Bodi itaratibu mapitio na maandalizi ya miongozo mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi wa makusanyo yanayotokana na matumizi ya hifadhi za barabara. Aidha, Bodi itakamilisha uundaji wa mfumo wa kielektroniki utakaotumika kusimamia makusanyo ya mapato yatokanayo na hifadhi ya barabara na mfumo wa kusimamia taarifa na takwimu za miundombinu ya barabara hapa nchini. Katika jitihada ya kupunguza changamoto za kupata fedha za kutosha kwa mara moja ili kugharamia matengenezo maalum ya barabara, Bodi itakamilisha taratibu za kupata fedha kutoka kwenye soko la mitaji na dhamana kupitia hatifungani ili kugharamia matengenezo hayo.

**386. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, Bodi imepanga kuendelea na ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote nchini na kuhakikisha mipango ya matengenezo ya barabara inazingatia mabadiliko ya tabia nchi ili kupunguza kiwango na athari za mabadiliko hayo katika kazi za barabara.

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB)**

**387. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) imeweka malengo ya kusajili Wahandisi 3,820, Mafundi Sanifu 500, Kampuni za Ushauri wa Kihandisi 18 na maabara 141 za kupima ubora wa vifaa tano (5). Vilevile, Bodi imepanga kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi Wahitimu 4,657 ambapo Wahandisi Wahitimu watakaokuwa wanaendelea na mafunzo ni 4,317 na Wahandisi wapya 1,200.

**388. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Bodi vilevile imepanga kuendelea kufanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini ili kuhakikisha kuwa shughuli zote za kihandisi zinafanywa na wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi. Bodi pia itaendelea na jukumu lake la kutembelea na kukagua miradi yote ya ujenzi ya kimkakati pamoja na barabara za Halmashauri pamoja na kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi watalaam na washauri. Aidha, Bodi itaendeleza jitihada za kuwashawishi wahandisi wataalam ili waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani kwa lengo la kusogeza huduma hii karibu na watumiaji.

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB)**

**389. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi imepanga kusajili Wataalamu 225 katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Usanifu Teknolojia ya Majengo, Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi wa Miradi. Aidha, Bodi imepanga kusajili kampuni 35 za Ushauri elekezi kwenye fani hizo zilizotajwa hapo juu. Bodi pia imepanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi 4,259 katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara pamoja na kusajili miradi ya ujenzi 1,775.

**390. Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile, Bodi imepanga kuwajengea uwezo Wahitimu 313 wa fani hizo kupitia mpango maalumu wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahitimu wa Vyuo Vikuu

(Architectural and Quantity Surveying Internship Programme – AQIP). Aidha, katika kutekeleza programu za kujengea uwezo Wataalam wa fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Usanifu Teknolojia ya Majengo, Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi Miradi, Bodi imepanga kuendesha mitihani ya kitaalamu kwa Wahitimu 340 katika fani za Ubunifu majengo na Ukadiriaji majenzi. Bodi pia imepanga kutembelea Vyuo Vikuu 5 ili kuwahamasisha kuanzisha fani za Ubunifu majengo na Ukadiriaji majenzi ili kukuza idadi ya Wataalam hawa nchini. Aidha, Bodi pia itafanya mikutano 5 na Wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari pamoja na kuendesha mashindano ya Insha kwa lengo la kuhamasisha Wanafunzi hao kusoma masomo ya Sayansi na hatimaye kusomea taaluma za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na taaluma nyingine zinazoshabihiana nazo.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB)**

**391. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Bodi imepanga kusajili jumla ya Makandarasi wapya 1,600 na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi 3,550. Aidha, Bodi itaendesha kozi za mafunzo sita (6) na mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika kituo kimoja. Vilevile, Bodi imepanga kufanya mkutano mmoja (1) wa mashauriano na wadau wa sekta ya ujenzi.

Bodi pia itaendelea kuendesha Mfuko maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia Makandarasi wa ndani (Contractor's Assistance Fund – CAF) pamoja na kuendelea kuhamasisha Makandarasi wa ndani kujiunga pamoja ili kuomba zabuni kwa mfumo wa ubia.

**Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC)**

**392. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Baraza limepanga kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ujenzi nchini; kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa Maendeleo wa Sekta ya Ujenzi pamoja na kuandaa jukwaa la Sekta ya Ujenzi na Wiki ya Huduma za Ujenzi. Vilevile, Baraza litaendelea kushiriki

katika utungwaji wa Sheria ya Majengo (Building Act), Taratibu za Majengo (Building Codes) na Viwango Msawazo vya ujenzi wa majengo na samani za Serikali. Baraza pia litaendelea kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kwa wadau wa Sekta ya ujenzi; kuendelea kuchapisha taarifa ya utendaji wa Sekta ya Ujenzi; kuratibu utatuzi wa migogoro inayotokea katika miradi ya ujenzi pamoja na kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha Sekta ya Ujenzi nchini.

**393. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kutoa huduma za ukaguzi wa kiufundi katika miradi ya ujenzi kwa wadau wa Sekta ya Ujenzi na kuendesha kozi 12 za mafunzo ya kujenga uwezo wa wadau 240 wa Sekta ya Ujenzi nchini. Aidha, Baraza limepanga kukusanya na kuchapisha takwimu za mwenendo wa bei za bidhaa na huduma za ujenzi kwa mwaka, kuandaa miongozo na taarifa za Sekta ya Ujenzi na kuanza kutumia wa kuhudumia wadau wa Sekta ya Ujenzi (CONTAS) na mfumo wa kuchakata taarifa na kutoa gharama za ujenzi na matengenezo ya barabara.

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji Tanzania (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre – TANT2)**

**394. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Kituo kimepanga kuendelea kusambaza teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji hapa nchini. Aidha, kituo kitaendelea kushirikiana na Kitengo cha Utafiti na Maendeleo Research Development Unit (RDU) cha Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kufanya tathmini na ufuatiliaji wa teknolojia mbalimbali mpya na mbadala katika ujenzi na matengenezo ya barabara nje na ndani ya nchi ili kuwezesha Wizara kupata teknolojia stahiki zenye ufanisi na gharama nafuu, kuandaa, kuchapisha na kusambaza majarida yake yanayoandaliwa kwa ajili ya ya usambazaji teknolojia kwa wadau, kutafuta maarifa na taarifa mbalimbali muhimu katika Sekta za Ujenzi na Usafirishaji. Vilevile, kituo kitaendelea kupokea na kusambaza majarida kutoka kwa wadau mbalimbali yanayohusu teknolojia, maarifa na taarifa muhimu katika Sekta za Ujenzi na Usafirishaji.

**395. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kazi nyingine zilizopangwa ni kuandaa na kuendesha mafunzo kwa wadau yanayolenga kutatua changamoto zinazoikabili Sekta za Ujenzi na Usafirishaji; Kuratibu shughuli mbalimbali za uanzishwaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT); Kushiriki katika kuandaa na kufanyika kwa Mkutano wa Vituo vya usambazaji wa Teknolojia Afrika (yaani 10th T2 Centre Conference) unaofanyika kila mwaka; na kuendesha makongamano ya Watalaam wa taasisi mbalimbali zinazohusika na miundombinu na usafirishaji ili kujadili na kutafuta majibu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta za Ujenzi na Usafirishaji. Pia kituo kitashiriki katika kufanya tafiti za matumizi ya teknolojia mpya mbalimbali katika ujenzi wa barabara ndani na nje ya nchi. Vilevile, kituo kitashiriki katika Kamati za Kujenga Uwezo za SADC chini ya ASANRA, Shirikisho la Barabara Duniani (PIARC) na International Road Federation (IRF) katika kubadilishana Tekinolojia na maarifa mapya.

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT)**

**396. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26 Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi Kampasi ya Morogoro imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: - kufanya mapitio ya mitaala (curriculum review) ya mafunzo ya ngazi ya Stashahada, kudahili wanafunzi wapya 150 katika ngazi ya cheti (NTA level 4) na kutoa mafunzo kwa wanafunzi 247 wanaoendelea na masomo ya stashahada katika fani za uhandisi Ujenzi, Umeme na Mitambo. Kudahili wanafunzi wapya 210 wa Elimu ya ufundi stadi (VET).na kuendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 440 wanaoendelea na masomo. katika Elimu ya ufundi stadi (VET). Taasisi vilevile imepanga kuendelea kutoa kozi fupi kwa jumla ya washiriki 450 katika kozi ya udereva wa awali na udereva wa magari ya abiria, washiriki 100 katika kozi ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya nguvukazi, kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya nguvukazi ya na kufanya tathmini ya mafunzo kwa vitendo yanayofanyika viwandani na wanafunzi wa kozi ndefu za Stashahada (‘NTA level 4’ na ‘NTA level 5’) pamoja na wanafunzi wa Elimu ya ufundi Stadi.

## I. MASUALA MTAMBUKA

### Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Barabara

**397. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ya kuwajengea uwezo wanawake ili kuongeza ushiriki wao katika kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara nchini. Katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imepanga kutoa mafunzo kwa Makandarasi wanawake juu ya namna ya kuomba na kujaza zabuni kwa ufanisi; kutoa mafunzo kwa wanawake na vikundi vya wanawake kuhusu kufanya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi, ikiwa ni pamoja na kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi baada ya mafunzo. Kazi nyingine ni kufuatilia kwa karibu kazi za barabara zinazofanywa na Makandarasi wanawake, ili kuhakikisha kuwa wanawake wanapata fursa sawa katika utekelezaji wa miradi ya barabara. Aidha, Wizara itaendelea kutenga miradi maalum (matengenezo/maendeleo) ya kuwajengea uwezo wanawake ili kuweza kukuza ushiriki wao na kukuza kampuni za wanawake wazawa, na pia kuhakikisha wanawake wanapata mafunzo na msaada wa kiufundi wa hali ya juu ili waweze kushindana kwa ufanisi katika zabuni za miradi ya barabara.

**398. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara pia imepanga kutembelea vyuo vya elimu ya juu ili kuwahamasisha wanawake katika fani ya uhandisi na kuendelea kuhamasisha wasichana wanaosoma masomo ya sayansi na hisabati katika shule za sekondari, kwa lengo la kuongeza idadi ya wasichana wanaojiunga na fani zinazohusiana na sekta ya ujenzi. Kazi zingine zilizopangwa ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara, ikiwa ni pamoja na kusambaza miongozo ya ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara, ili kuhakikisha kuwa kila mdau katika sekta ya ujenzi anapata ufahamu kuhusu namna bora ya kuwashirikisha wanawake katika miradi ya barabara.

### Mapambano dhidi ya VVU na Magonjwa Yasiyoambukiza

**399. Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu kujikinga na maambukizi ya VVU na magonjwa yasiyoambukiza kwa watumishi wa Wizara. Aidha, Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi waliotoa taarifa ya kuathirika na virusi vya UKIMWI kwa kuwapatia posho ya chakula ili waweze kupata lishe bora ili kupunguza makali ya virusi hivyo.

### Mapambano dhidi ya Rushwa

**400. Mheshimiwa Mwenyekiti**,katika mwaka 2025/26, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali katika mapambano dhidi ya Rushwa kukuza uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma. Wizara itaendelea kutoa mafunzo yanayohusu maadili na kuzuia vitendo vya rushwa kupitia mikusanyiko mbalimbali ya watumishi ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

## J. SHUKRANI

**401. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ninapohitimisha, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa watendaji wenzangu Wizarani. Kipekee nawashukuru sana viongozi wenzangu wa Wizara ambao ni Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb.), Naibu Waziri, Balozi Mhandisi Aisha Salim Amour, Katibu Mkuu pamoja na Dkt. Charles Enock Msonde, Naibu Katibu Mkuu. Ama kwa hakika, katika kipindi hiki kifupi nilichoongoza Wizara hii nimepata ushirikiano wa kutosha kutoka kwao katika usimamizi wa Wizara hii. Aidha, sitakuwa muungwana nisipoishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa moyo wa uzalendo na kujitolea waakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

**402. Mheshimiwa Mwenyekiti**, nitumie fursa hii kipekee kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mkuranga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika majukumu yangu ya kuwawakilisha na kuwasemea. Sambamba na hilo, niishukuru sana familia yangu, ya mbali na ya karibu, ikiongozwa na mke

wangu mpendwa kwa kuendelea kuniombea, kunivumilia na kunipa amani ya moyo wakati wote hususan nikiwa nje ya nyumbani kwa muda mrefu nikitekeleza majukumu yangu. Sina maneno mazuri zaidi ya kusema Ahsanteni sana, na Mwenyezi Mungu awabariki.

**403. Mheshimiwa Mwenyekiti**, utekelezaji wa majukumu ya Wizara umefanikiwa kupitia ushirikiano wa Serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na wa nje. Na hapa **Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa ridhaa yako, naomba kuwatambua wachache kati ya walio wengi walioshirikiana nasi kwa namna moja au nyingine kama ifuatavyo: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan International Cooperation Agency (JICA), OPEC Fund, Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Kuwait Fund, Barick, EACOP, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Japan, China, Norway, NSSF, Taasisi za fedha za CRDB, NMB, NBC na TCB na Asasi mbalimbali zisizokuwa za Serikali; Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi.

**404. Mheshimiwa Mwenyekiti**, naomba nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara (www.mow.go.tz).

## K. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/26

**405. Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi, 2,280,195,828,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 90,468,270,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi na Shilingi 2,189,727,558,000.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, Shilingi 85,028,585,000.00 ni za Mishahara ya Watumishi na Shilingi 5,439,685,000.00 ni za Matumizi Mengineyo.

Bajeti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inajumuisha fedha za ndani Shilingi 1,209,223,117,000.00 na fedha za nje ni Shilingi 980,504,441,000.00. Fedha za ndani zinajumuisha Shilingi 688,756,470,000.00 kutoka Mfuko wa Barabara na Shilingi 520,466,647,000.00 ni fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

**406. Mheshimiwa Mwenyekiti**, pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2025/26 (Kiambatisho Na. 1 – 5). Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja yangu.

**407. Mheshimiwa Mwenyekiti**, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, hoja imeungwa mkono. Ninashukuru sana kwa kuwasilisha Hotuba hii ya Bajeti kwa Makadirio na Mapato ya Matumizi ya mwaka wa fedha 2025/2026, ahsante sana.

Sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ili aweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Karibu sana Mwenyekiti.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti la Fungu – 98, Wizara ya Ujenzi, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taarifa hii iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne; Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, ambayo inaeleza kuhusu Muundo na Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake. Sehemu ya Pili, ni Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Kutathmini Makusanyo ya Maduhuli, Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Uzingatiaji wa Ushauri na Maoni ya Kamati. Sehemu ya Tatu inahusu Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Sehemu ya Nne, ni Majumuisho ya Maoni na Ushauri wa Kamati na Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake; katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kamati ilifanya yafuatayo:-

(a) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025;

(b) Kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(c) Kupokea na kufanya Uchambuzi wa Randama ya Wizara; na

(d) Kuchambua Mkadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025; ninapenda kulijulisha

Bunge lako kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa na Kamati. Hata hivyo, baadhi ya maoni na ushauri uliotolewa haukufanyiwa kazi kwa ukamilifu na kwa sababu hiyo, Kamati inapenda kuweka msisitizo kuhusu umuhimu wa utekelezaji wake, kama ifuatavyo:-

(a) Kamati ilishauri Serikali kuhakikisha kwamba, inalipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri, ili kuwezesha miradi kutekelezwa kwa wakati na kupunguza ongezeko la riba. Hata hivyo, Kamati hairidhishwi na utekelezaji wa agizo hili kwa sababu, kasi ya Serikali kulipa madai hayo ni ndogo ukilinganisha na deni lililopo na kiwango cha riba inayoongezeka;

(b) Kamati ilishauri Serikali kulipa kwa wakati fidia kwa wananchi ambao wametwaa maeneo yao, ili kupisha miradi. Kamati hairidhishwi na utekelezaji wa agizo hili kwa sababu, yapo maeneo yaliyotwaliwa na wananchi kuahidiwa fidia. Aidha, Kamati inasisitiza kwamba, iwapo Serikali haina uwezo wa kulipa fidia husika, maeneo hayo yarejeshwe kwa wananchi mpaka Serikali itakapokuwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Ujenzi iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi milioni 70. Hadi kufikia Februari, 2025 makusanyo hayo yalikuwa ni jumla ya shilingi milioni 61.21, sawa na asilimia 87.44 ya malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kwa makusanyo hayo. Hata hivyo, katika uchambuzi wake kamati imebaini kwamba, baadhi ya taasisi chini ya Wizara ya Ujenzi zinakabiliwa na changamoto ya kutopata fedha zitokanazo na huduma wanazotoa kwa taasisi nyingine za Serikali na hivyo kuathiri mwenendo wa upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu – 98, Wizara ya Ujenzi iliidhinishiwa shilingi bilioni 81.4 ikiwa ni Fedha za Matumizi ya

Kawaida. Hadi kufikia Februari, 2025, Wizara ilipokea shilingi bilioni 44.8 sawa na 55.04% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hairidhishwi na hali ya mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida, hususan Matumizi Mengineyo *(OC)* kwa kuwa, hadi kufikia Februari, 2025, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 1.59 sawa na 33% tu ya fedha iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za miradi ya maendeleo; kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo, Kamati imebaini kwamba, hadi kufikia Februari, 2025 kati ya shilingi trilioni 1.69 zilizotengwa kutekeleza miradi, Wizara ilikuwa imepokea shilingi trilioni 1.02 sawa na 60% ya makadirio. Kwa wastani, mapokezi ya kutekeleza miradi ya maendeleo unaridhisha, hususan fedha za ndani, ambapo kati ya shilingi trilioni 1.14 zilizotengwa, shilingi bilioni 721.87 zimepokelewa, sawa na 66.22%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi katika Mikoa ya Morogoro, Tanga na Dar es Salaam kati ya tarehe 12 – 19 Machi, 2025. Masuala mahususi yaliyobainika katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtiririko wa Fedha za Bodi ya Mfuko wa Barabara. Moja kati ya masuala mahsusi ambayo Kamati iliyafanyia tathmini ni mtiririko wa mapokezi ya fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Fund Board)* uliokadiriwa kukusanya shilingi bilioni 856.78 katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi wakati kamati inapokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ilibaini kwamba, mfuko ulikuwa umekusanya shilingi bilioni 819.66. Kati ya fedha iliyokusanywa, kiasi kilichohamishiwa katika mfuko ni shilingi bilioni 289.94 sawa na 35.37% na shilingi bilioni 529.72 sawa na 64.63% bado zilikuwa hazijahamishiwa katika akaunti za mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imebaini kwamba, kwa fedha hizo kutohamishiwa katika Akaunti ya Mfuko wa Barabara kwa wakati, miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara nchini

umeathirika kwa kiasi kikubwa. Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, inapeleka fedha katika mfuko huo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri; Kamati imebaini kwamba, Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* umekosa uwezo wa kulipa madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri wa ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Februari, 2025, *TANROADS* ilikuwa na jumla ya deni lililozalishwa la shilingi trilioni 1.299. Kati ya deni hilo, shilingi bilioni 187.605 ni deni la wakandarasi na wahandisi washauri wa ndani katika miradi ya barabara kuu, shilingi bilioni 974.589 ni deni la wakandarasi na wahandisi washauri wa nje na shilingi bilioni 136.983 ni riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika deni hilo, miradi inayoendelea ilikuwa inajumuisha jumla ya shilingi bilioni 507.759 na shilingi bilioni 652.213 ni deni la miradi iliyokamilika. Kwa deni hilo kuendelea kutolipwa, riba inazidi kuongezeka na inaathiri uchumi wa wakandarasi, hasa wa ndani na vilevile kuathiri maendeleo ya miradi ya barabara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fidia Kwa Wananchi Kutolipwa Kwa Wakati; Kamati imebaini kuwepo na changamoto ya muda mrefu ambapo, Serikali haijalipa fidia kwa wananchi ambao wameachia ardhi yao kupisha miradi mbalimbali nchini. Inakadiriwa kwamba, hadi kufikia Februari, 2025 kiasi cha fedha kilichokuwa kinadaiwa, kama fidia, ni jumla ya shilingi bilioni 123.643. Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa Serikali kushughulika fidia hizo, ambazo kadri siku zinavyozidi kwenda, kiwango kinaongezeka pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Viwanja vya Ndege Chini ya *TANROADS;* katika uchambuzi wa utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege kwa mwaka wa fedha 2024/2025 inayotekelezwa na *TANROADS,* Kamati ilibaini kwamba, kwa wastani utekelezaji wa miradi hiyo unaridhisha. Hata hivyo, baadhi ya miradi ilikuwa katika hatua duni za utekelezaji wake, ikiwemo Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma Awamu ya II, ambao umetekelezwa kwa 16%. Kamati inaishauri Serikali

kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kutoa huduma muhimu kwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utendaji wa *TEMESA* na Hali ya Vivuko Nchini; moja kati ya masuala ambayo Kamati iliyabaini katika Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti hii ni kuathirika kwa utendaji wa *TEMESA* kwa kukosa fedha za uendeshaji na ukamilishaji wa miradi. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha *TEMESA* kifedha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, hususan katika kuhudumia vivuko nchini. Aidha, Kamati imeishauri *TEMESA* kubuni vyanzo vipya na vyenye ufanisi zaidi, kwa ajili ya kukusanya mapato yatokanayo na huduma zitolewazo kwa taasisi nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Miradi ya Wakala wa Nyumba Tanzania *(TBA)*. Kamati imebaini kwamba, *TBA* ilitengewa fedha, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025 baadhi ya miradi ilikuwa haijapokea fedha kabisa. Miradi hiyo ni pamoja na Ujenzi wa Ghorofa za Watumishi wa Umma Kaloleni Kota, eneo la Kaloleni – Arusha ambapo ulitengewa shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha kwa *TBA* ili miradi hiyo na mingine ambayo ipo katika mpango kazi wa mamlaka ikamilike kwa wakati. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba *TBA* inabuni njia bora zaidi ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi ya pango katika majengo yake nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Fungu – 98 Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 2.28 ikiwa ni sawa na ongezeko la 28.87% ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha ulioisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Wizara ya Ujenzi hususan katika miradi ya

maendeleo ambapo kuna ongezeko la wastani wa 29.73%. Bajeti inayoombwa ina lengo la kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya Wizara ikiwemo

(a) Kuendelea na ujenzi wa barabra za kimkakati zenye kufungua fursa za kiuchumi na kuimarisha shughuli za kijamii ikiwemo utalii, kilimo, madini, bandari, viwanda, Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere na;

(b) Kuendelea na ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, nchi jirani pamoja na barabara za ulinzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maduhuli; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi milioni 85 kupitia Idara zenye vyanzo vya mapato ikiwa ni sawa na ongezeko la 21.43% ukilinganisha na malengo ya kukusanya shilingi milioni 70 waliyojiwekea katika mwaka wa fedha unaoisha. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza kiwango cha makadirio ya makusanyo ya maduhuli. Sambamba na hilo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 taasisi zote ambazo ziko chini ya Fungu – 98 zinakuwa na mkakati madhubuti wa kubuni vyanzo vipya vya mapato na ukusanyaji wa maduhuli na kuwasilisha taarifa ya mwenendo wa makusanyo katika kutoka kila taasisi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi ya kawaida, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 90.468 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 85.028 ni mishahara na shilingi bilioni 5.439 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Bajeti ya matumizi ya kawaida inayoombwa ni sawa na ongezeko la 11.13% ukilinganisha na bajeti kama hiyo ya mwaka unaoisha. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha za utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida ambayo inaongeza motisha kwa watumishi wa umma kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inaomba kuidhinishiwa shilingi

trilioni 2.189 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, fedha inayoombwa ni sawa la ongezeko la 29.73% ikilinganisha na bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo inagusa moja kwa moja vipaumbele vya Wizara ambavyo vimeainishwa hapo juu. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba ongezeko la bajeti ya maendeleo kwa kiasi kikubwa limetokana na ongezeko la fedha za nje ambalo imeongezeka kwa 79.55% ukilinganisha na ongezeko la asilimia 5.9 kwa mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake Kamati ilitathimini juu ya uwezo wa Serikali kutenga fedha za ndani katika kugharamia miradi ya maendeleo bila kuendelea kutegemea fedha za nje. Tathmini hii ina lengo la kuishauri Serikali kuweka mkakati madhubuti wa kuongeza fedha za ndani ili kuwa na uhakika wa kukamilisha miradi kwa wakati kwa sababu fedha za nje zina masharti yenye mchakato mrefu wa upatikanaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maoni na Ushauri wa Kamati; Maoni ya Jumla; Kamati inaipongeza Serikali kwa ufanisi mkubwa ambapo imeendelea kutoa fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya Fungu – 98 hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa muktadha huo na kwa kuthamini mtaji wa fedha za maendeleo unaotokana na kodi za wananchi Kamati inaishauri Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika utendaji kazi utakaochochea kuboresha huduma za Sekta ya Ujenzi nchini.

(b) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu na kuwepo kwa thamani ya fedha;

(c) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika kukusanya maduhuli kutokana na vyanzo vilivyopo na kubaini vyanzo vipya ambavyo vitaongeza wigo wa makusanyo hayo;

(d) Serikali ihakikishe kwamba huduma zitolewazo na taasisi zake zinakuwa bora ili kukidhi matarajio ya wadau muhimu wa Sekta ya Ujenzi.

(e) Kamati inaishauri pia Wizara kusimamia taasisi zake kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake yote kwa ufanisi.

(f) Kamati inaamini kwamba iwapo kutakuwepo na usimamizi madhubuti taasisi hizo zitaweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikali na pia zitaongeza tija na hatimaye kuboresha huduma za ujenzi na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mahususi: -

(a) Utekelezaji wa Miradi ya Barabara kwa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP);* Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwamba kupitia Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(Public Private Partnership)* iongeze jitahada za kuteleza miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja nchini. Lengo la ushauri huu ni kutumia utaratibu huu ili kuipunguzia Serikali gharama kubwa ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambayo Serikali imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake wa mfano katika utekelezaji wa Sera ya *PPP* kwa kutoa maelekezo kwa Wizara ya Ujenzi kushirikiana na Wizara ya Uchukuzi kuanza kujenga Barabara muhimu kiuchumi kwa Tanzania itakayoanzia Mkoa wa Tanga hadi Singida kupitia Handeni – Kiberashi – Chemba hadi Mtoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada kama hizi pia zifanyike katika miradi ya kimkakati ya barabara nchini ambayo watumiaji watakuwa na hiyari ya kupitia, kulipia au kuchangia gharama za utekelezaji wake.

(b) Mapato ya Bodi ya Mfuko wa Barabara; pamoja na malengo mema ya kuanzisha kwa Mfuko wa Barabara bado kuna changamoto kubwa ya mtiririko wa fedha katika Mfuko huo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha za Mfuko huo zinafika kwa wakati ili kutekeleza miradi mbalimbali nchini hasa matengenezo ya barabara.

(c) Fidia kwa Wananchi; Kamati imebaini kwamba baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali nchini ambao waliacha maeneo yao ili kupisha miradi iliyosimamiwa na Wizara ya Ujenzi bado hawajalipwa fidia. Kwa mara nyingine tena Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wote wanaodai fidia wanalipwa stahiki zao kwa mujibu wa sheria; na iwapo Serikali haina uwezo wa kulipa fidia katika maeneo waliyoyatwaha maeneo hayo yarejeshwe kwa wananchi.

(d) Madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri; Kamati imebaini kwamba Serikali imekuwa ikisuasua katika kulipa madai na madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri katika miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa barabara na ujenzi wa vivuko. Kwa Serikali kutolipa madeni hayo kwanza kunakwamisha jitihada za kuwawezesha kiuchumi wananchi ambao wanapata changamoto ya marejesho ya mikopo katika taasisi za kifedha lakini pia kuathiri mzunguko wa fedha nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizo kwa mara nyingine tena Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati madhubuti na wa kudumu ili kulipa madeni kwa wakati lakini pia kuwajengea uwezo wakandarasi wa ndani ili watekeleze miradi mingi zaidi.

(e) Uwekezaji katika elimu ya ufundi; Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya eneo muhimu ambalo Serikali inapaswa kuwekeza ni katika eneo la ufundi vya vyuo mbalimbali hususan vya kati ili kupata wataalam wa kujenga na kusimamia miundombinu hiyo. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wake Serikali iboreshe mazingira ya kufundishia katika vyuo vilivyopo na kujenga vyuo vipya kwa kuakisi mapinduzi makubwa ya teknolojia duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa namna ya kipekee naendelea kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yake ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, ninamshukuru Naibu Spika kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yake, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kumsaidia kuendesha kwa ufanisi vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako Tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Ninaomba niwatambue Wajumbe hao, lakini kutokana na ufinyu wa muda ninaomba majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Balozi Mhandisi Aisha Amour. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya sekta ya ujenzi na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bwana Baraka Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninaomba niwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Kyela na viongozi wote wa chama na Serikali kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa unyenyevu, kwa uaminifu, uadilifu na weledi wa viwango vya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 98 - WIZARA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) na bila kuathiri masharti yanayopatikana katika Kanuni ya 142 taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambayo inaeleza kuhusu muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

b) Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kutathimini makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

d) Sehemu ya nne ni majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya tano ni hitimisho.

1.2 Namna Kamati Iliyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti mbalimbali yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025 (Kanuni ya 117 (1));

b) Kujadili utekelezaji wa bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2024/2025;

c) Kupokea na kufanya uchambuzi wa randama ya Wizara (Kanuni ya 115 (1)); na

d) Kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Bunge uliojadili makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge iliwasilisha maoni yake kuhusu Bajeti ya **Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi** ili kutimiza masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 118 (9).

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa na Kamati. Hata hivyo, baadhi ya maoni na ushauri uliotolewa hayakufanyiwa kazi kwa ukamilifu, na kwa kwa sababu hiyo Kamati inapenda kuweka msisitizo kuhusu umuhimu wa utekelezaji wake kama ifuatavyo: -

a) Kamati ilishauri Serikali kuhakikisha kwamba inalipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri ili kuwezesha miradi kutekelezwa kwa wakati na kupunguza ongezeko la` riba. Hata hivyo, Kamati hairidhishwi na utekelezaji wa agizo hili kwa sababu kasi ya Serikali kulipa madai hayo ni ndogo ukilinganisha na deni lililopo na kiwango cha riba inayoongezeka;

b) Kamati ilishauri Serikali kulipa kwa wakati fidia kwa wananchi ambao imetwaa maeneo yao ili kupisha miradi. Kamati hairidhishwi na utekelezaji wa agizo hili kwa sababu yapo maeneo yaliyotwaliwa na wananchi kuahidiwa fidia. Aidha, Kamati inasisitiza kwamba iwapo Serikali haina uwezo wa kulipa fidia husika, maeneo hayo yarejeshwe kwa Wananchi.

2.2 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Ujenzi iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. Milioni 70**. Hadi kufikia Februari, 2025 makusanyo hayo yalikuwa ni jumla ya **Sh. Milioni 61.21,** sawa na **asilimia 87.44** ya malengo waliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kwa makusanyo hayo. Hata hivyo, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kwamba, baadhi ya taasisi chini ya Wizara ya Ujenzi zinakabiliwa na changamoto ya kutopata fedha zitokanazo na huduma wanazotoa kwa taasisi nyingine za Serikali na hivyo kuathiri mwenendo wa makusanyo.

**2.3 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha**

**2.3.1 Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi iliidhinishiwa **Sh. Bilioni 81.4** ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2025, Wizara ilipokea **Sh. Bilioni 44.8** sawa na **asilimia 55.04** ya bajeti iliyoidhinishwa kama ilivyoainishwa katika **Kielelezo Na. 1**.

**KIELELEZO NA. 1 – MCHANGANUO WA HALI YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KUFIKIA FEBRUARI, 2025**

| BAJETI | MAKADIRIO 2024/2025 | MAPOKEZI FEBRUARI, 2025 | % |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA (P.E) | 76,588,233,000 | 43,215,525,907 | 56.42% |
| MATUMIZI MENGINEYO (O.C.) | 4,819,205,000 | 1,590,552,847 | 33% |
| **JUMLA KUU** | **81,407,438,000** | **44,806,078,754** | **55.04%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi na hali ya mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida hususan Matumizi Mengineyo (O.C.) kwa kuwa hadi kufikia Februari, 2025, Wizara ilikuwa

imepokea **Sh. Bilioni 1.59** sawa na **asilimia 33** ya Fedha iliyotengwa.

### 2.3.2 Fedha za Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, Kamati imebaini kwamba, hadi kufikia Februari, 2025 kati ya **Sh. Trilioni 1.68** zilizotengwa kutekeleza miradi, Wizara ilikuwa imepokea **Sh. Trilioni 1.02** sawa na **asilimia 60.9** ya makadirio. **Kielelezo Na. 2** kinatoa mchanganuo wa hali ya mapokezi ya fedha za bajeti ya maendeleo.

**KIELELEZO NA. 2 – MCHANGANUO WA HALI YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KUFIKIA FEBRUARI, 2025**

| BAJETI YA MAENDELEO | MAKADIRIO 2024/2025 | MAPOKEZI FEBRUARI, 2025 | % |
|---|---|---|---|
| FEDHA ZA NDANI | 1,141,803,989,000 | 721,873,278,724 | 66.22% |
| FEDHA ZA NJE | 546,084,725,000 | 306,465,142,698.89 | 56.12% |
| **JUMLA KUU** | **1,687,888,714,000** | **1,028,338,421,422.89** | **60.9** |

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, mapokezi ya kutekeleza miradi ya maendeleo unaridhisha, hususan fedha za ndani ambapo kati ya **Sh. Trilioni 1.14** zilizotengwa, **Sh. Bilioni 721.87** zimepokelewa sawa na **asilimia 66.22**.

### 2.4 Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

### 2.4.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025, ni sehemu ya usimamizi wa Bunge kwa Serikali kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) kwa lengo la kutathmini hali ya mapokezi ya fedha, hatua ya utekelezaji pamoja na kubainisha changamoto za utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi katika mikoa ya Morogoro, Tanga na Dar es Salaam kati ya tarehe 12 – 19 Machi, 2025.

### 2.4.2 Miradi Iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

#### (a) Mradi Na. 6304 – Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT), Morogoro

**Mheshimiwa Spika**, mkataba wa mradi wa ujenzi wa jengo la makao makuu ya taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT), Morogoro ulisainiwa Februari, 2023 kwa lengo la kukamilika Mei 2024 kwa gharama ya **Sh. Bilioni 5.978**. Ujenzi wa jengo hilo ulianza rasmi Mei, 2024 na baada ya makubaliano ya kuongeza muda wa utekelezaji wake, mradi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ilitenga **Sh. Bilioni 2.0** kwa ajili utekelezaji wa mradi huo. Hadi wakati Kamati inatembelea ili kukagua ujenzi unaoendelea mnamo tarehe 12 Machi, 2025, mradi ulikuwa umepokea **Sh. Bilioni 1.8** sawa na **asilimia 90** ya fedha iliyotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iimeridhishwa na mapokezi ya fedha zilizotengwa katika mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maendeleo ya ujenzi. Hata hivyo, Kamati ilibaini ucheleweshaji wa malipo ya mkandarasi kutolipwa kwa wakati na hivyo kupelekea kuongezwa kwa muda wa utekelezaji wa Mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za kugharamia ujenzi huo kwa wakati kulingana na hatua mbalimbali za ujenzi.

#### (b) Mradi Na. 6727 – Ukarabati na Ujenzi wa Uwanja wa Ndege cha Tanga

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unasimamiwa na wakala wa barabara Tanzania (TANROADS). Gharama za ujenzi ni jumla ya **Sh. Bilioni 95.57** ambapo kati ya hizo, **Sh. Bilioni 91.7** ni ujenzi wenyewe na **Sh. Bil. 3** ni za usimamizi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine Serikali ilitenga kiasi cha **Sh. Bilioni 2.654** kwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa waathiriwa wa mradi wapatao 274. Mradi ulitarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 26 Machi, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inafanya ziara ya ukaguzi tarehe 13 Machi, 2025, mradi huo ulikuwa haujaanza kutekelezwa, na Serikali ilikuwa bado ipo katika hatua za kukamilisha mapitio ya pili ya usanifu *(design review)* kufuatia usanifu wa awali uliofanyika mwaka 2017. Serikali iliitaarifu Kamati kwamba, ujenzi wa uwanja wa ndege wa Tanga utaanza baada ya kukamilika kwa taratibu za manunuzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo kwa kuwa tangu kufanyika kwa usanifu wa awali Mwaka 2017, imepita miaka nane (8). Pamoja na jitihada ambazo zimefanyika, Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kwamba inafanya usanifu mpya ambao utazingatia mahitaji halisi ya kuwa na uwanja unaokidhi vigezo katika mkoa wa Tanga na maeneo jirani kwa kuzingatia ukuaji wa shughuli za kiuchumi na ongezeko la watu.

**(c) Mradi Na. 4101 – Ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge pamoja na Ujenzi wa Daraja la Mto Pangani**

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara iliyofanywa, Kamati ilikagua sehemu ya mradi huo wa barabara kuanzia Tanga – Pangani - Mkange yenye jumla kilometa 170.8 pamoja na kukagua ujenzi wa daraja la mto Pangani.525.

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (Bagamoyo) una jumla ya urefu wa kilometa 256. Barabara hii inaunganisha nchi za Tanzania na Kenya kwenye ushoroba wa Pwani ya Afrika Mashariki unaoanzia katika mji wa Malindi na kupitia miji ya Mombasa na Lungalunga kwa upande wa Kenya na Horohoro, Tanga, Pangani hadi Bagamoyo kwa upande wa Tanzania wenye urefu wa jumla ya kilometa 454.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliitaarifu Kamati kwamba, mradi huu umegawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza inahusisha ujenzi wa kilometa 50 za barabara kutoka Tanga hadi Pangani, Sehemu ya pili inahusisha ujenzi wa daraja la mto Pangani lenye urefu wa mita 525 pamoja na barabara zenye jumla ya urefu wa kilometa 25.6, Sehemu ya tatu ni ujenzi wa barabara ya kutoka Mkange – Mkwaja – Tungamaa yenye urefu wa kilometa 95.2, ikijumuisha barabara unganishi ya Kipumbwi yenye urefu wa kilometa 3.7 na Sehemu ya nne ni Bagamoyo (Makurunge) – Mkange (km 73.25).

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi uliofanywa kwenye kipande cha barabara hiyo unaonyesha kwamba maendeleo ya ujenzi yanaridhisha isipokuwa haikuridhishwa na kasi yake. Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi za ujenzi wa mradi huo kwa kuwasimamia wakandarasi kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ujenzi wa daraja la mto Pangani, Kamati iliridhishwa na hatua za kuanza kwa ujenzi wa nguzo za daraja hilo.

**(d) Mradi Na. 4144 – Ukarabati wa MV Pangani II na Maegesho ya Kivuko, Pangani Mkoa wa Tanga**

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA). Kivuko hicho kina uwezo wa kubeba mzigo wa tani 50 ikijumuisha abiria 100 (wa kukaa 50 na wa kusimama 50) na magari madogo 6.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchakavu wa Kivuko hicho, Serikali ilitenga **Sh. Bilioni 2.39** kwa ajili ya ukarabati. Kati ya fedha hizo, Serikali ilisaini Mkataba na Kampuni ya M/S Songoro Marine Transport Limited kama Mkandaradsi wa mradi kwa gharama ya **Sh. Bilioni 2.30**, na **Sh. Milioni 92.24** zilitengwa kwa ajili ya Mshauri Mwelekezi ambaye ni Dar es Salaam Maritime Institute. Mradi huo ulitarajiwa kuanza tarehe 30 Septemba, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inafika uwandani, Serikali ilikuwa haijatoa fedha hivyo kupelekea mradi kutoanza.

Kamati ilitaarifiwa kwamba hatua ambazo zimechukuliwa ni kutuma maombi ya malipo ya kiasi cha **Sh. Milioni 461.20** yakiwa ni malipo ya awali kwa ajili ya kumlipa Mkandarasi na kiasi cha **Sh. Milioni 18.44** kwa ajili ya kumlipa Mshauri Elekezi. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na kuchelewa kwa utekelezaji wa Mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, kivuko hicho ni chombo muhimu cha usafirishaji wa abiria na mizigo kati ya Pangani na Bweni katika Wilaya ya Pangani, Mkoa wa Tanga.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, mnamo Oktoba, 2020, kivuko hicho kilifanyiwa ukarabati ambao uliigharimu Serikali **Sh. Milioni 496**.[1] Miaka minne baadae, Serikali ilitenga tena kiasi cha **Sh. Bilioni 2.93** katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa kivuko hicho.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi na utekelezaji wa mradi huu kwa sababu kwa muda mrefu kivuko hicho kimekuwa hakitoi huduma inayokusudiwa. Kwa upande mwingine, napenda nirejee taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu usimamizi wa huduma za vivuko nchi na ukaguzi uliofanyika Agosti, 2021 ambapo kivuko hicho kilitajwa kuwa moja ya vivuko ambavyo viko chini ya kiwango na kwa sababu hiyo hakifanyi kazi kabisa.[2]

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathimini ya kina ya ulinganifu wa gharama kati ya ukarabati wa kivuko hicho cha zamani na ununuzi wa kivuko kipya ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na matumizi sahihi ya fedha za umma.

---

[1] https://www.temesa.go.tz/news/permanent-secretary-for-ministry-of-works-receives-mv-pangani-ferryafter-extensive-rehabiliation

[2] Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi wa Huduma za Vivuko *(Performance Audit Report on The Management of Ferry Operations)* ya Mwaka 2024 Uk. 3

**(e) Mradi Na. 4285 – Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya 3 (CBD – Gongolamboto)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya **Sh. Bilioni 231.66**. Mkandarasi wa mradi ni Kampuni ya SINOHYDRO Corporation Ltd kutoka China.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu una sehumu mbili (2) ambazo ni: -

**a)** Sehemu ya kwanza (lot 1)– inahusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 23.3, kutoka katikati ya jiji hadi Gongolamboto. Inahusisha barabara ya Azikiwe, Bibi Titi Mohamed, Nkrumah, Nyerere, Gongolamboto, barabara ya Shaurimoyo, Uhuru na Mandela hadi Tazara pamoja na barabara ya Lindi, kutoka Shaurimoyo hadi BRT Terminal; na

**b)** Sehemu ya Pili – inahusisha ujenzi wa miundombinu ya majengo ambayo ni karakana katika eneo la Gongolamboto, Kituo kikuu cha mabasi (Terminal) ndani ya uwanja wa ndege wa Julius Nyerere (JNIA) na kituo kidogo *(Feeder Station)* katika eneo la Banana.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa mradi huu ambao ulikuwa umefikia **asilimia 80** tangu uanze kutekelezwa Agosti, 2022. Aidha, Kamati ilibaini kwamba, Sehemu ya pili (Lot 2) ya mradi huu ilikuwa bado haijapata Mkandarasi ambapo taratibu za manunuzi ya kumpata ziko katika hatua za mwisho na kwamba tathmini imekamilika. Serikali ilitoa taarifa kuwa matarajio yao ilikuwa ni kukamilisha hatua zote na kusaini mkataba ifikapo mwezi Aprili 2025. Mkataba wa ujenzi utatekelezwa kwa njia ya Sanifu na Jenga *("Design and Build")*.

***Mheshimiwa Spika***, kamati iliishauri Serikali kutumia mafunzo ya utekelezaji wa mradi mmoja ili kuboresha miradi mingine inayofuata. Mfano, kipimo cha zege linalotumika kwenye ujenzi wa mradi wa BRT inagharimu kiasi kikubwa ambacho hakina uwiano na uzito wa mzigo unaobebwa wakati wa matumizi ya vituo na barabara.

**(f) Mradi Na. 4125 – Ujenzi wa Maegesho na Miundombinu ya Kivuko cha Magogoni, Eneo la Kisambusa**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu ni hatua muhimu ya Serikali kuhakikisha kwamba changamoto ya msongamano wa magari inatatuliwa katika maegesho na miundombinu ya kivuko cha Magogoni. Hata hivyo, hadi wakati Kamati inachambua taarifa ya mradi huu, utekelezaji wake ulikuwa haujaanza.

**Mheshimiwa Spika**, katika maelezo ya Serikali, Kamati ilibaini kwamba, Wakala wa Umeme na Ufundi Tanzania (TEMESA) uliomba Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kufanya tathmini ya mali za wananchi wanaoishi katika eneo la Kisambusa lililopo karibu na eneo la Kivuko Wilaya ya Kigamboni katika Mkoa wa Dar es Salaam. Tathmini iliyofanyika imebainisha kwamba **Sh. Bilioni 2.78** zinahitajika kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi ili kupisha utekelezaji wa mradi huo. Hata hivyo, hadi wakati Kamati iko uwandani, Serikali ilikuwa haijatoa fedha kwa ajili ya fidia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utoaji wa fedha ili mradi ukamilike kwa wakati. Aidha, iangalie uwezekano wa kuanza ujenzi wa daraja kutoka Magogoni hadi Kisambusa.

**2.5 Masuala Mahsusi Yaliyobainika Katika Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**a) Mtiririko wa Fedha za Bodi ya Mfuko wa Barabara**

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya masuala mahsusi ambayo Kamati iliyafanyia tathmini, mtiririko wa mapokezi ya fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Fund Board)* ulikadiriwa kukusanya **Sh. Bilioni 856.78** katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inapokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti, ilibaini kwamba, mfuko ulikuwa umekusanya **Sh. Bilioni 819.66**. Kati ya fedha iliyokusanywa, kiasi kilichohamishiwa katika mfuko ni **Sh. Bilioni 289.94** (sawa na

**asilimia 35.37**) na **Sh. Bilioni 529.72** sawa na **asilimia 64.63** bado zililkuwa hazijahamishiwa katika akaunti za mfuko.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, kwa fedha hizo kutohamishiwa katika akaunti ya mfuko wa barabara kwa wakati, miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara nchini umeathirika kwa kiasi kikubwa. Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inapeleka fedha katika Mfuko huo kwa wakati.

**b) Madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) imekosa uwezo wa kulipa madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri wa ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Februari, 2025, TANROADS ilikuwa na jumla ya deni lililozalishwa la **Sh.Trilioni 1.299**. Kati ya deni hilo, **Sh. Bilioni 187.605** ni deni la Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa ndani katika miradi ya barabara kuu, **Sh. Bilioni 974.589** ni deni la Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa nje na **Sh. Bilioni 136.983** ni riba.

**Mheshimiwa Spika,** Katika deni hilo, miradi inayoendelea ilikuwa inajumuisha jumla ya **Sh. Bilioni 507.759** na **Sh.Bilioni 652.213** ni deni la miradi iliyokamilika. Kwa deni hilo kuendelea kutolipwa, riba inazidi kuongezeka na inaathiri uchumi wa wakandarasi hasa wa ndani na vilevile kuathiri maendeleo ya miradi ya barabara nchini.

**c) Fidia Kwa Wananchi Kutolipwa Kwa Wakati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwepo na changamoto ya muda mrefu ambapo Serikali haijalipa fidia kwa wananchi ambao wameachia ardhi yao kupisha miradi mbalimbali nchini. Inakadiriwa kwamba, hadi kufikia Februari, 2025 kiasi cha fedha kilichokuwa kinachodaiwa kama fidia ni jumla ya Sh. Bilioni 123.643.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa Serikali kushughulika fidia hizo, ambazo kadri siku zinavyozidi kwenda, kiwango kinaongezeka.

### d) Ujenzi wa Viwanja vya Ndege chini ya TANROADS

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege kwa mwaka wa fedha 2024/2025 inayotekelezwa na TANROADS, Kamati ilibaini kwamba kwa wastani utekelezaji wa miradi hiyo unaridhisha.[3] Hata hivyo, baadhi ya miradi ilikuwa katika hatua duni za utekelezaji wake ikiwemo mradi wa ukarabati wa uwanja wa ndege wa Kigoma awamu ya II ambao umetekelezwa kwa **asilimia 16** pamoja na mradi wa upanuzi wa uwanja wa ndege wa Sumbawanga ambao umefikia **asilimia 50 tu**. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kutoa huduma muhimu kwa maeneo hayo.

### e) Utendaji wa TEMESA na Hali ya Vivuko Nchini

**Mheshimiwa Spika,** moja kati ya masuala ambayo Kamati ilibaini katika uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti hii, ni kuathirika kwa utendaji wa TEMESA kwa kukosa fedha za uendeshaji na ukamilishaji wa miradi. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha TEMESA kifedha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi hususan katika kuhudumia vivuko nchini. Aidha, Kamati imeishauri TEMESA kubuni vyanzo vipya na vyenye ufanisi zaidi kwa ajili ya kukusanya mapato yatokanayo na huduma zitolewazo kwa taasisi nyingine za Serikali.

### f) Utekelezaji wa Miradi ya Wakala wa Nyumba Tanzania (TBA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, TBA ilitengewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika mwaka wa fedha 2024/2025. Hadi kufikia Februari, 2025, baadhi ya miradi ilikuwa haijapokea fedha kabisa. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa ghorofa za watumishi wa umma Kaloleni Kota, Kaloleni –

[3] Randama Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi Uk. 351

Arusha ambapo ulitengewa **Sh. Milioni 500**, mradi wa ujenzi wa nyumba 20 za viongozi ambao ulitengewa **Sh. Milioni 50** pamoja na mradi wa ununuzi wa nyumba (Apartment) 12 Chimara uliotengewa **Sh. Milioni 500**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha kwa TBA ili miradi hiyo na mingine ambayo iko katika mpango kazi wa mamlaka ikamilike kwa wakati. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba TBA inabuni njia bora zaidi za ukusanyaji mapato yatokanayo na kodi ya pango katika majengo yake nchini.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 3.1 Umbile la Bajeti na Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. Trilioni 2.280** ikiwa ni sawa na ongezezo la **asilimia 28.87** ukilinganisha na Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika, Kielelezo Na. 3** kinaonesha ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026.

**KIELELEZO NA. 3 – ULINGANISHO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

| FUNGU 98 – WIZARA YA UJENZI | MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | 81,407,438,000 | 90,468,270,250 | +11.13% |
| **BAJETI YA MAENDELEO** | 1,687,888,714,000 | 2,189,727,558,000 | +29.73% |
| **JUMLA KUU** | **1,769,296,152,000** | **2,280,195,828,250** | **+28.87%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya ujenzi hususan katika miradi ya maendeleo, ambapo kuna ongezezo la wastani wa **asilimia 29.73**.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti inayoombwa ina lengo la kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya Wizara ikiwemo vifuatavyo: -

a) kuendelea na ujenzi wa barabara za kimkakati zenye kufungua fursa za kiuchumi na kuimarisha shughuli za kijamii ikiwemo utalii, kilimo, madini, bandari, viwanda, Bwawa la Kufua Umeme la Mwl. Nyerere;

b) kuendelea na ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, nchi jirani pamoja na barabara za ulinzi kwa kiwango cha lami;

c) kuendelea na ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano katika miji inayokua kwa kasi na majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma;

d) kuendelea na matengenezo ya barabara kuu, barabara za mikoa pamoja na madaraja ili kuhakikisha kuwa barabara zinapitika katika majira yote ya mwaka; na

e) kuendelea kuimarisha usafiri na miundombinu ya vivuko ili kuunganisha maeneo ya nchi kavu ambayo yametenganishwa na maji katika maeneo ya bahari, maziwa na mito.

**3.2 Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepanga kukusanya jumla ya **Sh. Milioni 85. 00** kupitia idara zenye vyanzo vya mapato, ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 21.43** ukilinganisha na malengo ya kukusanya **Sh. Milioni 70.00** waliyojiwekea katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza kiwango cha makadirio ya makusanyo ya maduhuli. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, katika mwaka wa Fedha 2025/2026 taasisi zote ambazo ziko chini ya fungu 98 – Wizara ya Ujenzi zinakuwa na mkakati madhubuti wa kubuni vyanzo vipya vya mapato na ukusanyaji wa maduhuli na kuwasilisha taarifa kuhusu mwenendo wa makusanyo ya kila taasisi Bungeni.

### 3.3 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Ujenzi inaomba kuidhinishwa **Sh. Bilioni 90.468** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. Bilioni 85.028** na mishahara (P.E.) na **Sh. Bilioni 5.439** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (O.C.).

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya matumizi ya kawaida inayoombwa ni sawa na ongezekeko la **asilimia 11.13** ukilinganisha na Bajeti kama hiyo kwa Mwaka unaoisha kama ambavyo **Kielelezo Na. 4** kinaonesha.

**KIAMBATISHO NA. 4 – ULINGANISHO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

| MATUMIZI YA KAWAIDA | BAJETI YA 2024/2025 | BAJETI YA 2025/2026 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA (P.E.) | 76,588,233,000 | 85,028,585,250 | 8,440,352,250 | +11.02% |
| MATUMIZI MENGINEYO | 4,819,205,000 | 5,439,685,000 | 620,480,000 | +12.87% |
| **JUMLA KUU** | **81,407,438,000** | **90,468,270,250** | **9,060,832,250** | **+11.13%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha za utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida ambayo inaongeza motisha kwa watumishi wa umma kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi, na kwa weledi.

### 3.4 Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara inaomba kuidhinishiwa **Sh. Trilioni 2.189** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha inayoombwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 29.73** ukilinganisha na bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha kama ambavyo **Kielelezo Na. 5** kinaonesha.

**KIAMBATISHO NA. 5 – ULINGANISHO WA BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

| BAJETI YA MAENDELEO | MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|
| FEDHA ZA NDANI | 1,141,803,989,000 | 1,209,223,117,000 | +5.9% |
| FEDHA ZA NJE | 546,084,725,000 | 980,504,441,000 | +79.55% |
| **JUMLA KUU** | **1,687,888,714,000** | **2,189,727,558,000** | **+29.73%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo inagusa moja kwa moja vipaumbele vya Wizara ambavyo vimeainishwa hapo juu. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba, ongezeko la bajeti ya maendeleo kwa kiasi kikubwa limetokana na kuongezeka kwa fedha za nje ambayo imeongezeka kwa **asilimia 79.55** ukilinganisha na ongezeko la **asilimia 5.9** kwa fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilitathmini juu ya uwezo wa Serikali kutenga fedha za ndani katika kugharamia miradi ya maendeleo bila kuendelea kutegemea fedha za nje. Tathmini hii ina lengo la kuishauri Serikali kuweka mkakati madhubuti wa kuongeza fedha za ndani ili kuwa na uhakika wa kukamilisha miradi kwa wakati kwa sababu fedha za nje zina masharti yenye mchakato mrefu wa upatikanaji wake.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali ambayo kwa ufanisi mkubwa imeendelea kutoa fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi, hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. kwa muktadha huo, na kwa kuthamini mtaji wa fedha za maendeleo unaotokana na kodi za wananchi, Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo: -

**a)** Kuongeza ufanisi na ubunifu katika utendaji kazi utakaochochea kuboresha huduma za Sekta ya Ujenzi nchini, kwa kuwa sekta hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi;

**b)** Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu *(sustainability)* na kuwepo kwa thamani ya fedha *(value for money)*; na

**c)** Kuongeza ufanisi na ubunifu katika kukusanya maduhuli kutokana na vyanzo vilivyopo, na kubaini vyanzo vipya ambavyo vitaongeza wigo wa makusanyo hayo. Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe kwamba, huduma zitolewazo na taasisi zake, zinakuwa bora ili kukidhi matarajio ya wadau muhimu wa Sekta ya Ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri pia Wizara kuzisimamia taasisi zake kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake yote kwa ufanisi. Kamati inaamini kwamba, iwapo kutakuwepo na usimamizi madhubuti, taasisi hizo zitaweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na pia zitaongeza tija na hatimaye kuboresha huduma za Ujenzi na kuongeza mapato ya Serikali.

### 4.2 Maoni Mahsusi

#### a) Utekelezaji wa Miradi ya Barabara kwa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwamba, kupitia Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(Public Private Partnership)*, iongeze jitihada za kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja nchini. Lengo la ushauri huu ni kutumia utaratibu huo ili kuipunguzia Serikali gharama kubwa za utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambayo Serikali imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (Rais) kwa uongozi wake wa mfano katika utekelezaji wa Sera ya PPP kwa kutoa maelekezo kwa Wizara ya Ujenzi, kushirikianana Wizara ya Uchukuzi kuanza kujenga barabara muhimu kwa uchumi wa Tanzania, itakayoanzia Mkoa wa Tanga hadi Singida, kupitia Handeni – Kiberashi – Chemba hadi Mtoro.[4] Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kumpata mwekezaji ili kuanza mradi huo ambao utachochea kukua kwa uchumi kwa kupunguza gharama za usafirishaji kati ya Bandari ya Tanga na mikoa mingine.

**Mheshimiwa Spika**, jitihada kama hizi pia zifanyike katika miradi ya kimkakati ya barabara nchini ambayo watumiaji watakuwa na hiyari ya kulipia ili kuchangia gharama za utekelezaji wake.

#### b) Mapato ya Bodi ya Mfuko wa Barabara

**Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge kwa lengo kutoa fedha za matengenezo ya barabara kwa kuhakikisha mtiririko endelevu wa fedha ili kukidhi mahitaji ya matengenezo ya barabara.[5]

---

[4] https://tanga.go.tz/new/samia-atangaza-barabara-ya-handeni-singida-kuhudumia-magari-ya-mizigo

[5] Sheria ya Barabara na Tozo ya Mafuta, Sura ya 220

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na malengo mema ya kuanzishwa kwa mfuko wa barabara, bado kuna changamoto kubwa ya mtiririko kwa fedha katika mfuko huo. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha za mfuko huo zinafika kwa wakati ili kutekeleza miradi mbalimbali nchini hasa matengenezo ya barabara.

**c) Fidia kwa Wananchi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali nchini ambao waliachia maeneo yao ili kupisha miradi inayosimamiwa na Wizara ya Ujenzi bado hawajalipwa fidia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, wananchi wote wanaodai fidia, walipwe stahiki zao kwa mujibu wa sheria na iwapo Serikali haina uwezo wa kulipa fidia katika maeneo waliyotwaa, maeneo hayo yarejeshwe kwa wananchi.

**d) Madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Serikali imekuwa ikisuasua katika kulipa madai na madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri katika miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa Barabara na ujenzi wa vivuko. Kwa Serikali kutolipa madeni hayo, kwanza kunakwamisha jitihada za kuwawezesha kiuchumi wananchi ambao wanapata changamoto ya marejesho ya mikopo katika taasisi za kifedha, lakini pia kunaathiri mzunguko wa fedha nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sababu hizo, kwa mara nyingine tena, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati madhubuti na wa kudumu ili kulipa madeni kwa wakati lakini pia kuwajengea uwezo wakandarasi wa ndani ili watekeleze miradi mingi zaidi.

**e) Uwekezaji Katika Elimu ya Ufundi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kwamba, uchumi wa nchi yetu unatarajiwa kuimarika kwa Serikali kuendelea kuboresha

miundombinu mbalimbali, Kamati inaishuri kwamba jitihada hizo ziende sambamba na kuwajengea uwezo watanzania kuwa sehemu ya maendeleo hayo. Moja kati ya eneo muhimu ambalo Serikali inapaswa kuwekeza, ni katika elimu ya ufundi kwa vyuo mbalimbali hususan vya kati ili kupata wataalamu wa kusimamia kujenga na kusimamia miundombinu hiyo. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wake, Serikali iboreshe mazingira ya kufundishia katika vyuo vilivyopo na kujenga vyuo vipya kwa kuakisi mapinduzi makubwa ya teknolojia duniani.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha kwa ufanisi Vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. | **Makamu** |
| 3. | Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | Mjumbe |

6. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. Mjumbe
7. Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. Mjumbe
8. Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. Mjumbe
9. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb. Mjumbe
10. Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. Mjumbe
11. Mhe.Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb. Mjumbe
12. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. Mjumbe
13. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. Mjumbe
14. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako Mb. Mjumbe
15. Mhe. Livingstone Jpseph Lusinde, Mb. Mjumbe
16. Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. Mjumbe
17. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. Mjumbe
18. Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. Mjumbe
19. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb.Mjumbe
20. Mhe. Mwatumu Dau Haji, Mb. Mjumbe
21. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. Mjumbe
22. Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Hamis Ulega, (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhe. Mhandisi Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb). Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Balozi Mhandisi Aisha Amour. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Ujenzi na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bw. Baraka I. Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

**5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya **Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**
05 Mei, 2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati kwa kutoa taarifa hiyo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya mawasilisho hayo mawili tunaanza na wachangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Rashid Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Ndulane.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii muhimu kabisa kwa ujenzi wa miundombinu ya barabara zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pongezi; nimpongeze sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kuwa kinara wa uboreshaji wa miundombinu ya barabara zetu vijijini kupitia *TARURA* pamoja na barabara zetu kuu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* kwa kazi nzuri ambazo zinaendelea kufanyika. Pamoja na changamoto mbalimbali za mvua, lakini tumeona *commitment* ya hali ya juu sana ya Wizara chini ya Waziri Abdallah Hamis Ulega, *Engineer* Amour, Naibu Waziri Godfrey Kasekenya, Mtendaji Mkuu wa *TANROAD*, Mohamed Besta na Watumishi wote wa Wizara hii; kwa kweli wanastahili maua yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona namna ambavyo hawalali ili kuhakikisha kwamba miundombinu kila mahali inarudi katika ubora wake, haswa yale maeneo ambayo yaliyokumbana na changamoto ikiwemo kule Kusini na kule Morogoro, lakini hata kule Tanga ipo barabara yetu moja ilipata kadhia, Meneja wa

*TANROADS* Mkoa alifika kwa wakati na kurejesha mawasiliano kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nianze na ziara ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoifanya hivi karibuni katika Mkoa wa Tanga. Mheshimiwa Rais alizungumza maono yake anayotoka kuiona Tanga. Akasema na kubainisha kwamba anataka kuiona Tanga ambayo imefunguka kwa upande wa miundombinu, iweze kuwasiliana na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara zetu ambazo zinatutambulisha hivyo. Barabara ya kwanza ambayo kwa bahati nzuri ameitaja ni hii ya kutoka Handeni – Kiberashi hadi Singida. Tunampongeza kwa hatua hiyo ya kusema sasa itajengwa kwa utaratibu wa *PPP*. Sambamba na hilo tunayo barabara yetu hii ya Tanga – Pangani – Bagamoyo ujenzi unaendelea na sasa tuko katika ujenzi wa daraja pale Mto Pangani. Ni imani yetu kwamba watazidi kusukuma Mafungu ili barabara ile iende kwa kasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo tunayo Barabara ya kutoka Mabokweni kwenda Maramba – Umba hadi Mkomazi. Barabra hii ipo kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na ni barabara ya kimkakati ya kuondoa msongamano katika Barabara ya Chalinze – Segera kwenda Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha na hata mpaka Musoma. Tunaomba sana na barabara hii sasa waitengee fedha ili sasa shughuli ziweze kuanza. Tukifanya hivyo tutakuwa tumesaidia sana kufungua Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri jambo moja. Barabara hii ya Chalinze – Segera ni barabara ya siku nyingi; na barabara hii kwa mujibu wa taratibu zao, kwamba uhai wa barabara ni miaka 15, hii ni zaidi ya miaka 30; na barabara hii sasa tunaweza tukasema imesha-*expire* haifai tena kwa matumizi. Kwa hiyo ninachoomba ni kwamba ni lazima kuwe na mpango wa kuiboresha barabara na hii. Kwanza ni nyembamba sana na mwaka huu imesababisha ajali nyingi sana. Inamgharimu sana Mkuu wetu wa Mkoa anashindwa kufanya kazi nyingine za maendeleo wakati wote yupo barabarani ili kuhudumia wananchi mbalimbali wanaopata shida kutokana na

ufinyu wa wembamba wa barabara hii. Kwa hiyo niwaombe sana waangalie uwezekano wa kuipanua barabara hii ambayo sasa imekuwa finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pia inatokana na ufanisi ambao umeongezeka katika Bandari ya Tanga. Shehena kubwa inashuka katika Bandari ya Tanga kwa hivyo inahitaji barabara pana ili magari haya yaweze kupishana kwenda kuchukua mizigo mbalimbali katika Bandari ya Tanga. Sambamba na kutoka Segera kwenda Same hadi Kilimanjaro ni barabara ambayo pia ni nyembamba na inapaswa kuongezwa haswa katika zile kona kuwe na upana wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Barabara ya kutoka Mombo - Lushoto kwenda mpaka Mlalo. Barabara hii na yenyewe imejengwa miaka 30 iliyopita. Ninakumbuka wakati huo mkandarasi alikuwa anatoka Kampuni ya *GBG*, ninadhani hata sasa hivi hapa nchini haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo tumeshaweka viraka vya kutosha lakini sasa imechakaa na haifai. Tunaomba na yenyewe sasa ije ifanyiwe upanuzi kwa sababu magari yanayoingia katika Wilaya ya Lushoto ni mengi sana, yameongezeka zaidi ya mara tatu wakati wana-*design* hii barabara iliyopo sasa. Kwa hiyo, niombe kilometa 36 kutoka Mombo mpaka Lushoto na kutoka Lushoto kwenda Mlalo mpaka Mtae na yenyewe imeahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami, tunaomba waongeze kasi ya ujenzi katika barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningetaka kuchangia ni kuhusu viwanja vya ndege. Mheshimiwa Waziri, Tanga ni Jiji, lakini katika Majiji Sita ya Nchi hii ni Tanga pekee ambayo ina kiwanja cha ndege ambacho ndege kubwa haziwezi kutua. Nimwombe sana, hakikisha katika viwanja vile ambavyo vinajengwa katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma na Mara (Musoma) basi mweke mkazo pia katika Jiji la Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunao Mradi mkubwa wa Bomba la Mafuta, lakini kama ambavyo Mheshimiwa Rais

ameahidi kuufungua Mkoa wa Tanga kiuchumi na kwa kilimo pia. Ni muhimu pia kuwa na uwanja mkubwa wa ndege ambao utawawezesha wawekezaji kuweza kufika Tanga kwa urahisi. Kwa hiyo, ni aibu sana katika Majiji yote sita ni Jiji la Tanga pekee ambalo kiwanja cha ndege kinaruhusu ndege ndogo tu ambazo si za zaidi ya abiria 12 kutua. Niombe sana kwamba, hili liwepo katika vipaumbele vya Wizara kuhakikisha kwamba tunaboresha ule uwanja wa ndege uweze kuwa na uwezo wa kutua ndege hata aina ya *bombardier* hizi ambazo zinakuja Dodoma na maeneo mengine basi ziweze kutua katika Mkoa wetu wa Tanga, ili tuweze kurahisisha shughuli za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ni ile changamoto ya kukarabati barabara ambazo zimekatika kutokana na hii kadhia ya mvua. Tunaomba sana na tunatambua kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, lakini pamoja na uchaguzi ni muhimu sana tukawekeza fedha kwenye yale maeneo muhimu ambayo barabara hizi angalau ziweze kupitika katika kipindi hiki ambacho tunatafuta mafungu makubwa kwenda kukamilisha miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Shangazi. Nilimtaja Mheshimiwa Francis Ndulane, Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kujadili hii Bajeti ya Wizara yetu muhimu ya Ujenzi. Kwanza nitangulie kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Serikali ya Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Ujenzi na hivyo kufanya fedha nyingi kupelekwa katika sekta hii. Tumeona miradi mingi imetekelezwa ikiwemo lile Daraja kubwa kabisa Afrika Mashariki lenye urefu wa kilometa tatu la Kigongo – Busisi. Pia tumeona namna Mheshimiwa Rais wetu alivyotupambania wananchi wa mikoa ya kusini na kuweza kuleta fedha nyingi ambazo miradi inaendelea ya ujenzi wa madaraja mapya. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye siku ya tarehe 16 Aprili, mwaka huu tuliambatana naye pamoja na Waziri wa Ujenzi, na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwenda kuangalia namna ambavyo Serikali inaendelea na ujenzi wa yale madaraja yaliyoathiriwa na Kimbunga Hidaya na Mvua za *El-Nino* pamoja na hatua nyingine muhimu zilizochukuliwa katika kufanya mawasiliano ya Barabara ya Kibiti – Lindi – Mingoyo yaweze kufanyika kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Abdallah Ulega, rafiki yangu na ndugu yangu kwa kweli anafanya kazi kubwa sana. Alikesha na wananchi wetu pale ilivyokuwa inatokea Barabara yetu ya Kibiti – Lindi – Mingoyo ilikatika katika maeneo ya Somanga – Mikereng'ende na kule Mto Matani. Kwa kweli amefanya kazi kubwa sana, ninampongeza sana. Pia, ninampongeza Naibu Waziri ambaye mara kwa mara alikuja kuangalia kazi na ubora unaoendelea kutekelezwa katika maeneo ambayo yanatengenezwa barabara hizi, madaraja na makalavati. Ninakumbuka kuna wakati tulikwenda naye mpaka kule Kipatimu kwa ajili ya kuangalia yale makalavati yanayojengwa na Kampuni ya *ME,* pale njia nne Kipatimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Katibu Mkuu dada yangu Balozi *Engineer* Aisha Amour, kwa kweli anafanya kazi kubwa na anaonesha namna alivyo mbobevu katika fani hii ya ujenzi wa barabara. Nimpongeze pia Dkt. Charles Msonde kwa kazi nzuri. Vilevile, nimpongeze pia Mheshimiwa *RAS* wangu wa Mkoa wa Lindi dada yangu, Mheshimiwa Zainab Telack, kwa kweli na yeye amekuwa akikesha kwenye yale maeneo ambayo yalikuwa yanaleta matatizo kati ya mwaka jana mpaka mwanzoni mwa mwaka huu, wakati tayari Serikali imeshachukua hatua mbalimbali za ujenzi wa yale madaraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze vilevile, pia Mheshimiwa *DC* wetu wa Wilaya ya Kilwa, Mheshimiwa *Comrade* Abdallah Nyundo anafanya kazi nzuri sana katika kusimamia ile miradi iliyopo pale Kilwa. Nimpongeze Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya *TANROADS Engineer* Besta pamoja na *Engineer* wetu ambaye

anasimamia Barabara za Mkoa wa Lindi, *Eng*ineer Zengo kwa kazi nzuri. Kwa kweli wametuonesha mfano mzuri na kwa kweli wanawajibika ipasavyo katika kuhakikisha mambo yanakwenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nipongeze hatua ambazo Serikali imechukua siyo tu kujenga madaraja bali pia kuangalia uwezekano wa kujenga sasa barabara zote ambazo zinaelekea Mikoa ya Kusini. Hizi barabara nyingi zimejengwa muda kidogo; ukiondoa ile barabara inayotoka Mtwara kwenda Masasi kupitia Mnazi Mmoja – Lindi na ile ambayo ilijengwa hadi kwenye tuta la Daraja la Mkapa. Barabara ya kutoka Somanga kwenda Masaninga ndiyo barabara ambayo ilifuata na imeonekana mara nyingi kunatokea changamoto nyingi. Ndiyo hiyo inaonesha maeneo ya Somanga, Mikereng'ende na kwingineko ambako Mheshimiwa Waziri umekuwa ukifanya kazi na juhudi kubwa kuhakikisha mambo yanakwenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba katika vile vipande ambavyo vitaanza kushughulikiwa hiki kiwe namba moja cha Somanga – Masaninga kwa sababu ndicho cha zamani zaidi na kimeharibika zaidi halafu kifuate kile cha kutoka Nyamwage kwenda Somanga kwa sababu hayo ndio maeneo barabara zake zina hali mbaya zaidi. Kwa hiyo, ningeomba hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchache wa fadhila kama sitozishukuru kampuni ambazo zinajenga yale madaraja yaliyoathiriwa na Mvua za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya. Mheshimiwa Waziri hapa umetuongoza kuzitathmini zile kampuni za kizalendo, ninaomba niseme hujakosea na ndiyo maana Mheshimiwa Rais amekuweka kwenye hiyo nafasi kwa sababu ameona upo makini na una uwezo wa kulitumikia Taifa hili kwa kiwango toshelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya MAKAPO aliyoitaja ambayo inaongozwa na Ndugu Joseph Mkuyu kwa kweli inafanya kazi ya kipekee, hajakosea kabisa. Kuna kampuni moja hujaitaj inaitwa *ME Constructors Limited* inaongozwa na ndugu yetu Bwana Makundi ambayo inajenga tundu 10 za makalavati kutoka Njia Nne kwenda Kipatimu. Ninajua ramani ya Kilwa

unaijua umeshawahi kuwa *DC* kule Kilwa. Kwa kweli Kampuni ya *ME Constructors* inafanya kazi nzuri sana, nayo ninaomba aiongeze katika orodha yake ya kampuni za kizalendo zinazofanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha kwamba, kampuni zetu sasa zimeiva. Ninaomba Serikali iendelee kuziamini siyo tu kwenye ujenzi wa madaraja na barabara bali pia hata kwenye maeneo mengine ya miradi ya maji na mingineyo, kwa kweli waweze kuaminiwa na kupewa nguvu, ili mzunguko wa uchumi wetu uweze kubaki hapa nchini na uongeze tija kwa Wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hizo kampuni za kigeni zimeajiri pia ma-*engineer* wazalendo. Pale tuna Kampuni ya Hainan ina wazalendo kina *Engineer* Kazungu wapo wanafanya kazi usiku na mchana. Kwa kweli tunashukuru kazi inakwenda vizuri ya ujenzi wa madaraja na makalavati. Pia, niishauri Serikali ninaomba Wizara na *TANROADS* ziendelee kuimarisha usimamizi, ili kuhakikisha hii miradi inayoendelea iweze kutekelezwa kwa wakati na iweze kujengwa kwa ubora unaotakiwa, ili kwa miaka mingi kama siyo kwa miaka yote basi tuweze kushuhudia hizi barabara zikipitika kwa ubora na hivyo tuweke historia sasa. Haya mambo yaliyotokea yawe kama historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili, ninaomba Serikali itenge fedha ya kutosha kwa *TANROADS,* ili kile kitengo kinachohusika na uchunguzi wa barabara kabla hawajatangaza zabuni, kiweze kufanya kazi yake vizuri ya kupembua hizo barabara na kuona ubora na udhaifu wake ikiwemo hiyo ya Somanga – Masaninga na Ndundu – Somanga, ili kuhakikisha kwamba itakavyokuja kujengwa basi iwe na ubora ambao utadumu kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba na kuishauri Serikali kwamba kuna vipande viwili vya lami pale Eneo la Nasaya katika Kata ya Kipatimu mita 300 tayari Mkandarasi ameshapatikana anaitwa Vesma na kuna Mkandarasi anaitwa *Hardcom International* mita 700 pale Kipatimu na taa zake. Ninaomba wale wakandarasi wasimamiwe haraka na kwa sababu kiangazi

kinaanza kuanzia mwezi huu, basi waweze kufanya kazi kwa haraka na tija iweze kupatikana ya barabara ile.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya nilimtaja Halima James Mdee, Mheshimiwa Mariam Kisangi ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi. La kwanza, kwa mujibu wa randama mafanikio ya utekelezaji wa bajeti; barabara mwaka huu mlipania kujenga kilomita 100 lakini utekelezaji wenu ni 26%. Wamejenga kilomita 100 *(26% performance)*. Barabara za Mikoa wamejenga kilomita 20 sawa na 20.9% *performance*. Ukarabati wa kiwango changarawe, wamekarabati kilomita 213 sawa na 23% *performance*. Madaraja *performance* yao ni 13%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zetu hapa wanaongea kwa mbwembwe, lakini ukija kwenye ufanisi ni chini ya 25%. Kwa hiyo, haya mambo siyo ya kujivunia sana. Siku zote nimekuwa nikisema ni muhimu sana wataalam wetu wa kuandika hizi hotuba wajaribu kufupisha maandiko ya hotuba. Wanajaza barabara nyingi, nyingine zinahusisha barabara ambazo zilishamalizwa. Kuna barabara zangu za Jimbo la Kawe toka mwaka 2020 zimekwisha lakini wanaziandika. Sasa, kwa nini tunakuwa tunajaza maneno mengi bila ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hizi fedha za Mfuko wa Barabara, hili ni takwa la Kikatiba. Amezungumza hapa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati Ibara ya 135(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza kabisa fedha zilizotengwa kwa madhumuni maalum, hazipaswi kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na tulitungia sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Barabara, Sura 220, vilevile imeitaka *TRA* ambayo ni Mamlaka ya Mapato kukusanya kwa niaba na kuziwasilisha kwenye mamlaka husika. Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka huu inasema kwenye yale maeneo yote manne yenye Mifuko, inasema Ukaguzi wa *TRA* ulionesha kwamba jumla ya shilingi trilioni 2.59 zilikusanywa na wao kwa niaba ya *REA,* Mfuko wa Maji, Mfuko wa Reli na kuhamishiwa Hazina *which* ni makosa, lakini bahati mbaya zilipohamishiwa Wizara ya Fedha, kilichotolewa kwenye Mifuko husika ni shilingi trilioni 1.4 tu. Shilingi trilioni 1.14 hazikupelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni ya miaka iliyopita ambayo ni mwaka mmoja uliopita Mkaguzi ametoa taarifa mwezi Machi mwaka huu. Anatuambia hapa Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi kwamba, kwenye eneo la *TANROADS* ama Mfuko wa Barabara kwa mwaka huu walitakiwa wapewe shilingi bilioni 800, wamepewa shilingi bilioni 200 halafu mnategemea miujiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Mkaguzi Mkuu katika zile shilingi trilioni mbili na kadhaa nilizozisema, Mfuko wa Barabara ulitakiwa upewe shilingi trilioni 1.4. Walichopewa ni shilingi bilioni 800 na shilingi bilioni 648 zimebaki Wizara ya Fedha. Kwa mwaka jana, shilingi bilioni 648, kwa Mfuko wa Barabara. Mwaka huu kwa mujibu wa Kamati ya Bunge 600 imebaki. Waziri wa Fedha na Wizara ya Fedha wanavunja Katiba halafu tunawaangalia tunajifanya kama hatujui na Bunge tunalalamika. Hatuwezi kuendesha nchi namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kusema kwamba ni muhimu sana kama Bunge tukasimama tunapotakiwa tusimame. Kama tuna Waziri anayeweza kukiuka maelekezo ya Katiba ya Nchi si mara moja fedha zinatozwa kutokana na tozo tulizozitoa kwa wananchi wa Tanzania kuchangia kwenye mafuta. Kila lita moja ya mafuta kwa mdundulizo wa mabadiliko ya sheria ya miaka zaidi ya sita, mwananchi anachangia si zaidi ya shilingi 500 au shilingi 600 tokea sheria hii ya tozo ianze. Sheria zinavunjwa, tunaangalia, fedha haipelekwi, kila mtu analalamika barabara hapa, unakuta barabara zimeandikwa nyingi. Wabunge waende

wakasome randama. Una kilometa moja, una kilometa mbili, una kilometa tatu, sasa barabara ya kilometa 200 wewe unapewa kilometa moja na unapiga makofi eh! Tumepata barabara. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Mdee dada yangu ninataka nimpatie taarifa tu kwamba Serikali imenikamilishia barabara ya kilometa 67 kwa lami nzuri na sasa hivi wanaanza kunifungia taa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Usinipotezee muda bwana sisi tunazungumza…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima unaipokea taarifa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu *cheap* hivi ndiyo vinaangamiza Taifa. Ninazungumza katika *broader aspect*. Ndiyo maana sijakaa hapa nikazungumza Barabara za Kawe kwa sababu ninazungumza masuala ya Kitaifa, nchi hii inahitaji barabara. Tumetunga sheria ili fedha za wananchi kupitia kununua mafuta ziweze kusaidia kurudisha maendeleo kwao. Fedha zinakatwa, zinakusanywa na *TRA* anabaki nazo Dkt. Mwigulu Nchemba pale Wizara ya Fedha zinafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda watuambie kuna matumizi mengine ya ziada ambayo Bunge halijui. Kwa sababu kama Bunge tunasema tunakusanya shilingi trilioni 44, au 46 kwenda kutekeleza mipango ya maendeleo, wanatuambia zimekusanywa. Ikija kwenye utekelezaji 20% wanapeleka wapi fedha? Watujibu. Isije ikawa tunapoteza muda hapa, fedha zinakusanywa zinaishia mifukoni kwa watu. Lazima watupatie majibu ya mantiki, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wakandarasi wazawa. Ukiangalia mwaka 2018/2019 wazawa walipata kazi ya thamani ya shilingi bilioni 187, wa kigeni wakapata kazi ya thamani ya shilingi bilioni 591. Mwaka wa Fedha 2022/2023 wazawa wakapata kazi ya shilingi bilioni 42, wageni wakapata kazi ya thamani ya shilingi trilioni 5.532. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia barabara zetu hatuzungumzi kilomita moja au barabara za vumbi, hizi kazi za njaa njaa, tunazungumza za bilioni, *Chinese companies more than 80%.* Nendeni kwenye randama mwangalie hizi shilingi trilioni 5.5 zingebaki kwa wakandarasi wetu wazawa kama hatuwazeshi tungefika wapi. Hivi kuna Kampuni ya Kitanzania ya Wakandarasi ina ubavu wa kwenda China na kupewa kazi? Nimeangalia *Airports* zetu tunazojenga, tunajenga viwanja vya ndege 15. Miradi mitatu bado kandarasi hazijapatikana, mradi mmoja ndio yule jamaa anaitwa Mayongo *Construction* ambaye amejenga Geita. Miradi 11 yote ni ya kigeni. Wakati yule aliyejenga Geita ameambulia shilingi bilioni zake 59 za kandarasi, *Chinese companies* shilingi bilioni 880, viwanja 15 vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi yetu, nilikuwa ninaangalia wakandarasi waliosajiliwa wako 13,000. Kuna Mfuko ule wa kusaidia wakandarasi ambao wana uwezo duni, ukisema wana uwezo duni. Eti Wizara imetenga shilingi bilioni nne! Yaani Mfuko Maalum wa kusaidia Wakandarasi wa Tanzania ambao labda wana uwezo wote mwingine isipokuwa pesa, shilingi bilioni nne? *What a shame? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme; hakuna wa kuibadilisha hii nchi zaidi ya sisi wenyewe. Tunasomesha watoto wetu, tunasomesha vijana wetu wakawe na hizi taaluma za ujenzi na majenzi, tutumie akili zaidi tusaidie Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee.

Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Kisangi, atafuata Mheshimiwa Omari Kigua na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu, Wizara ya Ujenzi. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kusimama hapa mbele kuweza kuchangia mchango wangu katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuitekeleza Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi kwa asilimia inayozidi 90. Ilani ya CCM Kifungu cha 29A kinasema, "Chama Cha Mapinduzi katika uongozi wake wa mwaka huu (Mwaka 2025) kitaimarisha miundombinu mbalimbali...", Ninanukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, "...kitaimarisha miundombinu mbalimbali pamoja na huduma za bandari, viwanja vya ndege reli, meli, vivuko, gati, na njia za usafirishaji wa umeme. Aidha, mitandao ya barabara za lami pamoja na madaraja mbalimbali yatakayounganisha nchi yetu na nchi nyingine". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona jinsi gani Daraja la Kigongo na Busisi linakwenda kukamilika. Daraja hilo muhimu limefanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, kinachoendeshwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Si jambo dogo, ni jambo kubwa sana. Pamoja na hayo, nimeshuhudia madaraja mbalimbali yakijengwa katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam. Daraja la Kigamboni, Daraja la Kijazi, Daraja la Mfugale, Daraja la Chang'ombe *VETA*, Daraja la Kurasini Uhasibu, lakini kivuko cha juu cha Kawe pamoja na miundombinu mingi tu ya Mwendokasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo makubwa sana yaliyofanywa na Serikali yetu hii ya Chama Cha Mapinduzi. Ninatambua katika Jiji la Dar es Salaam kumekuwa na ongezeko kubwa la watu. Idadi ya watu kulingana na Sensa ya mwaka 2022 ni watu 5,383,728. Kwa nini nimesema hivyo? Idadi ya watu

inaenda sambamba na uboreshaji wa miundombinu. Sambamba na idadi ya watu pia kuna ongezeko la vyombo vya barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu ninaomba niipongeze Wizara hii. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu wote pamoja na watendaji wote wa Wizara hii. Ninawapongeza kwanza kwa kuchukua hatua za dharura katika kurekebisha mawasiliano katika uharibifu wa kwenda pale Rufiji.  Walifanya kazi kubwa sana usiku na mchana. Hongera sana kwa mwanangu Mheshimiwa Waziri. Hongera sana sana sana pamoja na watendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye upande wa barabara nitaanza kuchangia nyumbani, Barabara ya *Kilwa Road*. Barabara ya *Kilwa Road*, kwanza niipongeze Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha kutoka kipande cha Mbagala Rangi Tatu mpaka Kongowe, ujenzi wa barabara nne. Ni jambo la muda mrefu lakini ninaishukuru Serikali imelipa fidia na kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kujenga barabara zile nne kutoka pale Rangi Tatu kwenda huko, bado turudi nyuma, msongamano umekuja sasa Rangi Tatu mpaka Zakiem msongamano wa watu. Je, kule tumekupangia mipango gani katika kuzitatua zile barabara, angalau tupate barabara nane sasa? Idadi ya watu imeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbagala ina watu takribani zaidi ya milioni moja kwa sasa hivi. Pia, kuna mwingiliano wa stendi za Kusini. Wananchi wanaotoka Kusini wote wanakuja pale Mbagala Rangi Tatu na maeneo mengine. Hivyo, Serikali iangalie njia madhubuti ya kuhakikisha tunaondoa msongamano kwa kuongeza zile barabara, tuweze kupata barabara nane kama kutoka Kimara mpaka Kibaha. Tuangalie huko twendako, tufanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuamua sasa kuweka kivuko Kigamboni cha watu wengine wa kampuni nyingine. Ni vizuri Serikali ikaungana na wadau katika kuboresha huduma ile. Sasa, changamoto ya kivuko cha Kigamboni,

mwananchi wa Kigamboni ana uhuru wa kuchagua; nipande Bakhresa au nipande kivuko cha Serikali. Hayo ni mambo mema sana na niiombe mambo hayo mema yaendelezwe katika sekta nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu niiombe, naona Barabara ya Mwendokasi ya kutoka Mbagala Rangi Tatu – Temeke – Bendera Tatu imekamilika mpaka Gerezani, lakini hatujaona mabasi ya mwendokasi. Tunaanza lini mabasi hayo? Mheshimiwa Waziri atakaposimama hapo ninataka leo aniambie, mabasi hayo yana changamoto gani mpaka leo hayajaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaona vinginevyo, basi tuhakikishe tunaingia ubia kama tulivyoingia ubia wa Kigamboni kwa Sekta Binafsi, nayo ichangie katika mabasi, tuweze kupata mabasi. Barabara zile miundombinu ile ya Serikali imetengenezwa kwa gharama kubwa kwa lengo la kuwasaidia wananchi wake. Sasa tunaomba kabla ya uchaguzi huu, tunaomba mabasi ya mwendokasi yaanze kuja Temeke. Kutoka Gerezani – Temeke – Mbagala Rangi Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye Barabara ya Kiwalani, nayo pia maeneo ya Mtoni Mtongani kwa Aziz Ali nako kumeanza kuwa na foleni. Ninaomba waangalie ni nini hasa kinachojaza foleni? Tumeona changamoto nyingi za barabara. Wanaongeza Barabara, lakini barabara ziendane; ushauri wangu barabara. Sasa *TANROADS* waangalie jinsi barabara zitaendana na vituo vya mabasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabasi hayana maeneo ya kusimama. Vituo maalum havipo, matokeo yake mabasi yanasimama katikati ya barabara, jambo ambalo linasababisha msongamano mkubwa. Hivyo basi, twendako niiombe Serikali yangu sikivu, wanapopanga bajeti ya ujenzi wa barabara wahakikishe wanaweka na bajeti za vituo vikubwa vya daladala, vikae mahali pa wazi na penye nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nitaongelea Barabara ya *Devis Corner* mpaka *Jet Corner*. Barabara hii ni mkombozi kwa

Wanatemeke lakini tunakoelekea nayo itakuwa na changamoto kubwa maeneo ya Buza. Buza sasa imekuwa ni sehemu ambayo ina mkusanyiko wa watu wengi. Watu wanaotoka Kilungule, wanaotoka Mwanagati, wanaotoka Temeke, wanaotoka huku, magari yanajaa Buza, matokeo yake sasa Buza nayo itakuwa kama Mbagala Rangi Tatu, hakuna pa kupenyea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile ilikuwa muhimu sana kwa sababu ukitoka Temeke ukienda Buza, ukipita Makangarawe Buza, unaingia unaenda sana Kilungule unatokea Mbagala ilikuwa ni msaada mkubwa na kimbilio la wananchi wa Mbagala. Tuendako msongamano unazidi kuwa mkubwa. Niiombe Serikali waangalie na wafanye tafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija hapo hapo kwenye barabara eneo la Temeke, Barabara ya Mandela: Barabara ya Mandela kutoka Kurasini Bandarini. Niipongeze Mamlaka ya Bandari; kwa kushirikiana na Serikali waliboresha kipande kile cha kutoka Bendera Tatu mpaka Kurasini, lakini kule kwingine bado. Barabara ile ni ya muda mefu sana, hata mwenyewe sijazaliwa ninaona (ile Mandela). Bado na yenyewe ninaomba itengewe fedha kuhakikisha barabara ile inakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa ya malori, kutoka Sokota mpaka ukifika *TAZARA* yaani hapo barabara inakuwa mtihani. Hata akitokea mgongwa kumpitisha inakuwa mtihani. Kila kitu pale kinakuwa mtihani. Kwa hiyo, niiombe pale *TAZARA* paangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Barabara nzuri sana ya Mchicha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, muda wako umekwisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia mchango wangu. Tulikuwa na Barabara ya Mchicha, lakini sasa barabara ile nayo imevamiwa. Niiombe Serikali ipange

utaratibu wa haya malori, mbona yanakwenda kila kona ya Mkoa wa Dar es Salaam? Barabara zetu zinaharibika. Je, wakati wa kujenga walilenga kwamba hizo barabara zitapitisha malori au yatapita magari ya kawaida ya wananchi?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninakushukuru sana sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam. Nimemtaja Mheshimiwa Omari Kigua, tutamalizia na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenipa nafasi na uhai kwa siku ya leo kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naye si mwingine ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye kwa hakika ameweza kuisimamia nchi hii na kutuongoza vizuri na hakika tuseme kwamba tumepiga hatua kwa sababu ya uongozi wake bora sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Ujenzi ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya, Katibu Mkuu Mheshimiwa Balozi Aisha na Naibu Katibu Mkuu ndugu yangu Msonde. Wote kwa pamoja wamekuwa wakifanya kazi nzuri. Tumekuwa tukiwaona wakitokea katika maeneo mbalimbali ku-*rescue situation* pale pahali ambapo barabara zimekuwa zikiharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama leo mbele ya Bunge lako Tukufu niweze kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kauli yake aliyoisema

pale Tanga siku anamalizia ziara yake Bandari ya Tanga. Alisema maneno yafuatayo:-

*"Ninakuelekeza Waziri wa Ujenzi na Waziri wa Uchukuzi, muone kwa namna gani mnaweza mkaisimamia Barabara ya Handeni – Kibirashi – Singida ijengwe kwa utaratibu wa PPP". (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale yalikuwa ni mawazo makubwa yenye busara ya hali ya juu sana. Sote tunatambua kwamba Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia imewekeza shilingi billioni 421 kwenye Bandari ya Tanga. Huu ni uwekezaji mkubwa sana. Utazirejesha fedha hizi kubwa kama barabara hiyo ambayo inaunganisha mikoa minne, kwa maana Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Singida haijaunganishwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, barabara hii ndiyo ambapo Bomba la Mafuta la ule Mradi unaotoka Hoima hadi Chongoleani – Tanga linapita. Sasa, ni barabara ambayo kwa hakika ina uhitaji mkubwa sana wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Hatuwezi tukaacha kuijenga kwa kiwango cha lami kwa sababu kwa sasa hivi haipitiki. Mikoa yote ya Kaskazini yote inategemea barabara hii, lakini kipindi cha mvua inakuwa haipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, hebu walisimamie elekezo hili la Mheshimiwa Rais. Uzuri ninampongeza kwamba ameisemea, sasa isibaki tu maneno Mheshimiwa Waziri, hebu nendeni mkakae kwa pamoja na Waziri wa Uchukuzi, waweze kuijenga barabara hii iweze kupitika kwa sababu *economic viability* yake ni kubwa sana. Tunatarajia shilingi bilioni 421 ziweze kurejeshwa ziweze kutengeneza barabara nyingine katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninataka kuchangia kwa siku ya leo ni barabara ambayo Mheshimiwa Shangazi ameizungumzia, Barabara ya Chalinze – Segera. Ni barabara ambayo ilijengwa miaka ya 1980. *Lifespan* yake imekwishapita, na barabara hii siku za karibuni hasa maeneo ya

Segera pale na maeneo ya Mkata kumekuwa kunatokea ajali mara kwa mara barabara hii imekuwa finyu. Watanzania wa miaka ile, idadi ya magari ya miaka ile sasa hivi magari ni mengi sana; shughuli za kiuchumi ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kuna umuhimu sasa kwa wenzetu wa Wizara ya Ujenzi, mwangalie ni namna gani ambavyo wanaweza wakatafuta fedha waweze kuijenga au kuikarabati upya. Nimeona amezungumzia Barabara ya Kusini kuanzia kwake Mkuranga kwenda Mtwara. Upo umuhimu kwa sasa hivi kuiangalia barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali hii ya Awamu ya Sita na Serikali Awamu ya Tano walijenga Daraja la Wami ambayo ilikuwa changamoto kubwa sana, tunashukuru. Sasa daraja lile lazima liende sambamba na kupanua Barabara hii ya Chalinze hadi Segera kwa sababu shughuli za kiuchumi ni nyingi, magari ni mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, nimwombe sana na wataalam wanasema, mimi si injinia. Wataalam wanasema barabara ikichukua muda mrefu sana, ile *lifespan* yake ikiisha maana yake atakapokuwa amechelewa zaidi, gharama ya kuja kuijenga upya itakuwa ni gharama kubwa sana. Twende tuepuke hilo Mheshimiwa Waziri, twende tuweke fedha tuweze kuijenga barabara hii iweze kuwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye eneo langu la Wilaya ya Kilindi, ninakuomba Mheshimiwa Waziri; wakati tulikuwa na mpango wa kujenga Barabara hii ya Handeni – Kibirashi – Singida tuone umuhimu sasa wa kujenga Barabara ya kuunganisha sasa kutoka Kibirashi kwenda Makao Makuu ya Wilaya Songe, ije iunganishe na Barabara ya Ngiloli hapa Gairo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni barabara ambayo ni *shortcut* na ambayo wananchi wengi wa maeneo hayo wataitumia. Hata wale wanaotoka Dodoma kwenda Tanga mara nyingi wanaitumia barabara hiyo. Mheshimiwa Waziri ninaomba alichukue eneo hilo na alifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, ameamua kujenga Madaraja ya Chakwale na Nguyami. Wametenga fedha nyingi sana. Madaraja yale yamekuwa na usumbufu kwa muda mrefu na madaraja yale ninataka niseme kwa ujumla kwamba, baada ya kukamilika yatasaidia wafanyabiashara, yatasaidia wakulima kuweza kupitisha mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mkandarasi yuko *site*; ninaomba wawasimamie vizuri madaraja hayo yakamilike ili yaweze kupanua shughuli za kiuchumi na halikadhalika za kibiashara kwa wananchi wetu ambao wanaitumia barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme jambo moja kuhusu madeni kwa wakandarasi wetu. Upo umuhimu wa kuweka utaratibu. Nimeona wanafanya jitihada za kulipa madeni, lakini spidi iongezeke. Watu hawa baadhi ya wakandarasi wazawa wamekopa katika benki na wanadaiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tusifanye mali zao kuchukuliwa, basi ninyi watu wa Wizara ya Ujenzi shirikianeni na Wizara ya Fedha waweke utaratibu yale madeni ya muda mrefu waanze kuyalipa ili tuwape nguvu Watanzania hawa ambao wana nia nzuri ya kuhakikisha kwamba na wao wanaijenga nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimwombe Waziri wa Ujenzi, mkandarasi yule ambaye wamempa kile kipande cha kilometa 20 kuanzia Handeni kuja Mafureta kilomita 20, kwa kweli anasuasua. Mheshimiwa Waziri amekuja amesema hata Waziri yule ambaye ni mtangulizi wake au wa nyuma alikuja akazungumza jambo hili. Nimwombe sasa, hebu atume timu yake wawasimamie mkandarasi huyu wa Kichina, ambaye hivi ninavyozungumza hayupo *site* na alikwishalipwa fedha zake zote, haidai Serikali sisi ndiyo tunamdai fedha na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Ulega, nina uhakika yeye na timu yake wanaweza kumsimamia mtu huyu aweze kujenga barabara hii. Kwa sababu wananchi wa Wilaya

ya Kilindi, wananchi wa Handeni wanahitaji barabara hii na wameisubiri kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nikushukuru sana sana kwa kunipa nafasi. Ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Omari Kigua. Nilimjata Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami nichukue fursa hii kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na nia njema ya Wizara ya Ujenzi pamoja na Serikali kuhakikisha kwamba miundombinu katika nchi yetu inaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Wizara kwa kauli yao kwamba bajeti yao itaendana pamoja na kazi na utu. Nami ninawapongeza kwa sababu utu wameshaanza kuonesha kwa kiasi kikubwa. Mambo mengi yaliyofanyika kwenye sehemu mbalimbali katika nchi yetu katika Wizara hii yanaonesha utu. Yanaonesha kwamba mna ana nia ya dhati ya kuhakikisha Watanzania wanakuwa vizuri kiuchumi na shughuli zao za maendeleo na za kijamii zinaendelea kila siku. Kwa hiyo, ninawapongeza sana na kwa niaba ya wananchi wa Iringa, kwanza kabisa niwapongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposimama hapa kwa mara ya kwanza mwaka 2020 niliongelea Barabara ya *Ruaha National Park* na nikaitengenezea *art* ambapo niliongeza masuala ya utelezi na ikanipa pia *nickname* kuitwa utelezi. lakini sasa wameonesha utu wa dhati kwa kutupatia barabara ile ambayo inakwenda kuchachamua uchumi wa wananchi wa Mikoa ya Kusini kwa kuendelea kuchachamua utalii wa Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru sana kwa barabara ile tulii-*sign* na tunaona kwa kweli kuna maandalizi yanaendelea. Tunaisubiri kwa hamu kubwa sana ile Barabara ya *Ruaha National Park* kilomita 104 na zaidi ya hapo kwa kuendelea kutu-*connect*

kwenye utalii. Tunawashukuru sana pia, kwa ujenzi wa barabara ya lami ambao umeanza kuanzia Iringa mjini kuelekea Kilolo kilometa 33.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru kwa kutaka kuufanya mji wa Iringa, kuwaongezea utu wananchi wangu wa Iringa Manispaa kwa kuwatengenezea Iringa *bypass* kilometa 7.3. Tunajua wamejenga mita 450, tunashukuru lakini tunafahamu vile ni vigongo ni milima mikali sana inayopasuliwa. Madaraja saba wameyakamilisha, ninashukuru kwamba walipoona mkandarasi anasuasua wamefanya tena *revisit* ya kutupatia Mkandarasi mzuri na Februari walitupatia tena shilingi bilioni nne kwa ajili ya barabara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile kwetu sisi ni ya muhimu sana, hasa kwa kufanya Mji wa Iringa uendelee kuwa lango la Utalii Kusini, hasa kwa kuangalia vivutio au kuangalia miundombinu ya utalii inayowekwa katika Mji wetu wa Iringa ikiwepo kivutio cha Kihesa Kilolo. Kwa kweli tunahitaji malori makubwa yanayokatisha katika Mji wa Iringa yakiwa yamebeba mbao na makaa ya mawe yakielekea mikoa sita ya Kaskazini, mikoa sita ya Kanda ya Ziwa na kwenda kwenye nchi nyingine za jirani za Tanzania ambazo zipo Kaskazini, tunaomba sana malori yale yasiendelee kukatisha katikati ya Mji wa Iringa, yapite Iringa *bypass*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Iringa *bypass* ikamilike wakati wanaendelea kupigapiga ili pale tusiendelee kuleta maneno mengi sana na watumiaji wengine wa kimataifa wa barabara ile, basi tunaomba waangalie namna ambavyo barabara nyingine za mchepuo zinaweza zikawekwa katika mji wa Iringa, kwa kuwa ni malengo yao kuangalia miji inayokua kwa haraka ingawa Iringa hawajaitaja, lakini Iringa ni moja ya mji unaokua kwa haraka sana ingawa ni Manispaa. Tuendelee kuwa na barabara za mchepuo ambapo wakitupatia ile Wilolesi ambayo tumeomba pia kama kilomita ngapi hivi ili ipite mchepuko basi watu wasiendelee kutumia ile barabara kubwa tuachie magari makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia kwa ajili ya Barabara ambayo inaanzia Iringa kwenda Itunundu - Pawaga ambayo ni kilometa zaidi ya 71.9. Wametupatia pale Iringa kwamba tutakuwa na Ikonongo - Pawaga kama kilomita tano wanatupatia. Tunaomba sana hizo kilomita tano mapema, kwa sababu wananchi wenzetu wa Jimbo lingine lile la Kalenga wanatumia sana huduma za kijamii zilizopo Iringa Manispaa, zikiwepo shule pamoja afya kama vituo vya afya pamoja na hospitali za wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakitupatia zile kilomita tano watatusaidia sana wale akinamama wengi wanaowahishwa kuja kwenye hospitali yetu ya rufaa ya Mkoa Iringa na ile ya wilaya watakuwa wakija vizuri sana na ndiyo utu wenyewe kuhakikisha kwamba akinamama wanapokuwa wanaongeza wapigakura wa Taifa hili wanasafiri kwenye sehemu salama ikiwepo barabara ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana pia kwa kuendelea kutambua kampuni zile za Mtwivila, *GSM* zilizopo Iringa lakini utu sasa ni kuhakikisha wale pia wanalipwa jamani, wanalipwa fedha zao wanazotudai, kwa sababu wale wana *network* kubwa. Huku wana watu wanaowauzia nondo, wale wenye nondo wameajiri watu, wale nao wanasomesha watoto. Kwa hiyo usipomlipa mkandarasi, kuna mnyororo mkubwa wa watu wengi huku ambao wanaendelea kupata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo utu ni kuhakikisha ule mnyororo mzima unao mtegemea mkandarasi wa Tanzania unakuwa na wenyewe una utu, unapata hadhi unajisikia raha kuendelea kuishi katika Taifa hili kwa kuwalipa wakandarasi ili yeye mkandarasi akalipe dukani, ili yule mtumishi wa dukani naye aweze kumhudumia mke wake, ili mke wake naye aweze kupika vizuri watoto wapate afya nzuri tusiwe tena na watoto waliodumaa, huo nao ni utu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Katika viwanja vya ndege ambavyo wamejenga katika nchii hii ni Uwanja wa Ndege wa Iringa ambao umekamilika kwa 93%. Tunaomba kile kipande kilichobaki kwa ajili ya jengo la abiria

na *tower* ya kuongozea, waanze kuijenga haraka kwa sababu ndege kubwa zimeshaanza kushuka katika Mji wa Iringa. Sasa bado tunakosa jengo la abiria na ile *tower* kubwa ya kuongozea ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru, lakini ndani ya Uwanja wa Ndege wa Iringa tuna Shule ya Msingi moja pale, Imeche ipo ndani ya uwanja wa ndege. Nimeongea sana na Waziri wa Elimu, nimeongea na TAMISEMI, nimechangia kwa maandishi TAMISEMI, ninaomba tena nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kwa sababu ndiye aliyekuwa na dhamana ya kutulipa fidia katika ile shule, tunaomba shule ile ihame ndani ya uwanja wa ndege iende nje ya uwanja wa ndege. Huo nao ni utu, kuwafanya watoto wale wasipate mapresha ya ndege kubwa zinaposhuka, lakini wasome katika mazingira ambayo ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jesca Msambatavangu. Waheshimiwa Wabunge muda wetu kwa asubuhi ya leo umeishia hapo lakini nina matangazo mawili.

Kwanza nitawatangaza wachangiaji watakaoanza kuchangia jioni ya leo. Tunaye Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi; hao ndiyo tutaanza nao.

Tangazo la pili ni wageni ambao wameingia mara nyingine kwa asubuhi hii ya leo. Tunaanza na wageni wa Mheshimiwa Spika; kuna wageni 25 wa Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson ambao ni viongozi wa Taasisi ya Taifa Letu Kesho (TK) kutoka Mkoani Mbeya, karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Tuna wageni waliokaa Jukwaa la Spika pia; hawa ni wageni wa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Waziri wa Ujenzi ambao ni Ndugu Khadija Ally, Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga; Sheikh Walid

Kawambwa, Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam; Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Pwani, Mzee Mwinshehe Shabani Mlao; na Wajumbe wa Kamati ya Siasa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Mkuranga, Alhaji Juma Magila na Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya ya Mkuranga, hawa hapa Wajumbe wa Halmashauri Kuu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kuna wageni wa Mheshimiwa Ulega pia ambao ni wakuu wa idara, vitengo, wataalam na wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara.

Wapo pia Wakurugenzi na Mameneja wa Mikoa kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara; Chama cha Umoja wa Makandarasi na Watoa huduma Tanzania *(TUCASA);* Chama cha Wakandarasi Wanawake Tanzania *(TWCA);* pamoja na Chama cha Wakandarasi Tanzania *(CATA)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wawakilishi wa Taasisi za Kifedha *(NMB, CRDB* na *Equity Bank);* Washirika wa Maendeleo (Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Uwekezaji Ulaya). Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya ya Mkuranga na wapigakura wake kutoka Jimbo la Mkuranga, karibuni sana wapigakura wanaotoka huko Mkuranga kwa Mheshimiwa wetu Abdallah Ulega. Ninaamini kwamba mnaelewa kazi yake ni nzito na nyeti, kwa hiyo Masheikh na wapigakura dua zenu na *support* yenu. *(Makofi)*

Tuna wageni tisa wa Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, ambao ni wahamasishaji wa matumizi ya Nishati safi ya kupikia kutoka *Bongo FM Radio* wakiongozwa na Ndugu Mariam Migomba, karibu sana. *(Makofi)*

Kuna wageni watano wa Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kutoka kampuni ya *IDEON* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Naibu Waziri Maliasili na Utalii ambao ni jamaa zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 41 wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, ambao ni Wanakwaya wa Mwangaza kutoka Longido, Mkoani Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine watatu ni wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambao ni viongozi wa Taasisi ya Taifa Letu Kesho (TK) kutoka Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ambaye ni Ndugu Ahmed Karia, Mratibu wa Taasisi ya Taifa Letu Kesho kutoka Moshi mkoani Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Felista Deogratius Njau ambaye ni Ndugu Lightness Kizanga, mdogo wake kutoka Moshi, Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni wengine waliokaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika na ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu wa Ujenzi ambao ni Sheikh wa Mkoa wa Pwani, Sheikh Hamis Mtupa; na Wachungaji wa Makanisa kutoka Mkuranga, karibuni sana wachungaji wetu pamoja na Sheikh wetu kutoka Mkoa wa Pwani wote. Karibuni wageni wetu wote katika ukumbi wetu. *(Makofi)*

Ninawashukuru Waheshimiwa wote kwa utulivu na kwa kuchangia na Mheshimiwa Wazri na timu yake wapo makini pale kwa kusikiliza. Kwa hiyo, niwatakie mchana mwema na ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni.

*(Saa 7.09 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI- KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea tunaanza kama mlivyotangaziwa mchana, Mheshimiwa Miraji Mtaturu, Mheshimiwa Sylvia na Mheshimiwa Dkt. Ritta.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nianze kuchangia hoja iliyopo mezani kwetu, hoja ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri mahiri kabisa Ndugu yetu Abdallah Ulega.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kunijalia uzima na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuweza kuchangia hoja iliyopo mezani. Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya katika kuongoza Taifa letu na zaidi katika sekta hii ameitendea haki kwani fedha nyingi zimetoka ambazo zimetekeleza miradi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameeleza. Ni dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba miundombinu ya nchi hii inatekelezwa kwa vitendo kama ambavyo iliahidiwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri ndugu yetu Mheshimiwa Abdallah Ulega pamoja na Naibu Waziri ndugu yetu Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote kwa kazi kubwa ya kusimamia Sekta ya Ujenzi ambayo kimsingi ni sekta inayochochea maendeleo ya sekta zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa wanayoifanya na hata Mheshimiwa Ulega, tulimwona kule Kusini akisimamia kwa dhati kazi ambayo ilikuwa imefanyika pale tatizo kubwa lililotokea la kuchukuliwa madaraja pamoja na barabara kufungwa alikaa takribani siku nne kuhakikisha kwamba wananchi wa Kusini wanaenda kupata mawasiliano. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani na pongezi hizo na mimi ninapongeza sana nimeona barabara zimejengwa katika taarifa madaraja lakini kama ambavyo haitoshi tumeona zaidi ya 66% imetoka kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, nami nikiwa Mjumbe wa Kamati hii tumeendelea kuona taarifa mbalimbali na tumetembelea miradi, tumeona mpaka Daraja la Pangani, tumeona Daraja lile la Kigongo Busisi ambalo leo sasa hivi limefikia 99% wananchi wale wa Kanda ya Ziwa wanaenda kufaidika na daraja lile ambalo ni refu kuliko lolote katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu kama Tanzania tunajivunia sana kuwa na mradi mkubwa kama ule na fedha Serikali imetoa hivi tunavyoongea hali inaenda vizuri, hivi karibuni wataenda kuzindua, tunaipongeza sana Serikali kwa dhamira ya dhati katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi nipongeze kwenye eneo hili la Chuo ambacho kipo pale Morogoro Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (*ICoT)*. Chuo hii ni muhimu sana, tumekitembelea mwaka juzi na mwaka huu tulivyoenda kutembelea tumekuta wameshatenga fedha na jengo limeanza kujengwa wametenga zaidi ya shilingi 2,000,000,000 ambazo kimsingi majengo haya yakiboreshwa kile chuo kitarudi kuwa na hadhi yake ambayo inastahili kwa sababu itaenda kuandaa mafundi ambao ni mafundi wa kati, wale *artisan* ambao ni watenda kazi katika Sekta ya Ujenzi ambao kwenye maeneo mengi wanapotea. Kwa maana ya Serikali kuendelea kukiboresha chuo kile inaonekana dhamira yake ya kuendelea kuwaandaa mafundi wa kati ambao watakuwa ni kichocheo cha shughuli za ujenzi katika nchi yetu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa

mnayoifanya pale Morogoro ya kuboresha chuo kile ambacho kimsingi kinarudi kwenye heshima yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kuomba na kushauri tusije tukawaza kuanza kufikiria kianze kuchukua watu wa *digrii* kibaki vilevile ili tuweze kupata mafundi wa kati ambao wataenda kusaidia kwenye sekta ya ujenzi. Kwa sababu hawa wanaomaliza *digrii* wengi ni mameneja lakini hawa ambao tunawapata kwenye chuo kile wanakuwa ni watenda kazi ambao wataenda kufanya kazi kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye reli na maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ninaipongeza Serikali kwenye jukumu la kuweza kupunguza foleni Dar es Salaam, tumeenda kutembelea *BRT* pale tumeona miradi mbalimbali inafanyika tumeona *commitment* ya Serikali katika kuhakikisha kwamba Mji wa Dar es Salaam unafunguka ni mji wa kibiashara ule. Kupunguza mwendo wa watu kwenda kwenye maofisi na kwenda kwenye huduma mbalimbali kumaliza zile barabara kwa maana ya mwendokasi pale Dar es Salaam. Ni mradi ambao ni muhimu sana tumeona hata wa Gongo la Mboto sasa pana funguka ili watu waweze kwenda haraka kwenye shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuomba jambo moja tu Mheshimiwa Waziri, tuhakikishe kwamba miradi ile inakwenda kwa kasi ili kazi iishe. Hivi tunavyoongea kuna baadhi ya maeneo imefunga inasubiri tufungue ili watu waendelee na shughuli zao. Kwa hiyo, kwa sababu ujenzi unaendelea maeneo mengi yamefungwa, kwa hiyo imekuwa tena ni tatizo katika Mji wa Dar es Salaam. Tuwaombe wakandarasi waongeze kasi kama tulivyoshauri kwenye Kamati ili tuhakikishe kwamba lengo letu linatimia la kupunguza ile foleni pale Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi Mheshimiwa Waziri nilikuwa nimeulizia suala la *EPC+F* nimeona kwenye hotuba yako umeeleza kwamba mme-*review* upya mpango huo sina haja ya kurudia lakini wananchi walikuwa wanataka kujua mwisho wa miradi hii kwa sababu ni kilomita zaidi 1,035.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili *specific* niongelee hii barabara ya Handeni - Kibirashi kuja Kwa Mtoro mpaka Singida. Nimefurahi ameeleza na nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuona namna ambavyo ameamua kwamba sasa ujengwe kwa upande wa *PPP* ili isaidie kwenda haraka kuweza kuunganisha na Bandari ya Dar es Salaam ambayo tumewekeza zaidi ya shilingi bilioni 421 ili thamani ya fedha tuipate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba twende haraka hiyo barabara tunahitaji sana tunaisubiri mikoa zaidi ya minne, lakini itawasaidia wateja wanaotoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda haraka kupeleka mizigo yao kwenye Mikoa ya Magharibi. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa tunaomba hii barabara kilometa 460 iweze kujengwa haraka na wenzetu wa *TANROAD* pamoja na *TPA* wamalize mchakato wa mazungumzo ili tuweze kuona matokeo na hamu ile ya Mheshimiwa Rais iweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi niongelee barabara yangu Mheshimiwa Waziri, Ikungi - Mang'onyi – Londoni kwenda Solya. Barabara hii wameanza kutujengea pale Ikungi wametujengea kama kilometa tatu hivi mpaka hospitali ya Wilaya na pale Halmashauri. Tunaomba wakitujengea kama kilometa 50 kwenda mpaka kwenye Mgodi wa Shanta ambao unazalisha fedha nyingi na kodi inatoka pale ili tuweze kuweka lami kuondoa vumbi ambalo linatimka kwa sababu magari mengi yanatumia ile barabara ili kusaidia afya ambazo zinaharibika za wananchi wetu, kuweka lami itasaidia kuongeza kasi ya uchumi. Wananchi watafaidika na mradi ambao umeweka pale kwa ajili ya kuleta uchumi mkubwa kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, barabara hii pia tunaisubiri tunaomba Waziri atusaidie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni suala la Mfuko wa Barabara, ninaomba sana fedha ambazo zinatengwa ziende kwenye maeneo yale kwa ajili ya kuboresha barabara ambazo zimeharibika nchini kwetu, kama Barabara ya Dodoma kwenda mpaka Singida imekufa kabisa. Tunaomba Waziri aiangalie kwa jicho la pekee. Baada ya maneno haya, ninaunga mkono hoja asilimia mia moja ili tuweze kuendeleza kazi nzuri waliyofanya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sigula, Mheshimiwa Dkt. Kabati na jiandae Mheshimiwa Asenga.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha leo kusimama katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa sana anayoifanya hasa katika Sekta hii ya Miundombinu. Ni hapa katikati tu nchi yetu imepita katika changamoto nyingi za kuwa na mvua nyingi, lakini Mheshimiwa Rais alipambana na kuhakikisha Wizara hii inapata fedha na kwenda kutatua changamoto za wananchi, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee sana ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu nzima. Sisi wote ni mashahidi tunaona namna ambavyo wanapambana huko barabarani kuhakikisha kwamba Sekta hii ya Ujenzi inakuwa imara. Tunawapongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi zote hizo ambazo nimezitoa, tunatambua kuwa maendeleo ni hatua na nchi yetu katika Sekta ya Ujenzi tumeona watu wengi wanapenda sana kubeza, lakini sisi Wajumbe wa Kamati tumezunguka nchi nzima, tumeona miradi mingi na mikubwa ambayo inafanywa na Serikali hii kwa kweli tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ningependa sana niongee na Watanzania niwaambie tunapenda sana kuwa watu wa kulaumu ka kudharau vya kwetu, lakini leo sisi Kamati ya Miundombinu tumepokea Wabunge kutoka nchi za wenzetu wanakuja kujifunza Tanzania ni namna gani tunatekeleza miundombinu yetu. Kwa hiyo, niwaombe sana Watanzania tuwe na tabia na tamaduni ya kujali vya kwetu na kuvipenda. Tanzania

kwenye Sekta ya Ujenzi tunafanya vizuri sana na ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na maoni na mapendekezo ya Kamati na hapa katika changamoto ambazo Kamati ilizibaini, ningependa sana kuzungumzia suala la ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo hasa kwenye miradi hii ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tanzania ni waelewa na maeneo mengi Serikali imekuwa ikiyataka kwa ajili ya kufanya uendelezaji ili kuleta maendeleo na wananchi bila wasiwasi wametoa maeneo yao ili kuhakikisha miradi hii hasa ya barabara inatekelezeka katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kumekuwa na changamoto ambayo sisi kama Kamati tumezungumza kuanzia Bunge hili limeanza mpaka hili Bunge la mwisho na majibu ya Serikali yamekuwa ni kwamba wanafanyia kazi. Ukiangalia maeneo ambayo wananchi wametoa kwa ajili ya ujenzi wa barabara na hapa ningependa nitumie Rukwa kama *case study* lakini ni maeneo nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nyingi ambazo wananchi wamepisha ili zitengenezwe, lakini wananchi wale mpaka leo bado hawajapewa fidia zao na kwingine wanakwenda zaidi ya miaka 10, miaka 15 na miaka 20. Tunaona kabisa hili si sawa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fidia kwa wananchi waliotoa maeneo yao siyo hisani, hii ni haki yao wanapaswa kupewa kwa wakati na wanapaswa kupewa fidia iliyo kamili. Sasa leo ukienda Mkoa wa Rukwa ukianzia Wilaya ya Nkasi, Wilaya Kalambo na Wilaya ya Sumbawanga kote utakutana na malalamiko ya wananchi wanaodai fidia kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ningependa nizitaje barabara hasa ukienda Chala pale zaidi ya nyumba 40 zimevunjwa na wananchi zaidi ya miaka 10 hawajapewa fidia zao. Wananchi hao wanaumia wana mapenzi na Serikali yao,

lakini wanaumia kwa sababu hawatendewi haki. Kwa hiyo, ningependa sana Mheshimiwa Waziri…

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nipende kumpa Mheshimiwa Sylvia taarifa Mji Mdogo wa Chala ambao sema kuna wananchi zaidi 40 ambao wanadai fidia zaidi ya miaka 11. Wananchi hao wamekuja, kila siku wana kikao, taarifa ambayo amejibiwa na *TANROADS* ni upotoshaji. Silaumu *TANROADS,* lakini ni taarifa ambayo hapa katikati haina uhakika wa kuwapa haki yao, haki yao inataka kunyang'anywa nao hao viongozi ambao wanaongoza kunyimwa haki yao ni Mzee Kilokoto na Mzee Kailinyi katika Mji Mdogo wa Chala.

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mbogo, hiyo ni taarifa au unachangia? Wewe mpe taarifa Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi, Sawa?

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema Mkoa wote wa Rukwa tuna changamoto hiyo na hata ukienda Wilaya ya *Sumbawanga DC,* kuna barabara ambazo zimepita ukianzia Barabara ya Muze -Ntendo pale kuna wananchi wametoa maeneo yao zaidi ya miaka 10 hawajapewa fidia. Pia kuna Barabara ya Kalambanzite kwenda Ilemba pale kuna wananchi wanadai fidia, lakini kuna barabara ya Ntendo - Luwa pale kuna wananchi pia wanataka fidia. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri na hii tunaiongea tukiwa *serious,* tukiwa tunamaanisha. Kwa kuwa, hili ni Bunge la Mwisho ninapenda Waziri atakapokuja kutoa majumuisho aje na majibu

ya msingi kutaka kujua hatma ya hawa wananchi na kama Serikali bado hatujajipanga kuwalipa fidia basi tuwarejeshee maeneo yao tutakapokuwa tayari tutayachukua tena ili wananchi hawa waweze kuendeleza maeneo yao kwa sababu wamekaa kwa muda mrefu hawajui wafanye nini hawaruhusiwi kuendeleza maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inataka wasipolipwa kwa wakati kila mwaka iongezeke riba ya asilimia sita, kama Serikali hii pia itakuwa ni hasara kwetu. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja kutoa majumuisho uje na majibu kuhusu hawa watu wa fidia za maeneo yao. Ninakushukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya. Taarifa zikiwa ndefu zinakula muda wako vilevile. Mheshimiwa Dkt. Kabati, jiandae Mheshimiwa Asenga na jiandae Mheshimiwa Silanga.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia jioni hii ya leo. Nami ninaomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu na nianze kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya, kuhakikisha miundombinu Tanzania inakuwa ya uhakika na kuwatendea haki wananchi wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba Watanzania wote sasa kwa kila mtu kwa dini yake aweze kumwombea Mheshimiwa Rais wetu ili tuweze kumpa kura za kishindo, kura za uhakika kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika nchi yetu. Niendelee kumpongeza Waziri wetu Mheshimiwa Abdallah Ulega, kwa kweli kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya na tuliona moto wake alipoteuliwa tu akaenda Dar es Salaam pale akatoa moto kwa wakandarasi ambao wamekuwa wazembe. Ninaomba moto huo uendelee afike nchi nzima akague miundombinu yote, lakini asiache kuja Iringa na aje katika Wilaya ya Kilolo ili aone miundombinu yote na akague barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana pia Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya, ambaye amekuwa akifanya kazi nzuri ya kumsaidia Waziri, lakini na kujibu maswali yetu vizuri sana hapa Bungeni. Nisimsahau pia ninampongeza Katibu Mkuu Balozi *Engineer* Aisha, kwa kweli nikupongeze kwa sababu ni mama ambaye ameonesha anaweza, hii Wizara siyo mchezo mchezo ni Wizara dume, lakini wewe mwanamke umeitendea haki. Nimpongeze pia Naibu Katibu Mkuu *Engineer* Masonde ambaye kwa kweli na yeye kwa kipindi kifupi ameunganisha nguvu sana katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijamtendea haki Meneja wangu wa Mkoa wa *TANROADS, Engineer* Msangi kama sitakuwa nimempongeza amekuwa ni kaka ambaye amekuwa akitujali hata Wabunge wa Viti Maalum akitusikiliza na kuendelea kufanya kazi pamoja. Kwa hiyo, ninampongeza ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mchango wangu sasa niuelekeze katika Kiwanja cha Nduli cha Iringa. Ninawapongeza sana Serikali ninaishukuru sana, sasa hivi tayari hata ndege zimeanza kutua katika Uwanja wetu wa Iringa pongezi nyingi sana kwa Serikali. Mheshimiwa Rais alikuja kuzindua na sasa hivi ndege zimeanza kutua. Nimpongeze pia Waziri wa Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kitu kimoja kwamba pale bado jengo la abiria halijajengwa, tunaomba waje wajenge na *tower* lakini pia kuna Shule ile ya Nduli ambayo kwa kweli watoto wamekuwa wakipata shida sana, hata Mbunge alichangia asubuhi, ninaomba wale watoto waletewe pesa kwenye Halmashauri iondolewe kwa sababu wamekuwa wakipata shida hata ufaulu wao sasa unapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia ujenzi wa Barabara ya Msembe, ambayo inakwenda *Ruaha National Park.* Kwa kweli, tunawashukuru sana kwa sababu, sasa hivi itajenga uchumi mkubwa wa Iringa na nchi nzima, lakini utalii na kazi zitaongezeka; wananchi wengi watajiajiri kupitia utalii katika Mkoa wetu wa Iringa. Niombe sasa fidia zilipwe kwa wakati, ili hii barabara iweze

kujengwa wakati fidia za wananchi hawa wa Msembe zikiwa zimeshalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niielezee Barabara ya Kitonga. Hii barabara nimekuwa nikiiulizia mara nyingi sana, ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu ya Tanzania, lakini barabara hii inaunganisha uchumi na Lango la nchi za *SADC*, lakini ujenzi wake umekuwa ukisuasua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara magari yanakwama kuanzia saa tatu, nne, saa sita, hata siku nzima. Tunaomba sasa utakapokuwa unajibu, Mheshimiwa Waziri, utuambie suluhisho ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumeshaomba, ikiwezeka, kuna barabara ile inayotoka Mahenge – Udekwa – Wotalisoli – Mlafu mpaka Ilula, utuambie suluhisho la hii Barabara, wananchi wanateseka sana. Nitashika shilingi kesho kama sitapata jibu la uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze barabara inayojengwa kutoka Iringa kwenda Kilolo kwa sababu, inaunganisha Majimbo matatu, Iringa, Kilolo na Kalenga. Kwa hiyo, ninawashukuru sana, lakini ninaomba sasa, ikiwezekana ijengwe pia, kutoka Kilolo – Kibaoni – Dabaga kwa njia ya lami ili kuweza kusaidia uchumi wetu wa Kilolo. Pia ombi langu lingine ni Barabara ile ya Dabaga – Nang'ange mpaka Boma la Ng'ombe; hii barabara imekuwa ikipitisha magari makubwa sana. Niombe, sasa hivi hii barabara ipelekwe kwenye hadhi ya mkoa iweze kukarabatiwa kila wakati ili uchumi wa Kilolo usiweze kukwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Barabara nyingine ambayo inatoka Dabaga – Itonya – Muhanga inakwenda mpaka Morogoro. Tunaomba hii barabara sasa ifunguliwe ili iweze kufungua uchumi wa hii mikoa miwili, itakuwa inawasaidia wananchi wengi sana kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Barabara hii ya Ilula – Mlafu – Wotalisoli – Mkalanga, inapita Kising'a inakwenda mpaka Kilolo, Makao Makuu, hii barabara ni ya kisiasa, lakini pia ni ya kiuchumi.

Tunaomba sasa hii barabara, hata kutokana na ufinyu wa bajeti, ikarabatiwe iweze kupitika kila wakati kwa sababu, sasa hivi kufika Makao Makuu ya Wilaya ya Kilolo wananchi wanazunguka, wanakwenda mjini ndiyo waende Kilolo. Ninaomba hii barabara iangaliwe kwa uzito wake na ikiwezekana ijengwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze pia, Serikali kwa utaratibu wa ujenzi wa *PPP*. Tunayo ile Barabara ya Mafinga – Mtiri – Mgololo, hii barabara ilikuwa ijengwe kwa Utaratibu wa *EPC+F,* lakini hatutajua itajengwa kwa utaratibu gani. Hii barabara pia, ni ya kiuchumi, kuna viwanda vya chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ninaomba sasa wakandarasi walipwe madeni yao kwa sababu, wanapolipwa pia na miradi mingi inakuwa inajengwa kwa haraka. Tunaomba, wamefanya kazi nzuri sana katika nchi hii, lakini wakandarasi wa ndani wajengewe uwezo kwa kulipwa mapema na barabara zetu ziweze kupitika muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niombe, hii Barabara ya Dodoma – Iringa ijengwe upya kwa sababu, viraka ni vingi mno. Kila sehemu viraka, kila sehemu viraka, sasa hii barabara ijengwe yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, Mheshimiwa Silanga, Mheshimiwa Antipas na Mheshimiwa Malima.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia Wizara yetu ya Ujenzi. Sisi, kama Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, chini ya Mwenyekiti wetu komredi, Mheshimiwa Selemani Kakoso kwa kweli, tumeisimamia sekta hii kwa karibu sana. Komredi Kakoso ni miongoni mwa watu wazoefu sana katika Sekta ya Miundombinu, amekuwa akituongoza katika Kamati kutokana na uzoefu wake kufuatilia miundombinu ya nchi hii, hususan katika Sekta ya Ujenzi. kwa kweli angekuwa *Engineer* sijui ingekuaje,

kama hapa tu sio *Engineer,* lakini ana uzoefu mkubwa kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, leo tuna-*discuss* bajeti ya Wizara ya Ujenzi hapa na Wizara ya Ujenzi inashika miundombinu yote ya nchi hii. Waziri au Mheshimiwa Rais hata angekuwa na uwezo akatenga Bajeti yote ya Serikali, sidhani kama ingetosha asubuhi ya leo kumaliza barabara na changamoto zote ambazo zinatukabili sisi katika nchi yetu. Hayo nimejifunza kutoka katika Kamati yetu ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambazo zipo katika nchi yetu ni kubwa sana na kadri zinavyopatikana fursa za kupunguza changamoto hizo, tunaishukuru Serikali na tunampongeza Mheshimiwa Rais na Wizara kwa ujumla; Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *Chief of TANROADS,* Mohamed Besta na wengine. Tunaona Mheshimiwa Waziri unahangaika, umekuja kule kwetu na helikopta, Mheshimiwa Waziri haujapanga mafuriko yale, yametokea tu, unaambiwa barabara imekatika inatakiwa pesa; umeenda Mtwara inatakiwa pesa. Kwa hiyo, yote haya yanataka pesa za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wengine wanaolalamika, Mheshimiwa Waziri, ninawaambia walishawahi kukaa siku moja wakasikia bajeti ya Serikali? Tunaposema trilioni 44 mathalani na wanaposema nchi yetu hii ni tajiri inaweza ikatoa kila kitu, walishawahi ku-*calculate* wakaona kwamba, kwa rasilimali tulizonazo tunaweza tukafanya yote kwa siku moja? Kwa wakati mmoja? Kwa miaka hata mitano au mitatu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kumaliza yote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunachokizungumza hapa ni umuhimu na sisi, kama Wabunge, tunatoa maeneo yenye changamoto nyie myapange kutokana na vipaumbele vyenu ili muweze kutatua sekta ya miundombinu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, sisi Kilombero, Mkoa wa Morogoro, ni miongoni mwa mikoa ambayo tunalalamika kila siku iunganishwe na mikoa mingine. Tuna Barabara yetu ile ya

kutoka Kilombero kuunganisha Ulanga – Lindi, unaifahamu, ilikuwa *EPC+F*. Tuna Barabara yetu ya Ifakara – Malinyi – Njombe, kuna Barabara yetu ya Ifakara – Mlimba – Njombe na ile nyingine inaenda mpaka Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hizi zinataka fedha nyingi sana na sisi tumeelewa Mheshimiwa Waziri, kama *point* niliyosema mipango ya Serikali, tunaiomba siku ikipatikana fedha, ikapatikana fursa, watusaidie sana kufungua barabara hizi. Tunaishukuru Serikali kwa sababu tumeambiwa tayari Barabara ya Ifakara – Lupilo kwenda Malinyi iko katika mpango. Hii inadhihirisha yale niliyoyasema kwamba, wakati wote tunalalamika, mwaka 2021 tumelalamika, mwaka 2022 tumelalamika, mwaka 2023 tumelalamika, leo tupo mwaka 2025 barabara ile imewekwa kwenye mpango. Kwa hiyo, hilo ndilo tunalosisitiza sana Mheshimiwa Waziri, tunavyozungumza hapa tunaomba sana watusaidie, inapopatikana fursa basi waweze kufanya hizo barabara ambazo tunazilalamikia wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla kutoka katika Kamati yetu, ninalotaka la kwanza ni kusaidia uchumi wa nchi yetu kutokana na tathmini ambazo zimefanywa na wataalam, hasa kuhusu bandari yetu kuunganisha na barabara na malori ambayo Wabunge wengi wameyasemea. Sisi tumeenda Dar es Salaam zaidi ya mara mbili, mara tatu na Kamati ya Bunge ya Miundombinu; Mheshimiwa Waziri katika vitu vinavyotuchelewesha ni kutokuunganisha reli yetu ikaenda kwenye Wizara ya Uchukuzi ama na barabara maalum, hata kama za chini, kuchukua yale makontena bandarini na kuyatoa nje ya Dar es salaam kwa utaratibu maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuendelea kuwa nchi ya namna hiyo Mheshimiwa Waziri. Pita pale Buguruni, huwezi tena kuwahi na wewe ni Mbunge wa Dar es Salaam, shahidi wa jambo hili. Njia gani wataalam wetu wa barabara wanaweza kufanya kuhakikisha kuna njia hata ya *underground* ama njia yoyote, kama ya juu ama ya wapi na hiyo *SGR* itaingia baadaye bandarini. Tutoe ma-*container* hata kama ni saa sita usiku, saa

saba usiku, ili tusi-*disturb* watu wa Dar es Salaam kwa sababu, ni uchumi wetu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu kama analalamika anaweza kukaa Dar es Salaam peke yake saa 24 hajatoka bandarini, hajatoka kilomita 50. Hiyo ni changamoto kubwa sana katika uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kama alivyosema Mbunge mwenzangu, ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, suala la malipo kwa wakandarasi. Mheshimiwa Waziri sisi tulitoa maoni na tulishauri, kama kuna uwezekano, wakandarasi wengi wanadai na ninajua wengine watalipwa, wangekuwa wanakaa nao hawa mara kwa mara waweze kujithibitishia kwamba, anasubiri atalipwa mwezi wa ngapi. Hii itatupa picha nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua changamoto niliyonayo pale Kilombero. Kwa mfano, Barabara ya ifakara – Kidatu, mkandarasi yupo pale, ukienda kukutana naye, *Raynods* analalamika. Sisi tuna Barabara hii ya Ifakara kwenda Mlimba, mkandarasi ndiyo jana nimeenda nimemkuta na *Chief of TANROADS,* jana, anamshinikiza aanze angalau kufanya ukarabati wa ile Barabara ya Ifakara – Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaweza wakagawanya wakaanza na wakatuambia, Waheshimiwa Wabunge kwamba, hawa kumi ndiyo watakaolipwa wataanza *site*. Hii itatusaidia sana, huwezi kufanya yote, Mheshimiwa Waziri, utapasuka na sisi tumeshakuelewa kuwa, wewe unasema hili sio shamba la bibi, tumeelewa ile lugha, lakini huwezi kufanya yote. Kwa kweli, kama utatuambia wakandarasi safari hii, miezi sita ama miezi hii mitatu, wanalipwa hawa 10 wa barabara moja, mbili, tatu; wewe Mheshimiwa Asenga subiri, wewe Mbunge fulani subiri, watu watasubiri Mheshimiwa Waziri. Tunaomba sana hii iwekwe wazi kwa sababu, kwenye Kamati imekuwa kila siku ni kero za malipo ya wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninachotaka kuzungumzia ni *TEMESA*. Mheshimiwa Waziri katika Kamati yetu kwa kweli, katika

taasisi ambayo tunaona kidogo nayo inaminywaminywa, basi ni hii ya *TEMESA*. Unakutana na Mkurugenzi Mkuu wa *TEMESA* anakuangalia usoni, hazungumzi, lakini unajua kuwa kuna changamoto za upatikanaji fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda kule kwa Mheshimiwa Waziri Aweso, Jimboni kwake, kuna kivuko pale kimekaa muda mrefu hakuna pesa. Tumeenda Kigamboni pale, tumeona kuna geti la Kigamboni, hakuna pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana. Mbunge wa Mwibara ananiambia hapa, *TEMESA* hawana hela. Sasa *TEMESA* ikikosa pesa hata magari yenu, *V8* hizi, yote yanakuwa kwenye changamoto kubwa sana ya kupata *service* na ni hatari kubwa kwa sababu, hata mimi kule Kilombero nina *TEMESA*. Kwa hiyo, haya nilikuwa ninazungumza kwa ujumla Mheshimiwa Waziri, kutoa maoni yangu, lakini kwenye jimbo langu, *specific,* unajua na kwenye kamati nimesema kuhusu Mangula Kona, Mheshimiwa Waziri, na umetuahidi utaisaidia kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapata mashaka sana ninavyosikia baadhi ya wakandarasi wanahofia kuukata mlima kwamba, utamumunyuka na wakati tuna wakandarasi wasomi wazuri. Katibu Mkuu wa Wizara ni *Engineer* mzuri, *Engineer* Besta yupo pale, *Engineer* wetu Mkumbo ni *Engineer* mzuri kabisa, ambaye anasimamia Mkoa wa Morogoro vizuri sana na ameniambia ameshaandika kitaalam kuhusu hiyo Barabara ya Mangula Kona. Ikikupendeza, wakati unajibu, Mheshimiwa Waziri, ukiizungumzia hiyo Mangula Kona utakuwa umenipa faraja kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ni taa za barabarani. Mheshimiwa Waziri, kwa kumalizia, kuna hoja ya taa za barabarani; tuliahidiwa katika Mji wa Ifakara, Jimbo la Kilombero. Ninaomba sana taa hizo zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silanga, Mheshimiwa Antipas na Mheshimiwa Malima.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu, ambayo imebeba uchumi wa Taifa letu, imefanya kazi kubwa na nzuri. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya, hasa sisi watu wa Kanda ya Ziwa kwa kukamilisha Daraja la Busisi. Ni kiungo kikubwa sana kwa Wananchi wa Kanda ya Ziwa, kwa maana ya kwamba, litawafaidisha sana kiuchumi katika maeneo ya kanda yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake. Niwapongeze watendaji, wakiongozwa na Katibu Mkuu, bila kuwasahau watendaji wangu wa Mkoa wa Simiyu, *Engineer* Mkumbo na timu yake, kwa kupanga mikakati mizuri katika mkoa wetu na kuhakikisha kwamba, mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu Mheshimiwa Waziri na timu yako, yapo maombi na mipango mizuri, ambayo tumeifanya katika Mkoa wetu wa Simiyu kupitia Kamati ya Ushauri ya Kimkoa. Zipo barabara ambazo zinatakiwa kupandishwa hadhi, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, ukifika muda katika mpango huu ambao tumependekeza na kuupeleka kwake, barabara hizi zitaunganisha kiuchumi mikoa tunayokutana nayo. Ninaomba nimwambie Mheshimiwa Waziri Barabara hizo ni Luguru – Lagangabilili – Migato – Ndololezi Bumera – Nyangokolwa – Somanda ni barabara ambayo inaunganisha wilaya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija barabara nyingine ambayo tumeleta maombi katika maeneo yako inapita kwenda Ndololezi – Nkuyu inakwenda mpaka Igegwa, ambapo kuna machimbo, kuna madini na vilevile kuna *airport*, ambayo inajengwa kwenye maeneo hayo. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, basi maombi hayo ayafanyie kazi kwa kupanua mtandao wa barabara. Barabara nyingi anazozijenga katika maeneo yetu, kwa mfano ya

Simiyu, ni barabara moja ambayo inapitika kwa muda wote. Kwa hiyo, kila baada ya muda mfupi wa miezi miwili, barabara lazima iharibike, lakini kwa barabara ambazo tumemtajia hizi, akizifungua, atatengeneza mwanya kwenye maeneo mengine ili iende vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo pia Barabara nyingine ya kutoka Gambasingu – Nkoma kwenda Mwamigagani, ambayo hii ikitengenezwa inakwenda kukutana na Wilaya ya Magu, kwa maana ya unaingia Mkoa wa Mwanza, katika hali ambayo wataalam wako Mheshimiwa Waziri walikuja kutuelekeza jinsi gani ya kufungua barabara. Kwa hiyo, niombe, barabara hizi ni muhimu sana, ukiichukua itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Makao Makuu ya Wilaya yetu ya Itilima. Kwenye utaratibu wa *TANROADS* kuna Barabara ambayo inatoka Bariadi – Kisesa, tunaomba uithibitishe. Ninaamini wataalam wetu walishakuletea taarifa, basi kipatikane kipande cha lami katika maeneo ya Makao Makuu, ili wananchi wa Itilima waweze kupata lami katika maeneo hayo, hasa kwenye upande wako wa *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumetumia fedha nyingi kujenga Daraja la Shibiti ambalo linaunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Manyara. Niombe, mwaka jana hapa kwenye Wizara ya Ujenzi, Wabunge wenzetu waliomba na waliongelea sana suala hili; nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, utaratibu wa fedha nyingi ambao tumewekeza kwenye Daraja la Sibiti, kama hatutatengeneza zile barabara za kutoka Sibiti – Kisesa kwenda Lalagu, ukitoka Lalagu unakuja Bariadi, unaenda Magu, itakuwa haina maana yoyote kwa sababu, tumewekeza fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri na timu yako, hili Daraja la Sibiti na barabara zake zote basi zifunguliwe, ili kusudi muda wote kazi zifanyike. Mheshimiwa Waziri akifungua Barabara ya Shibiti – Itilima – Kisesa mpaka Bariadi atakuwa ametusaidia sana katika kutekeleza majukumu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara hii ninayoizungumzia ya Kisesa, sasa hivi tunaenda kufungua Daraja la Busisi. Maana yake ni malori yanayotoka Dar es Salaam, yanayokwenda Uganda, yatatoka Dar es Salaam yakifika Singida yatapita Shibiti, yatapita Kisesa – Bariadi – Magu – Busagala yananyooka moja kwa moja kwenda Bukoba na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapofungua hizi barabara zina umuhimu mkubwa sana kwenye nchi yetu, lakini vilevile tunapanua miji kwa maana ya kwamba, miji ambayo itakuwa haipitiwi itakuwa imepata uchumi wa kutosha maana tutakuwa na pato kubwa la Taifa. Kwa hiyo niendelee kuishauri Serikali kwamba, upo umuhimu sana wataalam wetu kupitia *TANROADS,* kwenye maeneo ambayo tunayazungumzia kila tukija katika Bunge lako Tukufu hili, basi uyafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni, barabara zetu hizi tunazozitengeneza. Barabara ya kutoka Shinyanga – Migumbi – Musoma, barabara hii katika ujenzi wake imekuwa na viraka vingi sana, ni hatari kubwa sana kwa Taifa. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na wataalam wake, hasa Barabara ya kutoka Mwigumbi – Maswa – Bariadi, barabara hiyo kwa muda mchache haitamaniki, imekuwa na mabonde mengi sana kwa muda mchache. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, wapite tena kuangalia jinsi gani ya kumaliza tatizo hilo katika maeneo hayo; yapo mabonde makubwa sana utadhani lami imejengwa zaidi ya miaka saba, wakati ni lami ya miaka miwili, mitatu. Jambo hili tunapolizungumza basi wataalam walifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi kwa Mkoa wetu wa Simiyu, tuna Barabara moja tu ya *TANROADS* ndiyo maana tunaizungumzia sana, Barabara ya Kisesa – Bariadi – Itilima – Magu. Ikimpendeza Mheshimiwa Waziri nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, aweze kutembelea maeneo hayo ajifunze mwenyewe haya maneno tunayoyazungumza, ili kusudi akifika, basi akikaa na timu yako atakuwa anajua tunakushauri nini na kwa wakati gani. Tunayo barabara moja tu, ambayo ni inaungana na mikoa mingine nje kwa nje. Kwa hiyo, nimwombe

sana Mheshimiwa Waziri, achukuwe hili wazo ili alifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, zaidi niwapongeze sana Watumishi wa *TANROADS* kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa sisi Waheshimiwa Wabunge, lakini ni maana ya kwamba, nidhamu hii imejengwa kutoka Wizarani, wanateremka mpaka chini. Basi tuwapongeze, lakini tunachohitaji sisi ni kupata utendaji ulio bora, ili wananchi wetu waweze kupata huduma safi katika maeneo ambayo tunayazungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, ninaunga hoja mkono na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Antipas, Mheshimiwa Malima, Mheshimiwa Manyanya na Mheshimiwa Ulenge.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitajitahidi mchango wangu uwe mfupi kwa sababu, kuna mambo ninayotaka kuyasema kuhusu Malinyi. Mheshimiwa Waziri tulikuwa naye kule siku chache zilizopita, alitua na helkopta Malinyi, alijionea hali yetu. Kimsingi nina mawili; jambo la kwanza ni hali ya Barabara yote kutokea Ifakara mpaka Malinyi, lakini la pili, ni kuunganisha Wilaya ya Malinyi na Mlimba kupitia pantoni kwenye Kivuko cha Kikove.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuendelea niishukuru Serikali, Mheshimiwa Rais na timu yake yote. Kwanza mwaka huu tumetengewa, kwenye bajeti hii ya leo, kilometa 112 kutoka Ifakara mpaka Mtimbila, Malinyi. Kwa hiyo, ninaomba kwa niaba ya Wanamalinyi wenzangu basi, hilo jambo lianze mapema zaidi hata kama ni kidogokidogo, tunasubiria kwa hamu tuweze kupona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru pia, watendaji wote wa Wizara; Katibu Mkuu wa Wizara, Mkurugenzi wa *TANROADS* na wengine wote. Wamekuwa wakinipa ushirikiano mkubwa sana katika kipindi hiki cha mafuriko na masika, kukatika kwa barabara na hata katika hali ya kawaida tumekuwa

tukifanya nao kazi kwa ushirikiano mkubwa sana kwa hiyo, ninawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yangu makubwa ni mawili. Jambo la kwanza ni, Malinyi mpaka hivi ninavyozungumza hapaingiliki; hakuna gari linaingia wala kutoka kwa maana pamekatika sehemu mbili, barabara yetu kutoka Ifakari. Barabara ya kwanza imekatika jana, kwa maana na leo mawasiliano hakuna. Ukitoka Ifakara huwezi kusogea sehemu ya Namhanga, kipande cha Ulanga kimekatika, maana yake ni magari hayaingii wala kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ambayo Mheshimiwa Waziri amefika wiki iliyopita, pamekatika pale Malinyi Mjini, kilomita chache tu kufika kwenye mji hapaingiliki, barabara imefumuliwa na maji ambayo yametokana na Mto Furua. Kwa hiyo, sasa ni adha kubwa sana, maana yake ni wananchi kwenye baadhi ya vijiji, nyumba zimeingiliwa na maji, nyumba nyingine zimeanguka na changamoto zinazofanana namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika haya nina ushauri wa machache tu. La kwanza, ninajua *TANROADS* wanaendelea na tunashukuru tena, tumepata fedha bilioni 18 za Benki ya Dunia kwa ajili ya kujenga daraja hapa ambapo ninasema pamefumuka wiki iliyopita na hata hapa ambapo pamefumuka jana palishapangiwa tayari kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba tu, ninafikiri kuna haja ya kufanya *design* mpya kwa uharaka kulingana na hali maana kama pamefumuka, maana yake pameongezeka urefu tofauti na vile vipimo vya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa pale Madumba kwa maana ya Fuluwa, kuna ule mto ambao unatusumbua Malinyi siku zote na huwa ninauelezea hapa. Mto Fuluwa hauna kina, hauna kingo na ndiyo unaofurumusha maji kuweza kuharibu barabara za *TANROADS* na *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kila mwaka tumekuwa tukipata fedha kwa ajili ya marekebisho hayo ili kutibu barabara

kutokana na adha ya Maji ya Mto Fuluwa, lakini mwisho wa siku pamoja na daraja ambalo tutakwenda kujenga, tunashukuru lakini maana yake daraja litapitisha maji mengi zaidi. Pia, vijiji vya mbele navyo kule kwenye barabara za *TARURA* kuna uhitaji wa kutoa karavati. Pengine wenzangu wa TAMISEMI kama wapo hapa waweze kusikiliza na kuona kuna haja nao ya kufanya kama wanavyofanya ujenzi, kuyapokea maji yanayotoka Fuluwa kwa maana kujenga daraja ili tutoe zile karavati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Kiwale pia kuna haja ya kufumua zile *box* karavati, kuweka daraja kwa maana maji yatapita mengi sana kwenye daraja jipya ambalo *TANROADS* wanatarajia kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhiso kubwa la kudumu ni ku-*deal* na Mto Fuluwa wenyewe. Watu wa Ofisi ya Rais, Mazingira, wenzangu wa TAMISEMI wenye *TARURA* na *TANROADS* wenyewe, watu wa bonde na watu wa *TANESCO*, wamefanya Ifakara pale Mto Lumeno kwa ndugu yangu Asenga wametusaidia; wamechimba tuta kubwa na wametengeneza kina, sasa hivi angalau kuna unafuu. Kwa hiyo, ninaomba jambo la namna hii lifanyeke na Mto Fuluwa, itakuwa tumesaidia kwa kudumu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni jambo la kuunganisha Mlimba na Malinyi. Kwa mara ya kwanza tangu dunia imeumbwa tunatarajia kwa mwaka huu hilo jambo likatokee. Ni ahadi ya muda mrefu. Wakandarasi wamekuwa *site* na tumehangaika nao kwa muda mrefu na wengine tumewafukuza, tuna mkandarasi mpya sasa. Sijajua changamoto ni nini lakini kazi inakwenda taratibu sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ahangaike na watu wake pia; kwa maana ya *TEMESA*, ndiyo wana-*deal* na kile kivuko cha kutuvusha pale pakipona. *TANROADS* ndio wanaojenga lile *gutter* pale Kikoyo ili kutuunganisha na Ngalimila kule Mlimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kufikia kwenye maji kuna *section* ya *TARURA,* kuna sehemu kuna tobo linahitaji *box* karavati, kama milioni 315. Ninafikiri Serikali yote iko hapa, basi watu wa TAMISEMI na *TARURA* waone hili jambo. Nimeahidiwa na

Mkurugenzi kwa maana ya *Chief* wa *TARURA*. Tunaomba msaada zaidi, tunakumbushia, tuhakikishe kwamba kwenye ile sehemu panajengwa *box* karavati kwa wakati na *TANROADS* wanamaliza ile *gutter* kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kivuko kile cha TEMESA kidogo kuna changamoto. Kiko Mwanza, Songoro *Marine* anatengeneza, lakini nimeambiwa bado kidogo sana asilimia kama saba kumaliza ila ninadhani yule bwana anadai dai kidogo fedha. Hebu Serikali muangalie namna ya kufanya ili tusaidike kwa uharaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, matamanio yangu ni kuona pengine tukichelewa sana *by Christmas* mwaka huu, Malinyi tuweze kwenda kule Mlimba kupitia *shortcut* ya *pantone*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru; ni hayo tu kwa leo. Hata hivyo, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alifika basi ninaomba mambo haya yatekelezeke kwa uharaka sana. *Manager* wangu wa *TANROADS* wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya wananipa ushirikiano mkubwa sana na wananchi wote wa Malinyi tunawapa pole sana. Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Maafa, tunaomba tusaidike maana kuna nyumba kadhaa zimeanguka na kuna nyumba zimeingiliwa na maji, tunahitaji msaada kidogo wa madororo, wengine vyakula na vitu vya namna hiyo. Kwa hiyo, ninaomba sana tusaidike. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malima; wajiandae Mheshimiwa Manyanya na Mheshimiwa Ulenge.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi. Ninaomba nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa afya na tumeweza kuhudhuria katika Bunge lako Tukufu. Pia, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya katika nchi yetu. Tumeshuhudia kiwango kibwa sana cha miradi mikubwa ya maendeleo ikiendelea kutekelezwa na mingine ikikamilika. Mfano ni Daraja la Busisi. Binafsi nimefika, nimeona ni daraja la kisasa

kabisa ambalo wengi wamesema; ni daraja refu kuliko madaraja yote katika Ukanda wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa viwanja vya ndege pia unaendelea takriban nchi nzima. Nimepata nafasi ya kuona baadhi ya viwanja; Kiwanja cha Msalato, Nduli kule Iringa, Shinyanga na maeneo mengine. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii anayoendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega, Naibu wake na timu nzima kwa jinsi ambavyo wanaendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuchangia kuhusu Bodi ya Mfuko wa Barabara *(Road Fund)*. Kuna shida kwenye mtiririko wa fedha kutoka kwenye makusanyo. Mwaka wa fedha 2024/2025 Mfuko wa Barabara ulikuwa umepanga kukusanya shilingi bilioni 856.78, lakini inapofika mwisho wa kutoa hii taarifa walikuwa wamefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 819.66. Kiasi ambacho makusanyo siyo mabaya, ni mazuri, lakini kilichotokea ni kwamba fedha zilizokuwa zimehamishiwa kwenye Mfuko wa Barabara mpaka kipindi hicho wakati taarifa inatoka ilikuwa ni shilingi bilioni 289 tu, ambayo ni sawa na 35.37%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utaona fedha nyingi hazipelekwi. Shilingi bilioni 529.72 hazikuhamishwa kwenda kwenye Mfuko wa Barabara, ambayo ni sawa na 64.63%. Hii imeathiri sana ujenzi wa barabara na ukarabati wa barabara na madaraja. Kwa sababu fedha nyingi zinakusanywa kweli lakini hazipelekwi kwenye Bodi ya Barabara kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya miradi ambayo imeathirika sana na utaratibu huu ambao ninaona haufai ni pamoja na Barabara yetu ya kule Mpwapwa yenye urefu wa kilometa 98 inayoanzia *Kongwa Junction* – Mpwapwa – Kibakwe. Mkataba wa barabara hii ulisainiwa mwaka jana mwezi Februari, lakini baadaye mwaka jana karibu na mwezi Agosti mwishoni mkandarasi alihamia *site*. Mpaka leo tunavyozungumza hapa ujenzi haujaanza; ni kwa sababu ya uhaba wa fedha; lakini fedha

zimekusanywa kwenye Mfuko huu ambazo zilitakiwa ziende kule ili hawa wakandarasi walipwe na ujenzi ungeendelea. Wananchi wa Mpwapwa wanatamani kuona ujenzi umeanza na baadaye waone barabara yao inapitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri, fedha zikikusanywa kwa ajili ya Mfuko huu wa Barabara basi ziende kwa wakati na pia ziende ku-*support* miradi yote inayosubiri fedha hizi. Kwa hiyo, sisi wa Mpwapwa katika Mkoa wa Dodoma ndiyo wilaya pekee ambayo haijaunganishwa na barabara ya lami. Sasa tuna kiu ya kupata barabara. Kila siku tunamwona mkandarasi site lakini kazi haijaanza; na ujenzi huu umesemwa utajengwa kwa awamu. Kutoka Kongwa *Junction* mpaka Mpwapwa Mjini ni kilometa 32 tu, awamu ya kwanza itakuwa ni hiyo, lakini awamu ya pili itaanza Mpwapwa kuelekea Kibakwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa, majimbo yote mawili, tunatamani na sisi tuunganishwe na mkoa kwa kutumia barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia, linahusu madeni ya wakandarasi. Haya pia yanatuletea shida kwenye Wizara hii. Kwenye taarifa tumeambiwa kwamba Februari, 2025 Serikali ilikuwa inadaiwa shilingi trilioni 1.29 na shilingi bilioni 136.98 ilikuwa ni madeni kwa ajili ya riba inayotokana na kuchelewesha kulipa wakandarasi. Fedha hii ingeweza kutosha kujenga ile Barabara ya kutoka Kongwa mpaka Kibakwe, lakini tunawalipa wakandarasi kama riba kwa sababu ya kuchelewa kuwalipa. Kwa hiyo, wakati mwingine maendeleo yetu tunayachelewesha sisi wenyewe. Kwa nini hatuwalipi kwa wakati ili fedha hizi za riba zitumike kufanya kazi nyingine? Zitumike kujenga miradi mingine ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri sana mtiririko au madeni haya yalipwe kwa wakati ili tuepuke riba kwa sababu riba inaleta hasara kwa Serikali. Shilingi bilioni 136 si fedha ndogo, inalipwa na bado itaendelea kulipwa kama hatuwezi kubadilika tukawalipa wakandarasi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni ushirikishwaji wa wakandarasi wadogo. Nimeona kwenye…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia Mheshimiwa.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** ... ripoti tumeelezwa kwamba Serikali inajitahidi kuwashirikisha wakandarasi wadogo, lakini ninaona bado haitoshi. Wakandarasi hawa ndio hawa hawa ambao hawalipwi na ni hawa hawa ambao wanashirikishwa kwa kiwango kidogo. Kwa hiyo, wale walioshirikishwa wamefirisika...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** ... ninaomba sana wakandarasi walipwe kwa wakati...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, unga mkono hoja.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** ... washirikishwe kwenye miradi hii mikubwa ya maendeleo ili waweze kukua na wakikua baadaye miradi hiyo mikubwa mikubwa wanaweza kufanya wakandarasi wadogo ambao ni wazawa wa nchi yetu ya Tanzania. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Manyanya hayupo. Mheshimiwa Ulenge, Mheshimiwa Pallangyo, Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwenye enzi na utukufu kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge hili kwa muda na wakati kama huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii pia kuipongeza Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa inayofanya ya kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuunganika kwa kupitia mtandao wa barabara na nchi za Jirani; pia, mikoa yetu na wilaya zetu zinaweza kuunganika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa inayofanya licha ya changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi. Tumeona jitihada kubwa za Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha anakwenda sambamba na changamoto hiyo. Hivi juzi tumesikia ameongeza shilingi bilioni 30 ili kuweza kutatua changamoto zinazotokea kutokana na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii pia kuwapongeza watendaji wa Wizara wakiongozwa na Mheshimiwa Ulega, mtu bingwa kabisa. Nimeiona *speed* yake namna ambavyo aliwatia *pin* wale jamaa ambao walifungua kila sehemu ya Barabara ya Dar es Salaam halafu wakawa hawaeleweki. Nimependa ile *initiative;* anatenda kwa haraka na matokeo yanatokea kwa haraka. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake pale, mtu bingwa kabisa, Mzee wa busara *Engineer* Kasekenya mwenyewe, watendaji wa Wizara pamoja na taasisi zake. Ninachukua fursa hii kuwapongeza kwa kazi kubwa wanayofanya. Hakika tukiiangalia *TANROADS* iliyoanzishwa mwaka 2000 na kazi kubwa ambayo imefanya sasa hivi kwa Taifa letu licha ya changamoto ndogondogo zilizopo, ninasema *TANROADS* wanaupiga mwingi sana. Taifa letu linapata *connectivity* na watu wanaweza ku-*access* kutoka sehemu moja na sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa ninampongeza Mheshimiwa *Engineer* Mohamed Besta kwa kazi nzuri anazofanya. Mimi ninasema, wakati nikiwa *junior engineer* pale Wizara ya Ujenzi, ninakumbuka kabisa nilikuwa ninasoma *pavement material design manual* nikiona jina la Mhandisi Besta pale. Kwa hiyo, ni mtu mwenye *profession* yake anayoimudu. Tuendelee kumpa maua yake ili atusaidie kuiongoza *TANROADS* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kusema kwamba Mheshimiwa Waziri ametaja vipaumbele vya bajeti yake na moja wapo ya kipaumbele amesema kwamba bajeti hii itakwenda kutekeleza miradi ya mkakati na miradi ambayo inakwenda kufungua fursa za kiuchumi pamoja na kuondoa msongamano nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mkoa wa Tanga tuna barabara ambayo *economic potential* yake ni kubwa mno kwa Taifa hili. Barabara inayounganisha Makutano ya Kiomoni mpaka Makutano ya Mlingano, kilometa 39.5, *economic potential* ya barabara hii kwa Mkoa wa Tanga ni kubwa sana. Ninashangaa kuendelea kuona kwamba barabara hii kila siku inapigwa danadana. Kulikoni? Wanautakia mema kweli Mkoa wetu wa Tanga? Kwa sababu viwanda vyote vya saruji wanavyoviona Tanga vinategemea barabara hii. *The best limestone in Sub-Saharan African Countries* inatoka katika barabara hii na ni kilometa fupi sana, 39.5. Kulikoni isijengwe kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii licha ya kwamba ina *economic potential* kubwa katika Mkoa wetu wa Tanga lakini bado inaweza kuondosha msongamano wa Barabara ya Tanga – Segera ambayo sasa imeshazidiwa, kwa sababu hii inaweza ikawa ni *bypass* nzuri inayounganisha barabara kuu mbili; inaunganisha Tanga – Hororo kutoka Makutano ya Kiomoni na inaunganisha Tanga – Segera katika Makutano ya Mlingano. Barabara hii ni *potential*, ni *Tanga bypass* ambapo mtu anayetaka kwenda Mkinga akiwa anatokea Segera hana sababu ya kuingia Tanga Jiji, anaweza akapiga *border* akatokea zake Mkinga. Hali kadhalika anayetokea Mkinga kwenda Segera, hana sababu ya kuingia Tanga Jiji, anapiga kona anatokea zake Muheza mbele kwa mbele. Barabara hii ina umuhimu wa aina yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyote hivi vya saruji, viwanda wa liemba ambavyo viko pale, kwa nini hatuwatendei haki hata wafanyabiashara wakubwa ambao wapo ukanda huu? Fedha yote ya Mkoa wa Tanga, tunapoizungumzia Tanga Jiji inatoka kwenye ukanda huu kwa sababu ya saruji iliyopo pale na viwanda vile. Maana yake ni kwamba tunachelewesha hata wadau wengine wanaotamani kuja kufanya shughuli za kiuchumi kwenye Mkoa wa Tanga kwa sababu barabara ambayo ndiyo ina *best limestone* ipo nyuma na haiko katika kiwango cha lami mpaka leo. Hivi hatuutendei haki Mkoa wa Tanga na hatuwatendei haki Tanga Jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali, ninajua wameiweka kwenye kuifanyia upembuzi yakinifu na upembuzi wa kina; lakini *this story is of very long time*. Imechukua muda sana, inachosha kuisikia na tumechoka kusikia. *We real need this road for sure* kwa ajili ya maendeleo ya Tanga yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya upanuzi wa Bandari ya Tanga na barabara hii na yenyewe *connectivity* yake inaweza ikatumika moja kwa moja mpaka Bandari ya Mkoa wa Tanga bila hata kuingia kule mbele. *I am very sick and tired of this* kwa kweli. Nimechoka kuisemea na ninaisemea kwa uchungu na ninaumia. Kulikoni mna *hinder development* ya Mkoa wa Tanga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia alipozungumza kwamba anataka kuiona Tanga ambayo imeunganika kimiundombinu ni pamoja na barabara. Jamani ninaomba mtusaidie. Ninaona uchungu kusema kwamba ninaweza kushika shilingi ya shemeji yangu mpendwa, yaani kwa kweli ninaona shida, lakini kiukweli ninaumia, ninaumia, ninaumia *and I am sick and tire of this road*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Haya Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mbunge anaumia.

Mheshimiwa Pallangyo, Mheshimiwa Issaay na Mheshimiwa Msongozi wajiandae. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii ili nichangie kwenye hoja iliyoko mezani kuhusu bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Wizara ambayo ni muhimu sana na ambayo inasimamia wahandisi ambao kimsingi ndiyo ambao wanabadilisha dunia yetu tuweze kukaa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndani ya miaka minne akiwa ofisini ameandika historia. Ametufanyia kazi kubwa ambazo zote zimelenga kuboresha maisha ya

Watanzania. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Abdallah Ulega na Naibu wake, kwanza kwa hotuba nzuri lakini pamoja nao, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana ambayo wanaifanya pale Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninahudumu katika Kamati inayosimamia uwekezaji wa mitaji ya umma, kwa hiyo nimepata neema ya kutembea na kukagua miradi ambayo Serikali imewekeza. Nimeona miradi mikubwa kama vile Daraja la Kigongo – Busisi, ni mradi mkubwa wa kielelezo. Sasa hivi umemalizika na kazi hiyo imefanywa na Wizara hii ikisimamiwa na *TANROADS*. Vilevile Daraja la Tanzanite pia limemalizika, nalo limesimamiwa na *TANROADS;* nalo ni daraja kubwa; pamoja na barabara za lami nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma sasa hivi ni mkoa wa kimkakati. Mara ya mwisho tumekwenda kutembelea kule, kuna Barabara ya kutoka Kasulu kwenda Nyakanazi, ni mkeka. Kuna barabara inajengwa kutoka Kasulu kwenda Manyovu, nayo kazi inaendelea vizuri. Kwa kifupi sasa hivi Mkoa wa Kigoma ni *accessible by air*, kwa barabara na kwa treni pia. Nimpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo mazuri ambayo wanayafanya nchini nina machache ya kusema kuhusu hali ya barabara jimboni kwangu. Ninaomba niseme moja baada ya nyingine. Barabara ya Mbuguni, barabara hii inaunganisha mikoa miwili ya Arusha na Manyara; ni barabara ya siku nyingi sana. Ninashukuru Serikali imekwishafanya usanifu japo kwenye taarifa yake inasemekana kwamba usanifu umekwishamalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa ninategemea utoe mafungu mwaka huu huu ili ianze kujengwa. Hata Mbunge wa Kiteto hapa jirani, amesema anaiomba hiyo barabara ijengwe ili Manyara na Arusha ziweze kuwasiliana kiurahisi. Siyo hivyo tu, ni kiungo muhimu sana kwa biashara ya *Tanzanite* ambayo inachimbwa pale Mererani kwa ajili ya kupelekwa kwenye masoko Jijini Arusha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nilikuja kwenye *desk* lako mwaka huu usiiache, ianze hata angalau kidogo kidogo hii itatujengea heshima sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Barabara ya King'ori kuanzia Malula – Kibaoni – Ngarenanyuki, barabara hii inahudumiwa na *TARURA,* lakini tuliomba ipandishwe hadhi iweze kuhudumiwa na *TANROADS*. Barabara hii ni ya kimkakati kwa sababu inaunganisha barabara mbili kuu, barabara inayotoka Nairobi - Namanga – Arusha na Arusha – Moshi – Dar es Salaam, inazunguka Mlima Meru ikaifungia *Arusha National Park* katikati pale. Kwa hiyo, ikitengenezwa na kujengwa kwa kiwango cha lami itakuja kuungana na barabara inayohudumiwa na *TANROADS* kutoka pale Usa River – Oldonyosambu na kuhakikisha kwamba wananchi hawa ambao wanaishi upande ule maisha yao yatakuwa bora. Barabara hii inahudumia wananchi wa kata nane. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, sasa achukue *initiative,* hiyo barabara ipandishwe hadhi, kwa sababu *TANROADS* wana *access* na fedha kuliko *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuomba hapa kwamba sasa hivi Barabara ya kutoka Tengeru pale Sangisi kuelekea Holili, ambayo inajengwa ni njia nne, sasa hivi itajengwa mpaka Usa River kilometa tisa. Niliomba kwamba usanifu utakapokuwa unafanyika itengenezwe *route* barabara ya kuingia Tengeru Sokoni kwa ajili ya kuliboresha lile soko. Hii inawezekana, kwa sababu tunajua hii miradi mikubwa inakuwaga na *CSR*. Sasa ile *CSR* ambayo itakwenda halmashauri, badala ya kwenda halmashauri moja kwa moja wajenge ile barabara ya kuingia sokoni, lakini pia na kuboresha miundombinu fulani pale sokoni kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nyingine tena inakwenda Tengeru pale Chuoni. Hii barabara zamani ilikuwa ni ya lami, barabara nzuri sana, lakini iliachwa ikaharibika kabisa, kabisa. Mheshimiwa Waziri atakumbuka mwaka juzi tulikwenda kule chuoni, aliona Barabara hiyo ilivyokuwa imeharibika, lakini ile barabara ilikuwa ni ya lami, nzuri na imepandwa miti pembeni na ile barabara ni ya *TANROADS,* maana yake ndiyo inakwenda kuungana na barabara ya kwenda Mbuguni. Ninaomba iingizwe kwenye mpango ili iwekwe lami ili wanafunzi na watu wengine wanufaike. Kuna vyuo vingi sana pale eneo lile kuna Chuo cha Kilimo; kuna Chuo cha Mifugo; lakini kuna Nelson Mandela, ni taasisi ambazo ni muhimu zinahitaji kuwa *accessed* kiurahisi. Kwa

hiyo, tunaomba sana barabara hii nayo ijengwe kwa kiwango cha lami ili iunganike na Barabara ya Mbuguni ambayo imeshafanyiwa usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na kusema kwamba nilikwenda *Arusha National Park* wanalalamika kwamba, sasa hivi wana shida kubwa, magari ni mengi yanaingia hifadhini, kwa hiyo wanashindwa ku-*maintain* zile barabara. Ndiyo maana nimesema Barabara ya King'ori ni ya kimkakati, kwa hiyo niombe, ninarudia tena Mheshimiwa Waziri, Barabara ya King'ori iondoe *TARURA* ili ipande hadhi kama tulivyoomba, japo walisema kwamba haikidhi vigezo, lakini inakidhi vigezo kwa sabbau inahudumia na inapita kwa wananchi wengi sana kata nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache, niseme ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana kwa muda. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kabla hatujaendelea kuna wageni walioingia Bungeni jioni hii:-

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: Wageni 42, Mabalozi wa Mashina wa CCM kutoka Kata ya Nzuguni ya Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 30 wa Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE)* kutoka Jijini Dodoma wanaosomea Shahada ya Utawala na Rasilimali Watu. Karibuni. *(Makofi)*

Tunaendelea, Mheshimiwa Issaay, wajiandae Mheshimiwa Msongozi na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa baraka zake kwetu sote wakati huu na nyakati zote. Pia, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ya pekee katika utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa miaka yake minne katika kuingoza Serikali yetu. Kazi kubwa sana imefanyika

katika Jimbo la Mbulu Mjini na maeneo mengine kwa kadiri tulivyofanya ziara na kwa kweli tunamwombea tutamlipa kwa fadhila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii na Naibu Waziri kwa kadri ambavyo wanaiongoza Wizara hii;na wale wote waliotangulia wakati ule wakiongoza Wizara hii, lakini kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa letu walipata kubadilishiwa majukumu yao. Nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza Katibu Mkuu Balozi Aisha, na Dkt. Charles, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa ajili ya Wizara yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini pia, nichukue nafasi hii kwa namna ya pekee, leo nina mchango mdogo sana. Mchango wangu kwanza utajikita sana kwenye utekelezaji wa hii miradi ya barabara. Barabara inayoitwa Karatu – Mbulu- Haydom – Sibiti ni barabara inayounganisha mikoa mitano nchini. Tulifurahi sana tulipopata ule mpango wa awali wa kujengwa kwa *EPC+F,* lakini hadi sasa barabara hii kwa miaka mitatu hatujafanikiwa kupata hata kipande cha lami, baada ya kusaini mkataba mwaka 2022. Eneo hili la Mbulu – Garbabi limekuwa kero kubwa sana na kwamba hii kazi Mkandarasi ameitelekeza, ameshaondoka lakini pia hayuko *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande hicho kimekuwa kero kwa sababu mvua ikinyesha barabara zingine zote ni nzuri hata kutoka Karatu – Mbulu na kuendelea, lakini hicho kipande cha kilometa 25 hali ni mbaya sana. Kwa kuwa Mkandarasi hayuko *site,* wananchi wanapata shida kwa ajili ya kutengenezewa ile sehemu ya kilometa 25 kwa maana ya barabara ya mchepuo ama barabara ya kupita pembeni kwa ajili ya huduma. Jambo la kushangaza ni kwamba, kama upande wa lami umekwama sana tumepiga kelele muda mrefu kwa kutaka walau hata hiyo sehemu ya wananchi kupita kwa maana ya barabara ya kawaida, njia ya mchepuo haipo, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninategemea Waziri kwa namna anavyoona nimezungumza, nimeuliza maswali kadhaa hapa Bungeni, nimemsihi mara nyingi, lakini aache hiyo ya lami ambayo kwa sasa inasubiri malipo, atakapokwenda pale atuambie huyu Mkandarasi analipwa lini na atatengeneza hii barabara ya udongo kwa muda gani? Kwa sababu miaka mitatu hatuna kipande cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi tunasaini mikataba ambayo mbele ya safari au huko tuendako ni athari kwa Taifa na hata kwa huduma ya wananchi. Mkandarasi huyo amepewa kazi kule Dareda kwa Mheshimiwa Sillo, Jimbo la Babati Vijijini kilometa 25 bado hajaanza na Labay - Haydom kilometa 25 hajaanza na hii ya miaka mitatu aliyoisaini ameitelekeza hayuko *site* na wala vifaa haviko. Sasa wananchi wa Mbulu Mjini na maeneo mengine wangependa kufahamu, kwa sababu kadri ambavyo kazi imesimama athari ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemtumia Mheshimiwa Waziri picha nyingi za magari yanavyokwama kwenye hicho kipande na jinsi ambavyo athari ni kubwa. Pia kama itawezekana ni nafuu akatengeneza barabara ya kawaida halafu hiyo ya lami akasubiri hayo malipo yake ya lami, kwa sababu kila mwaka tunapitisha bajeti hapa ni kwa ajili ya huduma na kwa ajili ya hiyo huduma hicho kipande angeendelea kuhudumia huduma za kawaida za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikuwa nimefurahi sana kushika shilingi ya Waziri, lakini nitampelekea ki-*memo,* majibu yake yasiponiridhisha, ni nafuu kwa niaba ya wananchi nichukue hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kule Mlima Magara. Tunashukuru kazi kubwa imefanyika kwenye ile Barabara ya Magara, lakini daraja limejengwa. Pia, kwa namna ya pekee, Mlima Magara umepata zege kwa kilometa sita kati ya 15, lakini eneo hilo ni tete, mvua moja tu ikinyesha Mlima Magara magari hayapiti, barabara inakatikakatika. Sina chuki sana na hii Wizara lakini wao wanavyosaini mkataba wana matumaini, lakini Wizara ya Fedha haiwawezeshi hawa na wanakwama sana kwa sababu

wao kama hawawezi kumlipa Mkandarasi, Mkandarasi ni lazima aondoke *site* na hili tutalizungumza kwenye bajeti kubwa ya Serikali. Pia, eneo zima na barabara nzima ya Magara tayari usanifu ulishafanyika na kwa mujibu wa Serikali, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kujenga lami Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani - Magara - Mbulu. Eneo hilo ni muhimu linatuunganisha sisi na Mbuga za Wanyama, lakini pia na Mkoa wetu wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda nichukue tena nafasi hii kwa namna ya pekee kuona kwamba pengine hata katika ile hali ya utiaji saini wa hii mikataba au tunavyosaini, gharama ni kubwa sana ya ucheleweshaji baadaye tutadaiwa kama Serikali na kama nchi. Ili tusidaiwe tuangalie bajeti tunayopitisha kama inakidhi haja kwa ajili ya kulipa yale madeni, kwa sababu tumeambiwa 45% ya fedha za *TANROADS* ama za Wizara hii zimetolewa kwa maana ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Hata hivyo, nina hofu pengine katika hizo 45% nusu yake ni kulipa madeni ya miaka iliyopita ambayo inakuja kuvuruga bajeti ya mwaka huu ambayo tupo nao. Hili ninalizungumza kwa sababu, kama miaka mitatu iliyopita katika kilometa 25 za Mbulu – Garbabi hakuna hata kipande kimoja cha lami. Hatuoni kuwa madeni haya baadaye na bajeti tunazopitisha zinakosa tija kwa wananchi na kwa namna ambavyo wananchi walitarajia huduma hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninamwomba Waziri atakapoenda hapo pamoja na kwamba atamlipa lini na huduma hiyo ya barabara ya udongo itajengwa lini na yeye anatarajia kwenda Mbulu lini, mimi nitatangulia atanikuta kule Mbulu. Kwa sababu ninatarajia hata kuita Vyombo vya Habari vizungumzie hali halisi ya barabara hiyo kwa jinsi ambavyo hali ni tete. Mheshimiwa Waziri tunampenda, hana muda mrefu kwenye hii Wizara, lakini ameyakuta ayafanyie kazi ili walau Watanzania wapate amani, kwa sababu barabara ni kiungo muhimu sana kwa kadri ambavyo tunapata athari, hasa pale ambapo inajifunga na pale ambapo wananchi walitegemea lami, sasa ya udongo imekuwa kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi wa *EPC+F*. Je, hizo barabara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Issaay, ya pili hiyo, malizia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia sekunde mbili, tatu.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ya *EPC plus Finance* Waziri akija hapa atuambie zile barabara saba ikiwemo: Mbulu – Karatu – Haydom – Sibiti. Zile barabara nyingine kwa ujumla ziko saba, zina kilometa 2,035, tunazijenga vipi ili Watanzania wasikie hali hii kwamba walau mpango wa sasa wa Serikali baada ya ule wa awali kukwama sasa tutakwendaje hata basi kwa namna ambavyo wananchi wawe na taarifa kwa ujumla kupitia Bunge hili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waziri amekusikia, hongera.

Mheshimiwa Msongozi atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby na Mheshimiwa Mkenge.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niwe miongoni mwa wachangiaji katika bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka wa fedha 2025/2026 leo hii tarehe 5 Mei, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada ya *system* ya uchangiaji wangu lazima nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba miundombinu ya nchi hii inakaa sawasawa. Pia, nimpongeze sana Waziri mwenye dhamana kaka yangu Mheshimiwa Ulega, baba Tulia pamoja na Naibu Waziri wake pamoja na *delegation* yake kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Ni Waziri bingwa ambaye yuko makini na

ameonesha wazi kwamba ana uwezo mkubwa wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza sana Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Ruvuma, ama kwa hakika wametupatia chombo na chombo hiki kwa kweli kinaenda vizuri sana. Anafanya kazi nzuri sana, sana, sana, ni msikivu, mwenye uelewa mkubwa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua huyu bwana ili aweze kuisimamia miundombinu yetu ya Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa niende Songea Mjini nitachangia kiwilaya wilaya. Ninaomba nizungumzie Barabara ya *Bypass* ya Songea Mjini yenye urefu wa kilometa 16 ambayo kimsingi nimekuwa nikisema hapa Bungeni na hata mwezi Februari niliuliza swali ndani ya Bunge lako hili Tukufu kuhusiana na hii barabara. Majibu ya Naibu Waziri alisema kwamba Mkandarasi yuko kazini. Sasa nikajipanga na wanawake wenzangu ambao wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali katika Manispaa ya Songea, twende tukaone vifaa vilivyoko *site,* lakini hatujaona hivyo vifaa. Ninaomba leo Waziri atakapokuwa ana *windup* anieleze ni lini barabara hii ya *bypass* itaanza kujengwa katika Manispaa ya Songea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni barabara ya kutoka Songea kwenda Makambako yenye urefu wa kilometa 395 ambayo kimsingi inahitaji ukarabati. Barabara ile ina *vingundura*, yaani ina viraka; mabonde yanafika mpaka kwenye viuno kwa kweli inaleta shida. Kimsingi kutoka Songea mpaka kufika Makambako kwa kawaida unatakiwa utumie masaa manne, lakini tunatumia mpaka masaa sita mpaka saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana hii barabara ianze kujengwa, tumeambiwa kwamba wanalipa fidia, lakini wananchi wamesubiri kwa muda mrefu mno, maswali yamekuwa ni mengi kila tunavyorudi tunatoa mrejesho wa Vikao vyetu vya Bunge, tumekuwa tukiulizwa maswali mengi sana hii barabara ni kero ina malori mengi sana yanayobeba makaa ya mawe. Kwa hiyo, ninaomba sana hii barabara ni muhimu, kwa hiyo ikiweza

kurekebishwa, aidha kuongezwa kama ambavyo inasemekana basi tutashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Songea Vijijini nizungumzie Barabara ya Likuyufusi – Mkenda yenye urefu wa kilometa 124 inayounganisha Nchi ya *Mozambique* na Tanzania, ni barabara muhimu sana ya kimkakati. Barabara hii tuliambiwa mwaka jana hapa imetengewa fedha ya kujenga kilometa 60, barabara hii haijaanza kujengwa hata kilometa moja. Sasa ninaomba, kwa kuwa Mheshimiwa Ulega ni Waziri kijana ambaye tunamwamini na tunajua kabisa yaani angepewa pesa yote rangi zake zote tungeziona; lakini pamoja na hayo hiyo pesa ndogo ambayo anapewa ahakikishe kwamba anaenda kuanza kujenga ile Barabara ya Likuyufusi – Mkenda walau kuanza kwa kilometa 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa na amani na wananchi wa kule wanaendelea kuiamini Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi, lakini hebu watendeeni haki kwa kuanza angalau hata kwa kilometa 10. Hali kadhalika, Barabara ya Maposeni – Mgazini yenye urefu wa kilometa 70 tunahitaji ijengwe kwa kiwango cha lami kwa sababu ni barabara ya kimkakati na ni barabara ambayo tunaamini kabisa itaendelea kuchagiza uchumi katika Wilaya ya Songea na kwa wananchi wa Songea pamoja na nchi nzima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaenda Namtumbo. Pale Namtumbo pana Barabara ya Lumecha – Londo – kwa Mpepo yenye zaidi ya kilometa 300. Ninawaomba sana hapa imekuja lugha ya *EPC+F,* sijui *plus Five* ambayo tumekuja huko tena imeanza sijui nini, bado hii barabara haijaeleweka. Ninaomba Mheshimiwa Ulega atakapokuja hapa atueleze Barabara ya Lumecha – Msindo – Hanga – Kitanda, tujue hii barabara inaanza lini mpaka Londo kule kwa Mpepo. Ni barabara ya kimkakati ninaona Mbunge wa pale Mikumi anachekelea sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara hapohapo Namtumbo, Barabara ya Mtwara Pachani – Tunduru yenye urefu wa kilometa 305 inatoka Mtwara Pachani – Lumecha – Ligela –

Lingusenguse mpaka kule Mchomolo na kufika kule Mbesa mpaka Tunduru Mjini kilometa 305. Barabara hii kila bajeti inapokuja, ninalia na hii barabara ni kwa nini Serikali haipeleki pesa kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami? Sasa, ninaomba Waziri aje na majibu mazuri ili ioneshe kwamba baba Tulia yuko makini, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaenda Barabara za Nyasa. Nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali ambayo kimsingi miaka miwili iliyopita mimi nilipiga magoti hapa kikwetu tunasema "*niligalauka*" ndani ya Bunge, kulia kwamba Daraja la Mitomoni ambalo lilikuwa na changamoto watu wengi wamepoteza maisha pale. *Alhamdullilah,* sasa hivi Serikali tayari imeshaanza kujenga daraja lile, ambapo imeleta matumaini makubwa sana kwa Watanzania wanaoishi katika maeneo yale. Tunaishukuru sana Serikali, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mitano tena kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninaomba nichukue nafasi hii kuizungumzia Barabara ya *Mbamba Bay* – Litui, hapohapo Nyasa. *Mbamba Bay* – Litui, ina zaidi ya kilometa 100 tunaomba hii barabara ni barabara ambayo inahusisha masuala ya utalii inapita pembezoni mwa Ziwa Nyasa, hebu tujengeeni kwa kiwango cha lami ili na sisi tuendelee kuchanua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nizungumzie Barabara ya kilomita 56 Kigonsela – Mbaha. Barabara hii sasa hivi imeenda kuwa tunu zaidi. Ninaomba sasa wapende wasipende watuwekee, hii barabara ndiyo atakayokuwa anapita Mheshimiwa Makamu wa Rais, sasa sijui itakuwaje Mheshimiwa Ulega, Mheshimiwa Makamu wa Rais, anatoka pale Kigonsela anakwenda mpaka kule Mbaha kilomita 56. Tunaomba sasa ijengwe kwa kiwango cha lami Mheshimiwa Makamu wa Rais ajae ndiyo atapita hiyo barabara. Ahsante sana

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie Barabara ya Kitahi – Ruanda, yenye urefu wa kilomita 40, lakini barabara hiyo inakwenda mpaka Lituhi – Ndumbi kilomita karibu

50 au 60, pale Ndumbi pana bandari kwa hiyo, tukitoka pale Kitahi kwanza yule mkandarasi hajalipwa, hajalipwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa bajeti hii itoe mwelekeo wa kwenda kuwalipa wakandarasi wote ambao wamekuwa wakidai pesa zao, wanafanya kazi wanakuwa na madeni wengine wanapoteza maisha, wamekuwa na mapresha hawawezi hata kutoka ndani wanadaiwa na mabenki, wanadaiwa na watu binafsi tunaomba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa haya malizia.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, achia kidogo niunge mkono hoja. Baada ya maneno hayo ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii na wewe ni mtu makini, mtu mahiri. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Shabiby, wajiandae Mheshimiwa Mkenge na Mheshimiwa Noah Saputu.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji dakika ni chache tutakwenda kidogo haraka haraka. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* na timu yote ya *TANROADS* maana yake usipokuwa unasema ukweli unakuwa ni mchawi au mnafiki, kwenye ukweli lazima tuseme ukweli, kwamba *TANROADS* wanajitahidi sana lazima tuwapongeze na tuwape moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hizi pongezi tatizo linalokwamisha *TANROADS* ni pesa na lazima tuangalie pesa ndiyo kikwazo kikubwa kwa *TANROADS* lakini kila siku zinavyozidi kwenda barabara zinazidi kuongezeka. Kwa hiyo, changamoto kwenye *TANROADS* lazima ziwepo na barabara za zamani nazo zinachakaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kama hii ya Morogoro – Dodoma sasa hivi muda wake ule wa kutengenezwa

umeshafika lazima itengenezwe tena upya barabara nyingine ni mpya. Kwa hiyo, lazima tutafute chanzo Mheshimiwa Waziri lazima watafute chanzo kingine wapendekeze kwenye Kamati ya Bajeti wapate vyanzo mbadala kwa ajili ya kuweza kuisaidia *TANROADS* ipate pesa ili Waheshimiwa Wabunge wote tufurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye upande wangu wa Jimbo langu la Gairo Mkoa wa Morogoro na ukiangalia Wilaya ya Kilindi Mkoa wa Tanga kuna barabara moja muhimu sana tumekuwa mimi na Mheshimiwa Mbunge wa Kilindi Mheshimiwa Omari Kigua tunaifuatilia kwa karibu sana barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba watu wa *TANROADS* safari hii niwapongeze wametujengea madaraja makubwa sana ambayo katika historia ya ile barabara. Hata hivyo, pale Matare panahitaji makaravati tu makubwa ili barabara ile yote iweze kupitika kuanzia Gairo mpaka Kilindi na mwaka huu ninajua wameweka kwenye *feasibility study* kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile Barabara ukitoka Tanga kupitia Handeni – Kilindi - Gairo - Dodoma ni karibu sana kuliko barabara nyingine yoyote kwa kutokea Dodoma. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, aifuatilie sana hii barabara na Mheshimiwa Naibu Waziri alipita na Mheshimiwa Waziri alipita wakasema kweli barabara hii ni nyepesi, tunaomba kwenye *feasibility study* ifanyike waitafutie pesa ziwekwe pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwenye kipande kile cha Gairo – Nongwe, ile *feasibility study* ninafikiri imeshakwisha, tunaomba waitengee sasa pesa kwa ajili ya kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Pale Gairo Mjini alishapewa mkandarasi ninafikiri kama kilomita moja hivi kwenda mpaka hospitali ya wilaya, lakini ndiyo hiyo Barabara ya Nongwe alichimba chimba akapachafua lile eneo ameliacha kama ilivyo. Tunaomba tujue huyu mkandarasi kuna tatizo gani eneo lile? Ili aweze kumaliza kile kipande cha ile barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna yale maeneo ya milima maana yake tunaposema Nongwe milima yake ni mikubwa kuliko hata ile milima ya kwenda Lushoto. Kuna wale wakandarasi ambao wamewapa pale kwa ajili ya kuweka zege maeneo ya milimani toka mwaka juzi mpaka mwaka huu unaona bado wanasuasua magari mengi yanapata matatizo yanaanguka watu wenye pikipiki wanaanguka, wenye magari makubwa yanaanguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba wafuatilie. Kwa vile dakika ni chache naomba niwashukuru sana Wizara ya Ujenzi, wanafanya kazi nzuri, hongera sana. Ninaunga mkono hoja na ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkenge, wajiandae Mheshimiwa Noah Saputu na Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza kabisa ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuweka miundombinu ya barabara katika nchi yetu vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi Mheshimiwa Alhaj Abdallah Ulega kwa kazi kubwa anayoifanya na pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya, Katibu Mkuu Balozi Aisha, Naibu Katibu Mkuu ndugu yangu Charles Msonde na wafanyakazi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja niende katika baadhi ya barabara kwenye Jimbo langu la Bagamoyo. Miaka mitatu iliyopita pale katika Daraja la Mpiji linalounganisha Bagamoyo pamoja na Dar es Salaam, Serikali iliingia mkataba wa ujenzi wa daraja lile na wananchi wote katika vyombo vya habari wameona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mpaka leo ni mwaka wa tatu sasa tumeambiwa kwamba daraja lile makandarasi

alinyang'anywa tenda kwa sababu utendaji wake siyo mzuri. Lakini baadaye tukaja kuambiwa kwamba mto umepanuka *feasibility study* inafanyika upya, kwa hiyo mpaka sasa hivi wananchi wa Kiembeni hawaelewi lile daraja litakwisha lini na lile daraja ni kiungo kizuri sana kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo. Vilevile ni sehemu ambayo inaweza ikapunguza foleni kubwa sana katika Mji wa Bagamoyo pamoja na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, alitupie macho daraja hili kwa sababu wananchi wana matumaini makubwa kwamba mkataba umeshaingiwa na litajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda nizungumzie Barabara ya Mingoi – Kiembeni, barabara hii ni barabara ambayo ilikuwa katika ahadi ya Mheshimiwa Rais mwaka 2020 barabara hii ina urefu wa kilomita nane, imeahidiwa kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, lakini sasa hivi barabara hii imerudishwa mikononi mwa *TANROADS* baada ya kuwepo kwa *TARURA* kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii mpaka sasa hivi bado haijajengwa na hali sasa hivi na mvua zinazoendelea ni mbaya sana wananchi wa Kiaraka, Kiembeni, Minazi Minane, Tungutungu wanapata shida mno. Maji yanapita katika barabara kuu kama ni mto unatembea vile. kwa hiyo, tunaomba Serikali ichukulie umuhimu sana barabara hii ili wananchi hawa nao waweze kupita vizuri kabisa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya tatu ambayo nataka kuizungumzia ni barabara ya Makofia – Mlandizi, barabara hii ya muda mrefu sana na ipo ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi karibu kipindi cha nne au cha tano sasa hivi bado inazungumziwa na ujenzi bado haujafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, namfahamu wewe ni jembe la kazi, watu wanasema kwamba mzigo mzito mpeni Mnyamwezi, lakini bahati nzuri Mzaramo amepewa mzigo huu mzito. Ninaomba barabara hii ya Makofia – Mlandizi kitu cha kwanza fidia kwa wananchi kabla ujenzi

haujaanza. Wananchi hawa wakipata fidia itakuwa kidogo imeleta nafuu fulani, halafu ndiyo ujenzi uendelee pale pesa zitakapopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina matumaini makubwa katika hotuba ya Waziri, amezungumzia barabara hii, niombe Mheshimiwa Waziri ajitahidi kupambana na barabara hii, kwa sababu ni ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ambayo ninataka kuizungumzia ni Barabara ya Boko – Bagamoyo kama mnavyojua Bagamoyo kuna kongani kubwa ya viwanda ambayo itakuja kutokana na hotuba za Waheshimiwa Mawaziri waliopita pamoja na Bandari ya Bagamoyo. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri, barabara hii ya kutoka Boko kuja Bagamoyo ijengwe sambamba na hiyo. Kuna fidia ambayo watu wamefanyiwa tathmini mwaka wa nane kwa ajili ya upanuzi wa barabara hii bado haijafanyika, basi ninaomba wawasaidie fidia zao wale watu na hii barabara ikianza ujenzi wake kupanuliwa ili mambo ya maendeleo yaendelee vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ninayotaka kuizungumzia ni Barabara ya Tamko – Baobao – Mapinga. Barabara hii ni ya siku nyingi, nimeshuhudia mweyewe utiaji saini wake pamoja na Mradi wa *DART* awamu ya tatu walitia saini siku moja katika ujenzi, lakini bahati mbaya mpaka leo hii tunavyozungumza barabara hii inasuasua sana haiendi vile inavyotakiwa, miaka inaondoka vipande vinavyojengwa vidogo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunaomba kabisa barabara hii nayo itiliwe mkazo imalizike ilimradi wananchi wanaotoka Kibaha kuja Bagamoyo na maeneo mengineyo waweze kufaidika na barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nizungumzie barabara ya mwisho, Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge. Niishukuru Serikali barabara hii ujenzi unaendelea kama ilivyozungumza, lakini nina ombi moja Mheshimiwa Waziri, hii barabara ina umuhimu sana kwa Bagamoyo na sehemu zinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii barabara imeanzia Tanga, lakini niombe kama kungekuwa na uwezekano kukawa na mkandarasi ambaye anaweza kuijenga kuanzia Makurunge angefanya hivyo kwa sababu barabara hii inachechemua uchumi wa Bagamoyo na nchi kwa ujumla. Kwa sababu barabara hii itakapoanza kujengwa pale Makurungwe itakuwa na mambo ambayo yatasaidia kwanza mbuga ya Wanyama Saadan itafikika kirahisi watalii wengi watakwenda kutembelea Mbuga ya Wanyama Saadan itakapojengwa barabara kwa kupitia huku. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuna miradi ya uzalishaji chumvi katika maeneo ya Kitame pamoja na Saadan chumvi kule inazalishwa karibuni kila mwaka tani 100,000 zinashindwa kutoka kipindi hiki cha mvua kwa sababu barabara haipitiki. Kwa hiyo, ninaomba waitilie mkazo barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, kuna kiwanda kikubwa sana cha Bagamoyo *Sugar* ambacho kipo kule huduma zao za uzalishaji wa miwa na sukari zinakwama kipindi hiki cha mvua, hakuna kinachoendelea kutokana na barabara inakuwa mbovu haipitiki maroli makubwa hayawezi kwenda. Kwa hiyo, shughuli nyingi za maendeleo zinalala. Vilevile barabara hii itakapotengenezwa basi wazalishaji miwa wa pembeni *out growers* watapata fursa sasa ya kupeleka miwa yao katika Kiwanda cha Bagamoyo *Sugar* kwenda kuuza na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine na la mwisho ni taa za barabarani *TANROADS* wamejitahidi sana kutuwekea taa za barabarani Bagamoyo, lakini bado hazitoshi barabara inayoanzia *round about* katika mzunguko wake kutokea Kichemuchemu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkenge malizia.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, zinahitajika taa za kutosha. Kwa haya, machache ninaiomba Wizara iyatilie mkazo mambo hayo ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Noah Saputu, Mheshimiwa Tabasam, Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, Mheshimiwa Kilumbe, Mheshimiwa Kunti Mayala.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Nianze kwa kumshukuru sana Mungu kwa kunipa nguvu na afya ya kuwepo katika Bunge hili kwa siku ya leo na hata siku zingine zilizopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu itajikita zaidi kwenye yaliyotekelezwa lakini pia yale ambayo tunaomba Wizara hii iweze kutusaidia kukamilisha na nyingine kutekeleza. Nianze pia kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendelea kutuhudumia kwa nyanja zote afya, maji, barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri wetu Mheshimiwa Ulega pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa jinsi ambavyo wanajitahidi kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri kwenye ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwa kusema kwamba ninaanza na shukrani kwa Rais na Wizara kwa maana ya Mheshimiwa Ulega, mwenyewe kwa kukamilisha fidia ya wananchi wa Barabara ya Mianzini - Sambasha kuja Ngaramtoni kiasi cha shilingi bilioni 3.5. Kwa niaba ya hao wananchi tunashukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kutoa fidia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, hatutoi shukrani kwa maana ya ujenzi wa barabara hiyo unaendelea mkandarasi yupo kazini na mpaka sasa mkandarasi ameshalipwa zaidi ya bilioni 8.1, tunatoa shukrani nyingi sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, tunaomba kwamba mkandarasi yupo kazini, lakini bado anasuasua kwa sababu ile *flow* ya pesa ni kidogo. Kwa hiyo,

ninaomba sasa kumwomba kwa heshima kubwa Mheshimiwa Waziri na amekuja kwenye barabara hiyo tukazungumza kwa kweli tunakushukuru kwa msukumo wake, maana alipokuja alitupatia tena fedha kidogo mkandarasi akasogea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwombe kwa heshima kubwa tunaomba sana barabara hiyo kwa sababu tunaelekea huko tunapoelekea basi tuangalie angalau kabla ya kipindi hiki uweze kurusha hela kidogo, mkandarasi aendelee kwa kasi kubwa ili tuone wananchi wetu wanafurahia barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia mkandarasi huyo anaendelea vizuri kufanya kazi na Meneja wetu wa mkoa anafanya kazi nzuri sana kwa kweli kitu ambacho anatusaidia pale ambapo tunapata changamoto hasa katika mambo ya mafuriko, mambo ya nini anatusaidia sana Meneja wetu wa Mkoa. Mheshimiwa Waziri tunaomba barabara hiyo sasa kama ambavyo alikuja tukamwomba isiishie kule *forest* kwa sababu ikiishia *forest* itakuwa haileti maana kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba lile ombi ambalo tumemwomba mbele ya wananchi na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa akamwomba, Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Mkoa wa CCM akamwomba, basi ninaomba hilo alichukulie kwa uzito wa aina yake kwa sababu itapata maana kubwa sana pale ambapo itakuwa imekuja kuunganisha kwenye Chuo chetu cha *Forest* inayoenda Golomotonyi inakuja kuungana na Barabara ya Nemanga itakuwa imetusaidia sana katika kuleta maana halisi kwenye barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la mafuriko ambalo inakuja kuathiri Barabara ya *bypass* Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na *RAS* wameunda Kamati ya Wataalamu wakiwemo *TANROADS* na taasisi zingine kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanaenda kuangalia mafuriko hayo ambayo inakuja kukata hiyo barabara ya *bypass.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwombe ripoti hiyo itakapokamilika na kuwasilishwa basi achukulie kwa uzito wa aina yake kwa sababu barabara hiyo inakwenda kubomoka na

inaweza ikakatika. Ni barabara ambayo imetengenezwa kwa pesa nyingi zaidi kwa sababu usipoziba ufa utajenga ukuta. Nimwombe sana na anajua barabara ni siasa na siasa ni Barabara. Kwa hiyo, ninaomba hilo alichukulie kwa aina yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Barabara ya Arusha – Simanjiro – Kongwa kuja Dodoma, tunashukuru sana Serikali kwa sababu mmesaini mkataba wa kilomita 70 ambayo ni sawa na bilioni karibu 221,350,265,000, tunashukuru sana. Tunaiomba basi Serikali mkandarasi huyo kwa sababu amesaini mkataba ile mwezi wa pili, niombe sana mkandarasi huyo aingie kazini. Ili yale malengo yetu ya kujenga barabara hiyo. Kwa sababu kwenye jimbo langu nina kilomita 28 kutoka *T. Packers School* kuja *Losonyai*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ule upande wa Mbauda kilomita 22, kwa hiyo, jumla kwa upande wetu sisi tuna kilomita 50 ikienda tena mbele itakwenda kwenye Jimbo la Simanjiro ambayo nayo wataendelea na hizo kilomita zingine hadi kufika huku Dodoma. Kwa hiyo, naomba sana kuishukuru Serikali na nimwombe mkandarasi huyo aweze kuingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine tunaomba pia wakati wa ujenzi wa hizi barabara basi viwekwe vibanda vya bodaboda kwa sababu wana-*park* kila mahali bila utaratibu tunaomba sana hili nalo ni muhimu katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu ya muda ninaomba kuunga mkono hoja, lakini yote haya ambayo yamepangwa basi yakatekelezwe chini ya Waziri wetu Mheshimiwa Ulega. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tabasam wajiandae Mheshimiwa Mlaghila, Mheshimiwa Ng'enda na Mheshimiwa Majala.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema ninawiwa kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati kabisa kutoka moyoni ninaomba kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya katika masuala ya miundombinu hasa ya madaraja, barabara na miundombinu ya treni ya mwendokasi. Mheshimiwa Rais hakuwa peke yake, ni kwamba amefanya kazi hii akiwa pamoja na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wa Ujenzi waliopita kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule Sengerema, wananchi wa Jimbo la Sengerema wamenituma nishukuru; asiyeshukuru binadamu hata Mwenyezi Mungu hawezi kumshukuru. Kazi kubwa iliyofanywa kwanza kupata shilingi bilioni 730 kwa ajili ya kulipa mkandarasi ili amalize daraja, juzi nimepita daraja lipo 99% na Sengerema tumepitia wakati mgumu sana. Sasa wamenituma kwanza nije nimshukuru Mheshimiwa Rais na kumwambia Mheshimiwa Waziri Ulega, amekuja Sengerema darajani pale ameona, tulikuwa naye tunakwenda kuangalia miundombinu ya *ferry,* hizi *ferry* zilizotengenezwa ambazo ziko katika *package* ya kuja kufunguliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezunguka kote tumekwenda naye mpaka Buyagu kwenda kuangalia *ferry* ya Buyagu – Mbarika na ameona kabisa hali ilivyo. Wananchi wa Sengerema tulichosikitika ni kwamba, kila daraja likitajwa linatajwa kwa jina la Kigongo – Busisi, lakini wakati Marehemu Mfugale anali-*design* lilikuwa linaitwa Kigongo - Misungwi na Busisi - Sengerema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama hamtaki kuita Kigongo - Misungwi, huku kwangu iteni Kigongo – Busisi - Sengerema ili na sisi tuingie kwenye orodha ya madaraja makubwa duniani, kwamba Sengerema lipo daraja. Ninamwomba sana mtani wangu katika hilo. Baba Tulia, akija Sengerema aandike ule ubao, tunakwenda kufungua Daraja la Busisi - Sengerema.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanufaika wa hili daraja tuliopata machungu ya kutoka Sengerema kwenda Mwanza ni sisi watu wa Sengerema. Wale watu wa Misungwi wanasafiri kwa barabara ya lami kwenda mjini, lakini sisi Sengerema mpaka tuvuke, watu wa Geita mpaka wavuke, watu wa Kagera mpaka wavuke na watu

wa Kigoma mpaka wavuke. Kwa hiyo, watu wote unaowaona wanaotokea njia hiyo kabisa wako pamoja na Mheshimiwa Rais kumuunga mkono wanasubiri tarehe tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo watu wa Sengerema wamenituma nikuulize lini Mheshimiwa Rais anatia timu pale Sengerema na ufunguzi wa daraja usifanyike upande mwingine ambao hawalihitaji. Ufunguzi wa daraja unakuja kufanyika Sengerema, sawa Bwana mkubwa? Ninamwomba sana katika hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ufunguzi uwe Sengerema kwa sababu sisi ndiyo tutakaokuja pale. Zaidi ya wananchi wa Sengerema tupo 450,000, lakini ninamhakikishia 100,000 tutatia timu Busisi. Yeye aandae tu nyati wa kutosha, kama anatuletea ngamia tule ngamia na kama ni ng'ombe wawe ng'ombe wa kutosha. Kwa hiyo, tunakuja kufanya na sisi Sengerema tuna jambo letu katika hilo daraja. Mtani, ninafikiri Waziri amenielewa? Ninaomba nirudie tena, ananielewa Baba Tulia katika hili jambo? Ninamsihi sana yaani kwamba sherehe inafanyika Sengerema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu waliofanya kazi katika daraja lile tunaomba waandikwe kwa wino wa dhahabu. Alikuwepo pale Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano, Marehemu Magufuli. Pamoja na kufikiria, lile jambo lilionekana ni kubwa sana, lakini aliungwa mkono na wataalam wakiwemo Mawaziri waliokuwemo kwa wakati huo. Sasa hao nao waingie katika orodha, Makatibu Wakuu waliokuwepo waingie katika orodha. Pia, ma-*engineer* waingie katika orodha hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonisikitisha, pale tunaye *engineer* anaitwa Ambrose. Huyu Bwana anakaimu hii nafasi yaani toka ujenzi wa daraja mpaka anamaliza daraja bado wanamkaimisha tu, huwajamwamini tu kweli kama Wizara na kama anafaa kuwa *engineer*? Kasimamia madaraja yote, kasimamia maeneo ya kuweka vivuko na magati. Kwa hiyo, huyo hafai kweli kuwa *engineer* mtu wa namna hiyo, wanataka waadilifu gani? Inaumiza maana tukiwa tunakwenda naye pale

ninamwona namna anavyokuwa mnyonge, kwa sababu kwanza hajiamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninataka kushukuru tu katika hili jambo, lakini tuna barabara zetu; tumemaliza kazi kubwa tunaishukuru Serikali. Hizi barabara zetu zina changamoto. Kwa mfano barabara ya kutokea Kamanga - Sengerema ilikuwa imewekwa katika mfumo wa lami kilometa 32. Nimeshajengewa kilometa mbili na nilikuwa nimeweka kwenye bajeti zote mbili ya 2023/2024 na 2024/2025 kilometa 10, lakini yule mkandarasi hajalipwa pesa. Kwa kuwa tumemaliza kazi kubwa ya daraja kubwa, basi wafikiriwe na hawa wakandarasi. Pia, tunazo barabara zingine tena ambazo ni za moramu zinazohudumiwa na wakala wetu wa barabara *(TANROADS)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Wizara, hebu wajazeni fomu wawape Waheshimiwa Wabunge wa nchi nzima tulioko hapa, barabara ambazo ni za muhimu kabisa zinazopita kwenye majimbo yetu sisi tuwajazie fomu kwamba ikitengenezwa barabara hii, ina changamoto hii na mahali hapa kunahitajika daraja; sisi tujaze hizi fomu. Kwani akitugawia fomu kesho, tukamjazia sisi akajua ukubwa wa kazi, wanaokuja kule kufanya upembuzi wa hizi Barabara, hao watu wa Mheshimiwa Waziri, ma-*engineer* wake wa mikoa si wanaangalia zile fomu ambazo Wabunge tumeelekeza? Sisi ndiyo tunaozijua barabara na ndiyo tunaoishi na watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ambayo ninataka nimshauri pia ni sehemu za mitaro. Hebu angalieni sana hii mitaro, hizi *catchwater* na *mitre* ndiyo ulinzi wa hizi barabara. Pia, tunataka tumshauri akipata mzabuni akaagiza *package* kubwa China, anunue *Armco culvert*. Hizi barabara zinakuja kujifunga kwa sababu tu ya kukosa *Armco culvert* ambapo wakinunua wakawa nazo za *emergency*, barabara nyingi zingekuwa zinafunguka. Kwa mfano, kama barabara ya Lindi…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, malizia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ninampongeza sana Mheshimiwa Ulega kwa

ujenzi wa *ferry* na sisi Wilaya ya Sengerema, tumepata *ferry* mbili; *ferry* moja ipo kwa pacha wangu kule Mheshimiwa Eric Shigongo najua tarehe 30 tunakwenda kuzindua na *ferry* nyingine iko Buyagu – Mbarika. Hii tunaiombea pesa, kule imebakia pesa kidogo ile *ferry* na yenyewe tuichukue ili wakati tunafungua daraja na ile *ferry* iwe inapelekwa Buyagu – Mbarika kwani magati yameshamalizwa kujengwa na sisi tuwemo kuonekana Watanzania tulionufaika na Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, malizia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila, jiandae Mheshimiwa Kilumbe na tutamalizia na Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Tumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Huyu ni Rais ambaye amekuja kutimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu kuiweka Tanzania kuwa nchi ya asali na maziwa. Ni Rais ambaye pamoja na misukosuko mikubwa ambayo nchi yetu ilikuwa inaipitia, ikiwemo korona na vita vilivyotokea lakini yeye amesimama imara ameijenga nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata leo hii ukiangalia kuna watu wanazungumza kufunguka kwa madaraja makubwa kama Kigongo - Busisi huko Sengerema. Pia, leo tunazungumza ma-*flyover* yanayojengwa pale Jijini Dar es Salaam. Ninaomba niseme tumebarikiwa sana na ninaomba tuendelee kumuombea sana Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii Wizara tumepata Waziri bora kabisa ndugu yetu Komredi Ulega, akisaidiwa na ndugu yangu Mhandisi Godfrey Kasekenya. Hawa watu wanafanya kazi kubwa sana, lakini nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipowashukuru watendaji, hasa Mtendaji wa *TANROADS* kwa kazi kubwa anayoifanya. Anazunguka Tanzania nzima, anahangaika lakini anahakikisha kazi zinafanyika. Pia, wapo wanaomsaidia nao ni

ndugu zetu dada yetu Balozi Aisha Amour na Naibu Katibu Mkuu, mtu wa chapuchapu wa kufanya mambo yaende ndiyo maana sasa hivi mambo yanabadilika harakaharaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipomshukuru Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mbeya, kaka yangu *Engineer* Masige. Anafanya kazi nzuri, halali usingizi, chochote kinachotokea hata kwenye Wilaya yangu ya Kyela, kilometa 130 hata iwe usiku asubuhi utamkuta amefika, ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nimshukuru na niishukuru Serikali kwa ujenzi wa madaraja mazuri mawili ambayo yalikuwa yameharibika kabisa; nalo ni Daraja la pale Nsesi ambalo sasa limewekwa vyuma, lilikuwa ni mbao. Pia, Daraja la Ipyana lilikuwa ni mbao lakini pamoja na bajeti ndogo aliyonayo, amejitahidi ameweka chuma na daraja linapitika vizuri. Ninakushukuru sana kaka yangu *Engineer* Masige na ninamwomba Mungu aendelee kumpa uhai ili aendelee kuwatumikia wana Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina baadhi ya maombi; tunapozungumza utajiri na uchumi wa Tanzania, huwezi ukazungumza haya yote bila kuzungumza Barabara ya TANZAM. Unapozungumza mambo yote ya uchumi, unapozungumza Bandari ya Dar es Salaam, huwezi kuzungumza bila kuitaja Barabara ya *TANZAM*. Mheshimiwa Waziri, ninaomba Barabara ya TANZAM kutoka Igawa kwenda mpaka Tunduma imekwisha kabisa, pamoja na kile kipande cha Nsalaga. Nimpongeze, jembe amekuja, sasa hivi wakandarasi wanapiga hatua, tunaomba ashikilie hiyo *speed* wale watu wamalize ile barabara. Barabara ya njia nne pale Jijini Mbeya inakwenda kwa kasi, ameifanya hiyo kazi na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Barabara inayotoka Uyole kuelekea Kasumulu. Ninaomba, ile barabara sasa hivi inatimiza miaka 35, ilijengwa na kampuni ya Sogea. Sasa ile barabara mpaka sasa hivi bado iko hai. Ninaomba badala ya kusubiri ife kabisa hebu tufanye utaratibu tuweke *layer* ya *overlay,* itasaidia sana kusogeza muda mpaka tutakapopata pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la kwanza; ninaomba twende tukasaini mkataba wa Barabara ya Ibanda - Itungi Port - Kanjunjumele, (barabara yako ya Kanjunjumele). Ombi la pili; twende tukawalipe Wanakanjunjumele fidia zao; Wanakyela wanasubiri haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana tuendelee kusisitiza ujenzi wa barabara ambazo zitaleta manufaa na zile za ulinzi. Leo hii ninaomba nikushukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kusaidia uwezekano wa ujenzi wa barabara inayotoka Matema kuelekea Ikombe na kuunga kwenye Wilaya ya Ludewa. Ninafikiri hii ni barabara muhimu sana kwa wananchi na pia kwa ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo barabara nyingi ambazo zinahitaji ujenzi, lakini bado tunapambana na bajeti ambayo ni ndogo. Ninaomba sana kwa Mkoa wa Mbeya tuongezewe bajeti ya barabara. Ninasema haya kwa sababu kuu mbili; sababu ya kwanza ni tofauti ya mazingira yaliyopo kwenye huo Mkoa, kila eneo lina mazingira tofauti. Kule Kyela unapojenga barabara tupo chini kabisa, usawa wa bahari ni mita 400 tu. Kule barabara zote zinatakiwa ziinuliwe zaidi ya mita mbili kwenda juu ndipo utakapoweza kupita, lakini unapofika Rungwe unatakiwa uchunge mlima mita tano ndipo uikute barabara. Sasa kwa bajeti hii ndogo hatuwezi kufanikiwa. Ninaomba sana bajeti kwenye Mkoa wa Mbeya iongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana, hebu sasa hivi twende tutengeneze teknolojia mpya ambazo zilikuwa zikitumika huko nyuma kupunguza gharama. Ninaomba tuanze kujenga madaraja ya mawe *(arch bridges)*. Hayo madaraja mengine yapo lakini sehemu ambazo tunaona hatuwezi kutumia gharama kubwa hebu twende tujenge *arch bridges* kwani zinasaidia sana kupunguza gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara ijifunze sana kwenye makosa ambayo yamekuwa yakifanyika nyuma hasa tunapojenga hizi barabara. Kwa mfano, pale Jijini Dar es Salaam tunaendelea kujenga barabara kwa mtindo ambao tulitumia kwenye *BRT* ya hapa Ubungo na Kimara, lakini kwa sasa hivi

tunaenda Mwenge. Sasa zile barabara kwa nini bado tunaruhusu watu wapite juu ya barabara? Kitu gani kinasumbua watu wawe na *underpass*? Mimi ninaomba haya mambo tuyarekebishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mtaala wa elimu ya usalama na udereva kwenye barabara zetu. Sidhani kama mitaala yetu ilikuwa na barabara…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally, malizia.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Bado hatujajifunza kuendesha kwenye barabara mbili, ninaomba elimu hii itolewe ili tuweze kuzitumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ng'enda Kilumbe, tutamalizia na Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweke mchango wangu katika Wizara hii muhimu ya ujenzi. Kwanza ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa afya na uzima ili tuendelee kuwatumikia wananchi waliotuchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ningependa nichukue nafasi hii kwanza kupongeza sana hotuba nzuri ya bajeti iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli wamejipanga na nimpongeze yeye Mheshimiwa Waziri maana hii Wizara ni mpya kwake. Ametoka kwenye ile Wizara ya kitoweo (Uvuvi na Mifugo) na akaja kwenye hii Wizara, ameanza vizuri na ameanza kwa kasi. Nimwombe Mheshimiwa Waziri asirudi nyuma, aendelee na hiyo kasi. Hawa wakandarasi hawataki kuchekacheka nao sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze vilevile, Mheshimiwa Naibu Waziri, askari huyu wa *infantry*. Anafanya kazi vizuri na

tumekuwa tukishirikiana naye hapa Bungeni, anajibu maswali yetu mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwa ujumla, nipongeze Mamlaka ya *TANROADS* kuanzia Mtendaji Mkuu, na pongezi za pekee nimpe Meneja wangu wa mkoa *Engineer* Choma ambaye ameibadilisha sura ya Mji wa Kigoma, Manispaa ya Kigoma Ujiji kuwa ya kisasa na kwa kweli ukifika utajua kwamba *TANROADS* ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nianze kwa kuzungumzia suala la upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma na hatua ya maboresho makubwa ambayo yanafanyika. Hapa nilitaka niseme, niipongeze sana Kamati kwani imefanya uchambuzi wa kutosha na kueleza kazi ya maboresho yanayofanyika katika uwanja wa ndege iko kwenye 16%, lakini hawakusema ni kwa muda gani. Mimi ninataka nieleze, ni 16% katika kipindi cha miaka sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili jambo siyo jema kwa sababu zabuni ya upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma na hasa maboresho ya jengo la abiria *control tower* na hayo mengine ilitangazwa mwaka 2019. Mwaka 2020 waka mu-*award* mkandarasi waliyempa hiyo nafasi ambaye ni Kampuni ya Kichina inaitwa *CRCEG*, lakini mwaka 2021 hadi 2022 pamoja na kumu-*award* mwaka 2020 hakuna kilichofanyika na ikapita miaka miwili kimya kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023 Januari, wakasaini mkataba na mkandarasi huyu, mwaka 2023 Septemba ndiyo kazi ikaanza, leo tuko mwezi Mei, 2025 miaka sita ndiyo tunazungumza 16% ya kazi hiyo iliyotangazwa mwaka 2019. Kwa hiyo, jambo hili lazima niseme ninyi mngekuwa ni wananchi wa Mkoa wa Kigoma kwa kweli wangeona kero ya kazi hii ambayo imesuasua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo ambalo linafanya kazi hii isuesue ni suala zima la kuchelewa kuanza kwa kazi hii na hawakufanya ile kitu inatiwa *price adjustment,* mkandarasi anapiga kelele kwamba amepewa kazi wakati gharama

zimeshapanda kwa kiwango kikubwa, anaanza kazi katika kipindi cha miaka mitatu tangu wam-*award* na Serikali imepewa mapendekezo na mkandarasi na mpaka sasa hawajajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, namwona kwa kasi yake asaidie mjibu hizi hoja za mkandarasi zinazohusu *price adjustment,* wafanye *adjustment* ili waweze kumpa fedha aweze kuendelea. 16% katika miaka sita ni aibu! Kwa hiyo, jambo hili nilitaka nilisemee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwanja wa ndege wa Kigoma lina *project* mbili, moja ni hiyo ya maboresho na pili ni ya kupanua na kuongeza *running way* kutoka kilomita 1.8 hadi kufikia kilomita tatu. Sasa kuna wananchi pale ambao mli-*earmark* maeno yao kwamba hawa watapaswa watoke kwa ajili ya kupisha upanuzi wa hiyo *running way.* Kilichotokea tangu mwaka 2023 mwishoni walipowafanyia makadirio ya gharama za kufanya *compensation* mpaka leo wananchi wale hawajalipwa, wanashindwa kuendeleza maeneo yao, kwa maana hiyo *project* haiwezi kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Kamati imesema Wizara ya Ujenzi maeneo ambayo inatakiwa kuwa-*compensate* wananchi ni thamani ya shilingi bilioni 123.63. Hivi kweli hiki ni kiwango kikubwa cha kutufanya sisi tugombane na wananchi wetu? Kila ukifika huko au wanataka huyu Mama Rais wetu mpendwa aliyefanya kazi nzuri sana akienda huko kwenye kampeni watu waanze kubeba mabango ya *compensation?* Ninawaomba kama wanafikiri hawana mpango wa kuendelea na *project* ile kwa sasa walipeni wale wananchi halafu wao wataendelea taratibu, lakini kwanza wale wananchi wawe wamewatoa. Kwa hiyo, jambo hili kwa kweli limekuwa ni kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka nilizungumze ni mradi wa barabara itokayo Tabora kuja Kigoma. Ninataka niipongeze sana Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara nzima wamefanya kazi nzuri, mpaka sasa eneo lililobaki ni kama kilometa 17 tu ndiyo linalotakiwa kukamilishwa kuwekwa lami, pamoja na eneo la daraja kuelekea pale Kibaoni. Hata hivyo, taarifa zinasema kwamba mpaka sasa ni nguvu ya

wafadhili ndiyo inakwenda. Ile 10% maana pale tuna wafadhili wale wa *OPEC* na Abu Dhabi, ile 10% ya Serikali mpaka sasa hamjaweka, sasa tusije tukaenda huko mbele mkandarasi akakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachokiomba ni kwamba Wizara wasimamie ile 10% ya Serikali iweze kulipwa na wakamilishe kazi hii kwa wakati unaopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ninataka kulizungumza hapa ni suala la kibajeti ambalo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe malizia.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni kengele ya pili? Kwa kuwa haya bado tuna muda wa kuyazungumza, kwa kweli ninaunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia muda niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii ya ujenzi, bajeti yetu ya mwisho kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na uhai na kuweza kulizungumza Taifa letu kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze alipoishia Mheshimiwa Kilumbe kuhusu suala la viwanja vya ndege na Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha kesho, nitaomba aje na ufafanuzi na majibu ya mambo yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, ninaomba uwaambie wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini, Kata ya Kiwanja cha Ndege waliopisha upanuzi wa uwanja wa ndege ule tangu

mwaka 2016, walifanyiwa uthamini mpaka leo wamefanya upanuzi watu wengine wamewalipa fidia, wengine hawajawalipa, tunataka wananchi wa Dodoma kujua watu ambao hawajawalipa fidia na hawajawaambia chochote wanaendelea na lile eneo ama hawaendelei nalo? Nyumba zao zimeharibika, zimebomoka hawawezi kuendeleza, hawawezi kufanya chochote, ninataka aje na majibu. Je, yale maeneo bado wanayahitaji? Kama wanayahitaji mnalipa lini? Jambo la pili, kama hawayahitaji ni nini kauli yenu kuwasaidia kuwapa fedha ili waweze kurekebisha ama kukarabati nyumba zao ili waweze kuendelea na maisha yao? Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, atusaidie, Uwanja wa Dodoma wa Ndege wa Msalato unakamilika lini? Maana yake imekuwa ni kesho, keshokutwa, sasa hivi tunaona hata kazi zenyewe pale haziendelei ni majani tu ndiyo yanazidi kuota mle, kwa hiyo watusaidie pia uwanja wa ndege ni lini utaisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu lingine, ni mwaka wangu wa 10 ninachangia bajeti humu ndani tangu mwaka 2016 mpaka leo mwaka 2025 ninachangia bajeti ya Wizara ya Ujenzi, nikizungumzia barabara ya Kibirashi – Kiteto – Chemba mpaka Kwamtoro – Singida, mwaka wa kumi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii siyo ya leo siyo ya jana ni kwamba barabara hii imekuwa kwenye vitabu na ahadi za viongozi. Mheshimiwa Mkapa wa Awamu ya Tatu miaka yake kumi alimaliza, akaja Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Kikwete miaka 10 akamaliza 20, amekuja Hayati John Pombe Magufuli miaka mitano kamaliza, leo yuko Mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, ametoa kauli kwamba barabara hii iende ikajengwe kwa mfumo wa *PPP*. Mheshimiwa Waziri niliuliza swali hapa tarehe mbili na Mheshimiwa Naibu Waziri akanijibu kwamba mko kwenye mchakato. Mheshimiwa Waziri siamini kama Mheshimiwa Rais anatamani Watanzania wa nchi hii waendelee kusikia maneno yenu ya michakato na utaratibu. Mheshimiwa Rais anatamani kuona kazi inafanyika watu wako *site,* wananchi wanapata

huduma na siyo maneno yao matamu wanayowapa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka Waziri akija kuhitimisha awaambie hususani wananchi wa Wilaya ya Chemba kwa sababu hawana barabara ya lami kabisa kwenye Wilaya ile, ni hii wanayotuambia ya Kondoa ni vijiji vitano tu ambavyo vinapitiwa. Barabara ile sisi ni wakulima tunawalisha mpaka ninyi, ile barabara mkitupatia mtatusaidia kukuza uchumi wa Wilaya ya Chemba na wananchi wake, lakini na Taifa kwa ujumla. Akija hapa atuambie michakato yao wanayoendelea nayo ni lini inakamilika ya barabara ya kutoka Kibirashi - Kwamtoro mpaka Singida inaanza kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo miaka hii 30 leo ambayo wananchi hawa walisimamishwa pia na wao nyumba zao kujengwa walioko pembezoni, waliishawekewa 'X' wakafanyiwa uthamini, wana miaka 30 wanasubiri barabara ije haiji, wanasubiri fidia haiji. Atakapokuja kuhitimisha kesho, ninaomba aje aniambie na wananchi wa Chemba leo wanamsikiliza, kwamba ni lini mnakwenda kuwalipa fidia ambayo itakuwa ni stahiki ya leo siyo ya miaka 30 iliyopita, kwa wale ambao wanapisha hiyo barabara?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo natamani kulisema kwenye Wizara hii ni suala zima la uharibifu wa barabara zetu. Tunatumia gharama kubwa sana kujenga barabara, lakini matumizi yetu siyo rafiki pia. Leo ukipita barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, pembezoni unakuta ni *parking* ya malori, kila kona kingo za barabara zimekatika. Ninawaomba ninyi ni Serikali moja, wazungumze watu wa TAMISEMI, watu wa Uchukuzi, pia watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Trafiki wetu wamekuwa wakianzisha vituo wanavyotaka wao kukamata magari barabarani, ambako wanasababisha pia uharibifu mkubwa sana wa barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapolia barabara ni lazima tuweke na mifumo mizuri iliyo bora ya kuzitunza hizo barabara ili ziweze kutusaidia. Kwa hiyo ninaomba Wizara nilizozitaja, wakae chini, watengeneze mfumo rafiki wa kufanya majukumu yao bila

kuziharibu hizo barabara, baada ya muda mchache tena tuwe tunarudi tunalia barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la ukarabati wa hizi barabara. Ninaomba kuuliza wanisaidie, hivi hizi barabara wanapoweka viraka lazima kuwe na manundu makubwa yale? Yaani vile viraka wale watu wanaowapa kufanya ukarabati wa hizi barabara zetu, ukipita hii Barabara ya Dodoma – Morogoro, ukarabati wanaoufanya manundu vile viraka vimewekwa ni mafurushi, mafurushi ndiyo utaratibu, yaani ndiyo inavyotakiwa kufanywa hivyo ama ni nini? Kwa nini barabara zinazofanyiwa marekebisho zinakuwa zina manundu manundu? Hakuna namna bora inayoweza kuwekwa kukarabati zile barabara, hivyo viraka kuzibwa? Zikazibwa kiraka ambacho mtu akipita apite eneo ambalo liko limetulia badala ya kuweka yale manundu manundu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia watusaidie zile ni fedha. Wanaweka yale manundu manundu baada ya dakika mbili yamebanduka wanarudi tena wanaenda kuweka yale manundu manundu. Kwa hiyo, ninawaomba pia waweze kuliangalia hilo kwenye suala zima la ukarabati wa barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni ujenzi wa Daraja la Kelemasimba, Wilayani Chemba, Kata ya Mondo. Mheshimiwa Naibu Waziri wewe umekuwa ni mzoefu, lakini na wataalam pia ni wazoefu Katibu Mkuu na viongozi wengine. Alienda Mheshimiwa Bashungwa kwenye daraja lile, alijionea hali halisi ya lile daraja. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri kaka yangu Ulega hajawahi kushindwa na jambo, amefanya maajabu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ninamwomba hapa Dodoma Chemba siyo mbali, barabara tunayoipigia leo kelele hiyo ya Kibirashi, anaweza akatoka hapa akaangalia akaona namna gani hiyo barabara ina uhitaji, pili hilo daraja akajionee mwenyewe. Waziri alikuja akaahidi wananchi pale kwamba wataleta fedha ili tuweze kujenga lile daraja na ilikuwa likamilike tangu mwaka jana, lakini mpaka leo kimya. Wananchi wa Chemba wanatamani kujua daraja lile…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Wananchi wa Chemba wanataka pia wajue Daraja la Kelemasimba mtalijenga lini ili waweze kupita kwa amani na utulivu na kuendelea kuokoa vifo vinavyoendelea kutokea katika daraja lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa muda, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyu ndiye mchangiaji wa mwisho, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.10 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano Tarehe 7 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*